**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 16 Julai, 2007**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. John S. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mwuliza swali la Kwanza, ninapenda mtambue tu kwamba kwa sasa hivi, Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali humu Bungeni ni Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakhia Meghji.

Na. 214

**Kuifanya Vunjo kuwa Wilaya**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza :-

Kwa kuwa wananchi wa Moshi vijijini wameridhia kupitia Baraza la Madiwani kuwa Vunjo ifanywe Wilaya na Makao Makuu yake Makuu yawe Himo Njia Panda; na kwa kuwa wananchi wanangojea kwa hamu tamko la Serikali kuhusu suala hili: Je, Serikali inasemaje kuhusu ombi hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uundwaji au ugawaji wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria ya Serikali za Mitaa Na.7 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na.8 (Mamlaka za Miji) za mwaka 1982 na Sheria ya taratibu za uanzishwaji wa Mkoa na Wilaya Na.12 ya mwaka 1994.

Kadhalika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye mwenye mamlaka ya kugawa maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya pamoja na Tarafa. Aidha, viko vigezo muhimu vinavyotumika kuanzisha maeneo ya utawala, vigezo hivyo ni pamoja na:-

- Ukubwa wa eneo la kilomita za mraba zisizopungua 5,000;
- Idadi ya Kata zisizopungua 15;
- Idadi za vijiji visivyopungua 50;
- Idadi ya watu wasiopungua 100,000;
- Eneo lenye Jiografia inayozuia huduma kuwafikia wananchi kwa urahisi kama vile milima, miti, misitu mikubwa, visiwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya kuigawa Wilaya ya Moshi ilijadiliwa katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 21/10/2003. Baada ya kikao hicho, mapendekezo ya kuigawa Wilaya ya Moshi hayajawasilishwa kwenye kikao cha ushauri cha Mkoa wa Kilimanjaro *(RCC)* kwa ushauri na mapendekezo zaidi.

Namshauri Mheshimiwa Mbunge apelike suala hili katika Halmashauri yake ili maombi yapitishwe katika vikao halali na baadaye kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ni vyema wananchi wote wakafahamu kwamba ugawaji wa Wilaya au uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala inawezekana endapo Serikali inalo fungu la kuyajenga Makao Makuu ya Wilaya, gharama za uendeshaji na uwekaji miundombinu muhimu pamoja na watumishi wa Wilaya husika. Inakadiriwa kuwa kuanzisha Wilaya inagharimu Serikali shilingi bilioni 4.5 ambazo ni fedha nyingi na siyo rahisi kwa Serikali kuzipata kwa wakati mmoja kwa maeneo mengi. Hivyo, kuanzisha maeneo mapya kunafanyika kulingana na uwezo wa fedha za Serikali.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza: Kwa kuwa, Jimbo la Vunjo lina zaidi ya Kata 15 na zaidi ya vijiji 70 na zaidi ya wakaazi 150,000; Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba katika Wilaya 20 ambazo zitaanzishwa, Vunjo itakuwa ni mojawapo? Swali la pili; kwa kuwa mwaka jana hapa Bungeni, Naibu Waziri alikubali kwamba atapeleka milioni 50 kuanzisha Kituo cha Afya Himo, na mpaka sasa hivi hizo fedha hazijafika; Je, Naibu Waziri atakubaliana na mimi ni wakati sasa wa kupeleka hizo fedha?

**SPIKA:** Swali la pili la nyongeza halihusiani na swali la msingi na kwa hiyo, silikubali. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali la kwanza!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Jimbo la Vunjo kuna Tafara 2, Kata 15, Vijiji 78 pamoja na vitongoji 363 na wakaazi zaidi ya 200,000. Lakini, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba ugawaji wa maeneo unategemea uwezo wa Serikali. Kwa hiyo, Serikali itakapokuwa na hali nzuri na uwezo wetu wa

mapato ukituruhusu kwa wakati huo, ndipo Wilaya mbali mbali zitapewa kipaumbele. Tuelewe kwamba kuna Wilaya nyingi ambazo zimekidhi vigezo na Serikali kwa sasa - naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, haina mpango wa kuanzisha Wilaya hizo mpya 20 kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Serikali pale itakapokuwa na hali nzuri, nipo tutaanzisha Wilaya kwa awamu na siyo Wilaya 20 kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Na. 215

**Majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Majengo ya Ofisi za Utawala wa Serikali pamoja na Majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ni machakavu sana na imefikia hatua ya kuweza kuhatarisha maisha ya wafanyakazi wa Ofisi hizo; na kwa kuwa Jengo la *DC* lina zaidi ya miaka 150, yakiwemo na Majengo ya Idara ya Elimu, Kilimo, Maliasili, Ardhi na Ofisi zote kwenye Jengo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyashughulikia majengo hayo ili kuwanusuru watumishi hao wasipatwe na maafa wakiwa katika kazi zao ndani ya ofisi hizo?

(b) Pamoja na Halmashauri ya Wilaya kuandikia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Je, Serikali iko tayari kwenda kufanya tathmini ya majengo hayo na tathmini ya ujenzi wa majengo mapya katika bajeti ya mwaka 2007/2008 na 2008/2009?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba majengo mengi ya Serikali yaliyopo Pangani yamejengwa zaidi ya miaka 100 iliyopita kwa kutumia mawe, chokaa na udongo asilia.

Majengo ya Ofisi za Halmashauri na Mkuu wa Wilaya yamechakaa, yana nyufa katika nguzo na kuta hali ambayo inahatarisha usalama wa watumishi wanaotumia majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda usalama wa watumishi, Jengo la Mkuu wa Wilaya limekuwa likifanyiwa ukarabati mdogo mdogo ambao kwa kweli hautoshi. Jengo hili lina Ofisi ya Mbunge, Uhamiaji, Mshauri wa Mgambo, Afisa Usalama, Maji na

Mkaguzi Mkuu wa Ukumbi wa Halmashauri kama hatua ya muda mfupi. Hatua ya muda mrefu ni pamoja na kujenga jengo jipya la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na jengo jipya la Ofisi za Halmashauri. Kwa sasa eneo la ujenzi wa Ofisi za Halmashauri lililopo Mkoma linaendelea kupimwa na Idara ya Ardhi (W), michoro ya awali ya ujenzi wa Ofisi imekamilika. Shughuli zote hizo zimefanyika kwa kutumia fedha za Rukuzu ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Wakala wa Majengo Mkoa wa Tanga ameanza kufanya tathmini kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi mpya ili Serikali iweze kufahamu gharama halisi za ujenzi.

Ili kukarabati majengo yaliyopo Wakala wa Majengo amefanya makisio ya jumla ya shilingi milioni 73 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Pangani. Serikali inaendelea kutafuta fedha hizo ili ukarabati ufanyike kama mpango wa muda mfupi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a), Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imeshaanza taratibu za kujenga jengo jipya kwa ajili ya Ofisi za Halmashauri. Aidha, kuhusu Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Wakala wa Majengo ameshaanza kufanya tathmini hiyo. Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, Serikali linaendelea kulifanyia kazi suala hili ili kuhakikisha kuwa Mkuu wa Wilaya ya Pangani anapata Ofisi inayostahili.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali maiwili madogo ya nyongeza: Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Serikali imekwishaanza mipango ya majengo mapya ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Halmashauri, pamoja na mipango hiyo, bila shaka Serikali inafahamu kwamba mipango inaendelea.

Je, imetenga fedha katika bajeti hii kwa ili mipango hiyo ikikamilika waanze ujeenzi mara moja? Swali la pili; Inapofikia kwamba majengo mapya yamejengwa na kwa kuwa jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ni la kihistoria, Serikali ina mpango gani au mikakati gani ya kuhifadhi majengo hayo baada ya kukamilika majengo mapya ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba wenzetu Ofisi hii ya Pangani ina matatizo na ni chakavu, Serikali, hili inalitambua na ndio maana inafanya mipango ya aidha, kukarabati kwa muda mfupi na mipango ya muda mrefu, kujenga jengo hilo. Mkoa wa Tanga ulipeleka maombi maalumu Hazina kuhusu ujenzi wa Majengo ya Pangani pamoja na Hospitali ya Bombo.

Lakini, Hazina waliona kwamba la muhimu zaidi ni ukarabati wa Hospitali ya Bombo badala ya majengo ya Wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani. Kwa hiyo,

kwa mwaka ujao, hilo suala la majengo ya Pangani litapewa kipaumbele zaidi kulingana na hatari ambayo Serikali imeiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, kama kawaida, Serikali inahifadhi majengo yote ya zamani na itakapojenga jengo jipya pale Pangani, majengo yale ya zamani yatahifadhiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zetu za Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Laizer nimekuona! Kwanza, kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote, pokea pole kwa wananchi wa Longido kwa tetemeko la ardhi la jana.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa pole hizo na ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Halmashauri nyingi nchini zinafanana na matatizo ya Wilaya ya Pangani hasa Wilaya mpya zilizoanzishwa ikiwemo Longido.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kusaidia Halmashauri hizo ili nao waweze kuwa na makazi kwa watumishi wengi watakaohamia katika Halamashauri hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, mlipitisha Bajeti ya Serikali ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema wazi kwamba zile Wilaya mpya ambazo zimeanzishwa pamoja na Halmasharui zake, kwa mwaka huu zimetengewa Bajeti kidogo ya kuanza majengo mbali mbali ya Wilaya pamoja na Halmashauri.

Kwa hiyo, hizo Wilaya mpya zitatengewa fedha za ujenzi mwaka hadi mwaka hadi kukamilika.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunahamia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, ambaye leo amelivalia rasmi ili kuweza kuliuliza. *(Kicheko)*

Na. 216

**Chakula Kilichozalishwa Nchini**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inahimiza wananchi kulima na kuzalisha chakula kwa wingi ili kujitosheleza kwa chakula kifamilia na ziada kwenye Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(SGR)*:

(a) Je, ni kiasi gani cha mpunga na mahindi kimezalishwa katika Mikoa ya Iringa, Rukwa na Mbeya mwaka jana?

(b) Je, Serikali inaweza kununua kiasi gani cha chakula hicho?

(c) Je, ni nini hatma ya chakula ambacho bado kiko mikononi mwa wakulima hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali, ningependa pia kukupa pole na Waheshimiwa Wabunge kwa tetemeko la ardhi lililotokea asubuhi saa kumi na moja hapa Dodoma.

Mheshimiw Spika, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Kahalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mwaka jana katika msimu wa 2006/2007 wakulima katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Rukwa walizalisha jumla ya tani 311,387 za mpunga, kati ya hizo tani 20,263 zilizalishwa katika Mkoa wa Iringa, tani 217,206 katika Mkoa wa Mbeya na tani 73,918 katika Mkoa wa Rukwa.

Uzalishaji wa mahindi katika Mikoa hiyo ulikuwa jumla ya tani 1,113,882. Kati ya hizo tani 443,828 zilizalishwa katika Mkoa wa Iringa, tani 409,890 katika Mkoa wa Mbeya na tani 260,074 katika Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

(b) Serikali kupitia Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(SGR)* iliweza kununua jumla ya tani 43,195.079 za mahindi kutoka Mikoa hiyo. Tani 14,777 zilinunuliwa kutoka Mkoa wa Iringa, tani 2,178 zilinunuliwa kutoka Mkoa wa Mbeya na tani 26,238 zilinunuliwa kutoka Mkoa wa Rukwa.

Mahindi hayo yamehifadhiwa katika maghala ya *SGR* ya Makambako, Mbozi na Sumbawanga kwa ajili ya matumizi wakati upungufu wa chakula unapojitokeza katika maeneo mbali mbali ya hapa nchini. Kwa sasa *SGR* inanunua mazao ya mahindi na mtama tu. Utaratibu wa kununua na kuhifadhi zao la mpunga bado haujaanza.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali huhamasisha wafanyabiashara kununua ziada ya mazao ya chakula kutoka Mikoa hiyo na kuuza katika Mikoa mingine yenye upungufu wa chakula. Aidha, kuitokana na hali nzuri ya chakula iliyokuwepo nchini mwaka huu wa 2006/2007 mwezi Januari, Serikali iliruhusu wafanyabiashara kuuza chakula nje ya nchi. Ruhusa hiyo bado ipo hadi sasa. Hivyo, kama bado kuna mazao hayo mikononi mwa wakulima mazao hayo yanatumika na wakulima wenyewe kama chakula hadi msimu wa mavuno mapya utakapoanza na ziada waliyonayo wa uhuru wa kuiuza kwa wafanyabiashara ili kujipatia fedha kwa ajili ya matumizi mengine ya kaya.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya kumwuliza: Kwa kuwa katika maelezo na takwimu aliyotoa, amekiri kuwa ni sehemu ndogo tu ya chakula ambayo Serikali imekinunua; na kwa kuwa wananchi ili waweze kufanya kazi vizuri wanahitaji kupata soko la uhakika na bei nzuri. Je Serikali inasaidiaje katika hilo? La pili, ka tika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki ambayo tunayo, zipo habari ya kuwa Kenya wanaagiza Mchele kutoka Pakistan *Metric Tonne 250,000* kwa mwaka. Je, sisi tunalitumiaje soko hilo katika kuwasaidia wakulima wetu kupata soko zuri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, kwanza, nikiri kwamba Serikali haifanyi biashara ya kununua mahindi. Ile tani 150,000 ambazo Serikali inanunua kwa mujibu wa sheria ni kwa ajili ya dharura kunapotokea majanga ya njaa kwa muda wa miezi mitatu kabla ya kuagiza chakula kutoka nje ya nchi. Serikali haiwezi ikanunua zaidi ya kiwango kile hadi tutakapobadilisha sheria hii. Hata hivyo, kuna masuala ya Bajeti, Bajeti ambayo inatengwa kwenye *SGR* ni ndogo, haiwezi ikakidhi kununua chakula cha wananchi wote wanaolima. Lakini pia kuna gharama za wahudumu, kuna gharama za mizani, kuna gharama za kusafirisha yale mahindi na gharama za kutunza yale mahindi. Kwa mfano mwaka huu, mahindi yaliyopo tani 125,000, yanahitaji shilingi bilioni 1,200,000,000 kwa ajili ya kunyunyizia dawa. Kwa hiyo, kuna gharama kubwa sana ya kuhifadhi yale mahindi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba sasa hivi ni biashara huria, wananchi hao na wakulima wanaweza wakauza mahindi yao nje ya nchi wanapopenda na tunaghamasisha wafanyabiashara kuja kununua mahindi pale ambapo yapo mengi na kupeleka kwenye mikoa ambayo wana njaa, lakini pia hata kusaifirisha nje ya nchi. Kwa hiyo, biashara ya chakula sasa hivi kama nilivyosema ni huria, mpaka pale tutakapoona hali ya chakula nchini si nzuri, ndiyo tunaweza kuzuia yasiuzwe nje ya nchi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea jibu zuri la Naibu Waziri wa Kilimo kuuhusiana na mchele ya Pakistan kuuzwa Kenya kama ifuatavyo:- Ni kweli kwamba Serikali ya Kenya ina mkataba maalumu na Serikali ya Pakistan ambapo Serikali ya Pakistan inauza mchele Kenya na Kenya inauza chai Pakistan. Mkataba huu ulikuwepo kabla ya nchi tatu kuingia kwenye ule mkataba wa Soko la Pamoja na ni wa muda na kila mwaka huwa unarejewa kuona iweje. Kwa hiyo, sasa hivi bado unaendelea, lakini ni jambo la mpito na litafika mwisho moja wapo ya siku za karibuni.

Na. 217

**Kituo cha Ununuzi wa Mahindi – Peramiho**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, asilimia kubwa ya wananchi wa Jimbo la Peramiho ni wakulima wa mahindi ambao hulima zao hilo kwa ajili ya chakula na biashara; na kwa kuwa, kitengo cha Hifadhi ya Chakula cha Taifa *(SGR)* ni wanunuzi wakubwa wa mahindi hayo, ambapo mpaka sasa ni kituo kimoja tu katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Songea kinachotumika kwa ununuzi huo wa mahindi kupitia *SGR* (Kituo cha Mgazini):-

Je, Serikali kwa kushirikiana na *SGR* iko tayari kuongeza kituo kingine cha ununuzi kwa wakulima wa Kata ya Gumbiro na wale wa Kata ya Wino?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa *SGR* huwa inanunua mahindi katika kituo cha Mgazini kilichopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Vituo vingine ambavyo *SGR* hununua mahindi katika Mkoa wa Ruvuma ni Songea mjini pamoja na Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, *SGR* ina Kanda sababu za ununuzi, ambazo ni Kipawa, Arusha, Dodoma, Shinyanga, Makambako, Songea na Sumbawanga. Kanda hizo za *SGR* ndizo zenye maghala ya kuhifadhia mahindi na ndivyo vituo vikuu vya ununuzi wa mahindi ya *SGR*. *SGR* haimudu kusogeza huduma hii ya ununuzi kwa kila Halmashauri ya Wilaya hapa nchini kutokana na idadi ndogo ya watumishi wake, uchache wa vifaa vya kutendea kazi (maghala, mizani) kutokuwepo kwa huduma za benki huko vijijini na gharama kubwa za kuhamisha mahindi yanayonunuliwa kutoka huko vijijini hadi kwenye vituo vikuu vya ununuzi nilivyovitaja.Kutokana na hali hiyo, *SGR* haina uwezo wa kuongeza vituo vya ununuzi vya Gumbiro na Wino katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Namshauri Mheshimiwa Mbunge awahamasishe wakulima wa maeneo hayo kuungana pamoja kwa kuunda Chama cha Ushirika ili kwao iwe rahisi kuuza mahindi yao kwa pamoja kupitia Kituo cha *SGR* cha Songea ambacho ununuzi na hifadhi ya mahindi hufanyika na huduma ya uhakika wa malipo kupitia benki ipo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushuru na niombe radhi kwa kuwahi kuuliza swali la nyongeza kabla hujanipa ruhusa. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili makubwa sana ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri hana habari kwamba katika Kata ya Wino ninayoizungumzia kuna Ushirika wa mazao wa wananchi mzuri sana, wana ghala kubwa sana, wanafadhiliwa na mashirika makubwa sana kutoka nje na vifaa vyote vinavyohitajika viko pale na wanaweza kabisa kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Serikali. Je, haoni kwamba ni vizuri kukitumia Kituo hicho kwa kuirahisishia Serikali na wakulima katika uuzaji wa mazao hayo? Pili; Kwa kuwa mara nyingi Wizara imekuwa ikichelewa sana kutoa kibali kwa wakulima wa mahindi kuuza chakula hicho nje ya nchi na hivyo kuwasababishia wakulima hao kuchelewa kuuza mazao yao, kukosa masoko na kukosa fedha za kuondokana na umaskini na kujiandaa na msimu mwingine wa kilimo.

Je, Serikali sasa iko tayari inapochelewa kutoa tangazo la kuuza chakuola nje ya nchi na kusababisha matatizo hayo kwa wakulima hao, kutoa ruzuku maalumu ya kufidia hasara waliyoipata hawa wakulima? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** *SGR* ni hifadhi ya chakula ya Taifa na inatakiwa kununua katika maeneo mengi sana hapa nchini. Lakini, tumekuwa tunatoa umuhimu katika maeneo maalumu kutokana na uwingi wa mazao, na eneo mojawapo tunalolipa kipaumbele ni Jimbo na Wilaya ya Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa sababu ya mazingira maalum ya uzalishaji wa mazao katika eneo hilo. Lakini, kwa ajili ya ufinyu wa Bajeti na vile vile udogo wa *SGR* yenyewe, ni vigumu sana kujitanua mpaka tuweze kufika katika maeneo yote ambayo yanalima na kuzalisha mahindi. Lakini, ningependa nimshauri Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwamba kama tulivyojibu katika jibu la msingi, ikiwa tutanunua kila kitu na chama cha Ushirika kipo pale kwenye maeneo anayotaka Peramiho inunue, ningeshauri kile Chama cha Ushirika kinunue na Kituo cha *SGR* kiwe kinaenda kuchukua moja kwa moja badala ya kufungua Kituo katika eneo lile, huo ndio ushauri wangu. *(Makofi)*

Lakini, kuhusu kuchelewa kutangaza au kibali cha kuuza mazao ya chakula nje, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba suala la chakula na hifadhi ya chakula na usalama wa chakula, ni jambo linalohitaji kutazamwa kwa umakini mkubwa. Tukisema tu tuuze kila tulichonacho, tunaweza tukashtukia hatuna chakula na tukaanza tena kuagiza kutoka nje. Kwa hiyo, Wizara yangu kupitia Kitengo cha Hifadhi ya chakula, huwa inafanya tathmini na mwezi unaokuja itafanya tena tathmini ya kuhakikisha ni kiwango gani kimezalishwa ili tunapotoa uamuzi wa kuendelea kuuza nje, tuwe na uhakika kuna chakuna kinabaki hapa nchini. Chakula ni tofauti na mazao mengine, ukiuza chote, utakinunua kwa bei kubwa zaidi kutoka nje. Kwa hiyo, hiyo ndiyo msingi. Lakini, kwa sasa hakuna kilichochelewa kwa sababu kibali cha kuendelea kuuza bado kipo tangu mwaka jana Januari.

Na. 218

**Mikopo ya Mfuko wa Pembejeo**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya wananchi wa Kyela waliokubaliwa kupewa mikopo ya matrekta na mfuko wa pembejeo miaka miwili iliyopita bado hawajapewa mikopo hiyo na benki iliyoteuliwa kuwahudumia ya *international commercial bank (Tanzania) Limited* huku gharama za kufuatilia mikopo hiyo zimekaribia nusu ya mikopo yenyewe na kwa kuwa mapema mwaka jana wananchi hao walirudishwa na benki hiyo mfuko wa pembejeo ili watafutiwe benki nyingine na kwa kuwa mfuko wa pembejeo bado haujatoa tamko wala wazo lolote kwa wananchi hao wenye uchu wa maendeleo na ambao wameingizwa kwenye hasara kubwa ya fedha na muda katika kufuatilia mikopo hiyo:-

(a) Je, ni lini wananchi hao wa Kyela, husussan Abel Mwafongo na M. A. Kyamba, ambao wameniletea ushahidi wa kimaandishi watapata mikopo hiyo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwafidia kiasi gani kwa usumbufu na gharama walizoingia katika kuhangaika mikopo hiyo?

(c) Je, ucheleweshaji wa mikopo kwa muda mrefu kama huo unaendana vipi na kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Nne ya Ari Mpya, Nguvu na Kasi Mpya?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe Mbunge wa Kyela, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003 mfuko wa pembejeo ulianzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa kutumia mabenki. Aidha, mwaka 2003/2004 benki ya *International Commercial Bank* nayo ilishiriki katika utaratibu huo. Katika mazingira hayo Bwana a. Mwangoka na bwana M. A. Kyamba waliomba na kukubaliwa kupewa mikopo ya matrekta. Hata hivyo kwa sababu zilizokuwa nje ya uwezo wa Mfuko wa pembejeo, benki hiyo ilichelewesha utoaji wa mikopo, kiasi cha kukiuka mabadiliano ya mkataba wa mfuko wa pembejeo na hivyo kuamriwa kurudisha fedha kwenye akaunti ya mfuko. Aidha, majina yote yaliyokuwa yamekabidhiwa kwa benki hiyo yalirejeshwa kwenye Mfuko wa pembejeo kwa nia ya kutafuta njia mbadala kwa kuwahudumia wateja wake. Waombaji waliowasiliana na Mfuko baada ya sakata hilo hatimae walishughulikiwa na kupatiwa mikopo moja kwa moja toka mfuko wa pembejeo. Kwa bahati mbaya, waombaji wawili wa Wilaya ya Kyela hawakuwasiliana na mfuko wa pembejeo hali iliyosababisha wasipewe mikopo yao hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Mwakyembe Mbunge wa Kyela lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ili wananchi hao wakamilishe taratibu zilizobaki nawaomba wawasiliane na Mfuko wa pembejeo ili waweze kupatiwa mikopo waliyoomba.

(b) Gharama zilizojitokeza wakati waombaji wakifuatia mikopo yao, ni sehemu ya gharama ambazo hulipwa na waombaji wenyewe, wakikubaliwa kukopa hata wakikataliwa. Kwa sababu hiyo, hakuna fidia inayotolewa na Serikali kwa mwombaji kutokana na kufuatilia maombi yake ya mkopo.

(c) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kucheleweshwa kwa mikopo kiasi hicho, hakuendani na kauli mbiu ya ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. Hata hivyo tatizo hili limetokana mgongano na mgogoro wa kimkakati na hasa kutokana na benki kushindwa kutimiza majukumu yake kama mikataba iliyokuwa inataka. Pamoja na kuwapa pole wananchi hao nawaomba wawasiliane na Mfuko wa Pembejeo ambao kwa sasa umejipanga upya vizuri ili waweze kuhudhuriwa kwa kuzingatia falsafa ya ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uzembe mdogo tu katika kuwasilisha mahesabu unasababisha adhabu kali kwa Halmashauri na wananchi kunyimwa ruzuku. Sasa kwa nini uzembe upande wa vyombo kama hivyo vilivyowekwa na Serikali ambao unasababishia wananchi hasara kubwa nao sasa usimfanye mwananchi alipwe fidia yake badala ya kupewa pole tu ya mdomo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema uzembe huu haukutokana na mfuko, uzembe huu unatokana na benki walitofautiana, benki ilikuwa inataka mfuko wenyewe ndiyo ufuatilie watu ambao wanakopa wakati mfuko siyo uliokopesha, sisi tunawapa fedha benki kusudi wakopeshwe wale wakulima. Kwa hiyo, waliofanya uzembe ni mabenki siyo mfuko wa pembejeo.

Kwa hiyo, kama nilivyosema kwamba sasa hivi tumeshazungumza na benki na tunarekebisha huo mkataba hivyo vipengele ambavyo tunataka tuvirekebishe ili kila mtu asiumie, mwananchi asiumie yule mkopaji, mfuko wenyewe usiumie, lakini na benki yenyewe isiumie. Lakini pia ningewaomba wananchi kuwashauri wananchi ambao wanakopa kwamba wajaribu pia kufuata taratibu pamoja na kuwasilisha *document* zote zinazohitakiwa. Maana wakati mwingine wanaweza wakapeleka andiko lakini hakuna Ankara kifani (*proforma invoice)* kwa hiyo, sasa kama hakuna *proforma invoice.* Kwa hiyo, sasa kama hakuna *proforma invoice* hata mkopo hauwezi ukatoka utacheleweshwa.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika vipindi viwili sasa vya miaka ya fedha Serikali imekuwa inazungumzia kuhusu kuanzishwa kwa benki ya Maendeleo ya Tanzania, ambayo pamoja na mikopo mingine ingetoa aina ya mikopo hii kwa wakulima pamoja na wajasiriamali wakubwa wakubwa. Je, suala hili la kuanzisha au kuiimarisha benki ya maendeleo ya Watanzania imefikia wapi?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba tumeambia kwamba benki ya *TIB* iwe benki ya maendeleo na ndiyo maana tumeamua kwamba benki ya *TIB* iwezeshwe kupewa mtaji na Serikali imeanza kufanya hivyo lakini pamoja na hayo kwa mwaka wa fedha Benki ya *TIB* imeweza kupata mkopo ambao utaweza kuimarisha zaidi benki ya *TIB*.

Lakini labda nieleze pia kuhusiana na mikopo kwa mfano kama vifaa, matrekta n.k. tunategemea kipindi kijacho cha Bunge nafikiri mwezi Oktoba kuleta Bungeni sheria ya *lease financing*. Nafikiri hili litasaidia pia wakulima. (*Makofi*)

Na. 219

**Huduma ya Maji Karagwe**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Karagwe, linavyo vyanzo vingi vya maji ikiwemo mito na maziwa mbalimbali kama Ziwa Kajunju na kwa kuwa maji yamekuwa ni tatizo sugu kwa Miji ya Omurushaka, Kayanga, Nyakaiga, Ihembe, Rwambaizi na Vijiji vyote vya Kata ya Ihanda na Nyakahanga na kwa kuwa Mheshimiwa Rais, katika kampeni yake Karagwe alihidi kuwapatia maji wananchi hao:-

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuwapatia maji salama wananchi wa Karagwe?

(b) Kama mpango huo upo ni lini utatekelezwa?

(c) Je, Serikali inaweza kuelekeza ni maeneo gani yatapatiwa maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Jimbo la Karagwe, lenye vipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Serikali ilikuwa na mpango kuimarisha huduma ya maji katika Miji ya Omururonga na Kayanga. Mpango huo umetekelezwa kwa kukarabati chanzo cha maji cha Omururongo na kufunga mabomba ya kuelekea katika mitaa ya Kanyabuleza na mwisho wa lami mjini Kayanga.

Vile vile katika mpango huo, Serikali kupitia mradi wa *Nile Basin Initiative* imefanya ukarabati kwenye chanzo cha maji, mtandao wa mabomba na nyumba ya mtambo wa maji uliopo Katoma, pamoja na kufungu bomba kuu, kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji katika Mji wa Kayanga. Uimarishaji huo katika Mji wa Kayanga umekadiriwa kugharimu jumla ya dola za kimarekani 111,544 ambapo *Nile Basin Initaiative* imechangia kiasi cha Dola za Kimarekani 100,000 na Halmashauri ya Wilaya imechangia kiasi cha dola za Kimarekani 11,544. Aidha, Serikali kupitia mashirika ya *rotary club* na Mavuno, pia imefunga pampu ya maji katika chanzo cha maji kilichopo Nyakagera kwa ajili ya kusambaza maji katika kijiji cha Ihanda.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa programu ya Maendeleo ya sekta ya maji itakayotekelezwa katika miaka ya 2006/2025. Utekelezaji ulianza kwa kuandaa miongozo mbalimbali ya utekelezaji na kuchagua vijiji vitakavyohusika katika hatua ya kwanza ya utekelezaji. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 shilingi 349,866,000 zimepelekwa Wilayani Karagwe. Fedha hizo zimepokelewa na Halmashauri tarehe 29 Julai, 2007. Hivyo utekelezaji wa miradi utafanyika kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza programu miradi itakayofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Maeneo yatakayohusika katika miradi hiyo yamegawanyika katika sehemu mbili, ya kwanza ni miradi midogo midogo ambayo ndiyo fedha zimekwishapelekwa na miradi hiyo ni katika vijiji vya Nyarwerwe, Ruhita, Kibondo, Kayungu, Kashanda, Nyakahanga, Umurushaka, Kishao, na Kayanga.

Katika sehemu ya pili ya miradi kumi ya vijiji miradi ambayo itapelekwa ni miradi ambayo ifuatayo kuna miradi ya Kayanga, Bugene, Chabuhora, Nyakaiga, Chamuchuzi, Nyakahanga, Chanika, Kibingo, Kigorogoro na Iteera. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini vile vile nimpongeze kwa jinsi ambavyo ameweza kunijibu vizuri kwamba akina mama sasa kule jimboni kwangu Karagwe watafaidika na maji. Vile vile nimpongeze kwa kutaja vizuri vijiji vya jimbo la Karagwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka Mheshimiwa Naibu Waziri kama anaweza anisaidie kiasi cha fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili niweze kufanya ufuatiliaji sehemu ambazo amezitaja? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa jumla ya shilingi milioni 349,866,000/= zimeshapelekwa na zimepokelewa katika jimbo lake na katika Halmashauri yao. Hizi ni kwa ajili ya miradi ile midogo midogo niliyoitaja.

Pia miradi kumi ya vijiji niliyoitaja fedha zake hazitaweza kufahamika kwa sasa hivi kwani miradi hiyo kwanza tutapeleka mshauri mhandisi ambaye atakwenda kuifanyia uchunguzi na stadi ndogo ndipo tutajua fedha kamili kiasi gani zitakwenda katika miradi hiyo lakini ni matarajio yetu kwamba fedha hizo kuanzia mwezi wa 8 mwishoni zitakuwa tayari. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa Wizara inayofuata ya Nishati na Madini swali Na. 220 limeondolewa na Mheshimiwa Pandu kwa sababu amegundua kwamba hili lilikwishajibiwa katika vikao vilivyopita. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, kwa suala linalofuata.

Na. 221

**Mapungufu ya Sheria ya Madini**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Madini ina mapungufu mengi ambayo yanasababisha migogoro kati ya wachimbaji wakubwa, wadogo pamoja na wananchi; na kwa kuwa, Sheria hiyo haitambui uongozi wa Halmashauri au Mkuu wa Wilaya husika ambao ndio wako jirani na maeneo ya kazi, isipokuwa huhusishwa wakati migogoro inapotokea.

(a) Je, ni lini Sheria itarekebishwa kulingana na hali halisi kwa kuwa hivi sasa Sheria hiyo ndiyo chanzo cha migogoro na inawapatia mwanya wachimbaji wakubwa kuhodhi maeneo makubwa hata kama hawayafanyii kazi?

(b) Kwa kuwa, watu wenye leseni za utafiti wa Madini wana uwezo wa kuchukua eneo zaidi ya Tarafa moja; na kwa kuwa, Kisheria ndiyo wenye mamlaka zaidi juu ya matumizi ya ardhi katika eneo lao la utafiti au uchimbaji. Je, Serikali inasemaje endapo hao wakiamua kuwafukuza wananchi (wakazi) katika maeneo yao ya utafiti au uchimbaji ili mradi wana uwezo wa kuwafidia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya mwaka 1998 inayosimamia Sekta ya Madini nchini ilitungwa ili kuondoa kasoro zilizokuwepo katika Sheria ya Madini ya mwaka 1999 ambayo ilikuwa haikidhi mabadiliko ya Sera ya Kiuchumi zilizochukuliwa na Serikali katika miaka ya 1980. Aidha, Sheria ya Madini ya mwaka 1998 imefanyiwa marekebisho kadhaa kwa kujumuisha mawazo ya wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 Wizara yangu iliunda Kamati ya kudurusu Sera iliyotazama pamoja na mambo mengine maeneo muhimu yanayohitaji marekebisho katika Sheria ya Madini. Mchakato wa Serikali kuridhia mapendekezo ya kuboresha Sera hiyo upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu Na. 95 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998, mmiliki wa leseni ya utafutaji na uchimbaji wa Madini anawajibika kupata kibali cha maandishi kinachomruhusu kuingia na kufanya utafutaji na uchimbaji wa Madini kutoka kwa Mamlaka inayohusika kabla ya kuanza shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, leseni za utafutaji wa Madini huchukua eneo kubwa na wakati mwingine muda mrefu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mwekezaji anahitaji eneo kubwa la kufanyia utafutaji wa Madini ili hatimaye kubainisha eneo dogo lenye Madini yanayofaa kuchimbwa kwa faida.

Kwa mujibu wa Sheria ya Madini, ya mwaka 1998, leseni ya awali ya utafutaji wa Madini *(Prospecting Licence with Reconnaissance Period*) hutolewa kwa miaka miwili. Leseni hiyo haihuishwi. *Prospecting Licence* inatolewa kwa kipindi cha awali cha miaka mitatu.

Endapo mwekezaji atakuwa hajakamilisha shughuli zake za utafutaji wa Madini, leseni hii huweza kuhuishwa kwa vipindi vingine viwili vya miaka miwili miwili kwa sharti la kupunguza nusu ya eneo alilokuwa akilimiliki kila mara anapohuisha leseni yake.

Mtafiti wa Madini hasa Mamlaka zaidi ya matumizi ya ardhi mbali na shughuli za Madini. Aidha, Sheria ya Madini inamtaka mmiliki wa leseni ya utafutaji au uchimbaji wa Madini kufanya makubaliano na watumiaji wengine au wamiliki wa ardhi kwa lengo

la kutoa fidia kutokana na uharibifu au kupisha shughuli za utafutaji au uchimbaji Madini.

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria ya madini iliyopo hivi sasa inawaruhusu kweli wachimbaji wakubwa kuchukua maeneo makubwa sana na inawafanya wachimbaji wadogo wasiweze kufanyakazi ya uchimbaji na mara nyingi wachimbaji wadogo ndiyo huwa wanagundua ni wapi penye madini. Kwa kuwa hawa wawekezaji wakubwa wanachukua muda mrefu na wakati mwingine hawatumii maeneo hayo.

(a) Je, Serikali inaweza sasa ikamruhusu Kamishina akawaruhusu angalau wachimbaji wadogo wakawa wanafanyakazi wakati hawa wakawa wanaendelea na utafiti wakafanyakazi kwa pamoja? (*Makofi*)

(b) Kuwa na sheria kama hii ambayo inatoa mwanya kwa mwekezaji kuwa na kauli kwa kutumia sheria kumhamisha mwenyeji. Je, Serikali haioni kwamba ni hatari mwezekezaji akija akachukua eneo la Tanzania kwamba nataka kutafiti na akasema wananchi wampishe Serikali haioni kwamba ni hatari hiyo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Naona Waziri wa Nishati na Madini ametabasamu, majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa hairuhusu watu wawili wenye shughuli moja waifanyie pale pale na ndiyo sheria ambayo tunayo. Kwa hiyo, hatuwezi kuruhusu mchimbaji mmoja na mchimbaji mwingine wakafanya eneo hilo hilo. Hiyo inaweza kusababisha hatari kwa sababu madini wakati mwingine huwa watu wanagombana. Kwa hiyo, ndiyo sheria tunayo lakini vile vile tunamwomba Mheshimiwa Kabuzi, kama alivyosema kwamba wachimbaji wadogo ndiyo wagunduzi wa madini sheria ya kwetu ambayo tunayo haiko *discriminatory* mtu ambaye anaona eneo anapata eneo na anataka kulitumia aende akaombe leseni. Sasa hatuoni kwa nini hao wananchi wanaanza kufanya kwenye eneo hilo na hawachukui muda wa kwenda kwenye ofisi zetu ambazo ziko karibu na wao kuomba leseni ya kuweza kufanya shughuli na akishaomba hakuna atakayemgusa. (*Makofi*)

La pili juu ya kumhamisha mwenyeji. Sheria yetu inatambua kwamba wenyeji ama sisi sote tuna kitu kinachoitwa *surface right* lakini kitu ambacho kiko chini ya futi moja ni mali ya umma na hakuna mtu yeyote ambaye atahamishwa katika eneo lolote bila kufuata fidia stahili. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Kabuzi, kwamba hakuna utaratibu wowote ambao unawahamisha watu kienyeji isipokuwa tu kwa taratibu ya sheria ambayo tunayo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Naona bado Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza hawajaridhika.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watafiti hawa sheria inawaruhusu kwamba wanapewa miaka miwili wakifanya utafiti na baadaye wanaongezewa miaka mitatu. Ukifuatilia leseni zao hizo wanazopewa hasa eneo la

Nyalugusu wamekuwa wakitumia sheria hii kupokezana kimya kimya na kuwaweka wananchi wa eneo hilo wakinyanyaswa bila kutoa muda wa kwamba ni lini shughuli zao zitakwisha. Je, Serikali inaweza kufuatilia suala hili watu wa Nyalugusa waweze kufanya shughuli zao bila kuwa na wasiwasi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba sheria ambayo tunayo sasa hivi ina upungufu ambao hasa wakati wa kubadilisha majina, ama leseni mtu akakaa nayo kwa muda mrefu. Ndiyo sababu tunadurusu sheria hiyo ili tuweze kuwabana watu wajanja ambao wanaweza kukaa na maeneo kwa muda mrefu bila kufanyakazi ambayo inatarajiwa. (*Makofi*)

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema sheria iliyopo ni *first come, first serve* kwa maana ya kwamba anayewahi kuomba kibali ndiyo anayepewa ruhusa hiyo na kwa kutambua kwamba wachimbaji wadogo wadogo walio wengi ni wananchi wa kawaida ambao hata hiyo sheria hawaijua na zaidi ya hapo kwa kuelewa kwamba Wizara au haijawa na huo mfuko au haijafikisha elimu ya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo wadogo wakatambua haki hiyo. Sasa je, kwa sababu wao ndio, waliokuwepo pale mwanzo nao ndiyo wametafiti yale madini wakayatambua. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni haki yao wale watu kwa sababu hawajaelimishwa kwamba wachukue hizo leseni na hawajui na jukumu ni lao kwao Serikali. Sasa tufanyeje? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, sheria ambazo tunazo kokote duniani hazitambui kwamba kutojui ni haki na ndiyo sababu tumeweka katika ngazi zetu zote uongozi na kiongozi ni pamoja na kuwaelimisha wananchi ulionao. Nategemea Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na amekuja kwenye ofisi zetu mara kwa mara sasa amekwishajua na nina hakika jinsi anavyotembea kwenye jimbo lake atakuwa anatembelea yale maeneo na kuwaelimisha sasa nafikiri hakutakuweko na tatizo kama hili. (*Makofi*)

Na. 222

**Dawa za Wagonjwa wa Kisukari, Kiharusi, Saratani na Shinikizo la Damu**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (K.n.y. MHE. JOB. Y. NDUGAI)** aliuliza:-

Kwa kuwa wagonjwa wa kisukari, kiharusi, shinikizo la damu na saratani wanaongezeka sana nchini na kwa kuwa wagonjwa hao hulazimika kununua dawa kila siku. Je, Serikali inasema nini juu ya kuwasaidia wagonjwa hao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa idadi ya wagonjwa wa kisukari, kiharusi, shinikizo la damu na saratani inazidi kuongezeka. Sababu zinazochangia kuongezeka kwa magonjwa hayo ni pamoja na kukubalika kwa mitindo wa maisha, hususan mabadiliko ya ulaji wa vyakula na ukosefu wa mazoezi ya viungo vya mwili. Aidha, uwezekano wa kupata kiharusi na baadhi ya saratani unaongezeka jinsi mtu anapopata umri mkubwa hivyo hali ya maisha inavyoboreka ndipo magonjwa haya pia yanavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa dawa kwa magonjwa ya kisukari na saratani kwa mujibu wa Sera ya Wizara zinatolewa bila malipo, yaani Serikali inagharamia. Aidha, kiharusi hakina mahsusi. Serikali kupitia mfuko wa Bima ya Taifa ya afya inagharamia matibabu ya magonjwa yote kwa wananchi wa mfuko. Vile vile kwa wale ambao si wanachama wa mfuko huo na hawana uwezo wa kulipia, wanapewa dawa za magonjwa hayo kwa gharama za Serikali. Tiba ya magonjwa ya saratani inatolewa kwa gharama za Serikali kwa wagonjwa wote bila kujali uwezo wao kama miongozo ya kuchangia gharama inavyoainisha. Tatizo kubwa ni bei ya dawa za magonjwa haya ni kubwa ni hii huweza kusababisha dawa kukosekana katika hospitali zetu wakati mwingine. Hata hivyo Serikali inajaribu kuongeza bajeti ya dawa kila mwaka jinsi uwezo unavyoruhusu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa magonjwa haya yanaongezeka kwa kasi kuliko kipindi kingine chochote katika historia ya nchi yetu na kwa kuwa pamoja na maelezo kwamba mazoezi na mabadiliko ya maisha ni sababu mojawapo lakini tukienda mahospitalini tunaambiwa kwamba matumizi ya baadhi ya mafuta ya kula baadhi si salama.

(a) Je, Serikali iko tayari kutangaza hayo mafuta, ni mafuta gani na mengi yanatoka nje ya nchi? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa dawa hizi kwa kweli zinapatikana kwenye hospitali za Mikoa zaidi na hata kwenye Wilaya si sina hizi dawa kupatikana kwa ajili ya magonjwa haya na hasa Kisukari na magonjwa ya moyo. Je, Serikali kwa kuwa wagonjwa sasa wamekuwa wengi mpaka kule vijijini, ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba dawa hizi zinapatikana katika vituo vya afya na hata zahanati ambako tuna hakika kwamba yuko mtalaam anayeweza kuzitoa dawa hizi kuliko kupatika mijini tu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema kwamba anasikia ulaji wa mafuta si salama angependa kujua ni mafuta yepi ili Serikali iweze kuyatamka. Kwanza napenda kusema kwamba mafuta mengi ambayo yanaletwa hapa nchini huwa kabla hayajaingia nchini kuna Mamlaka ya Chakula na Dawa ambao inapitia na kuhakikisha kwamba ni mazuri. Lakini napenda kuchukua nafasi hii kutoa taarifa kwamba mafuta ambayo yanasababisha kuongezeka kwa *cholesterol* katika mwili yanaweza yakasababisha magonjwa haya kuongezeka. Hivyo kwa vile orodha ya mafuta haya ni mengi Wizara yangu inachukua nafasi hii basi ili kuweza kuwaelimisha wananchi mafuta yepi ambayo si mazuri na yepi ambayo wanashauriwa kushauri kutumia. Lakini zaidi mafuta yanatokana na mboga au matunda

ya mimea mara nyingi ndiyo yanashauriwa kutumika kuliko mafuta yanayotokana na nyama.Suala la pili, Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba dawa hizi hazipatikani. Ukweli ni kwamba dawa hizi zinatakiwa zipatikane katika hospitali za Mikoa, Wilayani na hata vituo vya afya. Kama pale inapoonekana dawa hizi hazipatikani kwa kuwatibu wagonjwa wa kisukari na wagonjwa wa moyo ni lazima wale waganga wakuu wa Wilaya au wa Mikoa waweze kuhakikisha kwamba hizi dawa zinapatikana katika *stock*. Kwa maana hiyo basi napenda kutoa wito na kuwaagiza Waganga Wakuu wa Wilaya, wahakikishe kwamba katika *pharmacy* zao dawa hizi za kisukari na dawa za magonjwa yanayotibu magonjwa ya moyo ziwe zinapatikana na hivyo kuzisambaza katika vituo vyote katika maeneo husika. (*Makofi*)

Na. 223

**Ubovu wa Barabara – Kigoma**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma uko nyuma sana kiuchumi tatizo linalosababishwa na kutokuwa na miundombinu ya barabara na kwa kuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete wakati wa kampeni aliahidi kushughulikia tatizo hilo:-

(a) Je, katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara za Kigoma – Uvinza – Kaliua – Tabora hadi Manyoni na Kigoma – Kasulu – Kibondo hadi Nyakanazi?

(b) Je, ni lini Serikali itaziwekea lami barabara za Mji wa Kigoma?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa barabara ya Kigoma – Uvinza- Kaliua - Urambo – Tabora – Manyoni, Serikali imetenga shilingi 4 bilioni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami sehemu ya Kigoma – Uvinza- Ilunde pindi usanifu wa kina wa sehemu hiyo utakapokamilika mwezi wa nane mwaka huu.

Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utaanzia Kigoma na zabuni ya ujenzi wa kilomita 35 za mwanzo zitaitishwa kabla ya mwisho wa mwezi wa nane mwaka huu. Sehemu zingine za Kaliua, Urambo, Tabora na Tabora Itigi hadi Manyoni usanifu wa kina umekamilika.Kwa sehemu ya Ilunde, Malagarasi, Nguruka hadi Kaliua usanifu wa kina utakamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha 2007/2008. Kwa barabara ya Kigoma-Kanyani-Kasulu-Kibondo-Kakonko hadi Nyakanazi. Katika mwaka huu wa fedha 2007/2008 Serikali imetenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya usanifu wa kina.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *Tanroads* Kigoma ilianza ukarabati wa kuiwekea lami barabara ya *Kigoma Station* hadi Ujiji kwa gharama ya shilingi 996.106 milioni. Aidha, katika mwaka wa fedha 2007/2008 ujenzi wa barabara ya *Kigoma Station* hadi Gungu kwa kiwango cha lami utaanza kwa gharama ya shilingi 850 milioni.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa umechelewa. Maswali yamekwisha na muda wa maswali pia umekwisha. Sasa matangazo. Tunao wageni Mheshimiwa Nazir Karamagi, Waziri wa Nishati na Madini, ameniomba niwatambulishe wageni wake ambao ni Bwana Ramadhani Hatibu, Kaimu Mwenyekiti, Bodi ya *STAMICO.* Pale alipo ningeomba asimame, aah yule pale. Ahsante karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Bwana Haruna Masebu, Mtendaji Mkuu wa *EWURA.* Karibu sana. Ningependa tu Waheshimiwa Wabunge wafahamu kwamba Haruna Masebu anatoka katika Jimbo la Urambo Mashariki. Karibu sana Haruna. Pale kijijini kwenu barabara kuu ya kwenda Kigoma ndipo itakapopita. Kwa hiyo, nakupa taarifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maria Hewa, ameniomba niwatambulishe wanawe wawili Digna Hewa na Flora Ajengu, wale pale. Sina hakika kwa nini mmoja ana jina tofauti. Lakini nadhani inawezekana huyu ameolewa. Vinginevyo hakuna sababu kwa nini mmoja aitwe Hewa mwingine aitwe Ajengu. Lakini ni binti zake. Waheshimiwa Wabunge kutakuwa na Makamishna wote wa Tume ya Huduma, tutakuwa na mkutano wa dharura hapo saa saba (7) mchana, ama mara baada ya kuahirisha shughuli za asubuhi hii. Tume ya Huduma za Bunge, ukumbi wa Spika saa 7 kamili au mara baada ya kuahirisha shughuli zetu kwa leo. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu wa Mwaka 2007 *(The Higher Education Students Loans Board (Amendment) Bill, 2007.*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Muswada huo umesomwa kwa mara ya kwanza. Unaofuata.

Muswada wa Sheria ya Utalii wa Mwaka 2007 *(The Tourism Bill, 2007)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu nao wa Sheria ya Utalii wa 2007 umesomwa mara ya kwanza. Unaofuata.

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma wa Mwanza 2007 *(The Public Service (Amendment) Bill, 2007*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Muswada huo pia wa kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma wa mwaka 2007 umesomwa kwa mara ya kwanza.

Waheshimiwa Wabunge hii Miswada kwa namna ilivyochapishwa mtakaouona huu *suppliment* namba 7 una Miswada miwili. Usithani huu ni *Tourism* peke yake.

Kwa hiyo, kuna nyaraka mbili hizi, *suppliment* mbili namba 7 na namba 8. Namba 7 ina Miswada miwili katikati huko utaukuta ule Muswada wa *Public Service* ingawa juu ni wa *tourism.* Nilikuwa naomba niseme hilo kwa sababu mtu anaweza akagafilika akadhani ule mwingine haujasambazwa. Ahsante sana. Katibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007/2008
### Wizara ya Nishati na Madini

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Kwa wale ambao walichangia mara moja nadhani watapata nafasi. Lakini wale ambao walikwishakuchangia mara mbili itakuwa vigumu kwa sababu tutamaliza asubuhi hii ili kuruhusu hoja kujibiwa jioni. Sasa nitawaita kwa mpangilio, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, na wakati huo huo Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya ajiandae.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima hata nikaweza kuwepo hapa siku ya leo. Pia nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Serikali yetu ya Tanzania kwa kuniwezesha kwenda kutibiwa India na namshukuru Mungu sana kwamba nimetibiwa vizuri na ninaendelea vizuri namshukuru Mungu na Mungu aibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa rambi rambi zangu za dhati kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi. Nichukue pia nafasi hii kuwapongeza sana Mawaziri wetu wa Nishati na Madini kwa hotuba yao nzuri walioiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 13 mwezi wa saba mwaka 2007. Naomba nianze kwa kuchangia uchimbaji wa madini. Suala la uchimbaji wa madini katika Mkoa wa Manyara. Mimi ni Mbunge ninayetoka Manyara na Mkoa wa Manyara ni Mkoa ambao Mungu ameupendelea sana kwa kuwapa rasilimali nzuri kama vile wanyama, misitu, madini na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na wachimbaji ninaowawakilisha katika Bunge lako Tukufu, ni pamoja na wananchi wachimbaji wa Mkoa wa Manyara. Hasa wa Mererani wachimbaji wa *Tanzanite. Tanzanite* ni madini pekee ambayo Mwenyezi Mungu amependa kutujalia kama zawadi Watanzania. Ni madini ambayo hayapatikani mahali pengine popote duniani isipokuwa ni Tanzania. *(Makofi)*

Kinachonisikitisha mimi ni kwamba Serikali imeamua kuyapuuzia madini haya hata kuyaachia kwa watu wa nchi zingine kuyatangaza kama kivutio cha nchi zao. Itakumbukwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema kwamba madini haya ya *Tanzanite* yaachwe mpaka Watanzania watakapopata teknolojia itakayowawezesha kuyachimba madini haya na kwa faida ya Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, madini yale yamekuwepo yakichimbwa pole pole na wawekezaji wa hapa hapa ndani, makampuni mbalimbali kama vile *Tanzania Gemstone.* Ilitokea wakati wachimbaji wale wa Tanzania wazalendo wamefikia hatua nzuri ya kuweza kupata uzoefu wa kuyachimba madini yale. Waliyachimba madini hata Serikali ilijua kwamba wazalendo wako pale na walipoweza kupata uzoefu ndipo Serikali ilichukua hatua ya kuwanyang'anya maeneo yale na kuwapa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninaweza kusema kwamba hii ni dhambi kubwa kwa sababu madini haya Mungu alitupa sisi Watanzania ili yaweze kutusaidia sisi kujenga nchi yetu. Baada ya Serikali kuona wale wazalendo wako pale na wanafanya vizuri na wanafanya Maendeleo kinachonishangaza ni kwamba kwa nini Serikali haikuchukua jukumu la kuweza kuyadhibiti madini yale badala ya kuwaondoa wachimbaji wazalendo na kuwapa watu wengine. Hii ni kama kuwanyang'anya watoto chakula chao mdomo na kukitupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inashangaza kwa sababu wachimbaji wazalendo wale wanachimba, walikuwa wakichimba sawa sawa na hao hao wageni waliopewa maeneo yale. Kwa hiyo, naweza kusema huo ni uonevu. Madini haya ya *Tanzanite* yaliweza kufanya mambo mengi ambayo yalionekana katika mji wa Arusha na Tanzania nzima. Kwa mfano, kama Serikali ingeweza ikawadhibiti Watanzania hawa wachimbaji ni kwamba tungeweza tukaijenga nchi yetu na tungeweza kujenga mashule, kujenga majumba makubwa ya kifahari, biashara mbalimbali kubwa kubwa, mashamba makubwa, kupitia madini hayo hayo. Na Serikali ikaweza kudhibiti vizuri, uchumi wetu ukakua, nchi yetu ikajengwa, mashule na kadhalika. Kwa mfano, mchimbaji mmoja wa pale Arusha, siwezi kumtaja jina. Yeye anamiliki hoteli ya *Mount Meru*.

Mwingine naye ni mchimbaji, ana shule inaitwa *Arusha Modern Secondary and Primary*. Huyo pia ni mchimbaji. Mwingine ana *Pansons Hotel.* Tunayo *Radio AAA FM* hizo zote ni juhudi za wachimbaji wazalendo. Je, kungelikuwa na wachimbaji kama hawa 100 tu si kwamba nchi yetu ingeleta sura nyingine mpya?Mimi nimetumwa hapa leo na wachimbaji wale wa *Tanzanite* wanataka kuuliza kwamba kwa mujibu wa Sheria ni kwamba Mererani sasa ni *controlled area.* Na kama Mererani ni *controlled area* ni

kifungu gani na kanuni gani ya sheria iliyotumika katika kugawa kuwanyang'anya wazalendo eneo lile na kuwapa wawekezaji wakubwa? Hilo ni moja. *(Makofi)*

Wao wanataka wajue ni kifungu gani cha sheria kilichotumika. Pili itakumbukwa kwamba wakati ule wa shambulio la Septemba 11, ikiwa Marekani ni wanunuzi wakubwa wa madini yote hasa *Tanzanite* walisusia kununua madini haya na ninakumbuka kwamba Serikali yetu ya Tanzania iliweza kutuma ujumbe kwenda Marekani akiwepo Waziri wetu wa Nishati na Madini. Mambo yaliyozungumziwa kule ni makubaliano ya kwamba kuwepo na *EPZ* katika eneo lile ili madini yote yaweze kupitia katika mkondo mmoja. Haya yalikuwa ni makubaliano ya *Tukson Protocol.*

Mheshimiwa Spika, naomba niulize Wizara kwamba makubaliano yale ni kwamba wameshayafanyia kazi au vipi na kama bado ningeomba *EPZ* yaani *Export Processing Zone* iweze kuwekwa Mererani kwa sababu Mererani ndipo madini mengi yanakotoka, aina mbalimbali za madini ikiwa ni pamoja na *Tanzanite.* Na pia Mererani ni katikati ya mikoa mitatu, Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ikiwa *EPZ* yaani *Export Processing Zone* ikijengwa Mererani ni kwamba wananchi watapata ajira pia itakuza jina la Mkoa wa Manyara, itakuwa ni kivutio pia ya Watalii watatoka sehemu mbalimbali kuja kuona eneo lile na Serikali itaweza kupata mapato na umaskini pia utapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena niende kwenye suala lingine la ile *auction* iliyokuwa inafanyika. Mara kwa mara na kila mwaka Chama cha *TANIDA* kilikuwa kinaandaa *auction* na wanakaribisha wageni kutoka nchi mbalimbali kuja kununua madini. Naona huu sijui ni mwaka wa ngapi, ile *auction* haifanyiki tena. Serikali haiandai tena ile *auction* au Wizara haiandai ile *action* pamoja na na *TANIDA.* Lakini ninachosikia sasa ni kwamba *auction* inafanyika *South Afrika.* Kwa hiyo, badala ya wageni kuja Tanzania kuja kununua madini ya *Tanzanite* wanakwenda *South Africa* kwenda kununua madini yale.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ishughulikie suala hili kwa sababu pia tunakosa mapato mengi kwa kuwaachia vitu vinakwenda holela. Naomba Wizara sasa iwe makini. Naomba tena nije kwenye suala la umeme. Mererani, umeme ni ghali sana. Naona kama ni ghali kuliko sehemu zingine zozote. Kwa sababu mtu wa kawaida, umeme kwa mita ni shilingi 100 mpaka 150 ambako mtu wa kawaida kwa mwezi analetewa bili ya shilingi 60,000, 70,000/=. Mtu wa kawaida hawezi kulipia umeme ule. Kwa hiyo basi mazingira yanaharibiwa kwa sababu inabidi watu wakate miti, mazingira yaharibiwe kwa sababu umeme ni ghali.

Mheshimiwa Spika, naomba nifikie hapo. Na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Nami naungana na wenzangu kumpongeza Waziri wa Nishati na

Madini, Mheshimiwa Nazir Karamagi, na Naibu wake, Mheshimiwa William Ngeleja, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi nichangia maeneo mawili. Eneo la kwanza ukosefu wa umeme Mkoa wa Kigoma na eneo la pili mafuta. Mkoa wa Kigoma sisi hatuna umeme. Ni kilio chetu cha muda mrefu. Tulikuwa tunaomba nasi tuingizwe kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya nne, Wilaya moja tu ya Kigoma Mjini ndiyo ina majenereta. Lakini hata yenyewe majenereta hayo ni mabovu. Na wala hayana uwezo mkubwa wa kuweza kuzalisha umeme wa kutosheleza. Hivyo wananchi hawana umeme.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sasa Serikali, ituangalie na sisi watu wa Kigoma kwa jicho la huruma. Na hili nalisema kwa sababu moja sasa hivi Mwenyezi Mungu ametujalia mwaka jana tumepata mvua za kutosha na mpaka sasa tuna umeme wa kutosha. Lakini vile vile kuna vyanzo vingine vya umeme. Mfano kuna gesi. Gesi ile imeunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Kwa hiyo, na sisi wanaweza wakatumegea kidogo na sisi tukaweza kufaidika kwa kupitia njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Kigoma tumeahidiwa kupata umeme kutoka kwenye chanzo cha maji ya Mto Malagarasi na hii vile vile ni ahadi ambayo iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Tumeahidiwa kupata pesa kutoka *MCC* msaada kutoka Marekani kwa ajili ya kuweza kututengenezea umeme wa kutoka kwenye chanzo cha maji ya Mto Malagarasi. Wasi wasi wangu endapo pesa hizo zitachelewa, Serikali itachukua mkakati gani wa makusudi wa kuweza na sisi kutuunganisha kwenye gridi ya Taifa? Tungeomba na sisi tufikiriwe kwa sababu na sisi tumechoka kusubiri na ahadi vile vile zinakuwa nyingi. Kwa hiyo, kama tukichelewa kupata pesa hizo tuwaombe na sisi watufikirie watuingize kwenye Gridi ya Taifa. Hilo nalizungumza kwa nia njema tu. Kwa sababu na sisi kule ni kilio chetu cha muda mrefu. Ninafahamu kabisa kwamba Serikali yetu inatujali na ina nia njema. Tungeomba mikoa ya pembezoni mtukumbuke.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika ukurasa wa 33 wa hotuba ya Waziri, kuna mradi ule wa jua. Sisi wa Mkoa wa Kigoma hatukuwekwa kwenye mradi ule. Tungeomba basi na sisi Serikali ituangalie kwa sababu sisi nasi hatuna umeme kwenye mradi ule ambao wametengewa watu wengine na sisi Mkoa wa Kigoma tungeweza kukumbukwa tukawekwa kwenye huo mradi wa jua. Angalau tukaweza kupata umeme huo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Waziri na sisi atufikirie kutuweka kwenye mpango huo. Kwenye mpango wa *UNDP* nimeona Mkoa wa Mara, Shinyanga na Mwanza wao wamewekwa kwenye mpango huo. Basi na sisi wajaribu jaribu kuangalia jinsi ya kutubaniabania huko kusudi na sisi tuweze kufaidika. Lakini vile vile ninasema hivyo kwa sababu gani kama tungeweza kupata umeme katika Mkoa wetu tungeweza tukapata wawekezaji wa kuja kuwekeza kwenye Mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vil wanawake na vijana wangeweza kufaidika kwa njia moja au nyingine kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Mkoa wa Kigoma tuna bahati, tuna michikichi katika mkoa wetu. Tuna matunda, kwa hiyo kama tungepata umeme tungeweza kupata wawekezaji wa kuja kutumia vitu hivyo kwa kutumia umeme.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi kule Mkoani wanawake wanajishughulisha na miradi midogo midogo ya kutengeneza mise. Lakini kwa sababu umeme ni wa kusua sua na umeme wenyewe uko katika Wilaya moja, uzalishaji unashindikana. Niombe Mheshimiwa Waziri atuonee huruma. Awaonee huruma wale wanawake na wale vijana wa kule ili tuweze tukapata umeme ili nasi tuweze kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tukipata umeme, tunaweza kabisa tukazalisha kwa kutumia viwanda hivyo hivyo vidogo kwa sababu michikichi ile baada ya kuwa imekamuliwa mawese yametoka, kuna mise na ile mise inatumika kwa kutengeneza mafuta na mafuta hayo huweza kutengeneza sabuni. *(Makofi)*

Vile vile mise, inaweza kutengeneza chakula cha mifugo. Lakini vile vile mise hiyo nayo inaweza vile vile yakitengenezwa matanuru yakaweza kutengeneza umeme, hivyo viwanda vidogo vidogo vikaweza kujiendesha kwa kutokana na mise ambayo imechomwa kwenye matanuru na kutengeneza umeme wenyewe. Tukiangalia kwa mfano nchi ya Malasia. Nchi ya Malasia wana viwanda vidogo vidogo ambavyo viwanda hivyo vingemetokana na mise hiyo.

Kwa hiyo, vinatengeneza umeme, umeme wa kuweza kujiendesha na vile vile umeme unaosalia wanaugawa kwenye gridi ya Taifa, hivyo kuweza kuendeleza nchi yao. Nasi tunaomba tujifunze kutoka kwa wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba hilo linawezekana. Nije *TANESCO, TANESCO* kuna ukiritimba wa uzalishaji umeme na ugawaji wa umeme. Labda kwa vile amepatikana kiongozi mpya wa Shirika hilo pengine utaratibu utabadilika. Sasa nilikuwa naomba tu niulize ni lini Sheria ya Umeme italetwa hapa Bungeni ili iweze kufanyiwa marekebisho kusudi wawekezaji waweze kupata nafasi ya kutengeneza umeme na kusambaza katika nchi hii ili Mikoa ile ambayo haina umeme iweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nichangie eneo moja tu na la mwisho, ni kuhusu mafuta. Kuna makampuni ambayo siwezi kusema ni makampuni ya ubabaishaji. Naweza kusema ni makampuni yanayokwepa kulipa kodi. Ukwepaji ule wa kodi unaleta madhara ndiyo maana hata waliochangia kwenye Wizara ya Fedhawalisema kwamba kuna makampuni ambayo hayasemi ukweli katika ulipaji wa kodi. Na makampuni hayo yanasababisha madhara makubwa katika mambo ya mafuta. Kwa mfano, haya makampuni yanayoleta mafuta ya *JET One*, mafuta ya ndege na kuchanganya mafuta hayo na dizeli na kisha kuyauza kama mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, makampuni hayo yanasababisha madhara makubwa kwa wananchi. Kwa sababu mafuta haya yanapokwenda kuuzwa kama mafuta ya taa na wakati siyo mafuta ya taa halisi huweza kusababisha madhara makubwa.

Katika Mkoa wa Kigoma Wilaya ya Kasulu wamefariki wananchi watano kwa kulipukiwa mafuta ya taa. Walinunua mafuta ya taa wakififikiri kwamba ni mafuta safi kumbe mafuta yale yamechanganywa. Matokeo yake mafuta yakalipuka, yakaua familia moja ya watoto watatu, mama na familia nyingine, baba akafariki kwa kulipukiwa na mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sasa Wizara ya Nishati na Madini itusaidie kulichukulia hili ili makampuni haya ambayo si waaminifu waweze kufanya mambo kwa uaminifu ili kunusuru maisha ya wananchi. Kwa sababu wanapofanya vile wananchi wanateketea, kwa sababu ya watu wachache wanaotaka kujilimbikizia mali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba *TRA* wawadhibiti watu hawa ambao siyo walipa kodi wakishirikiana na watu wa Nishati na Madini ili waweze kuwanusu wananchi. Wananchi wanakufa. Sasa hivi wananchi katika Wilaya ya Kasulu walikuwa wanaogopa kutumia mafuta ya taa wakidhani kwamba wakitumia yale mafuta ya taa pengine yamechanganywa na hayo mafuta ambayo si mafuta salama. Kwa wananchi wakarudi kutumia vijinga vya moto.

Mheshimiwa Spika, tunaenda wapi? Tunaenda mbele tunarudi nyuma. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ya Nishati na Madini iliangalie hili kampuni yaweze kuangaliwa jinsi yanavyofanya kazi. Si kwamba yanashindikana, yanaweza yakabanwa na yakaweza kufanya kazi vizuri tofauti na jinsi makampuni hayo yanavyojipangia yenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba kutoa ushauri labda pengine mafuta hayo ni katika ubebaji, pengine tenki linaweza likabeba petroli na kabla halijabeba dizeli, likabeba mafuta ya taa.

Sasa nishauri tu wakitoa petroli kutokana na labda pengine na magari yanakuwa machache, wakitoa petroli wabebe kwanza dizeli, wakishabeba dizeli ndiyo wabebe mafuta ya taa ili mafuta ya taa yasiweze kuchanganyika na petroli ili wananchi wasiweze kupata madhara.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu ni huu na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, ambaye ndiye msemaji anayefuata, naomba tutambue kuwepo kwa General Mboma, Mwenyekiti wa Shirika la *TPDC.* Karibu sana. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Balozi Fulgence Kazaura Mwenyekiti wa *TANESCO,* Ndugu Dr. Idris Rashid, Mtendaji Mkuu wa *TANESCO*, Ndugu Grey Mwakalukwa, Mtendaji

Mkuu wa *STAMICO* na Ndugu yetu Yona Kilagani, Mtendaji Mkuu wa *TPDC*, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, karibu.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia.

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwani tumekutana wote humu ndani leo, naamini tutatoa michango kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mdogo tu kwanza kabisa naomba niikumbushe Serikali kwamba wananchi wanalipa kodi kwa hiyo wanastahili kupata huduma.

Vilevile wakiwemo wananchi wa Mkoa wangu wa Kigoma pia wanastahili kupata huduma. Tukumbuke tarehe 22/5/2007 Mheshimiwa Rais alitembelea Mkoa wa Kigoma, wananchi walimpokea kwa vibatari kwa kuonyesha kwamba wana shida ya umeme, walikuwa wamebeba pia madumu kwa kuonyesha kwamba hawana maji na hiyo kwa upande wa vibatari ilikuwa ni kumkumbusha Mheshimiwa Rais kwamba tarehe 27/8/2005 wakati akihutubia katika Uwanja wa *Community Centre Mwanga* aliwaambia kwamba mtapata umeme wa *Grid* ya Taifa.

Kwa hiyo, ilikuwa katika kumkumbusha tu Mheshimiwa Rais ahadi yake. Kwa hiyo, Naiomba Wizara izingatie hilo ili Rais aonekane ni mkweli mbele ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, tunapewa ahadi nyingi ambazo nyingi hazina *time frame,* naomba nichukulie mfanoo mdogo tu kwa ruksa yako, Wizara ya Miundombinu walisema kwamba Barabara ya lami itajengwa kwa mkoa wa Kigoma lakini hatukupewa *time frame.* Kwa hiyo, naomwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini asirudie tatizo hilo bali atupe *time frame* ni lini umeme wa *Grid* ya Taifa utafika.

Mwaja Waheshimiwa Wabunge wote wa Kigoma tulipata bahati ya kuongeza na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha akatupa maelekezo juu ya Mkakati wa Mradi wa Umeme wa *Grid* ya Taifa ambao tutapatiwa Mkoa wa Kigoma na zilitengwa shilingi bilioni 10 kama sijakosea. Sasa sijui ule mradi umefikia wapi kwa sababu hata maelezo ya Mheshimiwa Waziri hayajatuonyesha *progress* ya ule mradi. Je, Mradi ule unaendelea au tayari umesitishwa?

Sasa hivi maana kuna mradi mpya ambao utaanzia mto Malagarasi, sasa nataka kujua kama miradi hii itakwenda sambamba? Au ule wa bilioni 10 tayari tumeshasitishwa tunasubiri huu wa Malagarasi? Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri anaweza akanipa majibu hayo.

Pamoja kwamba tunasubiri hiyo miradi ninaiomba Serikali ifanye utaratibu wa kutupatia jenereta nyingine katika Mkoa wa Kigoma. Tunazo jenereta tatu tu na zote nichakavu, ni jambo la kawaida kwa Mkoa wa Kigoma hasa pale mjini kuwa na mgawo wa umeme wa siku hadi tano mnakaa bila umeme yaani hicho ni kitu cha kawaida, mkibahatika wakati mwingine ni siku tatu. Sasa hivi nimeanya mawasiliano wanapata umeme kwa siku nne za wiki.

Kwa hiyo, tunaomba sana zile jenereta zimechakaa tunaomba tupatiwe huduma ya umeme, Maendeleo katika Mkoa wa Kigoma yanachelewa na hii ni kutokana na kukosa Nishati ya umeme.

Kuna wajasiriamali wengi sana kama vijana ambao wana vioski vyao wanauza maji na soda wanashindwa kufanya biashara yao kikamilifu kwa sababu si rahisi mtu aende akanyewe maji ya moto au soda ya moto. Kuna akina Mama wengi ambao wamejiajiri katika kusaga mise ambayo inatokana na michikichi, hao akina Mama si wote wanaotoka mjini wengine wanatoka Bitare, Bubango, Kiganza na Maembe. Wanakuja pale mjini eneo la *SIDO* kuja kusaga mise yao, wanalala pale mashineni kwa sababu hawajui umeme utarudi wakati gani. Kuna wakati ambapo umeme unarudi usiku inabidi wasage usiku ili waweze kuuza mafuta yao na warudi vijijini na hao akina Mama wamekopa. Kwa hiyo, wanatakiwa walipe hiyo mikopo yao.

Kwa hiyo, tunaomba sana pamoja na kwamba Serikali ina mpango wa kutufikishia umeme wa *Grid* ya Taifa nadhani Mheshimiwa Waziri atatueleza zaidi wakati wa majibu yake tupate hata jenereta moja ya kuweza kutusaidia maana imekuwa ni tatizo sugu sana la umeme katika Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kwamba umeme unakatika hatupewi taarifa kwamba umeme utakatika. Kwa hiyo, mali za watu zinaharibika, friji za watu zinaungua na hakuna fidia yoyote ambayo inapatikana kwa wananchi. Kwa hiyo, naomba hilo kwa sababu hata kwenye hotuba ya Kamati wameonyesha kwamba hilo tatizo lipo na ni tatizo sugu. Kwa hiyo, naiomba Wizara itoe wito kwamba *TANESCO* nchi nzima wawe na utaratibu wa kuwaarifu kwamba umeme utakatika siku ngapi kwa wiki ili wananchi wajiandae, kwa sababu wasije wakanunua vitu vyao vikaja pia kuoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa suala la umeme wa Kigoma Mheshimiwa Waziri amesikia atatutafutia ufumbuzi.

Naomba niende kwenye suala la umeme vijijini. Kwa upande wangu naona hili ni suala zuri lakini kwa upande wa Kigoma naona bado itakuwa ni ndogo kwa sababu hata huo umeme wa kueleweka hatujui utapatikana lini. Kwa hiyo, hapo naona kidogo kuna tatizo lakini naamini kabisa umeme vijijini ukipatikana tutatatua matatizo mengi hasa likiwemo tatizo la vijana kukimbilia mijini kwa sababu ya ukosefu wa ajira. Naamini kabisa kwamba hata *SIDO* wanaweza waka – *expand* wakafika vijijini na watu wengi wakapata ajira.

Mheshimiwa Spika, mimi nina ushauri kidogo kwa Serikali, naomba ianzishe utaratibu wa umeme wa jua hasa kwenye Zananati za vijijini na katika shule ili waweze kuhifadhi baadhi ya vifaa vinavyotumia umeme. Kwa upande wa Zahanati wataweza kuhifadhi dawa zao, kwa upande wa shule wataweza kufanya practical hasa katika maabara zao. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ianzishe mradi wa umeme wa jua katika Zahanati zetu za Vijijini na katika Shule pia.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba Serikali ianzishe utaratibu wa kutoa elimu kwa wafugaji hasa wanaoishi vijijini waweze kutumia biogas kama Nishati mbadala ili waweze kutumia umeme katika majumba yao. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie utaratibu huo kwa sababu walisema kwamba tufanye utaratibu wa kutumia Nishati mbadala ili tujiletee maendeleo. Kwa hiyo, naomba sana suala hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba niende upande wa *TPDC.* Naiomba Serikali iiwezeshe *TPDC* ili iweze kukamilisha Malengo ya Utekelezaji wa Mpango wa Hifadhi ya Mafuta ya Taifa yaani *Strategic Oil Reserve* na vilevile iende sambamba na utafiti wa gesi hapa nchini.

Vilevile naomba ikiwezekana *TPDC* iwe ndiyo chombo kikuu cha uagizaji wa mafuta nchini kwa sababu ya kusaidia ku – *control* bei ya mafuta kama ilivyo sasa kwa sababu wafanyabiashara wanatoa mafuta katika *source* tofauti. Kwa hiyo, ni vigumu sana kuwapangia bei na hasa ikizingatiwa kwamba tupo katika soko huria. Kama *TPDC* wakiweza wao kuleta mafuta maana yake itapangwa bei ambayo itakuwa ni ya Serikali na wale wafanyabiashara wengine itabidi wafuate bei ya Serikali kwa sababu ni vigumu mwananchi kukwepa kununua mafuta kutokana na *TPDC* kununua yanaletwa na wafanyabiashara. Kwa hiyo, naomba sana hilo suala.

Lakini kuna tatizo kidogo na nina mifano, mfano sasa hivi katika Mkoa wa Kigoma Diesel ni shilingi 1,500/= kwa lita, mafuta ya taa ni shilingi 1,200/= kwa lita na *petrol* shilingi 1,640/= kwa lita. Sasa inategemea aidha bei itaendelea kupanda kulingana na hali ya usafirishaji ulivyo wa gharama.

Tukiangalia bidhaa nyingine kwa mfano *cemen*t sasa hivi ni shilingi 17,500/= sasa hapo kidogo inakuwa ni ngumu kwa mwananchi ambaye anataka kujiendeleza na vitu kama hivyo.

Kwa upande mwingine mimi nasikitishwa na *TIPA* kubinafsishwa kwa sababu ubinafsishaji mwingine unaweza ukasababisha malengo fulani ya Serikali kutotimia au kupata vikwazo. Kwa mfano, *TPDC* kweli itawezeshwa kuleta mafuta nchini itayahifadhi wapi na *TIPA* tayari ilibinafsishwa, matokeo yake ni kwamba itabidi *TPDC* wakodishe tena *TIPA* ili waweze kuhifadhi mafuta yao au labda wa – *terminate* mkataba kitu ambacho naona kama pia itakuwa kina ugumu.

Nina ushauri mwingine kwa Serikali kwa upande wa suala zima la ubinafsishaji wa mali zetu na suala zima la uwekezaji. Naona huu ubinafsishwaji uangaliwe vizuri ili

usiweze kukwamisha juhudi mbalimbali za Serikali kama mfano nilivyochukulia hiyo *TIPA* na *TPDC.*

Tukiangalia mikataba mingine mingi ambayo ilionekana kama itakuwa ni *solution* kwa matatizo ya umeme yaliyopo nchini imekuwa si *solution* lakini imekuwa ni *problem* kwa mfano tukiangalia *NET GROUP SOLUTION* kwangu mimi naona kama haikuwa *solution* bali ilikuwa ni *problem* kwa sababu haikusaidia sana nchi kama ilivyotegemewa. Tukiangalia *IPTL* nao ulikuwa ni mkataba ambao haukuwa na tija na ndiyo maana mpaka leo Serikali inalipa bili tu za umma ambazo ni *capacity charge.*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia tatizo lingine la haya mambo ya ubinafsishaji na mikataba tunaona hii Richmond lengo lake lilikuwa ku – *produce* umeme wakati wa matatizo lakini haikufanya hivyo kwa hiyo ina maana haikuwa na tija kwa kipindi hicho. Kwa hiyo, tujitahidi kuangalia na tuwe makini na tujifunze kila mara kutokana na matatizo ambayo tunayapata.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mambo yangu ya kuchangia ni machache. Aidha nina salaam kutoka kwa wananchi na itabidi nizifikishe kama Mjumbe. Nilipata simu mbalimbali wananchi wanasikitika kuona kwamba Wabunge wa CCM wachache waliopata nafasi ya kuchangia wanasikitikia upandaji wa bei ya mafuta. Wanasema kwamba wao walikuwa wapi kushauri Serikali mafuta yasipande? Wanasema kwamba walipitisha Bajeti hiyo kwa mbwembwe. Kwa hiyo, waache hivyo hivyo kama ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuishia hapo na huo ndiyo mchango wangu, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, sasa namwita Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, atafutiwa na Mheshimiwa Kaika Telele wakati huo huo Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji ajiandae.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwa hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa wiki iliyopita wakati nachangia kwenye Wizara ya Miundombinu nilipitiwa sikuwapongeza na kuwatia moyo wananchi wa Wilaya ya Chunya kwa mafanikio makubwa waliyoapata mwaka huu na mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya kwanza imekuwa ya kwanza kwa ufaulu wa watoto wa Darasa la Saba kwenda Darasa la Tisa Mkoani Mbeya. Napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Walimu, Wazazi na Wanafunzi kwa *achievement* hii kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pia Wilaya ya Chunya tumefanikiwa kwa kuitia wito wa Waziri Mkuu tumefanikiwa kujenga sekondari 19 na vijana wetu zaidi ya 80%

wameanza shule. Napenda kuwapongeza sana Wananchi wa Wilaya ya Chunya hasahasa wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Wilaya, nawapongeza sana na naomba wasilegeze uzi juhudi hizi ziendelee na tuendelee kujenga madarasa ya watoto ambao wataingia *form one* mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa hotuba yao nzuri.

Katika ukurasa wa 26 anasema: "Hakika Malengo ya MKUKUTA, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 na Mipango na mikakati mbalimbali ya kijamii na kiuchumi nchini hayawezi kufikiwa bila kuongeza juhudi za kupeleka huduma bora za Nishati vijijini."

Mheshimiwa Spika, Wilayani Chunya kuna miradi ya kupeleka umeme vijijini ambayo imedumu kwa muda mrefu sasa na haijakamilika. Kuna mradi wa kutoa umeme Makongorosi kupitia Upendo kwenda Mamba mpaka katika kijiji cha Lupa Tingatinga. Mradi huu umeanza mwaka 2000 na bado haujakamilika, nguzo zimesimikwa mpaka Upendo nusu ya njia bado haujakamilika. Wakati Wizara inaanzisha miradi sehemu nyingine ya kupeleka vijijini na kuikamilisha, kuna tatizo gani? Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kuna tatizo gani la kumaliza mradi huu wa kutoa umeme kutoka Makongosi kwenda Lupa Tingatinga.

Mheshimiwa Spika, pale Lupa Tingatinga na Kata zinazoizunguka za Mtanila, Matwiga, Mamba wanalima sana tumbaku. Kwa hiyo, umeme ukienda pale utasaidia sana kuhifadhi mazingira kwani wakulima watakaushia tumbaku yao umeme badala ya kukata miti. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kwa nini mradi huu hauishi na sasa hivi una miaka zaidi ya mitano.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna mradi ule wa kutoa umeme njia ya panda ya Kiwanja kwenda Kijiji cha Mlima Njiwa, nao vilevile nguzo zimelazwa, wale wa Lupa Tingatinga nguzo zimesimikwa huu wa kwenda Mlima Njiwa nguzo zimelazwa nusu njia zinaweza zikaungua kama msitu ukiungua. Lakini kwa nini mradi huu hauishi? Na hapa Serikali inasema hatuwezi kuendelea kama umeme haupelekwi vijijini? Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kwa nini miradi hii ya umeme haikamiliki.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Sekta ya Madini. Katika ukurasa wa 38 Waziri anasema:

"Ili kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Madini na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa, Serikali katika mwaka wa 2007/2008 itakamilika mchakato wa kudurusu Sera ya Madini ya mwaka 1997 na kuandaa rasimu ya Sera mpya ya Madini. Utekelezaji wa Sera hiyo mpya na matokeo ya majadiliano kati ya Serikali na wawekezaji ambayo yanaendelea yatalazimu kurekebisha baadhi ya vipengele vya Sheria ya Madini ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya 75% ya Wilaya imeshikwa na leseni za kutafiti Madini za wachimbaji wakubwa wakubwa, 25% tu ndiyo imeachiwa kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya mwaka 1998 ya Madini Namba 5 inasema:

"Mchimbaji akipewa leseni ya kutafiti madini anapewa miaka mitatu, ikiisha miaka mitatu hajapata kitu anapewa *first renewal* ambayo ni miaka miwili na ikiisha tena hii miaka miwili hajapata kitu anapewa *second renewal* ya miaka miwili, jumla miaka saba basi ."

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya hawa wachimbaji wakubwawakubwa ambao wameshika 75% ya Wilaya ya Chunya ni wajanja sana. Wao akishapewa leseni ya kutafiti ikiisha miaka mitatu akipewa *first renewal* Sheria ya mwaka 1998 inasema aachie 50% ya eneo lake arudishe kwa Kamishna wa Madini ili Kamishna wa Madini aidha atangaze *tender* au awape wachimbaji wadogowadogo.

Lakini hawa wachimbaji wakubwa kwa ujanja wao badala ya kuachia hili eneo 50% analiomba eneo hilo kwa jina la kampuni nyingine. Kwa hiyo, anaendelea kulihodhi wakati wananchi hawa wachimbaji wadogowadogo wanabaki wanahangaika.

Mheshimiwa Spika, naomba inapodurusiwa Sera ya Madini ya mwaka 1997 na inapoangaliwa upya Sheria ya Madini ya mwaka 1998 naomba suala hilo liangaliwe sana kwani wachimbaji wadogowadogo wanahangaika wakati ni nia ya Serikali kuwawezesha wachimbaji wadogowadogo wakati hawa wachimbaji wakubwa wanahodhi maeneo bila kuyafanyia utafiti.

Mheshimiwa Spika, kama ikirekebishwa hali hii na wachimbaji wadogo wakapewa maeneo faida ni nyingi sana. kwanza wachimbaji wadogo watapewa maeneo ya kumilikia na kufanya utafiti, pili hawa wachimbaji wakubwa watafanya haraka kutafuta fedha za kufanyia utafiti kwa kuogopa kunyang'wa maeneo na wakifanya haraka ina maana migodi itafunguliwa na Serikali itapata mapato na Halmashauri itapata mapato na vijiji vinavyozunguka maeneo haya ya midogo vitapata mapato.

Naomba Mheshimiwa Waziri awe mwangalifu sana Sheria inapodurusu Sera ya Madini na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 anapoidurusu abadilishe ili wachimbaji wadogo wafaidike.

Serikali kwa nia njema tu imetoa mtambo wa kusaga mawe ambao umewekwa kwenye kijiji cha Pungutas karibu na Matundas. Vijiji vya kwetu vina hiyo hiyo *SS* Makongoros, Matundas. Huu mtambo ni mkubwa sana umeigharimu Serikali karibu dola 500,000/= na Serikali iliukodisha mtambo huu kwa mwananchi mmoja wa Chunya ili yeye ndiye aweze kutoa huduma hiyo kwa wananchi wenzake.

Mtambo huo nadhani haukukamilika kwa sababu mtambo haujafanya kazi una miaka minne sasa haujafanya kazi na mtambo haukukamilika kwa sababu Wilaya ya Chunya ni eneo kubwa sana karibu 46% ya Mkoa wa Mbeya ni Wilaya ya Chunya kwa hiyo, wachimbaji wako *scattered* kwenye sehemu ambazo ziko mbalimbali mno. Kwa hiyo, mtambo huu ungekuwa unafanya kazi vizuri kama ungepewa vitendea kazi kama gari moja au mawili ya kuwasaidia wachimbaji wadogowadogo wachukue michanga yao na mawe yao kutoka maeneo wanakochimba ili kuleta kuja kusaga kwenye mtambo ambao hawana.

Pia wangeongezewa au wakodishiwe vifaa kama pampu za maji, *compressor* zikawa nyingi ili waweze kuchimba. Bayati mbaya mtambo huo haujafanya kazi na ninavyoona mimi kuna malumbano kati ya huyu aliyekodishiwa analumbana sana na Serikali na Wizara lakini malumbano hayo hayaleti faida kwa wachimbaji.

Kwa hiyo, nia ya Serikali ambayo ilitaka kuwasaidia wachimbaji wadogowadogo haijatimia, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kwamba huu mtambo hatima yake ni nini.

Je, Serikali ni haki ambayo ni nzuri sana ya kuwasadia wachimbaji wadogo wadogo inaendelezwaje, au tutaendelea kulumbana na huyu mwananchi ambaye naye ana nia nzuri ya kuwasaidia wananchi wenzake. Lakini anachokosa ni vitendea kazi kama vile nilivyosema magari, *compressor* na *pump* za maji. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kunisaidia na kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Chunya kuwaambia kwamba mtambo huu hatma yake ni nini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi naomba kuunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa na mimi napenda kuwapongeza wananchi wa Chunya kwa mafanikio hayo.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea ni zamu ya Mheshimiwa Kaika S.Telele Mbunge Ngorongoro atafuatiwa na Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji wakati huohuo Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu ajiandae.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, na mimi nimpongeze Mheshimiwa Waziri Nazir Mustapha Karamagi na Naibu Wake Ndugu yangu William M. Ngeleja, Katibu Mkuu wa Wizara na Watalaamu mbalimbali wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuchangia maeneo mawili tu, Wilaya ya Ngorongoro kwanza Makao yake Makuu ni Loliondo na siyo Ngorongoro kama watu wengi wanavyofikiria, Loliondo kule ni kilomita kama 400 kutoka Arusha Mjini ambapo

ni Makao Makuu ya Mkoa. Wilaya hii ina kilomita za Mraba zaidi ya 14,000, Wilaya hii imeanzishwa mwaka 1979 kutoka Wilaya ya Monduli ambayo Wilaya ya Monduli nayo imezaa hiyo Ngorongoro, Simanjiro, Kiteto na Longido, hizi zote ni Wilaya za Wafugaji. Wilaya hii kwa kweli haina miundombinu yaani haina Barabara, umeme, mawasiliano, ni hivi karibuni tu kampuni za *Celtel* na *Vodacom* na ninatoa wito pia kwa *Tigo* wapeleke mawasiliano katika Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Wilaya za Mikoa ya Kusini kwa usahihi kabisa wamekuwa wakipiga kelele kwamba Mikoa yao iko nyuma sana kimaendeleo. Ni kweli kwa sababu hata mimi mimekaa Songea na hata Tunduru kwa kweli hoja yao ni kweli kabisa.

Lakini Wilaya hizi za wafugaji kama nilivyoeleza ni Wilaya ambazo zinaelezwa kwamba ziko katika Mikoa ya Kaskazini ambayo ina Maendeleo makubwa, Mikoa ya Kaskazini ni pamoja na Kilimanjaro, Arusha na Tanga.

Lakini kwa kweli ukiangalia kwa makini sana Wilaya hizi za Wafugaji si lolote si chochote kwa upande wa Maendeleo na kwa maana hiyo Wabunge wanaotoka Mikoa ya Kusini walikuwa wanaomba upendeleo maalum, kama hilo litakubalika basi vivyo hivyo kwa Wilaya za wafugaji zilizoko Kaskazini kwa sababu inakuwa kama wewe unatandika kitanda halafu unaweza *bed cover,* sasa hizi Wilaya za wafugaji kwa kweli unawafunika tu hawana hili wala lile na sisi tunaomba upendeleo maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngorongoro kwa mujibu wa taratibu za *TANESCO* tumeelezwa kwamba tutapata umeme mwaka 2015. Kwa kweli hii kwanza haiendani na kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Nne ya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya.

Mimi nashindwa kuelewa ni kwa nini twende mpaka mwaka wa 2015 kwa sababu Wilaya ya Ngorongoro ina maporomoko ya maji kule kwenye Mto Pinyinyi, Angarisero, Ng'arwa na hata Kisangiro. Ni maeneo ambayo yangefanyiwa utafiti wa kutosha tungeweza kupata umeme kwa haraka hata bila kwenda huko 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuuliza katika Bunge hili kwamba kwa nini Wilaya ya Ngorongoro ambayo ni kilomita chache tu kutoka Jamhuri ya Kenya na hasa Wilaya ya Narok na Wilaya ya Narok ina umeme wa kutosha sana. Hivi haiwezekani Serikali ikafanya utafiti tukapata umeme kutoka kule kwa sababu ni karibu? Lakini nilijibiwa kipindi kile kwamba Serikali kwa sasa haina mpango. Lakini bado mimi nasisitiza kwamba umeme ukitolewa kutoka kule kwanza gharama ni nafuu halafu ni karibu.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nia ya Serikali ipo ya dhati kabisa basi kutoka vyanzo ambavyo nimevieleza na kutoka hiyo nchi jirani ya Kenya. Kwa sababu, tuna matatizo kule tunafanya vikao mara nyingi vya ujirani mwema na vikao hivi vina *AlterNet* ama letu tufanye Loliondo Makao Makuu ya Ngorongoro na kesho tunafanya Wilaya ya Narok.

Lakini inapofika zamu yetu wenzetu wanasita, wanatuambia ama tufanye Arusha Mjini ama turudie Wilaya ya Narok na yote haya ni kwa sababu ya tatizo la umeme, sasa katika kuangalia pia na kuweka hadhi na heshima ya nchi maeneo kama yale Wilaya za pembezoni na Mikoa ya pembezoni ingeangalia sana kwa jicho la huruma na Wizara inayohusika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia alipokuja Ngorongoro tarehe 20/3/2007 kwa kweli aliwaahidi wananchi wa Ngorongoro kwamba mtapatiwa umeme na ni umeme wa *Grid* au wa *Hydro.*

Lakini akasema kwa sababu mipango ya Serikali inakwenda polepole na kulingana na fedha za Serikali nitawatuma watu wa *TANESCO* walete jenereta kwa kuanzia na mimi naunga mkono kauli ya Rais. Naomba basi hilo angalau hilo kwa kuanzia tupatiwe umeme wa jenereta lakini siyo sasa tunaletewa umeme wa jenereta halafu mkatusahau jumla kwa sababu ku – *run* jenereta nayo ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, na hili nimejaribu kufuatilia sana kwa Mheshimiwa Waziri akanipa matumaini na nina hakika kwa kweli hilo tutaendelea kufuatilia na ninadhani kwa kuanzia tunaweza kupata umeme unaotokana na jenereta.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia alipotembelea Wilaya ya Longido tarehe 19/3/2007 aliahidi wananchi wa Longido kwamba watapata umeme kutokea Jamhuri Kenya katika Wilaya ya Longido, na Ndugu yangu Lekule Laizer akanipigia simu akaniambia sasa wewe Ndugu yangu chukua umeme kutoka kwangu. Sasa naomba kama umeme huu utaanzia kule kwa Mheshimiwa Lekule Laizer, basi na mimi nipate lakini inaweza ikaanza kwangu na yeye vilevile akachukua kutoka kwangu.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie umeme Makao Makuu ya Shirika la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Miaka mitatu au minne iliyopita wakati Makao Makuu ya Wilaya ya Karatu, Karatu kwenyewe walipata umeme wa *grid* kutokana na fedha za *World Bank,* ilikuwa ni mpango wa Serikali kupeleka pia umeme Makao Makuu ya Shirika la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Lakini kinachosikitisha ni kwamba umeme ule umefikishwa katika lango kuu la kuingilia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, tumebakiza kilomitakama 32 au 33 ifike Makao Makuu ya Shirika na sisi tulikuwa tunategemea kwamba umeme ule ungefika Makao Makuu ya Shirika basi maeneo kama Mokilar, Endulen, Orpiro, Kakesyo, Inokonoka, Iyobi na Olbalbal ni vituo muhimu sana hivi kupata umeme.

Lakini kwa sababu umeme huu sasa umeishia kwenye lango kuu la Ngorongoro na kwa kweli nia ya Serikali ilikuwa ni kupeleka umeme hadi Makao Makuu, lilijitokeza ni suala la Hifadhi ya Mazingira kwamba Serikali ilikuwa inapeleka umeme wa *overhead cables* kwa kuweka nguzo na kupeleka umeme kule kwenye Makao Makuu ya Shirika. Lakini ikaonekana sasa kwa sababu ni eneo la Hifadhi, kuna wanyama na kadhalika na

inawezekana wakaja wakajikuna kwenye nguzo zile wakaziangusha ikaleta matatizo, ilikuwa ni hoja ya msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini tulitegemea pia Serikali ingesaidia Shirika hilo kuweka *underground cable* ili kupeleka umeme hadi makao makuu ya Shirika la Ngorongoro. Kwa sababu Shirika lile kwa kweli ni walipaji wazuri sana wa kodi ya Serikali, wanalipa kati ya shilingi milioni mia nane au bilioni moja kwa mwaka. Sasa kutokana na umeme mambo yao mengi hayaendi kwa sababu ya ukosefu wa umeme. Siyo tu Makao Makuu ya Shirika, lakini kuna hoteli zilizopo katika eneo la Ngorongoro, kuna *camp sites* kule. Hivi karibuni wametangaza maeneo ya kuweka *camp sites*, lakini tatizo limekuwa ni umeme. Naiomba Serikali kwa kuwa Shirika hilo ni walipaji wazuri wa kodi basi na wenyewe watazamwe kwa jicho la huruma kupelekewa umeme ili waweze kutekeleza mambo yao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tena nirudie kwamba tunaomba umeme japokuwa wa jenereta kwa kuanzia kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliagiza watu wa *TANESCO* wapeleke umeme haraka; na mimi nitaendelea kufuatilia kwa Wizara inayohusika na ndugu yangu Mheshimiwa Nazir Karamagi au ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja watanisaidia ili tuweze kupata umeme huo kwa ajili ya maeneo yetu hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, leo nataka nichangie kuhusu hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa hotuba yake nzuri, Waziri ametueleza hapa, lakini chochote kizuri lazima kiwe na kasoro. Nataka niongelee mambo machache ambayo nataka niikosoe Wizara ili tuweze kupata maendeleo nchini kwetu na gurudumu la maendeleo lipate kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, mimi nataka niongelee kuhusu *power station* ya Somanga-Fungu. Naishukuru sana Serikali kuwajali wananchi wa Kilwa, Rufiji na Mkuranga kwa kutupatia umeme unaotokana na gesi. Naishukuru sana Serikali na naishukuru sana Wizara, lakini bado kuna upungufu ile *power station* au kituo cha kuzalisha umeme cha Somanga-Fungu bado kina matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri alitueleza kwamba Kituo kile kimefanikiwa kwa asilimia 90, si kweli kwamba mafanikio yaliyopatikana pale ni asilimia 90. Tunasuasua, asilimia zilizopatikana ni 80 na bado mradi uko nyuma kwa miezi 10 sasa. Tuna matatizo mengi ya Mkandarasi kutokuwa na *speed* ya kufanya kazi, tuna matatizo ya watendaji wetu kumsukuma Mkandarasi ili aweze kufanya kazi yake vizuri na kazi ikamalizika kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaomba kura mwaka 2005 tulisema sana kwamba jamani mna Hazina ya gesi, lakini mtafanikiwa kupata umeme Kilwa, Rufiji na Mkuranga tuliwaahidi wananchi wetu. Mradi unasuasua, unachelewa sijui Mkandarasi anachukuliwa hatua gani au tozo fulani anatozwa kwa sababu ya ucheleweshaji wa mikataba ambayo ipo.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo mengine ya wananchi wetu ambako nguzo zinapita hawajalipwa kutokana na mimea ile, kuna minazi, kuna miembe, kuna mikorosho, wananchi wengi bado hawajalipwa fidia na cha kushangaza zaidi Mheshimiwa Waziri alisema hana kifungu cha kuwalipa bado sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abdul Marombwa Mbunge wa Kibiti alililisema hilo, na mimi ninalisema hilo wananchi wangu hawajalipwa fidia hizo, tunataka Mheshimiwa Waziri atutamkie hapa lini watalipwa fidia zao wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi ulitoa ahadi kwenye vijiji vile zinapopita nguzo za umeme kwamba watachimbiwa visima vya maji, mradi ulitenga shilingi milioni 500, visima vingine vilivyochimbwa havitoi maji, vijiji vya matandu, Njenga, Mitenja, Njianne, Tingi na kadhalika havijapata visima na mahali pengine maji hayatoki. Sijui Wizara imemchukulia hatua gani Mkarandasi huyo aliyepewa *tender* hiyo ya kuchimba visima wakati maji hakuna.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inapotoa ahadi na sisi vilevile wawakilishi wa wananchi tunatoa ahadi kuwaeleza wananchi, "jamani mtapata visima". Tunakwenda kule hakuna visima, Mbunge unaonekana mwongo, saa nyingine unaonyeshwa tu lile shimo halina maji. Kwa hiyo, nataka Wizara itwambie hapa wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake hatua gani imemchukulia huyo Mkandarasi ambaye alipewa *tender* ya kuchimba visima kando kando ya nguzo zilipopita mwa vile vijiji ambavyo vitafaidika.

Mheshimiwa Spika, nataka niombe Wizara kupitia *TANESCO* ituonee huruma sisi watu wa Kilwa, Rufiji na Mkuranga kutupunguza punguzo maalumu katika kuunganisha umeme. Sisi wenye Hazina kubwa ya gesi ni wakombozi wa Dar es Salaam, tulikuwa tunaiomba Wizara kuwe na punguzo maalumu la *service line*, tuwe na punguzo maalumu kupata mita, bei iliyopo sasa hivi ni laki mbili na kitu kuunganisha umeme. Tunaweza kuwa na umeme lakini hatuwezi kuwa na fedha za kuunganisha umeme majumbani. Wananchi watakuwa wanashuhudia nguzo za umeme tu kuliko kuweka umeme majumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiomba Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kutuombea *TANESCO* tulipe hizo fedha kwa awamu na tunaomba punguzo maalumu kwa watu wa Kilwa. Watuonee huruma tuna gesi, tumeliokoa Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya ombi hilo, nataka niende sasa moja kwa moja upande wa *Gypsum*. Kilwa ina hazina kubwa sana ya *Gypsum* ambapo madini hayo yanatengeneza sementi, ili sementi igande lazima iwekwe *gypsum* ili iweze kuganda.

Rasilimali hii ipo katika Kata ya Mandawa, Kilanjelaje na Mheshimiwa Waziri alinihakikishia kweli *gypsum* yetu ina ubora wa asilimia 90 na kuendelea. Nilikutana na Mheshimiwa Waziri akanieleza hilo, kwamba Mheshimiwa Mbunge ubora wa *gypsum* yenu ni safi sana. Lakini tunavyoongea hapa migodi ya Kilwa imesimama Mandawa, Hotelitatu na sehemu nyingine, Bonde la Makanganga, migodi imesimama hakuna mtu anayechimba *gypsum*. Ajira kwa vijana wetu na kwa wananchi hakuna, vikoroboi haviwashwi, wananchi hawana fedha.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mmoja. Mimi nilikwenda katika kijiji kimoja kinaitwa Hotelitatu. Baada ya kwenda pale nikaona migodi yote imesimama, hakuna kazi inayoendelea, nikamwita kijana mmoja bwana hebu kaniletee *sample* ya *gypsum*. Akaniambia Mheshimiwa Mbunge usiongee, mimi nataka shilingi 2,000 ngoja sasa hivi usiku nikakuchukulie ile *sample,* wananchi wetu wana njaa. Migodi imesimama kwa mtu mmoja au kwa kiwanda kimoja kususia kununua *gypsum* yetu.

Mheshimiwa Spika, tunapoteza fedha nyingi sana za Serikali za kigeni. Juzi nilimwona Gavana kwenye televisheni alisema ili Serikali iendelee tunahitaji fedha za kigeni. Hapo tunapoteza fedha za kigeni kwa wingi sana. Tumekwishapoteza takriban dola za Kimarekani milioni 7 kwa kuagiza *gypsum* toka Iran na Oman yenye ubora wa asilimia 72. Tunakwenda wapi? Tunawaambia nini wananchi wetu kwa upande wa ajira. Hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema habari za *gypsum* nataka Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake atoe tamko ni hatua gani anachukua, tumwite huyo mwekezaji tukae naye, tuongee naye ni kwa nini anaisusia *gypsum* yetu ya Kilwa. Tuna uwezo, Mheshimiwa Waziri aliniambia, nyie hamna uwezo, barabara zenu mbovu hamwezi ku-*supply*, hebu watupe *order* ya tani 5,000 tu, waone.

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho, nataka niongelee kuhusu Songosongo. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi yangu tulikwenda Songosongo. Wananchi wa Songosongo walisema wapo hoi mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wana-manda kile kisiwa ni kidogo, hakuna kitu kinachoota pale, hakuna biashara inayoendelea pale, mradi hautoi ajira kwa wananchi wangu, wananchi wapo hoi kweli kweli. Tuliwaandikia barua tukasema jamani, tunaomba *development levy* au tunataka tusaidiwe sisi Kilwa.

Mheshimiwa Spika, biashara kubwa ya wananchi wa Songo Songo wanayoifanya ni kuvua samaki. Samaki wamekuwa wajanja wanapatikana mbali sasa hivi. Vinahitajika vitu vya moto kuwafuata samaki huko. Vijana wetu wanakaa chini ya minazi hawana kazi, mradi hautoi ajira kwa wananchi wetu, mradi hauna boti pale mwananchi akiumwa kupelekwa kwenye hospitali kubwa ya Kilwa Kivinje.

Mheshimiwa Spika, maji pale ni tabu Songosongo, mradi unatoa maji kidogo ambapo kuna mashine inabadilika maji ya chumvi kuyafanya maji baridi. Maji yale kidogo wanayatumia wenyewe watu wa mradi, yakibakia ndiyo wanapewa wananchi

wangu. Tuna matatizo, tufikirie. Mheshimiwa Waziri, aniambie hapa tukutane na *Songas,* tukutane na Kampuni nyingine yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. Kwa sababu ninajua wanaweza na wameonyesha kwamba wanaweza na huko mbele nitaeleza kwa nini ninasema kwamba wanaweza.

Mheshimiwa Spika, kama mwakilishi wa Jimbo la Bukene, wananchi wa Bukene wameniomba niwafikishie malalamiko yao. Malalamiko haya ni kuhusu ahadi ya zamani kutoka kwa Rais Mstaafu kuhusu umeme wa Bukene na Ndala.

Mheshimiwa Spika, vilevile Rais wa Awamu ya Nne, alipokuwa anapita Bukene alikuta watu wengi sana akafurahi, mpaka akashangaa kwa nini asipate jukwaa hapo.

Maana aliona kabisa watu walivyokuja wengi kumpokea ilionyesha kwamba ilikuwa sahihi kama angekuwa na mkutano pale, lakini mkutano huo ulikuwa umepangwa kufanyika Nzega.

Lakini katika kuzungumza katika kituo hicho cha Bukene Naitombo aliahidi kwamba ahadi zote za Awamu ya Tatu, yeye atazichukua. Maana yake atatekeleza kupeleka umeme Bukene.

Mheshimiwa Spika, sasa katika Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya mambo yamekwenda vizuri mpaka mwaka jana. Katika bajeti ya mwaka jana ambayo tumeimaliza juzi kama wiki mbili zilizopita fedha zilikuwa zimetengwa na tukazipitisha.

Mheshimiwa Spika, toka hapo nilifuatilia mimi mwenyewe tangu kwa Mheshimiwa Waziri ambaye alikuwa wa Wizara hii, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha mpaka akaniambia kama mtani wangu, sasa wewe uitwe mwana-Msabaha, na mimi nikasema “Kalame”, Kinyamwezi maana yake *bee.*

Mheshimiwa Spika, nilivyokubali nikajua kwa sababu mila na desturi ya Wanyamwezi au Wasukuma kuna majina ya kwenye Ngoma. Kwa hiyo, nikajua kwamba jina hili la mwana-Msabaha maana yake ni la ngoma ya kwenye kutafuta umeme.

Mheshimiwa Spika, ngoma hiyo mwenyewe ngoma ambaye kwetu tunasema "mlingi" yule kiongozi wa ngoma ile ni Wizara ya Nishati na Madini. Kwa hiyo, nikakubali na nilicheza vizuri sana katika ngoma hiyo na nikafuatilia kwenye Wizara ya Nishati na Madini, *TANESCO* Vijijini, *steps* zote zimepita mpaka ikabaki fedha kutoka Wizarani kumpa aliyepata *tender* na kazi iishie tuhitimishe, ndipo tulipofika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, ikatokea la kutokea ambalo nilikwenda nikawaeleza wananchi wakakubali kwamba kwa maafa ni lazima tuangalie fedha zile ziende kwenye maafa, lakini ahadi hiyo hiyo nilikwenda kuipata tena kwa Waziri wa Nishati na Madini hapo juzi mwezi wa Aprili, 2007 kabla sijaenda nyumbani. Akaniambia kwamba ahadi zote na bajeti yote iliyopitishwa kwenye bajeti ya mwaka 2006/2007 itaendelea kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa nimeona shilingi milioni 50 zimetengwa, lakini bajeti yenyewe yote ya umeme wa kutoka Bukene kwenda Ndala vilevile zilikuwa milioni mia tisa na kitu. Sasa kinachonishangaza shilingi milioni 50 katika bajeti ya milioni 90, kulikoni?

Mheshimiwa Spika, kabla sijaja Bungeni nilikutana na vijana wanaofanya kazi ya useremala, wanaofanya kazi ya *welding*, wakaniamba mama sisi tatizo letu ni umeme. Kila kona naambiwa umeme, hivyo, umeme umekuwa kero. Umeme unatufanya sisi sote tuonekane waongo.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo na kwa sababu imebaki kuhitimisha na Mheshimiwa Waziri aliniahidi kwamba atahitimisha kwenye bajeti hii ya mwaka 2007/2008, naamini kabisa alichosema ni kweli na hizo shilingi milioni 50 maana yake ni kianzio, lakini mimi naogopa kurudi na nikawaambie nini wananchi wa Bukene; niwaeleze nini, nitawabebea mbeleko gani mimi?

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri anatakapokuwa anahitimisha hoja yake aeleze kwa nini ametupa shilingi milioni 50.

Shilingi milioni 50 maana yake ni hitimisho la umeme wa kwenda Bukene ili kuwasaidia vijana wale ambao wanahangaika kuleta *furniture* zao Nzega kwa ajili ya kukereza na vilevile vijana wanaotengeneza ajira zao kwa ajili ya kufanya *welding*. Pia akinamama ambao wapo tayari kufanya vitu kama vioski ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua umeme ni maendeleo na umeme ni uchumi; na Bukene ni mji mzuri na mji unaovutia kibiashara. Kwa hiyo, Bukene wakipata umeme wataweza kujikwamua kwa vitu vingi. Watatengeneza mashine zao wenyewe, watakomboa kwa kutumia umeme, na watatoa mchanga kwenye mchele wao na utakuwa *first class* kwa ajili ya kupeleka ndani na nje ya nchi. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind* up atueleze. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, mimi naogopa kwenda kusema tena hadithi ya umeme. Kwa hiyo, kama nilivyosema kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba tuongozane naye Waziri au Naibu Waziri twende tukawaeleze wananchi wa Bukene hitimisho la umeme huo liko namna gani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutimiza wajibu wa Jimbo, kwa sababu nimeingia hapa kwa ajili ya sauti hiyo, naomba niendelee sasa kushauri kwa mambo mengine ambapo nimesema Serikali ya Awamu Nne inafanya kazi vizuri.

Kulikuwa na maonyesho pale nje. Maonyesho yale ukiyatazama vizuri inaonyesha kwamba tukiyatekeleza hayo maana yake tunafanya maisha bora kwa kila mtanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie la kwanza kabisa kuhusu gesi asilia. Nimeona gari pale inayotumia gesi asilia. Nikawauliza wale vijana, wakanieleza kwamba wana gesi nyingi tu na tayari wamekwishaanza kuweka Vituo kwa Dar es Salaam. Kama kweli tuna nia nzuri kwa Watanzania, tunajua tukitumia mafuta kama petroli au dizeli tunawaumiza wananchi kwa sababu usafiri gharama zake zimepanda na vitu vyote bei zake zimepanda.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ni kuomba *political will* kwenye Serikali ya Awamu ya Nne na kama tukipata *political will* kwenye Serikali ya Awamu ya Nne, naamini kabisa wakisema tu, kwamba magari yote ya Serikali yabadilishwe yawe magari yanayotumia gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubadilisha gari moja niliambiwa pale ni shilingi milioni moja. Naamini shilingi milioni moja kwa kila gari siyo ghali, hata mimi kama hiyo gesi ingekuwa imeshafika Bukene ningeweza kubadilisha gari langu. Lakini ni kwa sababu hiyo gesi haijafika huko.

Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye vilevile kama ilivyofanya kwenye kubadilisha namba za magari, basi magari yote ya Serikali yabadilishwe na mabasi yote ya abiria yanayoweza kufika katika vituo walipofikisha hiyo gesi asilia yabadilishwe ili kushusha gharama za usafiri.

Waliniambia gari la *Shangingi* kutoka Dar es Salaam mpaka kufika Dodoma gharama yake ni shilingi 18,000 kwa kutumia gesi asilia. Sasa tunatumia petroli ya zaidi ya shilingi 100,000, wakati tunaweza kutumia gesi asilia kwa shilingi 18,000.

Hapo hapo tutashusha vilevile biashara ya petroli na dizeli kwa sisi ambao bado tunatakiwa kutumia. Lakini kwa ujumla yale ya Dar es Salaam, daladala, mabasi ya abiria yote yatumie gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale nje nimeona vilevile kuna vitu vya *solar lights*. Mimi ninajua kwangu kule umeme unaouzungumziwa ni wa kutoka Nzega mpaka Bukene moja kwa moja tu.

Huko ndani hakuna kitu mpaka hapo baadaye tulivyokubaliana. Kwa hiyo, ningeomba *solar lights* zisaidie katika mambo mengine hasa katika Vituo vya Afya, zahanati na *secondary schools* tunazojenga sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, tatizo linakuja ukitaka kuweka *solar lights* kwenye nyumba, balbu tano na televisheni unatumia shilingi milioni moja. Kwa mtu wa kawaida ni ghali.

Kwa hiyo, naiomba Serikali ipunguze kodi kama wanavyofanya watu wa Kenya ili tuweze kupata vitu vya *solar lights* katika Taasisi za lazima kama vile Vituo vya Afya, *Secondary Schools*, Vituo vya Polisi na kadhalika na watu waweze ku-*afford* kuweka taa katika nyumba zao. Hayo ni maisha bora kwa kila mtanzania.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwenye maonyesho nimeona Moto Poa. Moto Poa wale wanatengeneza kutokana na miwa. Lakini walisema wanapata inakwenda juu zaidi kwa sababu ya kodi.

Kwa hiyo, kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa kawaida na kwa ajili ya kusaidia mazingira mimi naiomba Serikali ipunguze kodi pale ili watu waweze kutumia Moto Poa tuweze kuondoka wote katika uchumi wa nchi hii na mwisho wa siku kila mtu awe na maisha bora katika nchi hii na sera yetu itakuwa imeshatekelezeka kiurahisi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda bado upo, naomba nizungumzie kidogo juu ya madini. Kwenye Jimbo langu kuna machimbo ya madini katika Kata ya Igusule sehemu inaitwa Mwanziro. Pale walikuwepo wachimbaji wadogo wadogo, kwa miaka mingi wapo pale wanachimba, wanajipatia riziki zao.

Bahati mbaya au nzuri tena juzi tuseme kwamba wamepewa *Sub-Sahara* wanachimba pale. Wale wananchi wachimbaji wadogo wadogo ambao walikuwa wamejitengenezea kazi zao *(job creation)* wameondolewa na bado hawajalipwa. Kwa hiyo, naomba waende katika utaratibu ambao unatakiwa ili waweze kupata chochote na wenyewe wajikwamue kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kama ingekuwa bado *stage* za mwanzo basi naomba washirikishwe na wenyewe wawekewe kipande kama vile walivyofanya kwenye *Tanzanite* kule Mererani, wamewatengea wachimbaji wadogo wadogo sehemu na huyo mtaalamu mkubwa ametengewa sehemu ili waweze kupata na wenyewe riziki zao.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Kabla sijasahau nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja. Nianze pia kwa kuitakia Wizara yetu mafanikio makubwa katika kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Bajeti ambayo leo tutaizungumza na hatimaye Bunge litatoa idhini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi nyingine ya pekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu alishiriki kuja kufungua *investment forum* Mkoa wa Ruvuma. Kwa kweli alipokuja kufungua *forum* ile ya uwekezaji alikutana na wachimbaji wadogo wadogo na alikuwa ni shahidi mkubwa baada ya kufanya ziara za Kiserikali huko nje ya nchi ya Tanzania na hususan Taiwan alikuta madini yakitoka Mkoa wa Ruvuma Wilaya zote tano yakiuzwa kule lakini na wawekezaji ambao si Wana-Ruvuma na wala si Watanzania wenyewe. Nafikiri nitumie nafasi hii kumwomba Waziri Mkuu, kwa sababu maagizo yale yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwepo, namwomba Mheshimiwa Waziri sasa ayafanyie kazi ili kweli tuweze kuwakomboa wachimbaji wadogo wadogo wa Wilaya zote tano za Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, niingie sasa kuwazungumzia wananchi wa jimbo la Peramiho, wapiga kura wangu ambao wameniweka hapa Bungeni. Leo nizungumzie kwa kufuata Jiografia ya jimbo la Peramiho. Tuna bahati nzuri sana mimi na Mheshimiwa Naibu Spika tunapakana. Anapomaliza Naibu Spika jimbo lake na mimi la kwangu ndipo linapoanzia kwenye Kata yangu ya kwanza ambayo inaitwa Kata ya Wino, hapo ndio tunapakana na Naibu Spika. Nafurahi sana Kata ile wakazi wake ni Wabena kama walivyo Wabena wa jimbo la Mheshimiwa Naibu Spika. Lakini ninachotaka kusema Serikali ina mpango na nimesoma kwenye bajeti wa kuunganisha umeme wa gridi kutoka Makambako kuja Njombe na kutoka Njombe, kwa maana hiyo tutakapomaliza jimbo la Njombe na hasa Jimbo la Mheshimiwa Naibu Spika umeme ule sasa unashuka katika jimbo langu la Peramiho kupitia Kata ya Wino, Mahanje, Gumbilo, Tanga na hatimaye utaingia Songea Mjini.

Mheshimiwa Spika, niseme bahati nzuri barabara hiyo ni ya lami haina matatizo kabisa na Kata hizo ninazokwambia ziko katika barabara ya lami. Sasa naomba niseme kitu kimoja, bahati nzuri wakati wale wawezeshaji wetu wa mradi huu walipokuwa wanakuja Mkoa wa Ruvuma mimi nilipata habari wanakuja. Mimi na *Finance Committee* ya Halmashauri yangu tulikwenda kuwapokea mpakani mwa Njombe na jimbo la Peramiho. Kwa kweli walifurahi sana wakataka kujua ni namna gani katika michoro yao na uletaji wa umeme ule nini kifanyike. Tulikubaliana umeme ule upite katika Kata ya Wino kwa maana ya vijiji vikubwa ambavyo viko barabarani Kijiji cha Igawisenga na Lilondo hatimaye uingie Wino kwa sababu tuna ushirika mkubwa ambao nimeuzungumza asubuhi wa mazao.

Zimewekwa *investments* kubwa kabisa, kuna zahanati na Shule ya Sekondari lakini tulikubaliana *sub station* ya umeme huo wa gridi ijengwe katika Mji wetu mkubwa kweli unaoitwa Madaba na ukitoka hapo basi utateremka mpaka kufika Songea Mjini. Unapofika Songea Mjini huku njiani nina uhakika kama tulivyoshauriana na wawekezaji

wetu kwamba utazingatia vijiji vyote vya Gumbilo, Tanga na vile vingine ambavyo viko barabarani na vina shughuli nyingi za kibiashara na naamini Waheshimiwa Mawaziri ambao wamepita njia hiyo wanakubaliana na mimi.

Mheshimiwa Spika, lakini ukishafika Songea mjini tatizo linaanza kuwa kubwa, hakuna umeme pale, hata sasa hivi tunatumia Majenereta lakini ni shida kubwa sana. Namshukuru na nimpongeze sana Mbunge wa Songea Mjini, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi kwa sababu kwa kweli amefanya kazi ya ziada kufuatilia suala hili la tatizo la umeme Songea mjini. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Peramiho lakini Makao Makuu ya Jimbo langu yako Songea Mjini.

Kwa hiyo, na mimi nina maslahi pale Songea Mjini. Namshukuru Dr. Nchimbi kwa sababu baada ya kwenda mimi na yeye kumwona Mheshimiwa Waziri ameahidi kabisa kwamba majenereta mawili mapya yataongezwa kuleta nguvu pale Songea Mjini na wananchi waweze kunufaika. Tunachoomba tu Mheshimiwa Waziri toka ahadi hiyo ilipotolewa mpaka sasa hivi utekelezaji bado na Mji wa Songea uko kwenye giza, kwa hiyo, tunaamini utatuambia nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, tukishatoka Songea Mjini ndio tunaelekea Peramiho ambako ndiko makao makuu ya jimbo la Peramiho tunaweza kusema yalipo, huko ndiko shughuli iliko. Mwaka jana Mheshimiwa Waziri, Dr. Ibrahim Msabaha nilimweleza ndugu yangu kuwa tuna fedha nyingi sana zimekuwa *allocated TANESCO* kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini, nilimuuliza, "unasema nini kuhusu mji maarufu sana wa Peramiho?" Kuna hospitali kubwa, kuna viwanda vikubwa, kuna biashara kubwa sana, *TANESCO* wangeweza kutengeneza fedha nyingi sana kwa kufanya *connection* ya umeme tena kutoka katika kijiji cha jirani cha Lilambo kwenda pale Peramiho, kilomita kama kumi na kitu tu, kwa nini msivute ule umem? Mheshimiwa Msabaha akaniambia Mheshimiwa Mhagama tatizo hilo limekwisha, nina majibu ya *Hansard,* nimeyakabidhi kwa Mheshimiwa Waziri. Ahadi ile ilitolewa humu ndani ya Bunge letu Tukufu na naamini ilikuwa ni ahadi ya ukweli lakini cha kusikitisha mpaka sasa hivi zoezi hilo halijafanyika. Ndiyo maana wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nilimwomba ndugu yangu Naibu Waziri tuongozane akajibu hayo maswali huko kwa nini hali imekuwa tofauti?

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba namshukuru sana Mheshimiwa Waziri baada ya kufanya naye maongezi hapa amenihakikishia kwamba atajitahidi kuonana na *TANESCO.* Nina barua, nina nakala ya faksi kutoka *TANESCO* ambayo nilikuwa nawasiliana na Wizara wakati wa bajeti ya mwaka jana na *TANESCO* makao makuu.

Walinihakikishia kwamba wamefanya *feasibility study* na kugundua kwamba Peramiho ni mahali ambako wakiwekeza kwa maana ya kufanya *extension* ya umeme wataweza kupata fedha kama *returns* ya uwekezaji wao watakaofanya pale. Kwa hiyo, ninaamini kabisa hili liko mikononi mwa Mheshimiwa Waziri na nina uhakika kwamba mwaka huu *TANESCO* wakishirikiana na Wizara, Peramiho itapata umeme. Lakini Naibu Waziri afanye haraka kuja, akawaeleze wale wananchi na kuwahakikishia hilo.

Mheshimiwa Spika, ukitoka Peramiho unakwenda katika Kata ya Mgazini. Kata ile ndiyo Kata ambayo alikuwa anaifagilia leo asubuhi Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ni wazalishaji wakubwa sana wa mahindi. Nilikuwa nataka kueleza kuwa tumeshaanza sisi kuangalia *alternative* ya kutumia mabunzi ya mahindi mengi yanayokuwa *produced* tani kwa tani kila mwaka; je, kwa nini yasitumike kutengeneza nishati mbadala ya umeme katika vijiji vinavyozunguka eneo lile?

Kwa hiyo, tayari tumeshafanya andiko zuri sana la mradi, nitaomba nilikabidhi Wizarani watupe *support* kwa sababu wamekuwa wakifanya *study* nyingi za umeme wa kutumia upepo na kadhalika, naomba wachukue na hili, inaweza ikatusaidia. Wakulima wa mahindi wa Rukwa, Mbeya, Ruvuma na Iringa tunaweza sisi tukatengeneza *alternative power* ya umeme kwa kutumia mabunzi ya mahindi kwenye maeneo tunayozalisha mahindi. Hilo lilikuwa ni ombi langu.

Mheshimiwa Spika, sasa nirejee katika tatizo lingine kubwa, machimbo. Kwa maana ninayojua ya haraka, tunapozungumzia madini ni kila kitu kinachochimbwa chini ya ardhi. Kata ya Wino kijiji cha Lilondo kuna machimbo makubwa sana ya kokoto za kujenga barabara. Leseni ya machimbo ya kokoto zile imetolewa kwa taratibu ya leseni nyingine kama za madini mengine yanayochimbwa katika maeneo mbalimbali.

Lakini yale machimbo ingawa yanamilikiwa na wakala wa barabara wa Mkoa, eneo lile limekuwa likileta usumbufu mkubwa kwa wananchi wa kijiji cha Lilondo na Kata ile ya Wino. Machimbo yale wachimbaji wanatumia baruti kwenye kuchimba zile kokoto. Lakini sasa *impact* ya machimbo hayo pale Lilondo imekuwa ni kubwa kimazingira, lakini kiafya pia kwa wale wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi machimbo yale baada ya kuwa yamefanyiwa kazi kwa muda mrefu mashimo yamebaki kuwa makubwa, hakuna shughuli nyingine za ku-*retain* masuala ya uharibifu wa mazingira zinazofanyika na mambo mengine mengi. *Pollution* na vitu vingine vingi naomba Wizara ifikirie ni namna gani basi kuanzisha miradi angalau ya kuweza kushirikiana na wananchi katika maeneo yale.

Miradi kama ya kurudisha hifadhi ya mazingira ya kuangalia kwamba wananchi pale hawawezi kuangalia *pollution* kwa maana ya kwamba kuathirika na hewa inayopatikana wakati wa shughuli za uchimbaji zinavyoendelea na miradi mingine tu mingi kushirikiana na shughuli za maendeleo na wale wananchi wa kijiji kile.

Nafikiri tukifanya hivyo itatusaidia sana. Wenzetu wengine wanaomilikiwa machimbo ya madini kama dhahabu na kadhalika tunashukuru wamepata mrabaha kitu cha namna hiyo, lakini sisi basi tuangaliwe kwenye Halmashauri yetu *kamrahaba ka* namna fulani ambako *hakafanani* na hiyo mirabaha mikubwa mikubwa kama ilivyosomwa na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake. Nadhani nikisema hivyo Mheshimiwa Waziri ananielewa na nimechangia kwa maandishi na nime-*produce documents* zinazoonyesha ukubwa wa tatizo na naamini kwamba wataweza kunipa majibu yenye faraja sana kwangu.

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee kusema kwamba suala la kuzingatia nishati ya umeme katika maisha ya Watanzania ni suala la msingi. Sitaki kurejea michango ya Waheshimiwa Wabunge wengine kama walivyosema. Tunaposema labda tutumie umeme wa *solar,* ni gharama sana kwa wananchi wetu. Tunaposema labda tutumie umeme wa namna nyingine kwa wananchi wetu ni gharama sana. Kwa hiyo, naona kwamba kwa kweli Serikali inatakiwa kuwa na mipango hiyo endelevu ya kuhakikisha wananchi vijijini wanapatiwa umeme kwa ajili ya kuleta maendeleo yao.

Nilikuwa napitia kitabu cha *Development Budget* hapa kila unapoangalia eneo ambalo linahusiana na umeme vijijini ama fedha hakuna au ni kidogo sana. Nafikiri kwa kweli hatutakuwa tunawatendea haki wananchi wa Tanzania. Uwezo wao ni mdogo, Serikali yao ndiyo mkombozi mkubwa wa kuwaletea maendeleo. Kwa hiyo, Serikali ndiyo inayotakiwa ijipange vizuri kuhakikisha kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania yanaweza kupatikana na naamini sekta hii ya nishati na madini pia ni sekta nyingine kiongozi katika kuleta na kuendeleza uchumi wa wananchi wa Tanzania hasa wananchi wa jimbo la Peramiho ambao kwa kweli ndio walishaji wakubwa wa chakula na hasa mahindi kwenye nchi nzima hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli hayo niliyoyazungumza kuhusu umeme Peramiho niendelee kusisitiza juu ya *Sub station* ya umeme wa gridi pale Madaba, machimbo ya kokoto pale Lilondo Kata ya Wino na majenereta ya umeme pale Songea Mjini, naomba Serikali iyape umuhimu. Lakini nashukuru kwamba Wilaya ya Mbinga tayari bajeti imeshatengwa, watapatiwa umeme, Wilaya ya Namtumbo watapatiwa umeme, Wilaya ya Tunduru umeme upo lakini utaendelea kuimarishwa ili Mkoa wa Ruvuma na wenyewe uendelee kung’ara katika maendeleo kwenye nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita msemaji anayefuata, nimevutiwa na jinsi Mheshimiwa Jenista Mhagama anavyotetea umeme ufike huko Peramiho na kila mahali. Anachonishangaza ni kwamba badala ya kumwalika mwenye dhamana ambaye ni Waziri , yeye amemwalika Naibu Waziri ndiyo akasaidie kutatua. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu. Awali ya yote nakupongeza wewe mwenyewe jinsi unavyotuendeshea Bunge letu. Lakini pia natoa *offer* ili uendeshe kwa starehe hii hali ya kukatika katika umeme sio nzuri, mimi ni mtaalamu nipo tayari kushirikiana na wataalamu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa jitihada ambazo zinafanyika za kuhakikisha kwamba Taifa letu linaondokana na matatizo ya umeme. Nitaungana pia na Mheshimiwa aliyenitangulia Mheshimiwa Jenista, kwa niaba ya wananchi wa Ruvuma kupongeza kazi ambazo mpaka sasa Serikali imefanya na Ubalozi wa *Sweden* kwa jinsi ambavyo tumejitahidi kuweza

kuhakikisha kwamba Ruvuma tunapata umeme wa kuaminika. Kwa kuwa mwenzangu ameshazungumza mengi, mimi nadhani niende moja kwa moja kwenye mambo ambayo ni ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 27 imezungumzwa sheria ya umeme, mimi naona ilichelewa. Nashukuru sana kwa kufikia sasa maamuzi hayo. Umeme ambao mteja anatakiwa kupata huwa una kiwango maalum na *TANESCO* inafahamu. Lakini ukiangalia katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam na miji mingine umeme uliopo ni nje ya *standard*. Kila mara umeme unachezacheza, umeme unakatika katika, vifaa vya watu vinaungua sana kiasi kwamba hata wanapokwenda kudai malalamiko kuhusu vifaa vinavyoungua kwa kweli utekelezaji wake wa malipo unakuwa ni mgumu kwa sababu hakuna sheria maalumu inayowalinda.

*TANESCO* ilijaribu kuweka Bima ya kuweza kuwasaidia wateja kama hao, lakini Bima ile pia haimwezeshi mteja ambaye ameunguliwa na vifaa kwa ajili ya kuchezacheza aweze kulipwa, yaani mpaka ionekane nje ya uwezo kwamba kweli huyu mteja anastahili kulipwa. Sasa katika sheria hii naomba izingatiwe ni jinsi gani mteja au muathirika wa umeme ataweza kulipwa haki zake. Kuwe na Bima maalumu ambayo mteja anaweza akashauriwa mwenyewe aweze kuingia katika bima ambayo ni ya *standard* ya juu, kati au ya chini aweze kuingia katika mazingira yepi? Hiyo itasaidia *TANESCO* iondokane na mzigo yenyewe kujikagua na kusema sasa hivi namlipa mteja au sitomlipa.

Kwa mfano, nyumba ikitokea imeungua kwa moto tunasema watu wa *Fire* watakuja, watapima, wanaangalia pale halafu ripoti ya mwisho inakuwa mpaka alete mtu wa *Fire.* Sisi *TANESCO* tunaishia kusema kwamba chanzo cha moto bado haikajajulikana, mtaalamu wa moto ndiye atakayesema kwamba ni chanzo gani. Kwa hiyo, inamtesa mteja. Mimi naona kwa kweli iko haja sasa kwa sura hii ya maisha bora kwa kila Mtanzania sheria hii ikawepo, Bima ya umeme iwepo ili yule aliyeathirika kwa umeme hata kama itakuwa ni kwa ajili ya *wiring* ya ndani ambayo inamhusu mteja au *wiring* ya nje ambayo inahusu shirika basi kuwe na chombo cha kati ambacho kitaweza kuwasimamia wateja pamoja na Shirika ama sivyo matatizo yetu yatakuwa bado hayajapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda pia kusisitiza kuhusu malengo ambayo sasa hivi *EWURA* inaingia na *TANESCO* kuhusiana na mikataba baina ya wateja na *TANESCO* kupata huduma inayostahili. Kwa hali ya sasa kwa mfano, kama huduma itatakiwa kwamba mteja baada ya kukatiwa umeme ahudumiwe ndani ya saa moja, foleni hii iliyopo Dar es Salaam, mfano mteja ameripoti toka Tegeta aanze kuondoka fundi toka Kinondoni mpaka Tegeta anafika saa ngapi? Itakuwa nje umeme mdogo kila mahali bado upo chini.

Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kurekebisha hii miundombinu zinahitajika karibu bilioni 1.3 fedha za Marekani ambayo ni sawa karibu na sh. trilioni 1.3 ya fedha za Tanzania. Sasa kama bajeti yetu haiwezi kuangalia *TANESCO* na ikaweza kuwapa hizo fedha, hicho kiwango kitafikiwa kwa kiasi gani? Kama kila siku tutapeleka kesi *TANESCO* itakuwa ni nini? Ndiyo maana hata wenzangu wanapomsifu sasa hivi

Mkurugenzi Mtendaji wa sasa kweli nafarijika kwa hatua alizochukua. Lakini mimi naona bado tunadanganya kwa sababu tumeangalia tu umeme ambao tulikuwa tunaukosa kwa sababu ya mgao. Lakini hali halisi ya kumsaidia Mkurugenzi huyu ni kumpa fedha, tumruhusu aweze kufanya kazi yake kama tulivyoona ana uwezo mkubwa.

Kwa nini Mtanzania anapopewa kazi anafungwa kamba shingoni? Mtanzania anapewa kamba ya *radius* ya mita 5, anawekwa mahali pasipo na nyasi anaambiwa kula unenepe. Akija Mzungu anaachiwa kwenye nyasi za kijani anapewa na chumvi anaambiwa mbona wewe hunenepi kama huyu mzungu kwa sababu zipi? Wote jamani tumepewa nafasi za kuwasimamia hawa watu na kuwasaidia watu, hizi nafasi sio zetu tumepewa na Mungu naomba tufanye maamuzi ambayo yanalenga kuwasaidia wananchi wenzetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa pia niongelee kidogo kuhusu *IPTL*, *AGRECO* na *RICHMOND*. Mimi binafsi sijali umeme unatoka kwenye Kampuni gani, iwe imetoka kwa Mtanzania, au kwenye Shirika gani ili mradi unatatua matatizo tuliyonayo. Wenzangu waliotangulia walizungumzia umuhimu wa kusogeza mazungumzo baina ya *IPTL* ili aweze kubadilisha ile mitambo iwe ya gesi na wakati huo kuweza kuleta unafuu kwa *TANESCO*. Lakini mkataba ule una-*favour* kubwa sana kwa *IPTL,* ana-*negotiate* wakati akiwa na raha zake kwa sababu hana hasara. Kwa kuwa hawa wanatarajia kumaliza mikataba yao karibuni; na kwa kuwa bado sisi tuna shida ya umeme je, kwa nini tusi-*bargain* nao?

Kama itawezekana kwamba wao wataweza kutuuzia bila ya kusema *capacity charges,* maana yake badala ya kuondoa hiyo mitambo waihamishe sehemu nyingine au iende ikawa tu imekaa mahali. Unaweza uka-*negotiate* wakati kama *independent power producers* wakatuuzia umeme badala ya kuiweka ile mitambo bila kazi na pengine umeme ukawa upo kwenye bei nafuu zaidi kuliko sasa kusema tungojee ule ambao *IPTL* inatuuzia kwa bei ghali kwa sababu inatumia mafuta. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuifanya *IPTL* ione kwamba ina *co-investors* wengine. Kwa hiyo, naomba sana tujaribu kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukatumia hiyo *advantage* lakini kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba nirudi kwenye uwekezaji ambao unafanyika pia ndani ya *TANESCO*. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia jinsi ambavyo nguzo zimesimama kwenye maeneo yao lakini hazijaweza kupata fedha za kumalizia miradi hiyo. Nguzo zina muda wa kuishi takriban miaka 18. Sasa nguzo inapokuwa imefukiwa chini kwa miaka 5 haijafanya kazi tayari imeshapunguza *life span* yake na imekaa pale wakati umeshika fedha ambazo zingeweza kufanya kazi katika maeneo mengine.

Naomba sisi Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu tufanye kama vipaumbele vingine tulivyofanya; kwa nini tusiwawezeshe hao wamalize ile miradi ambayo ilishaanza? Naona kwamba fedha zikitolewa tumalizie kwanza zile nguzo na yale matengenezo ambayo yameanza halafu kwa mwaka unaofuata tunaweza tukajipanga

katika miradi mipya ama sivyo tutakuwa tunapoteza fedha. Wakati ule bajeti labda ya kujenga hiyo *line* unaweza kukuta ilikuwa ni fedha kidogo lakini kadiri zile nguzo zinavyokaa na haitekelezi ile miradi, sana sana inazidi kufanya ile miradi inakuwa ghali zaidi. Uwekezaji wa leo sio sawa na wa kesho. Kwa hiyo, naomba hilo liwe kama angalizo kwa *TANESCO* tuweze kutoa kipaumbele kwa miradi ambayo imekwishaanza kule Mbozi na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo umuhimu wa kumalizia miradi hiyo uko katika maeneo mengi. Kwa mfano tuchukulie *line* ya Tegeta/Bagamoyo. Bagamoyo ni mji ambao sasa hivi una mahoteli makubwa lakini *line* inayokwenda Bagamoyo sasa hivi inapita maporini kiasi kwamba ikikatika siku mbili watu watakagua umeme porini, *line* ile haijaisha.

Kuzimika kwa umeme kwa Bagamoyo kwa muda wa saa mbili hasara yake ni kubwa sana, japo haionekani kwa macho. Lakini hata hivyo ile *line* kwa mfano ina *potential* kubwa sana ikapitisha umeme hata Bunju A, Bunju B, Kerege kule Mapinga mpaka Bagamoyo. Kwa hiyo, mimi naomba miradi kama hiyo tuipe nguvu ili sasa ianze kuzalisha na kuongeza fedha kwenye mfuko wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho naomba nirudi kwa wafanyakazi wenzangu. *TANESCO* ndugu zangu pamoja na kuhitaji kuboreshwa kwa maslahi lakini ukweli ni kwamba nitaendelea kusema kila siku mmenituma huku huduma zetu zinalalamikiwa. Hata kama kiongozi huyu sasa hivi Dr. Idrisa atafanya kazi kubwa kiasi gani ya kupanga safu huko juu kama huku chini sisi hatutajipanga vizuri ni tatizo kubwa, kwa nini? Jamani mwenzenu niko nje naona zaidi, tafadhali sana tujirekebishe wafanyakazi wa *TANESCO* wakati huu ni wa ukweli. Nawaombeni sana kwa heshima na taadhima nyinyi ni wana *TUICO* wenzangu sitatetea katika hilo tena.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme tu kwamba naunga mkono hoja na nazidi kuomba sana Shirika hili lipewe kipaumbele labda mwaka kesho litakuwa na bajeti nzuri zaidi kuliko ya mwaka huu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Mimi pale nilikuwa nimekwishakata tamaa kwa sababu kwa tangazo la asubuhi nilifikiri nisingefikiwa. Lakini nashukuru sana.

Kwanza, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ni kazi ngumu kila Mheshimiwa Mbunge hapa anaomba umeme, lakini uwezo wao ni mdogo, nawapa pole sana. Sasa ombi langu kwa Serikali kama tulivyofanya kwenye MMEM na kama tulivyofanya kwenye barabara Serikali ianze kujipanga vizuri kuisaidia Wizara hii ili angalau iweze kusaidia maeneo mbalimbali katika nchi yetu yaweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, sitasema mengi sana, niende moja kwa moja kwenye jimbo langu. Tangu mwaka 1995, nimefanya mambo mawili tu makubwa katika Wizara hii. Ombi langu la kwanza niliomba umeme wa kwenda Hungumwara mpaka Ngudu.

Maelezo niliyoyapata ni kwamba kutoka Ngudu kwenda Hungumwara umeme hauna nguvu na kwamba haungekuwa na manufaa sana kwa watu wa Hungumwara, lakini nashukuru sana angalau sasa hivi umeme huu umefanikiwa kupata nguvu. Sasa umeme huo umeweza kutoka Ngudu kwenda Malya, japokuwa umekwenda kwa kusuasua, lakini nimeona umeme utafika huku, nadhani zile sababu zilizowafanya umeme usifike Hungumwara sasa zimepungua.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la pili kwa Wizara hii la tangu mwaka 1996 ambapo niliomba umeme upelekwe kwenye *ginnery* mbili, mwingine upelekwe katika vijiji vya Ilula, Hungumarwa hadi Shirima. Katika *line* hiyo umeme ungeweza kupita kwenye *ginnery* mbili, *ginnery* ya Mwalujo na Sangu. Ukipita katika maeneo hayo ungeweza kupitia katika shule saba za sekondari ikiwemo Shule ya Sekondari ya Wasichana ya *A Level* ya Mwamashimba. Aidha, ingeweza kupita katika zahanati mbili na kituo cha afya cha Mwamashimba.

Nasikitika sana tangu mwaka 1996 jibu sahihi bado sijaweza kulipata na wala sijapata maelezo ya wazi kutoka Wizara hii. Nilikuwa napenda kupata maelezo mazuri kwenda kutoa taarifa kwa wapiga kura wangu lakini kwa masikitiko makubwa sana hakuna chochote kinachoendelea. Naomba sasa kwa leo Waziri anisaidie atamke kwa niaba yangu na wapiga kura wangu wote wasikie kulikoni? Lakini hapo hapo pamoja na kufahamu Mheshimiwa Waziri amepata mialiko mingi sana, na mimi leo naomba nimwalike aje mwenyewe au Naibu Waziri lakini akubali kitu kimoja. Nafahamu wengine walipofanya mialiko wameomba Mawaziri hawa wakafanye ziara mchana, mimi naomba waje wafanye ziara usiku, aje twende Ilula, Hungumwaro, Mwamashimba mpaka Shirima usiku, halafu tupite kwenye zile *ginnery* mbili usiku. Nasikitika sitampeleka kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana usiku ila nitampeleka zile za Wavulana.

Mheshimiwa Spika, naomba sana sana suala langu lipewe mmuhimu. Nasema hivyo kwa sababu wananchi hao niliowataja wanahitaji huduma ya umeme katika maeneo hayo. Ni maombi ya siku nyingi na ninafanya maombi hayo kwa sababu moja tu, kwa sababu nafahamu kwamba bila nishati ya umeme, maeneo yetu haya hatuwezi kuendelea kwa vyovyote vile.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea nishati ya umeme, naenda moja kwa moja kwenye madini. Mwaka jana nilipokuwa nachangia, nilitoa rai kwa Serikali, nikasema, "naomba sana Serikali iwe na mpango mzuri wa Wachimbaji wa madini. Tusifanye uchimbaji wa madini nchi nzima kwa mara moja, twende hatua kwa hatua". Sijui kama lilizingatiwa ama vipi. Lakini naomba sana, kwa sababu madini haya si yetu tu kama nilivyosema mwaka jana, ni ya watoto wetu, ni ya wajukuu zetu, watahitaji kunufaika na madini haya baadaye. Ni vizuri tukaenda hatua kwa hatua, mimi naamini kwamba tutapata faida kubwa zaidi baadae na manufaa makubwa zaidi kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumsaidia Waziri, aangalie majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini mwaka jana, tarehe 18 Julai, 2007 alipokuwa anajibu

Mheshimiwa Dr. Msabaha, alisema kwamba angezingatia maombi yangu. Kwa bahati mbaya amehama bila kuaga. Na mimi wasiwasi wangu hakukabidhi! Lakini naamini kuwa Katibu Mkuu alikuwepo na watendaji wa *TANESCO* na wa Nishati na Madini walikuwepo. Hebu naomba wakapitie *Hansard* hiyo tuone majibu yatakuwaje, ila leo naomba kuambiwa kulikoni? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Asante sana! Nunga mkono hoja! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakila, asante sana! Sijui hizi ziara zako za usiku, labda itabidi na Naibu Waziri wa Usalama wa Raia awemo katika ziara hiyo! *(Kicheko)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nami kupata nafasi ya kusema katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Nishati na Madini. Napenda kurejea salamu zangu ambazo nilikuwa nimezitoa tangu wakati wa bajeti kwamba kwa kweli sikuridhishwa na mwenendo wa Wizara hii toka mwaka jana kutokana na ahadi ambazo zilikuwa zimetolewa na hasa sisi Wabunge ambao tunatoka kwenye majimbo na tuliondoka kifua mbele tukisema kwamba umeme unakuja! Sasa narejea kwamba bado hicho kitu hakijafanyika na hata katika hii hotuba ambayo imetoka sasa hivi, bado hakuna mwelekeo wowote wa kupata umeme katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utangulizi pia ningependa kuitaka Serikali kwamba matatizo makubwa ambayo yanajitokeza sasa hivi hasa ya mafuta ni kwa sababu ya ushauri mbaya ambao tulipata hapo nyuma wa kuacha na kutokuwa na Shirika tulilokuwanalo la *TPDC* ambalo lilikuwa linasaidia sana ku-*regulate* na kusaidia kuifanya bei ikawa nzuri na matokeo yake wafanyabiashara wamekuwa na kiburi kwa sababu hakuna mbadala. Kwa hiyo, katika hili ningependa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho aelekeze namna gani ambavyo atakuwa amejipanga katika kuokoa suala la mafuta ambalo limekuwa ni kero kubwa hasa sisi tunaotoka mbali na Bandari. Sasa hivi dizeli kule nyumbani inauzwa kati ya shilingi 1500 na 1600 na katika maeneo mengine inafika mpaka shilingi 1700. Lakini tukifanya *TPDC* ifanye kazi na hata hawa *UWURA* na *SUMATRA* wakafanya kazi vizuri, basi wananchi wetu wanaweza wakafaidika na nishati ambayo ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa narudi kwenye hoja. Wilaya ya Nzega ni miongozi mwa Wilaya zilizokuwa na bahati ya kupata umeme miaka ya 1982/1983. Pale Makao Makuu ya Wilaya, tulipata, tunashukuru. Lakini cha ajabu, baada ya umeme kufika Nzega, ulikuwa ni umeme wa Nzega Mjini pale pale, basi! Nzega hata vitongoji vyake, ukitaja: Nyasa, Bulunde, Tazengwa, hakuna umeme! Umeme ni wa pale pale mjini, hausambazwi kwenda mbele zaidi ya Nzega. Kwa hiyo, hii ya umeme wa gridi ya Taifa isiwe ni kikwazo cha umeme kusambazwa vijijini maana ndiko kwenye wananchi. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuna mtiririko ambao tulikuwa tumeuzoea wakati ule. Mimi niko Bunge hili tangu mwaka 1995/1996, tumekuwa na mtiririko wa kuonyesha kwamba, baada ya vijiji hivi, vijiji kadhaa vinafuatia. Waziri hajaonyesha kabisa, na huu ni upungufu mkubwa kwa wenzetu hasa watendaji kutomshauri vizuri Waziri kwamba kuna mtiririko huu ambao ulikuwa umewekwa na tulikuwa tunauheshimu sana. Kwa

hiyo, hili ni sikitiko ambalo sisi ambao tumekuwepo muda mrefu, linatuathiri sana katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nzega imepitiwa na gridi ya Taifa, inakwenda mpaka Tabora. Pale katikati, kati ya Nzega na Tabora kilomita 120, kuna vijiji vya Wilaya ya Nzega ambavyo vimepitiwa na hiyo gridi ya Taifa na umeme wanauangalia ukipita pale kuelekea Tabora bila wao kuwekewa *transforma*; bila wao kupatiwa umeme mpaka leo hii tunavyozungumza. Na katika vijiji hivyo ambavyo vinapitiwa na gridi ya Taifa, upo mji maarufu sana! Na hapa Mheshimiwa Spika, nimekuletea mchele wa kutoka nyumbani ambao unazalishwa na viwanda vya kwetu, unaitwa "Tule na Bwana". Ni mchele safi, umechambuliwa, unanukia, ni kweli ni "Tule na Bwana". Unachambuliwa katika viwanda vinavyozalisha katika *Line* ya Jimbo la Bukene kule Mwamala. Jimbo la Bukene ni karibu sana na Mji wa Nzega, ni kilomita 30 tu kutoka Nzega. Tangu mwaka 1982, Jimbo la Bukene ni giza, wananchi wa pale wanakabiliwa na giza; wanaishi kwa jenereta, wananchi wa pale wana viwanda, wanazalisha mchele. Nitakupa Mheshimiwa Spika, upo kilo 25 ni safi, zawadi yako kutoka kwa wananchi wa Nzega na kilo 25 zingine nitampa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Waziri Msabaha na Waziri Yona, walikuja Ndala, walikwenda Bukene. Tuliwatembeza, tuliwasha koroboi (kibatari) ili waone athari ambazo wananchi wetu wanapata, wanatumia kibatari. Ninapozungumzia Bukene, ninapozungumzia Ndala, Puge, ni miji ambayo imekuwepo muda mrefu sana. Ni aibu kwa miaka 50 ya uhuru mpaka leo bado hawajapata umeme wakati gridi ya Taifa imepita pale pale.

Hili nalisema kwa uchungu na naomba wananchi wangu wanielewe, wanisikie, nina uchungu sana kwa sababu Rais Mkapa alikuja akawaambia kwamba, "kabla sijaondoka madarakani, mtapata umeme". Amesema Puge, amesema Bukene. Amekuja Rais Kikwete naye ameahidi vile vile. Sasa kwenye programu ya Waziri hakuna kitu, tunawaambieje hawa watu na mwaka jana tumerudi pale tumewaambia wakae mkao? Na nikienda sasa hivi pale Ndala, tayari walishaanza na *wiring*, wameshaanza kutandaza waya kwenye mji wa Ndala wakisubiri ahadi ambayo Bunge lako hili liliambia mwaka jana. Sasa katika programu hakuna!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tutaelewana vibaya! Naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, awaambie wananchi wa Wilaya ya Nzega, ni utaratibu gani ambao ameuweka mahususi angalau hii ahadi iwe ya mwisho. Wamekwishaahidiwa na Rais Mstaafu, wamekwishaahidiwa na Rais wa sasa kwamba watapata umeme. Je, wanapata umeme kwa utaratibu gani, kwa namna gani na kwa jinsi gani ili na wao waweze kupata umeme kwa Jimbo la Bukene na Jimbo langu la Nzega, Tarafa ya Puge, Mji wa Ndala, Puge, Kiniziwa, Busondo, Itilo, Utwigu mpaka Nzega yenyewe?

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia Ndala na Bukene – Mwamala, hatuzungumzii umeme wa hivi hivi. Pale Ndala kuna hospitali ya Mashirika ya dini, wanatumia jenereta. Kuna Chuo cha Elimu ya Taifa, wanatumia jenereta, kuna shule za sekondari wanatumia jenereta. Ni mji ambao una wakaazi wapatao 5000, wanatumia

jenereta. Bukene kuna Stesheni ya Reli, pale Stesheni wanatumia koroboi. Mwamala, kuna mashine za kusindika mchele, wanatumia jenereta ya mafuta ya dizeli ambayo imepanda hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nasisitiza kwamba katika hili, bado sijakubaliana na mtiririko alionalo Mheshimiwa Waziri. Hizi bilioni kumi alizoziweka, basi angetuambia katika fedha hizi Wilaya ya Nzega itapata ngapi kwa sababu tayari tulikwishakaa na kuanza kusambaza nyaya katika majumba yetu katika Jimbo la Nzega pamoja na Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nataka kusema neno moja juu ya usambazaji wa umeme kupeleka Kigoma. Katika programu ambayo nimeiona hapa tuliambiwa mwaka jana kwamba umeme utatoka Shinyanga, utakuja Nzega mpaka Tabora kupitia Urambo kwenda Kigoma. Kwa sababu tayari pale kuna nguzo, Serikali haihitaji kujenga *line* nyingine, badala yake ni kuimarisha hizi nguzo zilizopo kwa kubadilisha nyaya. Zile nyaya zilizopo ni ndogo, haziwezi kubeba uzito wa kilovoti 132, badala yake ni kuondoa hizo nyaya kwa kutumia nguzo zile zile, kutumia miundombinu ile ile. Ukatumia mpaka Tabora, ukasambaza mpaka Urambo, mpaka Kigoma ili maeneo hayo yote yaweze kuwa na umeme wa uhakika. Lakini katika programu ambayo ameiweka Mheshimiwa Waziri hajaonyesha utaratibu mzuri, ameifuta kabisa njia hiyo kupita Urambo–Tabora kwenda mpaka Kigoma. Kwa hiyo, napenda kupendekeza basi ibadilishwe ili iweze kuwekwa msongo wa 132*kv* kwenda Kigoma, kupitia Uvinza – Kaliua na Urambo kwa kupitia Tabota kwa sababu tayari pale kuna *line* ya nguzo kutoka Tabora – Nzega – Shinyanga mpaka Mwanza ambayo ni ya gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ninataka kuzungumzia juu ya madini, na hapa nianze kuzungumza juu ya wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wadogo hawa, mimi nawaita ni wavumbuzi. Lakini kwa huruma kubwa ni wachimbaji ambao Serikali imewaacha yatima. Wachimbaji wadogo wadogo wakishagundua machimbo, wakishaanza kuchimba, wakiishaanza kupata fedha, tayari Serikali inakuja na wawekezaji wakubwa, wanafukuzwa, wanaondolewa na malipo yake ya fidia ni kidogo sana, ndio maana kuna vurugu kubwa katika kuwaondoa wachimbaji wadogo wadogo. Kuna vurugu pale Isagehe, kuna vurugu pale Isungangwanda, kuna vurugu hata kule Matinje katika Wilaya ya Igunga kwa sababu wameondolewa hawa ambao wamegundua na kuweka wachimbaji wakubwa ambao wanawalipa kidogo sana. Ahadi ambazo Serikali imekuwa ikitoa mara kwa mara katika Bunge lako Tukufu ni kwamba wachimbaji wadogo wangeweza kuangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wanahitaji nyenzo ili baadaye waweze kuwa wachimbaji wa kati na ili baadaye na wao waweze kuwa wachimbaji wakubwa. Lakini kama hatujawatayarisha, hatujawawekea misaada, hatujawawekea mikopo, hatujawawekea nyenzo, daima dumu watabaki kuwa ni wachimbaji wadogo wadogo. Siku zote watakuwa wanaondolewa katika maeneo yao kuwapisha wachimbaji wakubwa ambao wanakuja na mitambo, nyenzo na mitaji, ambao wana uwezo mkubwa. Mimi ningeomba Serikali iwaangalie kwa makini wachimbaji wadogo kwa sababu ndio wananchi wetu ambao ni rasilimali watu. Tukiwawezesha hawa ni wazuri sana. Tumeona

katika michango mbali mbali wanatusaidia kweli. Katika michango ya kujenga shule za sekondari, michango ya maji, wanatusaidia kwa sababu kidogo wanakuwa na uwezo wa kifedha. Wachimbaji wadogo wapewe vifaa, wapewe na mikopo, wapewe na ujuzi kwa sababu tayari watakuwa wamesaidia katika kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, nikiwa hapo hapo kwenye madini, nilizungumza wakati nachangia kwenye bajeti. Wizara ya Nishati na Madini imewaachia wachimbaji wakubwa, wamekuwa wao ndio wenye amri, wamekuwa wao ndio wenye nchi hii na ushahidi upo! Nimekuwa nikilisema hili katika bajeti zote za Wizara ya Nishati na Madini, na bahati mbaya wachimbaji wakubwa mimi hawanipendi, kwa kusema ukweli. Hata wasiponipenda ni sawa. Nimekuwa nikisema mara kwa mara kwamba hawa wachimbaji wakubwa tunawaachia wanakuwa wenyewe, kila kitu wanafanya wenyewe. Wanachimba peke yao, wanafunga peke yao, wanasafirisha peke yao, baadae wanakuletea *return* wewe kwamba tumeuza hivi, soko lilikuwa baya! Tangu lini uliona mfanyabiashara akakuambia ukweli?

Mheshimiwa Spika, Serikali imejiondoa mno katika kuwaangalia hawa wachimbaji wakubwa, ndio maana nikasema katika bajeti ya mwaka huu kwamba hata huu mchanga ambao juzi umesombwa kutoka Kahama ni uzembe wa Serikali, ni kwa sababu tunawaachia wanafanya kazi wao wenyewe! Hatujasimamia ipasavyo! Ndio maana ukiangalia kwenye vitabu mapato kwenye madini yako chini sana. Tumekuwa tukipigia kelele mchanga ambao unapelekwa nje, *Japan* na mwingine kupelekwa Australia, wanachokifanya kwa sababu tumewaachia, wanachukua mchanga kutoka kwenye shimo lile la madini *(pit)*, badala ya kuupitisha kwenye *crasher*. Wanachukua moja kwa moja, wanapakia kwenye malori, wanapeleka moja kwa moja nchi za nje. Ule tayari unakuwa siyo mchanga peke yake, ni mchanga ulio na *concentration* ya dhahabu na bahati mbaya wanaousafirisha ni Watanzania!

Mheshimiwa Spika, hivi hata ingekuwa wewe ndiye unayesafirisha, wamechukua pale kwenye *pit* ambapo kuna *concentration* kubwa ya dhahabu, hauna nyongo? Wewe ni Mtume? Nikasema hapa, muwaondoe mliowashitaki, muwashitaki wachimbaji wakubwa, maana hao ndio wa kwanza ambao wametuibia……!

*(Hapa kengele ya pili ililia)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, Asante! Kengele ya pili hiyo. Nadhani unaunga mkono hoja ila unaomba marekebisho!

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nitaunga kwenye vifungu!

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nataka kuipongeza Wizara hasa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote. Hakika katika Bunge hili, hotuba iliyokuwa fupi sana kuliko zote ni hotuba ya Nishati na Madini, lakini imejaa sana! Kwa hiyo, kazi ni nzuri! Pili, naipongeza Serikali kumteua Alhaj Idris Rashid kuwa Mtendaji Mkuu wa

*TANESCO*. Waswahili wangesema, "*TANESCO* imepata dereva ajuaye, gari sasa itaenda mbio". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuishukuru Wizara ya Nishati. Kwa kweli Serikali nzima ya Awamu ya Nne kwa sababu sasa nguzo za umeme na nyaya za umeme zimeishafika Utete, nyumbani kwangu, Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji. Shukrani hizi zinatoka katika moyo wangu kwa sababu yako mambo yaliyonitokea mimi. Nyumba yangu nusu iliungua moto kutokana na kutumia petroli katika jenereta. Kuna watu wengine wengi wameumizwa na suala hili la ukosefu wa umeme. Kuja umeme kwa kweli ni jambo kubwa, na sisi sasa televisheni zetu zitawaka, friji zitatoa maji baridi na viwanda vidogo vidogo na ujasiriamali vitaendelea.

Mheshimiwa Spika, bada ya kusema hayo, baada ya kusikia kilio cha watu wengi ambao walikuwa wamekwishapelekewa nguzo, lakini umeme wenyewe haukwenda, mimi naomba Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha atuambie tu, ule umeme pale Utete utawashwa lini ili na sisi tusherehekee? Vilevile suala la bahati mbaya, umeme huu unatoka Songosongo, kuna vijiji unapitia, mathalani: kijiji cha Chiwanga, Chumbi, Nyamwage, Utunge, Nyanda Katundu na Kindwitwi, kabla hujafika Utete. Ninaomba kwa kuwa safari hii bahati mbaya hawamo katika programu, mradi ujao wa umeme vijijini, vijiji hivi vifikiriwe kwa sababu viko njiani. Pili, wananchi wa vijiji hivi ndio wanaolinda Bomba la Gesi kutoka Kilwa kuja Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, tumepata bahati ya uwekezaji katika kilimo cha pamba pale Mkongo, Rufiji, na mwekezaji analima hekta 40,000 za pamba na kaahidi kujenga jenereta na inajengwa. Kijiji hiki cha Mkongo kina kilomita 30 kutoka Ikwiriri ambako kuna umeme tayari. Tunaomba Serikali ipeleke umeme katika kijiji cha Mkongo kwa sababu operesheni za kusindika pamba au kuchagua pamba kutoka katika hekta 40,000, italipa gharama yote ya operesheni ya *TANESCO* kwa kuwapa umeme watu wa Wilaya nzima katika njia nzima inayopita gesi kutoka Songo Songo kuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ukienda mbele kidogo pale Mkongo, kilomita kama 80 kuna kijiji kinaitwa Mloka. Kijiji cha Mloka ndio kiini cha utalii kule Rufiji maana kipo pembeni mwa Mbuga za *Selous*. Usiku pana mambo pale mazuri tu, nawakaribisha. Lakini hatuna umeme. Kwa hiyo, kama umeme wa Songosongo ukishafika Ikwiriri na Ikwiriri ina jenereta mbili, tunaiomba sana Serikali ipeleke jereta moja kule Mloka ili shughuli za Utalii zipanuke. Ninasema hivi kwa vile kuna hoteli chache za kitalii. Umeme utatumika kule, *TANESCO* haitapata hasara hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme machache kuhusiana na shida zilizoletwa na upelekeji umeme Rufiji kwamba: mali za watu zimekatwa, mashamba, miti, mazao, mpaka leo fidia haijalipwa. Hivi sasa nazungumza, nimepigiwa simu, kuna matatizo, njia ya umeme kutoka Ikwiriri kwenda Kibiti, wananchi wamezuia kwa sababu hawajapata fidia ya mazao yao. Kama ukitoka pale unakwenda Mwanankupuka, kabla hujafika Kibiti, napo vilevile wanazuia, wanataka fidia zilipwe. Kwa hiyo, naiomba Serikali yetu na wadau wake *TANESCO* pamoja na *Songas* wafanye hima kuwalipa hawa wananchi nao wapate "Mkukuta" wao. Kwa kweli, itakuwa si jambo la busara kwa nchi yenye uwezo mkubwa kuwaonea wale wachache ambao mazao yao ndio msingi wao wa kupata

fedha za matumizi. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wakati anamalizia, aseme hii fidia kwa njia za umeme kule Rufiji italipwa lini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba sana, Mheshimiwa Waziri na Serikali nzima ikubali tu kwamba *Rural Electrification* haitakwenda kwa umeme wa gridi, lakini umeme wa *solar*. Wachina wamefanya hivyo na kila mtu amepata faida ya kuwa katika mwanga. Tunaomba mpunguze kodi zote za *solar appliances*, halafu muwawezeshe wajasiriamali kwa makusudi, watengeneze vifaa hivi kwa wingi ili bei yake ishuke na wananchi wengi waweze kutumia. Hiyo ndiyo njia tu itakayoweza kutusaidia katika programu ya umeme vijiji.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa mchango wangu ni kwamba naiomba Serikali ikubali kwamba uchimbaji wa madini umeanzishwa na Shirika la *STAMICO*. *STAMICO* imepigwa mateke, imefanywa hivi, vile! Lakini sasa wakati umefika tunaona lazima *STAMICO* irudishiwe nafasi yake, iwezeshwe. Kwa nini? Kwa sababu hivi leo, taaluma ya madini sisi hatuna, tuko ofisini, lakini hawa *STAMICO* wanaijua, wanaweza kutuambia tathmini, wanaweza kuratibu na vilevile kuangalia tunadanganywa au vipi! *STAMICO* inaweza vilevile kununua mitambo mikubwa ikiwezeshwa na ikawakodisha wachimbaji wadogo wadogo na huu utakuwa ukombozi mkubwa katika nchi yetu. *STAMICO* inaweza pia ikasimamia usafirishaji wa madini yote kabla hayajapelekwa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Lakini Waziri aniambie lini umeme utawashwa pale Utete. Asante sana! *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kupata nafasi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza, naanza kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika kukabiliana na matatizo makubwa na ya muda mrefu ambayo yamekuwepo kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa mfano mmoja dhahiri kwamba kwa zaidi ya miaka 11, kumekuwepo na utata kuhusu hatima ya kijiji cha Kakola ambacho kiko pembezoni mwa Mgodi wa Bulyankhulu. Kijiji hiki toka mwaka 1996 kimekuwa katika matatizo ya kutokueleweka kama kitakuwepo au hapana baada ya eneo hilo la Kijiji kutolewa miliki kwa mmiliki wa mgodi. Lakini kwa kasi ya ajabu, Waziri na Naibu wake wametusaidia na hasa mimi mwenyewe ambaye nimekuwa kila wakati nikiwaulizia jambo hilo kwamba baadaye wameweza kukubaliana na hao wenye mgodi kuliacha eneo hilo la kijiji na hivyo hicho kijiji kitakuwepo. Nawashukuru sana na kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na pongezi hizo, napenda niwakumbushe na hasa Mheshimiwa Waziri, makubaliano yaliyofanyika wakati wa ule mkutano uliohusu kupatikana kwa kijiji cha Kakola. Moja ya hoja kubwa iliyojitokeza, ni maeneo ya kufanyia kazi wachimbaji wadogo wadogo. Kakola ni eneo ambalo ni la wachimbaji na wengi wamekuwepo pale baada ya kuwa *re-located* kutoka eneo ambalo ni la mgodi kwa

sasa, na wengine wametoka maeneo mbali ya nchi yetu, hawana shughuli nyingine yoyote. Toka miaka hiyo ya 1995/1996 wamekuwa hawana eneo la kufanyia kazi. Lakini kwa bahati mbaya karibu maeneo yote ya Wilaya ya Kahama ambayo yana dalili za kuwepo madini, yametolewa leseni kwa kampuni kubwa kubwa kwa ajii ya kufanya utafiti kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamelalamika kwamba leseni hizi zinapotolewa kwa makampuni makubwa kufanya utafiti, wachimbaji wadogo wadogo hawapewi nafasi yoyote ya kufanya shughuli zao na hili limekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyoahidi wakati ule, naomba *process* ya ku-*negotiate* ifanyike kwa sababu maeneo mengi yanamilikiwa na kampuni kubwa. *Process* ya ku-*negotiate* na kuwaomba hao wenye leseni wayaachie maeneo hayo ili yatengwe maalumu kwa wachimbaji wadogo wadogo, iongezewe kasi. Nasema hivyo kwa sababu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 15, kwa kweli taarifa ambayo imetolewa imetushitua kidogo. Watu wa Kahama na wengine wamenipigia simu kwa kuonyesha manung'uniko yao hasa kutoka sehemu hiyo ya Kakola ninayoizungumzia.

Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mchakato huu umepiga hatua kubwa kwenye Wilaya ya Geita na Tarime, lakini Kahama bado haujaanza. Ukiangalia matatizo ya Kahama au Bulyankhulu yamekuwepo kabla ya hayo maeneo. Walichokiuliza watu hawa ambacho hata mimi mwenyewe kilinikera moyoni ni kwamba maeneo haya ya Geita na Tarime yamekuwa na vurugu. Tarime wao wanajulikana wamekuwa ni walalamishi sana na sehemu kubwa ya madai yao wamekuwa wakidai kwa nguvu. Lakini sisi Kahama hatuna historia hiyo. Sasa sidhani kama Wizara inataka hii iwe ndiyo *Presidency*. Utaratibu sasa wa kuwafanya watu waombe wanachokita naomba sana wana Kahama ni wapole, ni wasikivu ni watiifu kwa Serikali yao. Tusiwafikishe mahali ambapo watapoteza subira wakawa kama hawa ambao wameanza kuonyeshewa mfano kwamba wao wamepewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie pia kuhusu taarifa na matatizo ambayo yapo kuhusu mapato yatokanayo na madini. Kuna taarifa nyingi ambazo zinaonyesha mapato ambayo Serikali inapata kutokana na madini ni kidogo. Kwanza, hivi juzi Gavana wa Benki Kuu katika mkutano wake na vyombo vya habari, katika maeneo ambayo alionyesha dhahiri kwamba yana matatizo katika kuchangia pato la taifa ni pamoja na Maliasili na madini na kwa bahati mbaya akasema kwamba tunakuwa omba omba kwa sababu hatusimamii vizuri rasilimali zetu. Wengi tukizungumza nao kuhusu pato la madini hasa wanaopigia upatu eneo hili wanasema kwamba madini yanatusaidia sana hasa wakilenga kipengele kile cha *balance of payment* kwamba kuna *export* kubwa. Kwa hiyo, inasaidia ku-*balance* vitabu vyetu vya *international trade.*

Mheshimiwa Spika, lakini watalaamu wetu walitoa tahadhari, ukiangalia Gazeti la Rai la tarehe 14 – 20 walitoa tahadhari kwa Mheshimiwa Waziri, wakisema kwamba Serikali itaweza kupambana tu na matatizo yaliyopo kwa sasa kwa kuongeza nguvu kwenye sekta ya kilimo na wakasema wazi kwamba mauzo ya dhahabu na samaki

hayainui uchumi. Msinibishie mimi, muwabishie wao na taarifa hizi zimekuwa zikitolewa kila wakati na wao wanavyosema hivyo wamefanya utafiti.

Lakini pia si watalaamu hao tu wapo wengi pia ambao wamekuwa wakionyesha wasiwasi wao na mmoja wao ni pamoja na taarifa ya wakaguzi wa *Alex Stewart.* Mnaijua vizuri sana, upungufu uliopo, kuna mapungufu mkubwa wa *record keeping,* kuna upungufu mkubwa wa *accounting for the expenditure* zinazokuwa zimetumika kwenye shughuli hizi za uendeshaji wa miradi ya migodi mikubwa. Kwa bahati mbaya sisi Watanzania kwa sababu hatuna *access* ya kuingia kwenye vitabu vile kwa sababu migodi hii inamilikiwa kwa asilimia 100 na wageni au watu wa nje, tunakuwa hatuna nafasi ya kuweza ku-*confirm* ni kwa kiasi gani taarifa tunazopewa zinakuwa sahihi. Kwa hiyo, inabaki sisi raia wa kawaida kuamini kwamba pengine kuna matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna taarifa zenye utata ambazo zimekuwa zikitolewa na kampuni zenyewe za madini. Pamoja na kwamba tumekuwa tuki-*distribute* taarifa za intaneti lakini kuna taarifa moja ilitolewa kwenye vyombo vya habari tarehe 26 Julai, 2006 ikielezea mgodi wa Tulawaka ambao unamilikiwa kwa asilimia 30 na kampuni *M.D.N. Northern Mining*. Wanasema kwamba makisio yao ya kupata faida yalizidi kiasi walichotegemea kwa ile *quarter* ya pili ya mwaka huo. Walitegemea kupata *operating profit* ya dola milioni tano lakini walipata dola milioni 15. Taarifa hizi walizitoa kwa ajili ya *potential shareholders* wao kuwachangisha huku jamani mambo ni manono kweli kweli!

Katika mgawanyo wa hiyo *operating profit* kampuni ya *M. D. N.* pamoja na Kampuni ya Pangea ziligawanywa asilimia 30 kwa 70 na kampuni hiyo ya *M.D.N.* ikatumia hiyo asilimia 30 yake ya hizo dola milioni 15 kwa ajili ya kupunguzia deni lake kwa watu wake wa nje. Sasa hapa unajiuliza kiuhasibu *operating profit* ni kabla ya kuondoa *amortization* ya *capitalized expenditure. Is not a profit available for shareholders and is not a profit* ambayo unaweza ukaitumia kuweza kulipa madeni lakini wao wanaitumia *which impliedly* inayoonyesha kwamba hii ni faida.

Mheshimiwa Spika, lakini pia pamoja na ripoti za taarifa za faida hiyo kumekuwepo pia *contradiction* kwa suala zima la kifusi. Kifusi kimezungumziwa na Mheshimiwa Selelii. Sasa hivi tunazungumza kwanza *copper concentrate* maarufu kama mchanga wa dhahabu. Taarifa za Kampuni ya *Bulyanhulu Gold Mine* zinasema kwamba hawawezi wakachejua dhahabu inayokuwa imebaki kwenye kifusi kile na hivyo wanalazimika kusafirisha nje ya nchi. Hili ndilo limekuwa jibu la Serikali muda wote na hili ndilo limekuwa jibu ambalo hata Mheshimiwa Naibu Waziri alilitoa juzi hapa wakati akijibu swali la Mheshimiwa Mbunge mmoja tarehe 6/7/2007. Cha kusikitisha ni kwamba kwanza tuelewe kampuni *Bulyanhulu Gold Mine* wanatumia utalaamu wa kisasa sana katika kuchejua dhahabu kwenye mgodi wao. Katika viwango vya kawaida haiwezekani mtu wa kawaida wa kijijini akaweza ku- *extract gold* kutoka kwenye *copper concentrate*.

Lakini kumekuwa na taarifa ambazo tunazielewa na kuzisikia kwamba watu wanaiba kifusi hiki na wanaweza kutoa dhahabu. Sasa unaweza kujiuliza hivi kweli kama *Barick* na mitambo yao na *computerization* yao wameshindwa, hivi wanazidiwa na wanavijiji kuweza ku-*attract gold? There is a problem* na ningependa sana Serikali ielewe kwa hizi ni dalili kwamba kuna tatizo. Kwa hiyo, tujaribu kuimarisha kuangalia usimamizi wetu wa rasilimali zetu hizi kama alivyosema Mheshimiwa Selelii, taarifa hizo ni mimi nimezisikia wanachokifanya, kwa sababu pia tukumbuke kuna Watanzania wanaofanya kazi kule mgodini, wanatoa taarifa wanasema kwamba kinachofanyika ni kwamba kifusi kile sicho ambacho kinakuwa kimepita kwenye *crasher*, kuna kifusi kingine kina-*sneak* halafu kinatolewa kwenda kwenye makotena moja kwa moja. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iimarishe usimamizi kwenye sekta hii. Tukumbuke kwamba njia pekee ya kuimarisha sekta hii ni kuhakikisha kwamba Watanzania tunakuwa na umiliki katika hii migodi. Naomba nikumbushe Serikali kwenye ahadi ambazo tulizitoa wakati wa kuomba kura kwenye ibara ya 39 Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kifungu G kinasema kupitia upya Sera ya Madini na (1) na (2) kinazungumzia ili kutoa ushiriki wa Serikali na wananchi katika umiliki wa migodi mikubwa kwa utaratibu wa *equate participation* tukishakuwa na utaratibu huu kwa namna yoyote inayowezekana maana yake ni kwamba Watanzania watakuwa na hisa, Watanzania wataingia kwenye bodi, wakishaingia kwenye bodi watakuwa na uwezo wa kuchagua mkaguzi, watakuwa na uwezo wa ku-*determine* au kusema *accounting policy* inafanyika namna gani. Bila kufanyika hivyo mgodi unamilikiwa na asilimia 100 na mtu wa nje hatuna uwezo wa kuweza kuingia ku-*check* vitabu kama viko sahihi au laa.

Kwa maana hiyo, naiomba Serikali isimamie vizuri na mapema iwezekanavyo iweze kutekeleza hiki kipengele cha Ilani yetu. Watanzania tupate umiliki kwenye migodi na kwa sababu hili eneo lina malalamiko ya wananchi, naomba Serikali isikubali tena au isiendelee kama alivyosema Mheshimiwa Bujiku Sakila, Madini haya ni kwa ajili yetu na vizazi vijavyo. Tusiende ku-*encourage investment* kwenye eneo hili wakati bado tuna matatizo. Na *experience* ambayo tumekuwa nayo kwa miaka kumi iliyopita imeonyesha kwamba tunachoambulia ni makelele, manung'uniko na *public discontent*. Sasa hili linamomonyoa sana heshima na matumaini makubwa kwa wananchi kwa Serikali yao na Chama kitukufu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia kuhusu umeme. Vijiji vingi vya Kahama havina umeme. Kuna umeme uko pale Ilogi, kwa muda mrefu sisi wananchi wa Kahama na wa Bukombe tumekuwa tukiomba kwamba umeme unaokwenda Bukombe u-*energize* pia baadhi ya vijiji ambavyo viko jimbo la Msalala. Tumesema *route* ya umeme ipitie Runguya, ipite Segese halafu ipite Itobo halafu ikaingilie Kusini mwa Bukombe kwenye sehemu inayoitwa Kanegele Gerezani halafu ndiyo iende Bushirombo. Haya ndiyo maombi ya wananchi wa Kahama na ndiyo maombi ambayo pia Mheshimiwa Luhahula wakati anachangia alisema. Na tumekuwa tukiwasiliana na Serikali kila wakati, upembuzi yakinifu uliofanyika unaonyesha *route* hii na *route* nyingine ya kupita Bukoli ambayo sehemu kubwa inapita porini gharama

yake karibu inalingana. Sasa tunaomba kuliko umeme upite porini, upite kwenye vijiji hivi ili watu hawa nao pia waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, ili kupambana na tatizo la kuongezeka kwa bei ya mafuta kiholela naiomba pia Serikali iiwezeshe *TPDC* kuagiza mafuta. Hili limezungumziwa na wengine na mimi naomba nilisisitize tu. Lakini pia katika kufanya hivyo Serikali iisaidie *TPDC* ili iweze kuagiza mafuta, itavyoweza kuagiza mafuta bei ya mafuta kwenye soko itakuwa angalau *stable*. Bila hivyo huwezi ukamlazimisha mtu ashushe bei wakati yeye ameagiza kwa gharama kubwa, atakuambia unavyoniambia niuze kwa gharama ya shilingi 1450 *the minimum cost* niliyo-*incur* ni shilingi 1400 kwa sababu meli yangu ilikwama baharini kwa wiki mbili, utamlazishaje auze kwa bei hiyo? *We can only do that* kama tutakuwa na hiki chombo chetu ambacho kitakuwa kinaagiza mafuta na kuyauza kwa bei ambayo kweli inaleta tija kwa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali ilete sheria Bungeni ili kuondoa ukiritimba wa *TANESCO*. Vyombo au vyama vingine wawekezaji wanaweza kusambaza umeme vijijini kwa *solar energy* na vyombo vingine waweze kufanya hivyo, kwa sasa haiwezekani kwa sababu ambaye amepewa *exclusive right* ni *TANESCO*. Bila hivyo tutaendelea ku-*energize* vijiji vyetu kwa gharama kubwa na hatutaweza kuvifikia kwa sababu uwezo wa *TANESCO* ni mdogo. Tubadilishe sheria, turuhusu watu angalau wa-*participate* kwenye *remote areas* ambazo haziwezi zikafikiwa na gridi ya taifa kwa siku za karibuni. Kwa kumalizia ningependa kuunga mkono ombi la Mheshimiwa Bujiku kwamba umeme wa kutoka Ngudu kwenda Malya uharakishe. Huko wakwe zangu wanahangaika sana pia wana giza naomba wawahishiwe umeme. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi vile vile kama Mheshimiwa Bujiku Sakila. Tulikuwa na wasiwasi kutoka na orodha ambayo ilikuwa imetolewa kwamba labda hatutaweza kufikiwa lakini namshukuru Mwenyezi Mungu na pia wazungumzaji ambao wamezungumza wakahakikisha kwamba wanaweka nafasi kwa wengine ambao tumeomba kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutambua hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini ambayo imesomwa hapa siku Ijumaa na Waziri Nazir Karamagi. Vilevile napenda kutambua na kupongeza kwa dhati kabisa Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mnyaa katika Wizara ya Nishati na Madini. Kwa kweli nilifurahishwa zaidi na vipengele ambavyo alieleza na hasa hasa mahitaji yetu ya umeme itakapofika mwaka 2020 maana yake tuna *Min Tiger Plan* na naamini kabisa kwamba Serikali itaweza kuona hilo na hesabu ambazo amezipiga kwa sababu yeye ni mtaalamu na kuweza kulitekeleza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ambalo ningependa kulizungumzia ni suala dogo tu la takwimu ambalo nilikuwa nimechangia kwa maandishi lakini napenda lifahamike Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake ukurasa wa 5 ibara ya 8 amesema kwamba sekta ya Nishati ya umeme mwaka 2006 ilikua kwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie vizuri takwimu zake kwa sababu kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2006 na bahati nzuri mimi Waziri Kivuli wa Uchumi, kwa hiyo takwimu zinakuwa katika vidole, sekta hii ya umeme ilikua kwa asilimia *negative* 2.5 hivyo haikukua kwa asilimia 3.3. Kwa hiyo, naomba watu wa Wizara Nishati na Madini, waweze kuangalia. Wakitaka kuthibitisha waende ukurasa wa pili wa kitabu cha uchumi ibara ya saba watakuta takwimu sahihi za hali ya uchumi. (*Makofi*)

Pili, katika suala hilo la takwimu katika taarifa ambayo Wizara imeleta taarifa na takwimu muhimu sekta za Nishati na Madini Julai, 2007 ukurasa wa 33 wanazungumzia migodi mikubwa ya madini iliyopo nchini. Taarifa hii pia ina makosa mengi tu kwa sababu tunavyofahamu sasa kampuni ya *Barick* inamiliki jumla ya migodi 4 na hapa *Barick* haionekani kabisa na bahati mbaya ni kwama hata *North Mara Gold Mine* ambayo ilikuwa ya *Precadom* wameshawauzia *Barick* na Wizara imeshindwa kurekebisha hayo. Kwa hiyo, naomba hiyo irekebishwe kwa sababu takwimu za Wizara ya Nishati na Madini zinafuatiliwa kwa karibu sana duniani kote. Kwa taarifa yako tu jana nilikuwa nasoma katika Gazeti la *Wall Street Journal* nikakuta mijadala yote ambayo inaendelea Bungeni ya Nishati na Madini wameirekodi kwa sababu nadhani ya kwamba tuna wawekezaji wakubwa sana ambao wapo katika sekta hii. *(Makofi)*

Suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni suala la *production sharing agreement* ambayo ina-*negotiate*. Sasa kati ya *Tulo Oil* ya *Ireland* na *TPDC*, Serikali imetoa taarifa hii katika takwimu ambazo wamezitoa. Lakini katika ramani ambayo imeonyesha, wameonyesha kwamba kuanzia mpaka wa Burundi na Tanzania katika kijiji cha Kagunga mpaka Mji wa Kigoma mpaka Ujiji kuelekea katika Jimbo la Kigoma Kusini ni eneo ambalo hawa watu wa Tulo wameomba kwa ajili ya kufanya uchunguzi kama kuna mafuta.

Sasa tulikuwa tunaomba hii ramani iweze kuwa wazi zaidi tuweze kujua, kwa sababu inawezekana kabisa kwamba tukajikuta mji wote wa Kigoma uko *under exploration* na baadaye inaweza ikapelekea mambo ya watu kuhamishwa na kitu kama hicho. Kwa hiyo, nilikuwa naomba *details* hizi ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo nataka kulizungumzia ni suala la *review* ya mikataba ya madini. Mheshimiwa Rais, tarehe 30 Desemba, mwaka 2005 aliliahidi Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Awamu ya Nne, itafanya mapitio ya mikataba yote ya madini na Kamati ikawa imeundwa chini ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Laurence Masha, ikakamilisha kazi yake na ikaundwa Kamati ya kufanya mawasiliano na hayo makampuni ya madini yaani *negotiation team* ambayo inaendelea na kazi yake mpaka sasa. Toka mwezi Septemba, 2006 kwa maana ya kupitia mikataba yote ya madini na kuweza kuona ni jinsi gani ambavyo taifa letu linaweza likafaidika na mikataba.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha ni kwamba mwaka huu Serikali imetia sahihi mkataba mpya wa madini na kampuni ya *Barick* ambayo inamiliki Mgodi wa

Buzwagi kinyume kabisa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kinyume kabisa na taratibu ambazo zinaendelea sasa hivi. Kinachosikitisha ni kwamba mkataba huu umesainiwa na Waziri wa sasa wa Nisahti na Madini, kwa kutumia mikataba ya zamani. Kwa maana hiyo ni kwamba badala ya Waziri kusubiri Mikataba *review* zake ziishe ili mkataba mpya utakaposainiwa uwe na maslahi ya taifa. Waziri akaenda *ahead* tena, wala hakusainia hapa nyumbani, akawaita *Barick London* wakasaini mkataba *London* na hatujui ni kwa maslahi ya nani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunahitaji maelezo ya kina kabisa ili tuweze kujua kwa nini mkataba mpya na Kampuni ya *Barick* umesainiwa wakati bado taifa linaendelea kupitia mikataba ya madini? Kwa nini Mkataba huu umekwenda kusainiwa *London* na haukusaniwa Dar es Salaam kama jinsi ambavyo mikataba mingine yote imesainiwa? Vitu kama hivyo ndivyo huwa vyanzo vya rushwa, hivyo ni vema Serikali iweze kutoa taarifa ya kueleweka tuweze kufahamu na hizo *terms* za hiyo Mikataba mipya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili la *review* ya mikataba kuna suala ambalo limekuwa likijadiliwa sana. Suala la asilimia 15 *additional capital allowance on re-deemed capital expenditure* kwa kampuni ya madini. Kipengele hiki kilikuwa kwenye sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 1975 kikaendelea kuwepo kwenye sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004. Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini inatuambia kwamba kipengele hiki kimeondolewa. Lakini tunafahamu wenye mamlaka ya kuondoa vipengele vya sheria ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Lakini hii tena bila woga kabisa katika taarifa mbalimbali, Wizara inaeleza kwamba tumeondoa kipengele hiki. Sasa kwa mamlaka ya nani? Bunge lilikaa lini na kufanya *amendment* ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 ili kuweza kuiruhusu Serikali iweze kuondoa kipengele hiki? Mimi sina tatizo kuondolewa kwa kipengele kwa sababu itatusaidia tuanze kupata kodi ya mapato mapema zaidi lakini tatizo langu ni heshima ya Bunge. Siku zote tunazungumza kwamba ni lazima Bunge liheshimiwa, *executive* hawana *powers* za kubadilisha sheria; za kufanya marekebisho ya sheria bila Bunge kuweza kutoa baraza zake. Kwa hiyo, naomba Waziri pia anipatie maelezo tuweze kujua kwa nini na kwa taratibu zipi sheria hii imebadilishwa na kama wamebadilisha bila baraka ya Bunge ni lazima tushauri Kamati ya Bunge inayohusiana na masuala ya haki za Bunge, iweze kukaa kuwaita wahusika Mawaziri, Kamishna wa Madini na kadhalika, waweze kutoa maelezo kwa nini wanaingilia uhuru wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wazungumzaji wengi wanazungumzia suala hili na ni kilio cha wananchi na mzungumzaji aliyepita amezungumzia kwamba ipo kwenye Ilani ya chama chake, kwamba ni lazima sasa umefikia wakati Serikali iwe na hisa kwenye makampuni kwenye migodi mbalimbali. Lakini hili siyo jambo jipya. Kwa mfano, katika Mgodi wa Bulyanhulu, Serikali ilikuwa na hisa ya asilimia 15, lakini katika hali ya kushangaza kabisa Serikali imeuza hisa zake za mgodi wa Bulyanhulu kwa Kampuni ya *Barick*, baada ya Kampuni ya *Barick* kununua hisa zake kutoka Kampuni *Satons* ya *Canada* vile vile ambayo ilikuwa imilikiwa na Bwana *Sinclair.*

Suala linalokuja ni kwamba tulikuwa tuna hisa kwenye baadhi ya migodi, tumeuza hisa zetu. Sasa hivi tunazungumzia tena kuwa hisa tena, ni kwa nini? Kwa hiyo, ina maana kwamba tunarudi nyuma? Zamani tulikuwa tuna hisa tumeziuza tena bahati mbaya nasikia hisa hizo tumeuza kwa gharama ndogo.

Zamani hisa zetu zilikuwepo katika mgodi wa Bulyanhulu ni takriban trilioni 1.1 lakini tumeuza hisa hizi kwa jumla ya dola milioni 5 ambazo ni sawa sawa na shilingi bilioni 5 tu yaani ni asilimia moja tu thamani halisi ya hisa ambazo tulikuwa nazo Bulyanhulu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali itupatie maelezo ya kina kabisa kuhusiana ni kwa nini hisa hizi ziliuzwa na kuna mipango gani ya kuhakikisha kwamba hisa hizo zinarejea. Tunakuwa kama nchi nyingine ambapo Serikali za nchi zina hisa mbalimbali katika migodi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tu kwamba madini ni moja ya sekta nyeti katika nchi yetu, tuna migodi 9 sasa hivi ya madini, tuna rasilimali kubwa sana ya madini ambayo tukiitumia vizuri nchi yetu itakwenda mbele sana. Mchango wa sekta ya madini katika uchumi bado ni mdogo ingawa sekta yenyewe inakua.

Kuna tatizo ambalo limetokea sasa hivi kwamba kampuni moja inakuwa kama ndiyo *giant* katika sekta nzima ya madini. Tuna jumla ya migodi 7 ya dhahabu, katika hiyo, migodi minne inamilikiwa na kampuni moja, Kampuni ya *Barick* na inaendelea kununua makampuni mengine na kampuni hii imeonekana kwamba ina nguvu sana, ina *influence* sana katika maeneo mbalimbali ya Serikali ya Wizara na kadhalika. Ni kampuni ambayo ina *influence* sana katika maamuzi mbalimbali ya kisera yanayohusiana na masuala ya madini.

Kwa hiyo, naiomba Serikali iwe makini sana kuweza kuangalia, tusijukute tunakwenda kwenye *monopoly* ya kuwa na kampuni moja ambayo ita-*dictate* ni vitu gani ambavyo inataka tukajikuta kwamba sisi tunabakia kimashimo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa angalizo tu ni kwamba katika migodi minne ambayo kampuni ya *Barick* inamiliki ambayo thamani ya mali zilizoko ardhini ni *metric* tani 650 ya dhahabu. Wakiendelea kuzichimba kwa *rate* ambayo wanaichimba sasa hivi itatimia miaka 18 tu madini yote haya kuishi.

Kwa hiyo, kama tusipofanya *investment* za uhakika na tukapata mapato ya kutosha katika haya madiwani tukawekeza katika maeneo mengine ni kwamba baada ya miaka 18 tutabaki na mashimo matupu, tutabakia na historia na tutashindwa kukielezea kizazi kinachokuja maliasili ya nchi jinsi ilivyotumika.

Kwa hiyo, naomba Serikali iwe makini sana katika maamuzi yake na naomba nipate hayo majibu ya kwa nini tumesaini mkataba mpya wa madini wakati bado tunaendelea na *review* ya mkataba?

Kwa nini Serikali imebadilisha kipengele cha asilimia 15 katika *Income Tax Act* ya mwaka 2004 bila kupata baraka za Bunge na ni kwa nini tuliuza asilimia zetu 15 za

hisa za mgodi wa Bulyanhulu kwa thamani ndogo sana na nini tunaweza tukakifanya kuhakikisha kwamba tunakuwa na hisa katika migodi mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia wa takriban dakika sita hautuwezeshi kuendelea na mchangiaji yeyote. Kwa upande wangu sasa wachangiaji ndiyo tumefikia mwisho. Ninalo fundisho la siku ya miundombinu muda ulikuwa mfupi sana kwa Kamati ya Matumizi, ikaleta shida kidogo.

Kwa hiyo, leo saa 11.00 nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mpangilio ambao atakuwa amekubaliana na Mheshimiwa Waziri. Haki yake ni dakika 15, lakini akiongeza basi atachukua kutoka kwa zile dakika 60 za Mtoa Hoja. Atafuata Mheshimiwa Mtoa Hoja Waziri ambaye kwa saa moja, dakika 60 au zozote zitakazokuwa zimesalia itatufikisha saa 12.15, tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, kama nilivyosema kwa kuwa muda sasa hautoshi kuendelea, basi nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 6.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza watendaji wote wa Wizara na pia kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa waliyofanya na wanayofanya mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wengi wanahitaji umeme hasa vijijini na katika suala la kupanda kwa mafuta kuna waathiri hasa wananchi vijijini. Je, Serikali itaanza lini utaratibu wa kuanza kwa umeme wa *Biogas* ili tuepukane na mikakati ya muda mrefu sana? Naomba jibu kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, bila umeme wimbo wa kunusuru mazingira ni ndoto, bali tutafute ngoma tuanze kucheza, kama ilivyo desturi yetu Afrika.

Mheshimiwa Spika, nchi zilizoendelea zipo hapo kwa ajili ya kuwa na umeme, kwa sababu ya matumizi mbalimbali ya ufundi, majumbani, sayansi na teknolojia na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine wanapoongelea umeme ufike katika vijiji vyao, sisi wengine hatujui ni lini hata makao yetu makuu ya Wilaya yatapata umeme. Mfano, ahadi za kuleta umeme Mji Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Namanyere utaletwa lini?

Mheshimiwa Spika, umeme wa makaa ya mawe utafanyiwa kazi kwa ukamilifu lini? Achaneni na umeme wa maji ni umaskini na ubabaishaji maana mnategemea mvua isiyo na uhakika (Mungu).

Mheshimiwa Spika, madini yamejaa Nkasi, je utafiti ni kiwango gani kipo cha *ruby*, dhahabu na vito vyake utafanyika lini? Umeme Nkasi, Namanyere *town* tunaomba.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Naibu wake Mheshimiwa William Ngeleja, Katibu Mkuu Ndugu Arthur Mwakapugi na watendaji wote waliosaidia kufanikisha kuandaa vizuri hoja hii. Naunga mkono hoja kwa hali zote.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeamua kuandika mchango wangu kwa maeneo ambayo nitapenda Waziri anipatie maelezo ambayo wana Rukwa wanapenda kusikia majibu yake.

Mheshimiwa Spika, hali ya umeme kukatika katika kila mara kwenye gridi ya kutoka Mbala, Zambia umeanza kuwa ni kero, hali hii ilifikia hata mwezi uliopita Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alipokuwa Sumbawanga alijionea mwenyewe adha hii. Kwa nini hali hii tuiruhusu kuendelea? Maelezo tunayataka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali mbaya ilivyo kwa sasa, nini mipango ya *TANESCO* katika kuufungua Mkoa wa Rukwa na Kigoma kwa kuwa Gridi itakayotoka Tunduma, Sumbawanga, Mpanda hadi Kigoma ili ikakutane na ile inayotoka Uganda kupitia Mubukula, Bukoba. Nini angalizo la Serikali kuhusu gridi ya *Western Corridor*.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa uliwahi kufanyiwa utafiti wa mafuta katika Bonde la Rukwa *(Lake Rukwa Basin)* na mitambo ilifanya uchimbaji wa awali, lakini hatukuambiwa matokeo yake mpaka sasa. Hivi Serikali inasema nini kuhusiana na utafiti huo?

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuupatia Mkoa wa Rukwa mradi wa umeme nuru. Pamoja na hilo, tunaomba mitambo yake ianze kuingizwa kwa wingi na tuanzie kwenye zahanati zetu pamoja na shule za sekondari. Hii ni pamoja na kuiomba Serikali isaidie kututafutia mwekezaji wa uhakika kwa ajili ya makaa wa mawe wa Namwele. Tunaomba tujue kama Wizara inalifanyia nini suala hili ambalo ni la muhimu sana kwa kuokoa mazingira ambayo kwa Rukwa ni ya kufa na kupona.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini ni wa lazima sana na ni vizuri sana tukubali kutafuta njia nyingine za kuongeza mfuko wa umeme vijijini. Nashauri kuwa tusisubiri Serikali kuchangia toka Bajeti yake kila mwaka, bali tuanze kuwataka wadau wote

wanaotumia umeme popote walipo, wachangie kiasi fulani cha fedha kwa kila *unit* waitumiapo, hii ni kama mfuko mafuta unavyochangia ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wa madini wadogo wadogo wasiwe wanapendelewa wale tu wanaochimba dhahabu au almasi, wapo pia wanaochimba madini mengine kama *Gemstones, Rubijs*, *Emerlalds* na kadhalika ingefaa nao wapewe umuhimu wake. Hawa wapo Sumbawanga nao wasaidiwe, wapewe mikopo kwa vifaa vya kuwakomboa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanza udhibiti wa bei ya mafuta. Lakini tunaomba dawa ya kudumu iwe ni kuwa na mpango wa hifadhi ya mafuta chini ya uongozi wa *TPDC*. Bila kufanya hili, tutaendelea kuendeshwa na wafanyabiashara wengi nia mbaya ya kulivunja Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hivi nini azma ya Serikali kuhusu *IPTL*, mbona tangu miaka mitatu iliyopita Serikali ilikuwa na nia ya kuinunua *IPTL* lakini hatuelewi kitu gani kinazuia uamuzi huo kutekelezeka? Kwa kuwa mwekezaji wa mitambo hiyo ya *IPTL* ameonyesha kwa kupitia vyombo vya habari kuwa hataki kuuza *IPTL,* je, Serikali inaweza kuingilia suala hili kwa njia ya kidiplomasia?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote na tunawaunga mkono Mawaziri na watendaji wao.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, naomba kueleza toka awali kuwa naunga mkono hoja na hasa zaidi upande wa sekta ya nishati, hii imeonyesha maendeleo makubwa sana katika siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, upande wa nishati, Wizara imeleta maendeleo makubwa *Mnazi Bay*, Mtwara kwa kuwezesha kuchimba gesi asilia na kuzalisha umeme hasa kwa maeneo ya Mikoa ya Mtwara, Lindi na pengine Ruvuma nawapongeza Wizara kwa ushirikiano walionao na Kampuni ya *ARTUMAS* toka Canada katika utekelezaji na hatua nzuri waliyofikia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kumekuwepo na matatizo mengi yasiyo ya lazima katika kufikia mkataba wa kudumu *(Franchise Agreement)* ambao matokeo yake ni kutokamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kama mambo yote yangekuwa yamekwenda sawa, hivi sasa eneo lote la Mikoa ya Lindi na Mtwara yangekuwa yamepata umeme wa uhakika kuanzia mwishoni mwa Desemba 2006, mpaka leo kasi sio nzuri. Umeme unapatikana Mtwara Mjini na eneo la Mingoyo Nyangao. Bado Mji wa Lindi haupati umeme pamoja na Wilaya za Masasi, Nachingwea, Ruangwa, Newala na Tandahimba. Malalamiko katika Wilaya hizi ni makubwa, wananchi hawaelewi ni nini kinachotokea kwa nini wenzao wa Mtwara wanapata umeme na wao haieleweki watapata lini.

Mheshimiwa Spika, kinachocheleweshа zaidi ni umangimeza, malumbano baina ya watendaji. Inaelekea kila mmoja anaonyesha umwamba wake toka *TPDC*, *TANESCO*, *EWURA*, HAZINA na kadhalika. Nashukuru kwamba katika sakata hili Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu hawahusiki.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri awalazimishe watendaji hawa wakamilishe kutiliana sahihi kwa mkataba kati ya *ARTUMAS* na Wizara ili mradi wa kusambaza umeme kati ya Nyangao na Ndanda ukamilike. Hizi ni kilometa 36 ambazo zikiunganishwa basi Wilaya zote nilizozitaja zitapata umeme wa uhakika. Wananchi hawaelewi sakata linaloendelea Wizarani, wanachoona ni ucheleweshaji wa kutekeleza kila walichoahidiwa. Namwomba Waziri akamilishe mapema mno na sio kungoja mpaka mwisho wa mwaka wa fedha. Kazi iliyobaki ni kidogo tu, naomba ikamilike walau Septemba, 2007.

Mheshimiwa Spika, eneo la *Mnazi Bay* imegundulika gesi asilia yenye uwezo wa kuzalisha umeme *300 MW*. Kutokana na matatizo tuliyonayo ya dharura na muda mrefu, napendekeza Wizara ikamilishe maendeleo ya mradi huu ili tuunganishe kwenye Gridi ya Taifa kupitia Dar es Salaam ama Kidatu. Mradi huu mzuri utakaoondoa kabisa shida ya umeme nchini upewe kipaumbele cha pekee ili tuweze kujitegemea kinishati. Hapa inabidi tuamue upesi ili kazi hii isichukue muda mrefu kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALHAJ PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, ningeomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana na yenye kuleta matumaini kwa kuzingatia kuwa nishati ni vyenzo muhimu katika kumkomboa Mtanzania na kuleta maisha bora kwake. Naipongeza na kumshukuru sana pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kushirikiano anaonipa katika kutatua kero mbalimbali za Wilayani mwetu.

Mheshimiwa Waziri, nilianzisha mawasiliano na *TANESCO* na pia Wizara yako kuhusu miradi mikubwa miwili ya wawekezaji wanaokuja kumwekeza Wilayani kwetu Urambo hususan katika Jimbo la Urambo Magharibi. Huu ni mradi wa *Ginnery* na mradi wa *Bio-diesel* wa *Bio-ethanol* miradi yote hii italeta ajira nyingi sana katika eneo letu na kwa hiyo kusaidia katika utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara hii ni kwamba naomba sana Mheshimiwa Waziri muiweke katika mipango yenu ya utekelezaji ya mwaka huu hususani katika kuongeza nguvu za umeme (msongo) ili uwiane na mahitaji ya viwanda hivi. Ujenzi wa *Ginnery* umekwishaanza na ujenzi wa viwanda vya *Bio-diesel* na *Bio-ethanol* unatarajiwa kuanza Novemba, 2007. Tafadhali tusiwakatishe tamaa wawekezaji hawa na wananchi wa eneo hili ambalo ni aghalabu kupata wawekezaji hawa wamekuja kwa miujiza ya Mwenyezi Mungu tu.

Mheshimiwa Spika, narudia kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na timu yake yote wakiwemo watendaji wa Shirika letu la *TANESCO* wakiongozwa na Dr. Idris Rashid, nina matumaini makubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa shule ya sekondari ya Nkowe kule Ruangwa, Lindi walimu wao na wazazi walioijenga shule hii leo hii wanaomba wakusikie wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, ni lini watapata umeme pale shuleni kwao kutoka umbali wa mita kama 900 tu unapopita umeme. Kwa kweli ahadi za *TANESCO* Ruangwa na Lindi zinawanyong'onyesha kabisa, tafadhali wanaomba wakusikie.

Mheshimiwa Spika, kutoka Ruangwa Mjini hadi Mbekenyera ni kilomita tisa tu, huko kuna watu wengi, madini na sekondari ya kutegemewa wananchi walijiandaa kila kitu ikiwa ni pamoja na kung'oa mikorosho kupisha waya za umeme. Wako tayari kuchimba mashimo ya nguzo lakini ahadi kibao hadi sasa hamna kitu, sasa unsemaje?

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo gesi ya *Mnazi Bay* na umeme wa *ARTUMAS* uelekeao Ndanda hadi Masasi, je, ni lini au tufanye nini ili tupate *line* pale Nanganga ili wakazi wa Malolo, Mnacho, Nandagala hadi Muchenga nao wapate? Ni karibu sana kama kilomita 19 tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante na kazi njema.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Kwanza nichukue pia fursa kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Nazir Karamagi kwa hotuba yake nzuri yenye kuonyesha dhana nzima ya Nishati na Madini nchini mwetu. Aidha, nampongeza sana Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote waliomsaidia Mheshimiwa Waziri kufanikisha kazi hii nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pongezi za dhati kwa Serikali yetu na Chama cha Mapinduzi kwa kuvalia njuga (kuweka mikakati imara kabisa) ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 hasa kwa suala la nishati ya umeme vijijini. Moja ya rasilimali nyeti sana ya kuleta maendeleo ya wananchi wetu ni nishati ya umeme. Utekelezaji wa suala hili kwa ari, nguvu na kasi mpya ni mafanikio, kwanza ya wananchi na pili kwa Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme ni muhimu sana katika suala zima la kuondoa umaskini wa kipato na hata umaskini wa fikra. Nashauri Serikali na Wizara kuhakikisha nishati ya umeme inasambazwa haraka vijijini ili wajasiriamali hasa

waliochukua mikopo ya biashara waweze kuendesha biashara zao vijijini kwa ufanisi na kwa faida. Biashara nyingi za akinamama ni mama lishe na biashara hii hushamiri zaidi saa za jioni ambapo wananchi wengi wapo majumbani kwa mapumziko kama giza inaanza saa 1.30 au 2 usiku ni dhahiri biashara hizo zitaathirika.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu bali gharama za kufanya biashara kwa *(profit)* faida itakuwa ngumu bila umeme. Kwa hivyo, sambamba na uhimizaji *SACCOS* nchini, Serikali iharakishe usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, lazima tuelewe pia kwamba tuko kwenye dunia ya utandawazi ambayo tuna ushidani mkubwa wa masuala yote ya maendeleo. Wafanyabiashara wengi sasa hivi kutoka nchi zinazoendelea, wanatumia *internet* kufanya biashara na hii inarahisisha kazi. Kwa mfano, unaweza kutafuta soko la bidhaa unazozalisha kupitia *internet* unaweza hata kufanya makubalinao ya bei na hatimaye kusafirisha bidhaa hizo na kupata malipo bila kusafiri kwenda nje ya nchi kwa mfano tu. Kwa hivyo, naishauri Serikali kuzingatia huu ushindani ambao siyo tu itainua maisha ya wananchi wake kibiashara bali kuinua uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, *SACCOS* zetu sasa hivi zinaweka kumbukumbu za fedha kwa *manual system*. Lakini baada ya miaka 5 hadi 10 wakopaji watakuwa wengi na fedha zitakuwa nyingi kwenye mzunguko. Taasisi hizo zitahitaji kuweka kumbukumbu kwa kutumia *computer (computerised loan tracking)* bila umeme vijijini ama kwenye vituo vya *SACCOS* zetu kuweka kumbukumbu kwenye *computer* haitawezekana na hivyo *data* ambazo siyo sahihi zitapoteza imani ya wakopaji au upotevu wa fedha kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, nina taarifa kuwa Serikali ilitenga fedha za kufikisha umeme kwenye baadhi ya vijijini kwa siku nyingi na hii ni pamoja na kufikisha umeme kijiji cha Dongobeshi, Wilayani Mbulu. Nguvu zimewekwa kitambo, lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema nini kuhusu shirika la *TANESCO* ambalo licha ya Serikali kutengeneza fedha kijiji cha Dongobesh kupatiwa umeme siku nyingi kutopatiwa umeme hadi leo?

Pili, nishati ya *solar* ni rahisi na tayari wananchi vijijini wana uzoefu wa kutumia pale penye fursa. Serikali imeweka mikakati gani kuhusu *solar power* vijijini na hasa Mkoani Manyara ambako kuna fursa kubwa ya wananchi kufanya biashara? Narudia nawapongeza sana Wizara na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Waziri wa Nishati na Madini kwa kuwasilisha hoja yake hapa Bungeni kwa ufasaha mkubwa. Ni hotuba nzuri, inayotoa matumaini kwamba yale malengo yaliyo katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, yanaweza kufikiwa. Nishati ni kichocheo kikubwa cha maendeleo. Kutokana na

niliyoyabaini na kwa niaba ya wananchi wa Rungwe Mashariki, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mchango wangu utajikita katika suala moja tu, ukamilishaji wa miradi michache ambayo tayari ilikwishaanza miaka sita iliyopita na ambayo mpaka sasa haijakamilika kupelekea uharibifu wa nguzo, nyaya na vifaa vingine ambavyo ni ghali lakini vile vile ni hasara kwa *TANESCO* na Taifa. Kwa maana ya utangulizi mchango huu naurudia kwa mara ya nne au tano mfululizo ninapochangia kwa maandishi hoja ya Mawaziri wa Nishati na Madini katika miaka hiyo.

Miradi ninayoizungumzia ni ifuatayo na ipo katika jimbo la Rungwe Mashariki na inahusu umeme. Kwanza Kandete - Luteba nguzo zimesimikwa wananchi waliombwa na wakajitolea nguvu kazi kwa kuchimba mashimo na kusimamisha nguzo. Kwanza Kandete - Mpombo (Mwakaleli – Mpombo).

Pili, nguzo zilisimikwa miaka mitano iliyopita, tatu, Isange - Mbigili. Nguzo zilisimikwa miaka mitano iliyopita. Mbigili kuna mnara wa *mobitel* (*Tigo*) ambao hutumia jenereta ya mafuta. Mteja huyu mmoja tu anatosha kufidia gharama za kukamilisha mradi, mbali na mahitaji mengine, nne, Kandete - Matamba (Mwakaleli - Matamba) nguzo pia zimesimikwa takribani miaka mitano iliyopita, tano, msongo wa *Kv 33* toka Mbambo mpaka Ipinda. Utekelezaji wa mradi huu utafikia asilimia 70 ukaachwa. Nguzo zimesimikwa umbali wote wa kilomita saba, nyaya zimesambazwa kwa zaidi ya nusu umbali. Vikombe vimewekwa kwa zaidi ya robo ya umbali.

Kazi hii ilifanyika miaka mitano iliyopita. Mradi limeachwa bila kukamilika, nguzo zinaanguka, nyaya zinaibiwa. Wananchi wanamebaki wanashangaa, Mbunge wa Kyela amewahi kuuliza swali kuhusu mradi huu unaunganisha Wilaya ya Kyela na Wilaya ya Rungwe kwa *kv 33.* Akajibiwa zilihitaji shilingi milioni 25 tu na ahadi ikatolewa na Waziri wa Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wake ili ukamilike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, yote niliyotaja niliyataja vile vile mwaka 2006. Mchango wangu kuhusu haya uko katika ukurasa wa 106 - 109 ya Taarifa Rasmi ya Bunge *(Hansard)* ya mkutano wa nne, Kikao cha Ishirini na Nne, tarehe 18 Julai, 2006. Nashauri miradi iliyoanza, inayoendelea itekelezwe kwanza. Tuna imani kubwa na uongozi mpya wa *TANESCO* chini ya Dr. Idris Rashid. Naamini Dr. Rashid atazingatia niliyoyaelezea hapo juu.

Mheshimiwa Spika, nahitimisha kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, natanguliza shukurani zangu kwa Waziri na Naibu Waziri na wasaidizi wake ambao wanafanyakazi kimahiri. Vile vile nisiwe msemaji mkuu niende moja kwa moja katika kuchangia. Wananchi wanaiomba Serikali ya Awamu ya Nne, iweze kuwakumbuka katika awamu hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kabisa katika ziara ya Mheshimiwa Rais, aliwaambia wananchi hao kuwa wasiwe na wasiwasi, awamu hii ni ya wananchi wa Mkoa huo. Kigoma tukipata umeme Mkoa wetu unaweza kuwa na neema kwa sababu watapata viwanda vya kusindika samaki, viwanda vya kutengeneza *fuel* kutokana na michikichi iliyopo Mkoani Kigoma. Vile vile tutapata kiwanda cha kutengeneza mafuta ya kula, tutapata kiwanda cha kutengeneza sabuni na mengineyo kama vile mazulia.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ni lini itatuletea umeme? Ahsante.

**MHE. SEVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza Wizara hii kwa kazi yake nzuri pamoja nakupongeza. Nina mambo machache yanayonisumbua pamoja na wananchi wa Mkoa wa Kagera. Ni lini Serikali itatuonea huruma kuwa na sisi umeme wetu kuliko kutumia wa Uganda. Siyo kusema hatuna mito mikubwa tunayo isiyo kauka naomba Serikali itoe tamko ni lini tunafikiriwa.

Pili, umeme vijijini, kuna wananchi wengi wanapenda kuweka umeme na wengi wameshajiandaa, wameshafunga waya ndani, naomba Serikali inijibu ni kwa nini na nini kinachokwamisha na wanavyokwenda *TANESCO* hawapati majibu ya kuridhisha, naomba tena.

Kuhusu kilimo cha umwagiliaji naomba Serikali iweze kuona kilio cha wana Kagera ambao wana sehemu na ardhi nzuri sana yenye kustawisha kilimo hicho cha umwagiliaji.

Naomba Serikali kuhusu nishati mbadala, wananchi wapo wengi wanajitahidi sana kulinda nishati kwa mfano juzi Kamati tulienda Sabasaba, tumeona mambo mengi sana. Kuna mtu mmoja anaitwa Nachiket W. Potnis anatengeneza mkaa wa takataka mkaa mzuri sana. Wanajiita *Appropriate Rural Technology Institute* wanapatikana kwenye Ofisi zao Dar es Salaam, *Asia Street near Jamhuri Police Post* yaani nimewekwa maelezo kamili ili Serikali iwakumbuke ni watu muhimu.

Pili, kuhusu geti kuna mambo makubwa kwa wananchi mwekezaji mambo anayofanya siyo ya kibinadamu. Naomba Wizara yako ifike ione kijiji Nyurungusu Katoma wawezuia wananchi kulima kwenye mto wao wanakochota maji, wameweka sumu na kuwa kinachoendelea wanaripoti polisi kila siku hakuna msaada. Kwa hayo machache naomba majibu na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, usambazaji umeme Wilayani Mbulu. Mradi wa kupeleka umeme mji mdogo wa Dongobesh kutoka Bashnet (kilomita 20) ulioanza mapema mwaka huu. Utekelezaji wa mradi huu ni wa pole pole mno.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme kwenye mji mdogo wa Daudi kutoka Kituo cha Mbulu ulikuwa uanze kutekelezwa mwaka wa fedha 2006/2007 haukuanza. Mradi huu sasa utaanza lini? Nakumbusha ahadi ya Serikali ya kupeleke umeme katika miji midogo ya Maghang na Meretedu toka Itaydom (kilomita 15) na Tlawi – toka Mbulu (kilomita sita).

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Niwapongeze Waziri Mhrshimiwa Nazir Karamagi, Naibu Waziri, Mheshimiwa William Ngeleja, Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia kwenye baadhi yasehemu ya hotuba hii. Kuhusu nishati, kwa kuwa sera ya Chama cha Mapinduzi ni kuhakikisha kwamba Wilaya zote zitapata umeme wa uhakika na kwa kuwa hivi sasa kuna baadhi ya Wilaya hazina umeme wa uhakika kama vile Wilaya ya Urambo. Je, ni lini Wilaya ya Urambo itapata umeme wa uhakika katika kukamilisha azma ya Ilani hiyo, kwani tayari kuna nguzo zilizoanza kutandikwa njiani?

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Nzega imepata umeme wa uhakika na kwa kuwa Wilaya hiyo ina majimbo mawili ambayo ni Bukene ambayo inayo idadi kubwa ya wananchi ambao wana nyumba za kudumu na wanayo mazao ya biashara, je, ni lini Wilaya hiyo itapatikana umeme?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ofisi ya madini mikoani, ofisi hizi zitambuliwe na kutangazwa kwa wananchi ili wanapopata taarifa za madini au kutambua madini yalipo iwe rahisi kwao kupeleka taarifa hiyo, kukarabati ofisi zilizopo na zipewe vitendea kazi vya kisasa na hati za kumiliki maeneo kwa wachimbaji wadogo wadogo ziangaliwe upya ili haki hiyo wasipoteze na kuondoa mgongano na wawekezaji kwani wachimbaji hao hawana uwezo na kufuatilia hati hizo Makao Makuu. Hivyo watengenezewe ofisi za usajili kwenye maeneo ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira, kwa kuwa wachimbaji wakubwa huacha mashimo ambayo hayawezi kuzibwa kwa sababu mara tu wanapotoa mchanga huenda mahali pengine, je, Serikali/Wizara ina mpango gani wa kuziba mashimo hayo ili mazingira yaweze kuhifadhiwa, pia kuondoa hatari ya madimbwi ambayo kuna wakati mvua hujaza maji na kuhatarisha watoto wa maeneo hayo kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ushauri, wawekezaji washauriwe kurudisha udongo kwenye maeneo hayo kabla ya wao kusaini mikataba. Wanapochambua mchanga unaokwenda nje basi unaobaki urudi maeneo hayo yalitoa udongo/mchanga huo. Maafisa Madini wa Mkoa/Wilaya wahusishwe kikamilifu na kupewa taarifa ya kazi hiyo baada ya kuzibwa ili afanye ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyuo vya madini, taaluma hii itangazwe ili wanafunzi wengi waweze kujiunga kutokana na utandawazi wa uchimbaji madini ambao hivi sasa tumepata wawekezaji wengi na kuna aina nyingi za madini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, utafiti utengewe fedha za kutosha kwani bila utafiti madini hayatapatikana au kupoteza aina zingine za madini. Kwa mfano, *Tanzanite* iligunduliwa na wananchi ambao ni wazee wa zamani ni vema sasa uwe wa kisasa kutokana na sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, napongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Mchango wangu katika Wizara ya Nishati na Madini kwanza napongeza sana kwa ujenzi wa Kituo cha Kupoozea nguvu ya umeme cha Makambako, Njombe.

Ombi langu, naomba kukamilisha umeme wa Gridi ya Taifa kwa Kidugala na Wanging'ombe, niliahidiwa kabla ya mwezi Machi, 2007 na Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Pia, naomba umeme uwekwe kipaumbele uwekezaji wa nishati ya upepo pale Makambako kuna nguvu kubwa sana tungepata megawati nyingi kwa nguvu ya upepo. Utafiti umeshafanyika. Pia ufanyike utafiti wa kutosha wa madini katika Milima ya Kipengere na pale Kidugala na maeneo mengineyo katika Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya madini, Shirika letu la Madini la Taifa *(STAMICO)* naomba lipewe nguvu na kuboreshwa, pia wafanyakazi hasa wataalamu wa madini wazalendo watumike ipasavyo. Pia Chuo cha Madini Dodoma upande wa *Geology* watumike sana kwa upande wa kushauri Serikali na vijana wanaomaliza chuo waajiriwe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile shule za sekondari kwenye Jimbo langu la Njombe Magharibi tunaomba tuwekewe umeme wa Gridi ya Taifa kwenye nguzo za umeme ziko pale zimepita na sehemu zingine ziwekwe nguzo. Shule hizo ni Wanging'ombe – Kata ya Wangong'ombe Njombe, Kidugala – Kata ya Imalinyi – Njombe, *Mount Kipengere* – Njombe, Ilembula Selo – Njombe, Igwachanya Sekondari, Wanike Sekondari, Saja Sekondari – Njombe, Lududa Sekondari – Njombe na Maria Nyerere Sekondari – Njombe.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Nazir Karamagi, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara hii na taasisi zote chini ya Wizara hiyo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri sana. Pia nampongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Sasa nilete mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme vijijini Jimboni Karagwe, mwaka jana nilivyouliza swali la msingi kwamba ni lini vijiji vya Jimbo la Karagwe vitapatiwa umeme nilijibiwa kuwa upembuzi yakinifu tayari ulishakamilika na Serikali ilikuwa mbioni kupeleka umeme vijijini Karagwe. Naibu Waziri alitaja sehemu zitakazopatiwa umeme kuwa ni Kayanga - Rukaka, Rukaka - Ndama, Ndama hadi Kakiro, Kakiro – Runyaga na Kakiro - Rwambaizi.

Sehemu nyingine ni Nyakahanga - Bisheshe - Nyakagenja, Nyaishozi, Ihembe. Pia Serikali ilitaja sehemu za Nyakahanga - Rwabwere - Kamagambo - Nyakagoyagoye hadi Nyakaiga.

Mheshimiwa Spika, sijaona lolote katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nikumbushe kuwa Rais katika kampeni zake aliahidi kuwapatia umeme wananchi wa Nyaishozi na Nyakasimbi. Wakati wa kutimiza ahadi za Rais ni leo. Naomba kuwasilisha.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa kusimamia Sekta ya Nishati na Madini kwa makini sana. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri pia kwa ushirikiano anaokupa kusimamia shughuli za Wizara, naunga mkono hoja.

Kuhusu nishati, naomba nikumbushie ombi langu la siku nyingi la kushusha umeme katika kijiji cha Manchali kwenye njia iendayo Mpwapwa. Makadirio ya kazi hii yalikwishafanywa tangu mwaka 2003/2004. Ninayo ahadi ya Wizara kwa barua ambayo wananchi wa Kata ya Manchali walishafahamishwa kushusha umeme kwenye eneo hilo kipindi cha mwaka 2004/2005. Naomba nikumbushe kuangalia utekelezaji wa ahadi hiyo. Natanguliza shukrani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, kwenye eneo la Jimbo langu la Uchaguzi Kijiji cha Haneti ipo kampuni inayotafiti upatikanaji wa madini katika eneo hilo ambayo imeonyesha uhusiano mzuri na wananchi. Wanakijiji wa Haneti wanaomba kuwa pamoja uhusiano mzuri unaoonyeshwa na kampuni hiyo katika hatua hizi za awali Serikali kwa maana ya Wizara iwafahamishe maeneo yaliyoainishwa katika utafutaji wa madini ili kuepuka migongano ya migogoro ya ardhi kwani wananchi wanahofu hapo baadaye wasije wakajikuta wamemezwa na eneo la machimbo wakati madini yatakapogunduliwa.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa hapa ni wananchi kueleweshwa tu kwamba kampuni hiyo imetengewa eneo mahususi la kutafiti wa madini wanayotafuta. Nawatakia kila la kheri na narudia kuunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nafurahi kushukuru kampuni ya mgodi ya *Resolute Tanznaia Ltd.* kuanza kulipa kodi ya Halmashauri *(Local Government Levy)* kwa kiasi cha dola za Marekani 200,000 kila mwaka. Naipongeza hatua hiyo na kuiomba Serikali kuongeza walau ifike dola za Kimarekani 500,000. Pamoja na shukrani hizo nina hoja kuhusu umeme.

Katika Bajeti iliyopita ya mwaka 2006/2007 Wizara iliahidi kuipatia Wilaya ya Nzega umeme kwa miji midogo ya Ndala na Bukene. Kwa kuwa hadi sasa hakuna dalili zozote za kutekeleza ahadi hiyo. Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi hizo? Kwa mwaka huu Ndala kupitia Puge wametengewa shilingi ngapi? Kwa hizo, shilingi bilioni 10 za mwanzo Nzega imo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, Kampuni ya Madini ya Kahama inayosafirisha mchanga kupeleka Japan na Australia kwa kisingizio cha madini mengine

zaidi dhahabu yakomeshwe ili mchanga huo uchambuliwe hapa hapa nchini. Kama uwezo wa kujenga kiwanda cha kusafishia haupo kwa sasa na teknolojia haipo nashauri mchanga huo uwekwe hadi pale teknolojia na mtambo wa kuchambua madini utakapojengwa mfano ni Mwadui kwenye mgodi wa Almasi.

Pia Serikali iingilie kati ajira za watumishi wageni walioletwa na wawekezaji kwenye fani ambazo Watanzania wapo. Haiwezekani mwekezaji akaleta wahasibu, wapishi na hata walinzi kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania. Wizara yako ikishirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana iingilie kati juu ya pengo kubwa la mishahara la wafanyakazi wazalendo na wafanyakazi wageni. Tofauti yao ya malipo ni kubwa ya kutisha. Naomba majibu ya uhakika na matumaini kwa Watanzania.

**MHE. MOHAMMED S. SINANI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Mimi ningependa kuchangia juu ya madini ya chumvi. Kwa bahati mbaya Waziri hakutaja kabisa madini ya chumvi katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie namna gani inaweza kuwasaidia wazalishaji wadogo wadogo wa chumvi itokanayo na maji ya bahari *(Solar Extraction Salt)*. Wazalishaji hawa hutoa ajira kwa wananchi ambao huishi kandokando ya Bahari ya Hindi hususani akinamama. Pia wanatoa fedha nyingi za kigeni ambazo Serikali ingezitumia katika kuagiza chumvi nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iwasaidie wazalishaji hawa ili waendeleze shughuli zao ili kuongeza ajira na kipato kwa wananchi wengine. Iwapo Serikali itatilia maanani suala hili iwezekano wa kuzalisha chumvi ya kusafirisha nchi za nje utakuwepo. Wazalishaji hao wapo lakini wanakosa msaada wa Serikali .

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yak nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Sekta ya Nishati na Madini na pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo nikianza na sekta ya nishati. Kwa kuwa mabwawa ya maji ya Mtera, Kidatu, Pangani na Nyumba ya Mungu yamejaa maji, na kwa kuwa mabwawa haya ndiyo yanayozalisha umeme (Gridi ya Taifa), je, ni sababu zipi za msingi zinazofanya umeme usisambazwe vijijini vikiwemo vijiji vya Lipeta, Godegode, Makutupa, Mbori, Berege, Mima, Chunyu, Nghambi, Tambi, Nana, Majani, Mwenzele, Chitemo, Sazima, Igoji, Iwondo, Kisokwe, Idilo, Mzase, Msagali na kadhalika. Pia lini vijiji hivyo vitapelekewa huduma ya umeme?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa gharama za umeme ni kubwa, je, Serikali itakubaliana na ushauri wangu kwamba iwapo gharama za umeme zitapunguzwa *TANESCO* itapata wateja wengi?

Kwa kuwa tatizo la kukatika katika kwa huduma ya umeme bado linaendelea na kwa kuwa mitambo mingi imechakaa ikiwemo mitambo ya Wilaya ya Mpwapwa na hasa kipindi cha mvua inapopiga radi umeme hukatika, je, lini vitawekwa vidhibiti radi hasa maeneo ya Wilaya ya Kongwa na Mpwapwa?

Kwa kuwa nguzo ya umeme/waya zimepita milima ya Kongwa, je, Serikali ina mpango gani wa kupitisha nguzo zingine za umeme kupitia Kongwa - Nghambi, Chunyu, Msagali, Iyoma, Kosokwe hadi Idilo ili vijiji hivyo vipate huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, iwapo vijiji nilivyovitaja vitapata umeme, basi vijiji hivyo vitaanzisha miradi mbalimbali viwanda vidogo vidogo. Huduma ya umeme kwenye zahanati shule za sekondari na msingi *(solar pannel/energy)* vijijini na mashuleni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya madini, kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa kuna madini na kwa kuwa madini hayo yanachimbwa na wachimbaji wadogo wadogo ambao wana zana duni, madini hayo yanapatikana vijiji vya Mlembule, Kingiti na vijiji vingine, je, Serikali itatuma wataalamu ili waweze kufanya utafiti ili kujua ni maeneo gani yana madini mengi na madini ya aina gani.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali itawasaidiaje wachimbaji wadogo wadogo wa Wilaya ya Mpwapwa ili waweze kuboresha uchimbaji wa madini hayo kwa kuwapatia zana za kisasa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mikopo midogo midogo ili ziweze kuwasaidia kuendeleza miradi yao midogomidogo ya uchimbaji wa madini Wilayani Mpwapwa?

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri na kazi kwa ujumla wanayoifanya siku hadi siku. Naomba nichangie machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu gesi asalia, Serikali kupitia Wizara hii izisaidie taasisi binafsi zinazojihusisha na matumizi ya gesi asilia ili ziweze kutoa mafunzo kwa wananchi. Hii itasaidia kwa matumizi ya majumbani na pia itapunguza uharibifu wa mazingira. Lakini pia itawasaidia kuongeza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, naiomba Wizara itimize ahadi ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa mnamo mwezi Machi 2006, wakati alipokuwa akizindua shule *(Dr. Didas Secondary School)* ambayo iko eneo la Chanika - Videte, kuelekea Kata ya Msongola, Wilaya ya Ilala, Chamazi hadi Mbagala Wilaya ya Temeke. Tunaomba Wizara iwasaidie wananchi wa maeneo haya. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja%.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru sana kwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Mjini yaani Jimbo la Njombe Kusini, kuunganishwa na umeme wa Gridi. Sasa hivi umeme katika Mji wa Njombe ni *stable* sana. Umeme huu sasa umekwishafika hadi kwenye Kiwanda cha Chai cha Luponde katika kuendelea na safari yake kuelekea Ludewa. Naomba vijiji ambavyo umeme huo unapita vipatiwe umeme wakati shughuli za kufika Ludewa zinaendelea. Vijiji hivyo ni hivi vifuatavyo, Nundu pamoja na sekondari ya Yakobi, Njoomlole, Madobole karibu kabisa na kiwanda cha Luponde, Kona na Kitulila. Naunga mkono hotuba hii.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri, pia pongezi kwa Katibu Mkuu na timu yake nawapa pole kwa kazi ngumu ya kutufikisha hapa. Sababu hiyo inatosha kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie machache, katika hotuba ya Waziri sikusikia mkakati wa bomba la mafuta toka Dar es Salaam hadi Mwanza ukoje, hii ni ahadi ya CCM kutekeleza hilo, mradi huu utasaidia mfumuko wa bei ya mafuta na pia kuwa rahisi kudhibiti bei mbaya ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, wakati ujenzi wa mradi wa maji toka Ziwa Victoria hadi Kahama na Shinyanga ulilenga kuchukua umeme toka Inonelwa na kupita katika vijiji vya Buhingo, Seeke, Nyamanyiuza, Mbalama, Isesa hadi Ihelele na kazi hiyo *TANESCO* Wilaya iliniomba tuambatane nao kuwaomba wananchi wa maeneo kutodai fidia kwani faida kubwa ni wao kupata umeme na umma ulikubali. Lakini baadaye Serikali ilibadilisha nia na kuchulia upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika tayari ni usimikaji wa nguzo hadi Ihelele, waya kwa ajili ya kazi hiyo upo *site,* vikombe na *transfoma* nayo ipo, ni kwa nini Serikali isiruhusu huyu mkandarasi akafunga umeme kwa sababu ya vijiji hivyo? Serikali haioni kuwa vurugu itatokea iwapo mkandarasi huyu atakuja kung’oa nguzo zake au mkataba ukoje hasa?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo cha kupozea umeme wa gridi ya Taifa Mabuki una hatua gani? Umeme unaotoka Mwanza Kisesa na baadaye hadi Sumve umepita katika vijiji vya Bujingwa, Kanyerere (pana *center* na sekondari), Kolomije (pana *center* kubwa, sekondari, kituo cha afya na kadhalika) Bugomba ipo njiani je, Serikali inaahidi nini kwa vile *TANESCO* Wilaya maombi hayo imeyaleta kwenu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, kwa kuwa kampuni za utafiti zinapaswa kusalimisha eneo fulani baada ya miaka mitatu, *East Africa Mine* itakamilisha lini utafiti wake, tangu mwaka 1994 hadi leo. Mbaya zaidi hashiriki kuchangia hata maendeleo ya Kata/Kijiji mfano ni kwa kampuni ya *Sub Sahara* ambayo ndani ya mwaka mmoja

imechangia *US 4500* kwa kukamilisha vyumba vitatu vya shule ya sekondari Lubiri. Nawapongeza sana na pia Serikali naomba mfikishe ahsante hiyo. Wananchi wanaomba eneo lao la Buhunda lirudishwe na wachimbaji wadogo wadogo wapewe eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ni unyanyasaji kuwanyima eneo la kulitumia. Serikali inasemaje kuvipa umeme vijiji vya Kasololo, Nduha hadi Sumbugu wakati umeme upo *Manawa Ginnery* pia ni kilometa nne tu toka Inonelwa kwenda Kijima.

Mheshimiwa Spika, mwisho narudia, tena kuunga mkono hoja hii na nawaomba Wabunge waruhusu Wizara ipewe fedha.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza nimpongeze Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara hii kwa jinsi wanavyojitahidi kufanya kazi zao na kuiwezesha Wizara kukidhi japo si kwa asilimia zote mahitaji ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi na kwa kuwa Kamati hii imeweza kutembelea miradi mbalimbali ya Wizara ya Ardhi, kulijitokeza suala la ukosefu wa miundombinu katika maeneo ya miradi kwa mfano tunalo Shirika la Nyumba ambalo lina mradi wa ujenzi wa nyumba za kuuza katika eneo la JKT, Mbweni, mradi huu ulizinduliwa rasmi na Serikali na nyumba ziko tayari kasoro umeme hakuna, hivyo tatizo hilo limesababisha ununuzi wa nyumba hizi kutokuwa na kasi kwa vile mtu anaona taabu kuishi gizani na hasa ukizingatia ni nje kidogo ya mji.

Mheshimiwa Spika, hivyo Shirika hili linazamisha mitaji yake kwa kukosa soko la nyumba zake. Hivyo naomba Wizara hii kupitia Shirika lake au wahisani kujali umuhimu wa umeme katika maeneo ya aina hii ili pia hata Watanzania wanaoshawishika kupata maisha bora kupitia nyumba za shirika hili waneemeke na kuzidi kutangaza biashara na ubora wa nyumba hizi nzuri za shirika hili na hasa ukizingatia kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, alikuwa Mjumbe wa Shirika hili la Nyumba na anazifahamu hizo nyumba za mradi wa JKT Mbweni na Boko.

Mheshimiwa Spika, si miradi hiyo tu bali Wizara ijali maeneo yote ili kuweza kufikia malengo yetu ya hali bora ya kila Mtanzania. Wizara pia iangalie maeneo ya shule zetu za sekondari zilizoko hatua chache kutoka unapopita umeme wa gridi ya Taifa zipatiwe umeme ili kuboresha taaluma mashuleni. Palipo na miradi ya maji pia iwepo nguvu kubwa ya umeme ili kutawala *pressure* ya usukumaji wa maji na kusambazwa vyema katika maeneo ya makazi ya Watanzania.

Nashauri pia Wizara ione umuhimu wa kutanguliza miundombinu ya umeme katika maeneo ya miji inayotarajiwa kuanzishwa na Wizara ya Ardhi kwa mfano viwanja

vinavyopimwa na kugawiwa kwa raia, umeme uwepo ili kuongeza thamani ya maeneo hayo na kukuza ujenzi wa maeneo hayo na kukua kwa miji yetu. Ikumbukwe kuwa palipo na umeme umaskini hupungua haraka kwa vile miradi mingi hufikiwa vyema.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nirudie tena kuishukuru Wizara hii ila nisisitize zaidi tena kupatiwa umeme JKT Mbweni kwa vile na mimi ni mkazi wa eneo hilo na nimekuwa na kuishi gizani kwa muda mrefu pamoja na wakazi wenzangu tunaomba kupatiwa umeme. Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia tena hoja hii kama ifuatavyo, kwa kuwa wakati akijibu au kutoa ufafanuzi kuhusu hoja nilizotoa wakati wa hoja ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa Kampuni ya MEREMETA ilifilisika na shughuli zake zimechukuliwa na Kampuni ya *Tangold* na kwa kuwa katika hotuba yako Waziri hakutaja kabisa kuhusu kampuni hii ambayo ni mali yetu Watanzania na kwa vile haikutajwa pia popote na kwa vile kwa maudhui ya jina lake kampuni hii inaelekea kuwa chini ya Wizara hii, naomba ufafanuzi wa kina kuhusu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kampuni ya *Tangold* iliandikishwa lini na wapi? Pili, wanahisa wake ni Serikali kwa asilimia mia moja, je, Wakurugenzi wake ni nani kwa majina, tatu, hadi sasa tangu kuandikishwa, kampuni hii imepata faida au kiasi gani na baada ya kuuza dhahabu kiasi gani? Na nne, kwa kuwa kampuni ya MEREMETA ilifilisika kwa maelezo ya Serikali, Waziri anaeleza nini kuwa kwa taarifa ya Alex Stewart, kampuni ya MEREMETA ambayo nayo ni ya Serikali ni kati ya makampuni ambayo hayakuwasilisha mahesabu yake kwa ukaguzi? Na je, Serikali ililipa dola za Marekani kiasi gani wakati wa *liquidation* ya MEREMETA?

Mheshimiwa Spika, kwa vile kampuni ya Alex Stewart ni kampuni tuliyoilipa fedha nyingi sana mathalani kwa mwaka 2005/2006 kampuni hii inasemekana imelipwa kiasi cha shilingi 14,175,753,189.46 napenda Waziri aliarifu Bunge hili:-

(i) Taarifa kwa mwaka 2005/2006 ilipata faida au hata mapato kiasi gani kutokana na sekta ya madini kama na kutokana na taarifa ya Alex Stewart? Yeye anasemekana kulipwa 1.9% ya *3% royalty* yetu.

(ii) Je, kati ya makampuni yaliyosemekana katika taarifa ya Alex Stewart yalikataa kukaguliwa ni mangapi hadi sasa yemetimiza jukumu hilo la kisheria na kutokana na ukaguzi huo faida au hasara au mapato ya Taifa yaliyopatikana ni kiasi gani?

(iii) Kwa kuwa taarifa ya Alex Stewart ilionyesha kuwa makampuni yalitakiwa kulipa kwenye *Escrow A/c* fedha kwa dola za Marekani, je, hadi sasa kiasi gani kimelipwa kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira katika mfuko huo kwa lengo la uhifadhi wa mazingira yetu kama mkataba ulivyosema kufuatana na taarifa hiyo?

Kwa vile Mheshimiwa Waziri wakati akifafanua hoja nilizotoa wakati wa hoja Waziri Mkuu, pamoja na mambo mengine alieleza kuwa Kampuni ya *RandGold*

*Resources Tanzania Limited* ina mkataba wa ubia na Serikali kupitia kampuni yetu ya *Tangold,* je, ni nini matokeo ya kazi zinazofanywa na makampuni hayo katika mgodi wa Buhemba na nje ya Buhemba? Hadi sasa Taifa limefaidika vipi na matunda ya kazi zao?

Je, *RandGold Resources (T) Limited* wanalipwa asilimia ngapi ya mapato na *Tangold* kwa mujibu wa mkataba huo na ni kazi zipi hasa zinafanywa na wabia hao ambazo *Tangold* haiwezi kufanya?

Mheshimiwa Spika, *RandGold Resources* iliandikishwa wapi kama kampuni mama?

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashauri kwamba sheria inayotaka 50% ya eneo irejeshwe kama mwenye leseni hakuliendeleza katika muda ulioruhusiwa, itekelezwe bila huruma. Maeneo yanatolewa katika leseni ya mwanzo, yapunguzwe ili kuruhusu watafutaji zaidi waweze kuingia katika ujasiriamali bila kusababisha migongano.

Pili, napenda kufahamu kama matokeo ya uchunguzi wa dhahabu uliofanywa na *Anglo-American Exploration Company* katika Jimbo la Kalenga, yanafahamika Wizarani?

Nashauri Wizara itume mtaalam Wilaya ya Iringa, kubaini kama kuna uwepo wa dhahabu. Pia naiomba Wizara ifikirie kupeleka umeme toka Ref. Vijiji vya Magulilwa, Igula, Mgama, Kiponzelo na Wenda (Mseke).

Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo kwenye *paragraph* 1(a) na (b); watafutaji wanapewa maeneo makubwa mno na kiasi cha kuwanyima watafutaji wengine wadogo wadogo kuchangia katika ukuzaji wa pato la Taifa, wengine wanaruhusiwa kutafiti katika maeneo makubwa kwa Wilaya au Mkoa. Hii siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, *Anglo-American Exploration Company,* walifanya uchunguzi Jimboni Kalenga mnamo 1996 - 1999 kubaini uwepo wa dhahabu. Nilibahatika kupata taarifa *(privately)* kwamba, dhahabu ipo sehemu kadhaa lakini kwa vile wao wanahitaji kiwango kikubwa cha dhahabu kitakachokidhi gharama za miundombinu yao, waliacha uchunguzi kimya kimya. Ningeomba kujua matokeo ya uchunguzi huo.

Jimbo la Kalenga lina vijiji vikubwa ambavyo sasa vinastahili huduma ya umeme. Naomba vijiji hivyo vifikiriwe chini ya *Rural Ernergization Fund;* vijiji hivyo ni Magulilwa, Igula, Mgama, Kiponzelo na Wenda (Mseke).

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja moja kwa moja na kuitakia kila la kheri hoja iweze kupita bila matatizo. Natumaini katika majumuisho utasemea hili hata kama ni ahadi tu.

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii ngumu na nyeti.

Kilio changu ni kupata umeme kutoka Wilayani Mahenge; Ruaha –Mwaya – Mbuga. *Line* hii ina Kata nane na vijiji karibu 20, vipo barabarani. *Line* hii ina uchumi na huduma za jamii zifuatazo: Kinu cha kuchambua pamba – Mwaya; Makazi ya wafanyakazi wa mbuga za wanyama za *Selous,* ambapo Serikali imejenga nyumba za wafanyakazi 50; Kituo cha Afya cha Mwaya na Ruaha; Shule za Sekondari kumi na Shule za Msingi 13.

Mheshimiwa Spika, nimeona katika bajeti ukurasa 26, kwa mwaka 2007/2008, zimetengewa shilingi bilioni kumi kwa ajili ya Mradi wa Umeme Vijijini. Naomba unifikirie kupata umeme kuanzia Shule ya Sekondari ya Regina Mundi – (Mahenge), kupitia Ruaha - Chorombola – Mwaya, kwenye kinu cha pamba hadi Mbuga kwenye makazi ya wafanyakazi wa Mbuga ya *Selous.*

Najua kuna mgogoro kati ya Kampuni ya *Interstate Vs* wachimbaji wadogo katika eneo la Epanko. Kkwa sasa sehemu ya mgodi huo imefungwa kwa sababu ya mgogoro huo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, awapatie leseni wachimbaji wadogo waendelee na kazi ya utafutaji wa madini, ibaki sehemu yenye mgogoro kati ya *Interstate* na Mworia tu, wachimbaji wadogo hawana mgogoro na *Interstate.* Naomba suala hili lifikie tamati, limechukua muda mrefu mno naomba tuwasaidie wachimbaji wadogo. Najua wapiganapo fahari wawili ziumiazo ni nyika. Wapewe usemi wachimbaji wadogo, mgogoro wa *Interstate* na Mworia uendelee.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Bunda, inapitiwa na nyaya za umeme zinazopeleka umeme kutoka Mji wa Bunda kuelekea Mugumu, Wilaya ya Serengeti. Njia hiyo ya umeme inapita katika Vijiji vya Mcharo, Kisangwa, Kisoleli, Salama A, Sanzate, Mngeta na Kyandege. Ingawa umeme umeshushwa, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kusambaza umeme katika vijiji hivyo.

Shule za Sekondari za Sirari katika Kijiji cha Changuge, Shule ya Sekondari ya Sarera, Salama Mikomarino, Mihongo na Chamriho (Mugeta), ambazo ziko kati ya Kilomita 2 – 5 kutoka njia ya umeme ni busara zifikiriwe kupewa umeme ili kuboresha Elimu ya Sekondari. Aidha, Shule za Sekondari ya Hunyari na Kijiji cha Hunyari, kifikiriwe kupewa umeme. Ubalozi wa Japan umekubali kujenga Hosteli katika Sekondari hii kwa masharti ya kuwepo mpango wa kufikisha umeme katika shule hii ya Sekondari

Mheshimiwa Spika, mwisho, ili kuongeza mapato ya *TANESCO*, ni vizuri maombi ya wananchi katika Mji wa Bundam ambayo yanachelewa sanam yashughulikiwe kwa haraka. Aidha, Shule za Sekondari za Kunzungu, Rubana, Dr. Nchimbi, Nyiendo na Kabasa, ambazo zipo katika eneo la Mji wa Bunda, zipewe huduma za umeme, ili kuimarisha utoaji wa huduma za elimu. Yapo Makampuni ambayo yako tayari kutoa *Computer* kwa Shule za Sekondari, lakini kutokana na kukosekana kwa huduma za umeme, mpango huo unashindwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri sana, wanayoifanya kwa umakini na uharaka.

Naomba suala la umeme Kwediboma –Songe, tulipitisha mwaka jana wakati wa bajeti 2006/2007 na hakuna lililofanyika. Mwaka huu naona tumetengewa shilingi milioni 50, nina wasiwasi kama nayo haitafanyika wananchi wamepungukiwa na imani, lakini naamini Waziri, kwa kauli zake za uhakika, hili litafanyika. Naomba uwahakikishie wananchi wa Kilindi ni lini sasa umeme utawaka Songe – Makao Makuu ya Wilaya? Wananchi wako tayari kutumia nguvu zao endapo zitahitajika.

Kuhusu suala la madini, naomba vibali vinapotolewa, kipaumbele wapewe wachimbaji wadogo. Limekuwa suala la kisiasa sasa, kwani wananchi wanaona wanaonewa, wanagundua madini halafu wakubwa wanapewa *plot* kwenye maeneo hayo. Ingawa Naibu Waziri binafsi, pamoja na Kamishna Dr. Kafumu, Wanasheria Dr. Kalemani na Salome Makange, Mkurugenzi wa Kanda Mlabwa, Mkurugenzi leseni Bw. Sameja, wote wametoa ushirikiano mkubwa sana, lakini naomba utekelezaji kwa hilo. Pili Mikataba iliyopo iliyokiuka utaratibu, kwa vile najua kuwa suala hili mnashughulikia, unawaambia nini wana-Kilindi?

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri na kutaka ushirikiano wake.

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ninao ushauri mdogo tu: Kwa vile mafuta yameonekana ni vyema sasa juhudi za kuchimba mafuta hayo sasa zifanyike kabla gharama hazijapanda sana. Nashauri iwekwe mipango mizuri ili mafuta hayo yasije yakawa ndio chanzo cha mizozo kama vile ilivyo Nigeria. Wananchi watayarishwe vyema ili nao waweze kuchukua nafasi zao za kulinda uchumi huo. Majadiliano ya pande mbili (SMZ na SMT) yanahitajika, kwa lengo la kupata muafaka ili kila upande ufaidike.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa usafirishaji wa *Tanzanite* unahitajika na uchimbaji holela wa vito na watu wa nje udhibitiwe. Usafishaji na ukataji wake ufanyike nchini na katika maeneo ya uchimbaji, juhudi zifanywe za uhifadhi wa mazingira. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa hotuba yao nzuri sana. Kutokana na hilo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu lenye jumla ya vijiji 75 ni vijiji viwili tu vyenye umeme (Tunduma na Mpemba), ambavyo vyote viwili viko kwenye njia ya umeme utokao Zambia. Kutokana na hali hiyo, kwa jumla eneo la Jimboni Mbozi Magharibi ni kati ya yale yaliyo nyuma sana kimaendeleo nchini. Kwa kuwa eneo hili kuna Uwanda wa Juu na Uwanda wa Bonde la Ufa na kuna maanguko ya maji ambayo yalifanyiwa utafiti miaka ya 80 na kwa jumla kuna jua la kutosha, wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi wanaomba wapatiwe umeme wa nguvu ya maji kwa Kata za Myunga, Chitete na Chilulumo. Umeme jua kwa Kata za Chiwezi, Msangano, Chilulumo, Kamsamba, Ivuna, Nkangamo, Kapele na Ndalambo ili kuwawezesha kufanya shughuli za maendeleo kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, napenda nikuhakikishie kuwa, Jimbo langu lina maeneo mengi yenye maanguko ya maji yaliyofanyiwa utafiti miaka ya 80, yalikuwa kwenye mpango wa utekelezaji sambamba na usambazaji maji vijijini ujulikano kama *Mbozi West Water Supply and Electrification – DANIDA* walihusika.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu umeme usioaminika katika Miji Midogo ya Tunduma na Vwawa na Vijiji vya Mpemba na Mlowo Wilayani Mbozi.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo tajwa hupata umeme kutoka Zambia, lakini kila siku umeme huu hukatwa kwa saa zisizopungua nne; kuanzia saa mbili usiku na mara nyingine kwa wiki nzima. Pia umeme huu ni wa *low voltage* na hivyo kusababisha uharibifu wa vifaa na mitambo mbalimbali katika maeneo hayo. Kutokana na uhafifu wa umeme huo, majokofu ya kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya Tunduma, yameshindwa kufanya kazi na pia kutokana na giza linalotanda baada ya kuzimika umeme huu, matukio ya uhalifu wa kutumia nguvu kama kupiga watu na nondo, kuwakata na mapanga, kuwapiga risasi na kupora mali, yameshamiri katika maeneo hayo. Ombi la wananchi wa Wilaya ya Mbozi ni kuunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa, ambao ulionesha ufanisi mkubwa wakati wa kipindi cha majaribio yaliyofanyika kwa wiki moja.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi lina madini ya aina mbalimbali, ambayo kwa bahati mbaya, Serikali haijachukua jukumu la kuyachambua, badala yake yanaporwa usiku na wajanja ambao wanayachimba bila ridhaa ya Serikali.

Naomba kwa niaba ya wananchi wa Mbozi Magharibi, Serikali itupie macho eneo hili na kuweka Mpango Mkakati wa kuweza kuvuna rasilimali hii ambayo ndiyo inaweza kuinua uchumi na maendeleo ya jumla ya wananchi wa Jimbo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake, kwa jitihada zao za kuboresha Sekta za Nishati na Madini. Nitazungumzia zaidi Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kisarawe wamenituma niwaeleze kuwa kero zao kubwa ni kukosa umeme vijijini, bei za juu za umeme na mafuta na pia pale Wilayani kunakopatikana umeme, kuna bughudha ya kukatikakatika. Wanahitaji umeme wa kuaminika na hasa ufike vijijini. Ingawa hotuba yako inatueleza kuwa mpango wa umeme vijijini umeanza kutekelezwa, utekelezaji huo haujaonekana Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani, hasa Wilaya ya Kisarawe unapakana na Dar es Salaam. Kwa kuwa umeme ni ghali nchi nzima, wananchi wa Dar es Salaam na Pwani yenyewe sasa wameacha kabisa kutumia umeme kwa kupikia, kuchemsha maji, hata kuendesha viyoyozi na vipozeo. Kwa hiyo, misitu ya Mkoa wa Pwani, imekwisha kwa ukataji wa kuni na kutengeneza mkaa, vinavyotumika badala ya umeme. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara, ihimize Mpango wa Umeme Vijijini uwe chini ya *TANESCO* au wawekezaji binafsi, kama tulivyoupitisha ndani ya Bunge hili. Napenda kuwakumbusha mambo yafuatayo:-

Kwanzaa, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliahidi kupeleka umeme kwenye Vijiji vya Masaki, Maneromango, Msanga na Mzenga, kwa kuunganisha umeme kutokea Mlandizi na pia kutoka Makao Makuu ya Wilaya.

Pili, Wizara yako Mheshimiwa Waziri, kupitia Waziri aliyekuwepo kabla, aliahidi kutekeleza Ahadi ya Rais Kisarawe kuanzia usanifu mwaka huu wa kalenda. Kwa bahati mbaya sana, mwaka huu sasa umekwisha, lakini mambo haya yote hayajaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa, vijiji vya Mkoa wa Pwani ikiwemo Wilaya ya Kisarawe, ndiyo tegemeo kuu la Jiji la Dar es Salaam kwa bidhaa mbalimbali za chakula, ikiwemo mihogo, matunda na mbogamboga. Dar es Salaam itanufaika sana na wananchi wa Pwani pia watapata maendeleo kama Serikali itafikisha umeme kwenye vijiji vya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, ajira zitaongezeka vijijini na vijana wengi wanaofurika Dar es Salaam kutafuta ajira, watabaki vijijini. Vijiji navyo vitaanzisha miradi, ajira zitaongezeka, matunda kama machungwa, maembe, mananasi, mafenesi na kadhalika, yatasafirishwa na mapato ya wananchi yataongezeka. Wanafunzi wa shule za sekondari watapata nafasi ya masomo ya sayansi na teknolojia, hasa kompyuta kama wanavyopata wenzao katika Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, nategemea Mheshimiwa Waziri kuwa, katika kujibu hoja zake, atatueleza azma ya Wizara yake kutukomboa hasa kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais na Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wa Wizara, kwa hotuba nzuri na ninaiunga mkono hoja hii. Naomba tamko au kauli ya Mheshimiwa Waziri katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Tarafa nzima ya Mlola kuendelea kubaki gizani. Umeme wa *grid* umekuwepo Lushoto Mjini tangu enzi za mkoloni, lakini Tarafa nzima ya Mlola; Kata za Malibwi, Mlola, Makanya na Ngwelo, zinaendelea kuwa gizani hadi leo. Hali hii inaathiri ubora wa maisha ya wananchi na utoaji wa huduma katika sekondari kumi, zahanati nane, Vituo cha Afya, shule za msingi 30 na kadhalika. Umeme wa *grid* utasambazwa lini katika Kata hizi kwa kutumia *line* zilizofika Kwekanga na Mlalo?

Pili, kusitishwa huduma za kuunganisha umeme Lushoto ni lini mita na vifaa vya kuunganisha umeme vitapelekwa Wilayani Lushoto ili huduma kwa wateja iendelee? Naunga mkono hoja hii.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nampongeza yeye, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote katika Sekta ya Nishati na Madini, kwa jitihada zao za kuboresha huduma katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wana kiu kubwa ya kupata huduma ya umeme katika maeneo yao, hususan katika Vijiji vya Wilaya ya Ileje. Kwa mantiki hiyo, tunaiomba Serikali, iharakishe kukamilisha uanzishaji wa Wakala wa Nishati Vijijini, pamoja na Mfuko wa Uwezeshaji ili huduma za umeme vijijini ziweze kuanza mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona maelezo ya kina kuhusu Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira. Kwa kuwa sehemu kubwa ya makaa ya Mgodi huo yapo katika Wilaya ya Ileje, ningependa kupata maelezo ya kina kuhusu maendeleo ya mgodi huo, pamoja na ushirikikano na washirika wetu nchi ya China. Ningependa pia kufahamu mikakati iliyopo ya kuiwezesha Wilaya yetu ya Ileje kufaidika na mgodi huo, kama ilivyo kwa Wilaya nyingine zinavyofaidika kutokana na madini yaliyomo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, hawajafika Ileje, napenda kutumia nafasi hii kuwakaribisha wafanye ziara rasmi Ileje ili wajionee hali halisi ya kijiografia ya Wilaya yetu na rasilimali hii ya makaa ya mawe ilivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mdogo, nawatakia kila la kheri na ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Katika bajeti ya 2006/2007, Wizara ilitenga kiasi cha shilingi bilioni kumi kwa ajili ya umeme kwa Mkoa wa Kigoma. Kutokana na hali ya ukame iliyojitokeza, kazi hiyo haikufanyika. Mbona fedha hizo hazikutengwa katika bajeti ya 2007/2008?

Ni dhahiri kwamba, yapo matumaini makubwa ya kupata umeme kwa Mkoa mzima, lakini kwa upande wa Wilaya ya Kibondo umeme wake utatoka Shinyanga kwenye Gridi ya Taifa. Ni lini umeme huo utafika Wilaya ya Kibondo ili kuwasaidia wananchi hao ambao wamekaa giza tangu Uhuru?

Pili, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 33, aya ya 76, inaeleza uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala kwa maeneo yasiyo na umeme. Mimi nimeshangaa kuona Mkoa wa Kigoma usio na umeme, haukupangwa na badala yake imepangiwa kuongezwa umeme Mikoa yenye umeme kama vile Mbeya na Mtwara. Vilevile katika utekelezaji wa mradi unaofadhiliwa na *UNDP/GEF*, umepangiwa kuendelea katika Mikoa ya Mara, Kagera na Shinyanga, kwa madai kwamba ni kuendeleza uzoefu uliopatikana Mkoa wa Mwanza. Kwa nini mradi huu hakuzingatia Mikoa isiyo na umeme? Napenda kupata maelezo juu ya hilo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Nawashukuru Waziri na Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri iliyofanyiwa utafiti wa kina.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kulipongeza Shirika la *TPDC,* kwa kutuletea/kuthibitisha upatikanaji wa gesi ambayo itaweza kutumika kwa kupikia nyumbani na kutumika kwenye magari badala ya kutumia mafuta kwenye magari hayo.

Ningeshauri Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuisaidia *TPDC* ili iweze kutimiza au kupeleka gesi hiyo kwa matumizi ya nyumbani kwenye Miji ya Dar es Salaam na hatimaye mpaka vijijini, ambako wanakata miti kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kupikia. Itasaidia kwa kiwango kikubwa kutunza mazingira yetu na hii iende sambamba na kuhakikisha *filling station* kwa ajili ya gesi ya magari zifungwe kwa kuanzia kwenye Miji yote mikubwa na baadaye nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, taa za barabarani nyingi haziwaki; kwa nini *TANESCO* isitumie umeme wa jua kwenye taa zote za barabarani ili kupunguza gharama kwa sababu umeme wa jua ni wa bei rahisi zaidi?

Kuhusu madini, Shirika la *STAMICO* liimarishwe ili liweze kusimamia shughuli zote za madini hapa nchini ili liweze kuwasaidia zaidi wale wachimbaji wadogo wadogo kwa ushauri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata majibu ni kwa nini mpaka leo Tanzania hatuna viwanda vya kuchoronga vito na kuchekechea madini hapa nchini? Ningependa kujua mchanga unapopelekwa Japan; Serikali inatambua vipi madini kiasi gani kilichopatikana na ni madini ya aina gani yaliyopatikana?

Mheshimiwa Spika, kuna kampuni kama *Barrick (T) Limited* na *Resolute (T) Limited,* zimekubali kuilipa Serikali Dola za Kimarekani milioni saba; kwa nini fedha hizo zisitumike kujenga viwanda vya kuchorongea/kuchujia madini hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie ni jinsi gani ya kutunisha Mfuko wa Umeme Vijijini zaidi, kwa sababu tukiwa na umeme wa uhakika vijijini, itakuwa ni rahisi hata *SIDO* kuweza kuwasaidia wakulima kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao yao kule kule na kuvisafirisha vikiwa tayari.

Mheshimiwa Spika, hii itapelekea kwanza, kuwa na ajira kutoka kwenye vile viwanda na pili wakulima wataweza kuuza bidhaa zao kwa bei nzuri zaidi na hatimaye kupata maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, mambo ya muhimu, *TPDC* ipewe nafasi ya kuagiza mafuta halafu wao ndiyo wayauzie makampuni ili ku-*control* bei.

Mheshimiwa Spika, *last week* ndege ya *Air Tanzania Corporation* ilishindwa kujaza mafuta *Kilimanjaro International Airport (KIA),* ilibidi ikajaze mafuta Dar es Salaam kwa sababu kampuni iliyokuwa inapeleka mafuta *KIA* ilikuwa imegoma. Je, tusipokuwa na mipango yetu wenyewe na hawa watu au makampuni wakitia mgomo si nchi itayumba kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, ningeshauri *TPDC* warudishiwe mamlaka haya, ikiwezekana *TIPPER* iwe *controled* na *TPDC* ili waweze kuhifadhi mafuta na hatimaye kuyasambaza na ku-*control* bei hii ambayo inapanda bila kujali maslahi ya Watanzania walio wengi. Natumaini maswali yangu yatapatiwa majibu na ushauri kuzingatiwa.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme kutoka Maporomoko ya Rusumo utaanza lini? Tatizo la upungufu wa mita na *transformer* unaosababisha maombi ya watu kutofungiwa umeme kulundikana utakwisha lini ili watu waliokwisha kulipia umeme wapate umeme?

Shirika la *TANESCO*limekwishasimika nguzo katika sehemu zifuatazo: Biharamulo Mjini hadi Shule ya Sekondari ya Biharamulo; Biharamulo Mjini hadi Ruziba; na Biharamulo Mjini hadi Kituo cha Wakulima *(FEC).* Nguzo hizo zimewekwa pale kwa muda mrefu sana; je, ni lini Miradi hiyo itakamilika ili wananchi wapate umeme?

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nichangie Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Nianze kwa

kumpongeza Waziri, kwa hotuba yake nzuri.  Aidha, nawapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, naomba kuchangia hotuba hii katika maeneo machache yafuatayo:  Ninaishukuru Serikali kwa kutekeleza Mradi wa Umeme wa *Electricity IV* kati ya mwaka 2000 – 2004 katika Wilaya ya Kondoa.  Mradi huu ulihusu ujenzi wa *Sub-station* Mjini Kondoa na kupeleka umeme hadi Kibaya Wilayani Kiteto. Ninaishukuru Serikali kwa kuvipa umeme vijiji vilivyo katika njia ya umeme. Aidha, ninaishukuru Serikali kwa kupeleka umeme katika Vijiji vya Soya na Hamai, Jimboni Kondoa Kusini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizi, ninasikitika kusema kuwa, tangu Mradi wa *Electricity IV* ukamilike, Serikali haijafanya juhudi yoyote ya kusambaza umeme kwa vijiji jirani vya Piho, Dalai, Cheku, Waida, Pongai, Sori, Kelema, Balai, Madaha, Charuku, Mapango, Mwailanje, Isusumya, Songambele, Magaza na Nkulari. Vijiji hivi vipo karibu sana na njia ya umeme na hakuna gharama kubwa ya kufikisha umeme katika vijiji hivyo. Vijiji vyote hivyo vimekwishapeleka maombi ya kupatiwa umeme *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, ninaomba Serikali kupitia Shirika lake la *TANESCO* na Wakala wa Nishati Vijijini, ifikirie kuvipatia umeme vijiji nilivyovitaja kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nataka nichangie linahusu nishati mbadala. Niipongeze sana Serikali kwa jitihada kubwa ya kuendeleza nishati mbadala nchini.  Nchi yetu ina utajiri mkubwa wa nishati ya jua.  Nishati hii inapatikana katika maeneo yote nchini. Ninaishauri Serikali itumie utajiri huu, kusambaza umeme huu haraka nchini hususan vijijini. Hivi sasa Mradi unatekelezwa katika Mikoa minane ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Mara, Kagera, Shinyanga na Mwanza. Mradi upanuliwe na utekelezwe katika Mikoa yote. Aidha, umeme uelekezwe zaidi katika maeneo ya vijiji ambavyo viko mbali na umeme wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, ninaomba wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Jua Mkoani Dodoma, kipaumbele kitolewe kwa tarafa za Farkwa na Kamtoro katika Jimbo la Kondoa Kusini, kwa sababu tarafa hizi ziko mbali sana na umeme wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache, ninaomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:**  Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mungu kwa kwa kunijalia uzima na kunipa uwezo kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.  NampongezaMheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha vyema hotuba yake, yenye kuonesha utendaji mzuri na yenye mategemeo kwa nchi yetu. Pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Waziri. Lakini pia, nawapongeze wale wote waliomsaidia Waziri kuandaa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara hii pamoja na wafanyakazi wote, kwa juhudi kubwa waliyofanya wakati ukame ulipotokea katika nchi yetu. Ukame ambao ulisababisha mabwawa ya maji kukauka, hali ambayo ilisababisha upungufu mkubwa wa uzalishaji umeme. Kwa juhudi kubwa kubwa zilizofanywa kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, Wizara ilirejesha hali ya kawaida ya upatikanaji wa nishati kwa kipindi kifupi sana, hali ambayo haikutegemewa na wengi. Hali hii inafaa kupongezwa na kuigwa na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuiomba Wizara kuwa ari na nguvu zilizotumika katika kurejesha umeme nchini, zitumike katika kusambaza nishati hii mijini na vijijini. Kama inavyoeleza Ilani ya CCM, pamoja na kutekeleza Ahadi za Viongozi wetu wa Kitaifa, pamoja na kuwasaidia Wabunge katika majimbo yao, kwa sababu nao walitoa ahadi wakati wa kampeni. Juhudi hizi zikichukuliwa ni kuipa heshima Serikali yetu na Chama chetu na pia ni kuongeza mapato na kukuza uchumi wa nchi na watu wake wote kila mahali.

Mheshimiwa Spika, kuna usemi unasema ni asilimia kumi tu ya umeme unaotumika katika vijiji vyetu. Kama ni kweli, hicho ni kiwango kidogo sana ukilinganisha na ukubwa wa nchi yetu. Hakuna lisilowezekana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri tokea kuteuliwa kuiongoza Wizara hii. Aidha, nampongeza Dr. Idrissa Rashid, kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* na nina matumaini kuwa ataliimarisha Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2006/2007, Kijiji cha Ihanja kiliwekwa katika mpango wa kupatiwa umeme katika mwaka wa fedha 2006/2007. Hii ilitokana na ahadi za muda mrefu za Serikali za kupeleka umeme Ihanja, kufuatia kuwekwa nguzo za umeme tangu 1998 na kisha kuzichukua kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme Ihanja ni utekelezaji wa Mpango wa kupeleka umeme Kijiji cha Ikungi na Puma na kisha Manyoni. Vijiji hivyo vilikwishakupatiwa umeme isipokuwa Kijiji cha Ihanja, kwa nini? Narudia kueleza kuwa Ihanja kuna *Ihanja Technical Secondary School* pamoja na Kituo cha Afya, Polisi, Misikiti na Makanisa. Baada ya kuwekwa katika Mpango wa 2006/2007, mimi Mbunge wao niliwajulisha wananchi kuwa watapatiwa umeme kwa vile wameingizwa katika Mpango wa 2006/2007. Hivyo, nasisitiza umeme Ihanja upelekwe haraka kama ilivyoahidiwa mwaka 2006/2007, kwani wananchi walisikia na wamefanya *wiring,* wanasubiri umeme. Je, usipopelekwa hali itakuwaje na *RC* amewahakikishia suala hilo?

Kijiji kingine ni Sepuka, ambapo katika 2006/2007 kilikuwepo katika Mpango wa Serikali, kwa kuwa na Sepuka A na Sepuka B. Naomba huku nako Mpango wa 2006/2007 utekelezwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kutanguliza hongera kwa shughuli nyingi ambazo Wizara inafanya kwa ajili ya huduma za wananchi.

Mheshimiwa Spika, umeme ni chanzo cha maendeleo na ndio maana maeneo yenye umeme yanakuwa na maendeleo zaidi kuliko sehemu ambazo hazina umeme. Kwa kuwa umeme ni muhimu, naomba nipate maelezo kuhusu umeme Namanga/Longido. Mwaka 1997 Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, alifika Longido/Namanga na kutoa ahadi kwamba, ifikapo mwishoni mwa mwaka huo, umeme ungekuwa umefika Namanga.

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini wakati huo, Mheshimiwa Daniel N. Yona, aliahidi kwamba, mwishoni mwa mwka 1999 umeme ungefika Namanga. Kwa masikitiko mwaka 2006, kwenye bajeti ya mwaka 2006/2007, umeme wa 330kv Arusha/Nairobi ulipangiwa shilingi 8,700,000,000. Naomba kujua hizo fedha bado zipo au zimepelekwa kwenye miradi mingine? Kwa masikitiko, bajeti hii ya 2007/2008, Mradi huu haukupangiwa fedha. Naomba ufafanuzi, ahadi ya Serikali kuhusu umem,e Namanga/Longido imekuwa ya muda mrefu ambapo wananchi wameanza kukata tamaa kabisa.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, amefanya ziara Wilayani Longido na akatoa ahadi kwamba, haiwezekani umeme ukafika Namanga/Kenya, usifike Namanga/Tanzania. Akatoa ahadi namnukuu: "Ni lazima mwaka huu umeme toka Kenya tutavuta kuja Namanga na Longido kwa fedha zetu wenyewe hata bila fedha za wafadhili, nami nitakuja kuzindua umeme hapa."

Mheshimiwa Spika, naomba kujua Serikali au Wizara, imepata ahadi hiyo ya Rais Wilayani Longido? Wizara inawaambia nini wananchi wa Longido kuhusu umeme huo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, napenda kuelezea Mgodi wa *Ruby* unaoitwa *Longido Ruby Mine.* Mgodi huu ni maarufu sana nchini kwa kutoa *Ruby* nzuri. Mgodi huu ni wa muda mrefu sana, unaozalisha madini. Naomba kujua Serikali inapata kiasi gani kwenye mgodi huu?

Pili, kuna utaratibu ambao migodi inachangia vijiji vilivyoko kweye maeneo ya migodi, lakini, mgodi huu haujawahi kuchagia mradi wowote kwenye kijiji husika. Naomba Wizara itoe taarifa kwenye mgodi husika nao watoe misaada kwa vijiji vinavyouzunguka. Kwa sasa uhusiano wa wa nchi na watendaji wa mgodi huo sio mzuri kabisa. Naomba msaada wa Wizara, kabla hali hiyo haijawa mbaya zaidi na kusababisha ugomvi mkubwa. Nawatakia kazi njema na mafanikio kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. kwa kazi nzuri. Nampongeza pia Naibu Waziri na timu yake yote ya wataalamu.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 18 Julai, 2006 wakati tunapitisha bajeti ya Wizara hii, katika hoja hiyo nilichangia kwa maandishi na kumwomba Waziri anieleze kama vifungu hivyo vitaipa nguvu *TANESCO* kufikisha umeme Peramiho. Majibu ya Mheshimiwa Waziri, nanukuu: "Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu au kumpa ufafanuzi Mheshimiwa Mhagama kama ifuatavyo: Mimi nakubaliana na Mheshimiwa kwamba, Mji wa Peramiho ni Mji muhimu na Serikali imepanga kwamba katika mwaka 2006/2007, kazi ya kujenga na kufikisha umeme Peramiho itafanyika."

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, naomba kufahamu kama *TANESCO* itatimiza ahadi hiyo kwa mwaka huu wa fedha wa 2007/2008, vinginevyo, ninaomba Wizara ikatolee maelezo kwa wananchi kwa nini ahadi hii haijatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, madhara yatokanayo na machimbo ya kokoto katika eneo la Lilondo na Lipokela. Kware ya Lilondo ilianza mwaka 2000, mwaka 2004 *TANROADS* walimilikishwa eneo la ukubwa wa heka 19.5. Makazi ya wananchi yako mita 800 toka eneo husika la uchimbaji. Uchimbaji hufanywa kwa kulipua (kutumia baruti).

Hadi sasa ukubwa wa eneo lililochimbwa ni mita za mraba 49,000. Athari zinazowapata wananchi ni pamoja na kelele za mlipuko wa baruti zinazosababisha mshituko kwa wananchi; vumbi; na mashimo makubwa yenye muonekano wa uharibifu mkubwa wa mazingira

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maliasili hiyo ya madini iko katika eneo la kijiji halali kilichosajiliwa, ni vyema haya yafuatayo yafanyike: Wamiliki wa kware hizo washirikiane na wananchi katika kurudisha hali ya mazingira bora, kwa kupanda miti kuzunguka eneo hilo ili kuzuia vumbi na kelele; na kuchangia shughuli za maendeleo za wananchi katika maeneo husika *(Cooperative Society Respinsibility).*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuipongeza timu nzima ya Wizara kwa utendaji mzuri.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa kuwa asilimia chini ya kumi ya Watzania ndio wanaopata umeme; na kwa kuwa hata hao asilimia kumi siyo wote wanaoweza kutumia umeme kwa matumizi ya nyumbani kama kupikia; na kwa kuwa sera na maelekezo ya sasa kuhusu matunzo ya mazingira yamefanya mkaa kuwa ghali sana (shilingi 25,000 – 30,000 kwa gunia) Dar es salaam; na kwa kuwa makampuni kama *Moto Poa Ltd*. yamefanya jitihada kutafuta njia mbadala. kwa kutengeneza majiko maalumu *(Moto Poa Stove)* na mafuta maalumu (Moto Poa – Mafuta Mazito), yanayotokana na mazao mbalimbali kama mihogo, *jatrofa, sunflower,* ambayo bei yake ni ndogo, matumizi yake hayana athari kwa mazingira na mtumiaji; je, Serikali iko tayari kushirikiana na Kampuni hii, kufanya utafiti wa kina kuona namna bora ya kuendeleza mradi huu na kufikia nchi nzima ili kuwanufaisha wananchi wa kawaida?

Pili, kwa vile tayari bei ya jiko na mafuta na wakipunguziwa *Import Duty* na *VAT,* bei itakuwa ndogo zaidi; Serikali ina mpango gani wa kuiondolea Kampuni kodi hizo ili mwananchi wa kawaida anufaike na wakati huo huo nishati hii mbadala isaidie jitihada zetu za kuhifadhi mazingira?

Tatu, kwa utaratibu huo huo, Serikali ina mpango gani wa kusaidia *TPDC* ambayo ni kampuni yetu katika jitihada zake za kutengeneza majiko ya gesi asilia na matumizi ya gesi asilia kwa magari? Kwa nini Serikali isitoe mtaji zaidi kwa Shirika hili ili azma ya yetu ya kupata nishati mbadala iweze kukamilika ikiwa ni pamoja na kuwaondolea kodi na ushuru wote wanaotozwa hivi sasa? Inashindikana nini kufanya hivi iwapo makampuni ya nje tunawapa *Tax Holiday?*

Nne, ni kitu gani kinaifanya Serikali kusita deni la Dola za Marekani 1,898,562 na riba ya Dola 62,929 kwa wakili wa mdai *M/S Hunton & Williams*, wakati deni hili limetokana na uamuzi wa Serikali yenyewe wa kusitisha mkataba wa uagizaji mafuta kati ya Shirika la *TPDC* na *Addax* mwaka 1999/2000? Serikali haioni kwamba, deni hili licha ya kuendelea kupanda kadri tunavyochelewa kulipa, pia linawakatisha tamaa uongozi na watumishi wa *TPDC?* Tano, kwa kuwa nchi yetu inaelekea kuwa na baraka ya kujaliwa kiasi kikubwa cha gesi asilia ambayo ni mkombozi mkubwa katika nchi yetu kwa upande wa nishati: Ni kwa nini ili kuwa na utaratibu mzuri wa nishati hii, Serikali isiwe na mpango wa unaoeleweka wa kuweka makampuni yote yanayoshughulika na gesi chini ya usimamizi wa *TPDC* na au kuunda chombo *(Regulator)* chini ya *TPDC?*

Mwisho, kwa kuwa Duniani kote, Serikali zinahangaikia utafutaji na usimamizi wa nishati; ni kwa nini Serikali baada ya bahati na neema hii, inasita kutenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa nishati hii? Je, ni kweli jambo zito hili linastahili kupewa shilingi 315 milioni tu? Ningependa kupata maelezo ya kina kwa nini tunashindwa kuona eneo hili kama *priority area* ili patukomboe baadaye?

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Katibu Mkuu, Ndugu Athur Mwakapugi na Wataalamu wote, kwa hotuba na mpango mzuri sana.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara ilituahidi kupeleka umeme katika Vijiji vya Handeni na Kiwanja katika Kata ya Lang'ata, eneo la Nyumba ya Mungu na Vijiji vya Kwakoa na Ngulu, vyote katika Wilaya ya Mwanga. Tunategemea kuwa mwaka huu wa fedha, Wizara itatekeleza ahadi yake.

Napenda pia nikumbushe kuwa wananchi wa Mwanga, waliilipa *TANESCO* mwaka 2004 ili iwaunganishie umeme kati ya mwaka 1998 na 2004, lakini hadi leo hawajapewa umeme walioulipia. Katika vikao vya mwaka 2002, 2003 na 2004, nilipewa ahadi kuwa ifikapo Desemba, 2004, wananchi hao watapewa umeme. Naomba suala hili litatuliwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Asante.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba nzuri, ambayo ameitoa asubuhi hii. Ni ukweli usiopingika kwamba, hotuba yake imetoa mwelekeo mpya na hivyo, kutujengea matumaini mapya katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo nchini mwetu.

Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha, naomba kuchukua nafasi hii kupongeza sana mipango yote iliyowekwa mbele yetu.

Ninaomba nikumbushie miradi mbalimbali ambayo ipo katika Wilaya ya Siha. Nafurahi kwamba, Makao Makuu ya Wilaya ya Siha (BOMA), yemeunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa. Hata hivyo, Viongozi wa Wizara waliopita, walifanya ziara katika Wilaya Mpya ya Siha na kuahidi kwamba, watahakikisha kwamba, vijiji vifuatavyo vinapelekewa umeme Kata ya Siha Kaskazini; Kijiji cha Mowo Njamu, Nrao Kisangra, Nshre-hehe, Samaki Maini Mesa na kadhalika. Kata ya Siha Kati; Kijiji cha Naibilie, Makiwaru, Ngaritati, Olkolili na Kijiji cha Olmelili. Aidha, katika Kata hii bado Vijiji vya Donyomoruou na Ngumbaru hakuna kabisa dalili za kuunganishiwa umeme kutoka kituo cha jirani cha kusambazia umeme kilichopo katika Kijiji cha Lawate.

Kipo kilio cha muda mrefu cha wananchi wa *West Kilimanjaro*, ambao Kata nzima haijaunganishwa na umeme ambao tayari upo Wilayani Siha. Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. R. Msabaha, ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini na baadaye Waziri Kamili, aliahidi Wizara itaangalia uwezekano wa kupata umeme katika Kata hiyo kwa kupitia Mpango wa Wizara uitwao *Energizing Rural Transformation Programme* au Mpango unaofanana na huo. Kata ya *West Kilimanjaro* ndiyo yenye mashamba makubwa ya *TBL, NAFCO, NARCO* na kadhalika. Si hivyo tu, ndiyo Kata ambayo *LONDROS Gate* ipo, ambayo hupitisha watalii wengi ambao wanapanda Mlima Kilimanjaro. Napenda tu kusema kwamba ni mgongano kutokuwa na umeme katika eneo la *West Kilimanjaro*, ambalo Taifa zima linajua umuhimu wake kwa kuongeza Pato la Taifa.

Kata hii ni maarufu kwa mazao yafuatayo; njegere, viazi, mbogamboga, mbao (msitu wa Taifa upo katika eneo hili), shairi, ngano, maharage na kadhalika. Kwa kifupi, tatizo la umeme katika Wilaya Mpya ya Siha ni lile la kushindikana kutawanyika kwa umeme katika maeneo mbalimbali. Usambazaji wa umeme katika maeneo niliyoyataja ni tatizo kubwa, jambo ambalo linawanyima wananchi wa wilaya hii kushiriki kikamilifu katika kupambana na adui umaskini. Nimewahi kuwasiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri katika suala hili na pia Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Aidha, nimewasiliana na Viongozi wa Shirika la Umeme Tanzania na nimepata ahadi ambazo naamini zikitekelezwa, tatizo la umeme katika Wilaya ya Siha litakuwa limekwisha.

Narudia tena kusema naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Ninaomba sana matatizo niliyoyaainisha hapo juu, yaweze kutatuliwa. Nashukuru kwa jitihada ambazo zimejitokeza kwenye baadhi ya maeneo ya Siha.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nimesoma Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini kwa umakini sana. Hotuba ni safi na fasaha. Hata hivyo, ningependa kupata ufafanuzi ufuatao:-

Kwanza, umeme kwa Wilaya ya Kasulu, ambayo imesubiri kwa zaidi ya miaka 46 sasa, tegemeo lake ni Mradi wa Umeme utakaofadhiliwa na Mfuko wa *MCC* kupitia Maporomoko ya Mto Malagarasi. Je, endapo *MCC* watachelewa kwa sababu yoyote iwayo, nini *fall back* ya Serikali katika Mradi huu? Je, isingekuwa busara kuendeleza Mradi wa Maporomoko ya Mwoga yaliyopo Kasulu ili baadaye umeme wake uingizwe katika mfumo mkubwa wa umeme; uwe wa Gridi au huu wa Malarasi?

Pili, Ukurasa wa 33, kifungu cha 76; kwa nini Mradi wa Umeme wa Jua utekelezaji wake usilenge Mikoa isiyo na umeme kwa mfano, Kigoma?

Mikoa ya Rukwa na Ruvuma imepangiwa katika Mradi huo. Kwa nini Mikoa yenye umeme wa uhakika kama Mbeya na sasa Mtwara, iwekwe tena kwenye Mradi wa Umeme wa Jua? Tunagawanaje rasilimali chache hizi? Hivi Mkoa wa Kigoma ni lini utakuwa *priority* katika Sekta ya Nishati katika nchi yetu? Kigoma inashangaa na mimi ninashangaa na hata watu wenye nia njema na usawa wa nchi yetu, wanashangaa! Napendekeza Mkoa wa Kigoma uwekwe katika utekelezaji wa Mradi huu.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba ya Bajeti na namna ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Aidha, naipongeza Wizara kwa namna ya pekee, kwa jinsi ilivyoshughulikia maombi ya wananchi wa Sikonge kuwaletea umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taarifa za awali zinazothibitisha baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Sikonge kuwa na madini, wataalamu wenu wa Tabora walikwishafika. Naiomba Wizara iendelee kufanya utafiti wa kina ili wananchi wa Sikonge nao waweze kufaidika na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, toka umeme wa Gridi ya Taifa upelekwe Sikonge ni maeneo ya Kijiji cha Tutuo na Sikonge Mjini tu ndiyo yamepata umeme. Vijiji vilivyopo njiani mfano Pangale, Mpombwe, Ibaya, Mlogolo na Mkolye, havijapatiwa umeme, ingawa jitihada zimeanza Kijiji cha Pangale. Naiomba Wizara kupitia *TANESCO,* ipeleke umeme Kijiji cha Mole na Usanganya, pamoja na Kata za Chabutwa, Ipole, Kipanga na Kiloleli.

Mheshimiwa Spika, wakati wa zoezi la utengenezaji wa barabara ya nguzo za umeme toka Tabora – Sikonge, baadhi ya wananchi waliharibiwa mazao yao na

kuahidiwa na *TANESCO* fidia, lakini mpaka sasa fidia hiyo haijatimizwa. Naiomba Wizara ihakikishe ahadi hiyo inatimizwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naitakia kheri Wizara kwa utekelezaji wa shughuli zake kwa mwaka ujao wa fedha. Naunga mkono hoja.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kwa dhati ya moyo wangu, kuipongeza Serikali kwa kuhakiksiha kuwa ujenzi wa Gati la Mafia sasa unaanza, ujenzi wa uwanja wa ndege na kupata vifaa vya ujenzi wa barabara. Kwa niaba ya wananchi wa Mafia nasema shukrani.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Idara zake.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kutaka kufahamu kuhusu nishati ya umeme, ambayo ndiyo tunayoitumia katika Wilaya ya Mafia na ukizingatia kuwa Mafia ni kisiwa na ni lazima tuweze kuiokoa kimazingira kwa kuboresha na kutunza misitu asili michache iliyopo. Hivyo, utunzaji huo ambao inabidi lazima ufanyike kwa kuokoa misitu iliyopo. Njia kuu ni kuboresha nishati iliyopo Mafia kwa maana ya kwamba, majenereta mawili yaliyokuwepo ni mabovu na pia hayatoshelezi nishati yake kwa watumiaji.

Je, ni lini Wizara itatuletea mashine (mitambo), yenye uwezo wa kuzalisha *megawatt* mbili ambazo kwa sasa zinaweza kukidhi mahitaji hapa Mafia?

Mheshimiwa Spika, Mafia kuna kisima cha mafuta, kilichochimbwa toka mwaka 1954 na Kampuni ya *BP.* Je, ni nini hatma ya kisima hicho? Je, Kampuni ya *MOUREL AND PROM,* ambayo imeingia Mkataba wa Utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia; kwa nini isikabidhiwe kisima hicho ili ijulikane kama yapo mafuta au hakuna?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo, nataka pia kufahamu Mradi wa Umeme wa Kutumia Upepo *(Windmill),* utaanza kama Shirika la Umeme *(TANESCO),* lilivyoahidi miaka mitatu iliyopita?

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nawashukuruni tena Viongozi wangu wote wa Serikali na Chama changu cha Mapinduzi, kwa kuanza kufungulia milango ya maendeleo Wilaya ya Mafia. Hongereni wote na Mola atawabariki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kumpongaza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu mbalimbali wa Wizara hii, kwa kuandaa hotuba nzuri na iliyokidhi haja ya kuendeleza sekta hii katika nchi yetu.

Pili, mchango wangu ninauelekeza katika mambo yafuatayo: Ukosefu wa vifaa vya *service line* ni sugu kwa muda mrefu katika Mji wetu wa Korogwe na Wilaya Korogwe kwa ujumla. Wapo wateja wengi sana ambao wamelipa fedha zao kwa ajili ya kuwekewa umeme majumbani kwao, lakini inashindikana kwa sababu hakuna vifaa vya *service line*. Wananchi wamechoka kusubiri, imefikia hatua sasa *TANESCO* – Korogwe hawachukui fedha tena kwa kuogopa lawama. Hivi hali hii imesababishwa na nini?

Mheshimiwa Spika, hii ni biashara; hivi kweli *TANESCO* – Korogwe wameshindwa kununua vifaa vya *service line?* Naomba tatizo hili litafutiwe ufumbuzi wa haraka. Ninaomba pia kupatiwa majibu ya kuridhisha. Wananchi wa Korogwe wamechoka kupata ufumbuzi. Jambo hili ni sugu, ninaomba lipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu toka nimeingia ndani ya Bunge hili mwaka 1995, niliomba Kijiji cha Kwameta kipatiwe umeme. Mimi mwenyewe nimefanya jitihada kubwa ili kijiji hicho kutimiza vigezo vyote vinavyostahili. Idadi ya nyumba zinazostahili kupatiwa umeme zimekamilika. Wananchi wengi kwenye nyumba hizo wameweka *wiring.* Zipo ahadi zaidi ya mara mbili kwamba, watapatiwa umeme kwa awamu, lakini leo hii nimekuwa Naibu Waziri sijapata umeme huo. Ninaomba sasa mwaka huu nipatiwe umeme katika kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, Mjini wa Korogwe umepata hadhi ya kuwa *Korogwe Town Council.* Mji unapokuwa na hadhi hiyo ni lazima ue na umeme. Yapo maeneo ya *Mtonga Juu Habitat,* Kwasemangube, Kilolerwengera, Darajani na Relini, ni muhimu maeneo haya kupata umeme. Hapo ndipo hadhi ya Mji wa Korogwe itavyoonekana, lakini hali sivyo ilivyo sasa. Ninaomba kupata majibu hivi ni kwa nini? Ninaomba kupatiwa umeme Mji wa Korogwe?

Mheshimiwa Spika, ninashauri sana na kuomba umeme uwekwe kwenye sekondari zangu za Korogwe Mjini. Sekondari hizi zote zipo karibu sana na nguzo kuu za umeme. Sekondari hizo ni Chifu Kimweri, Old Korogwe, Kilole, Ngombezi, Semkiwa na Kwamndolwa. Shule hizi zipo Mjini lakini hazina umeme. Inasikitisha kuona umeme unapita juu ya shule na shule haina umeme. Naomba sasa shule hizo nipatiwe majibu ya kupatiwa umeme kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Wizara husika isaidie kufanikisha kupata umeme kutoka chanzo cha umeme cha *Ngombezi Sisal Estate,* usaidie Wilaya ya Korogwe. Wataalam wanasema Ngombezi kwa kutumia maji ya Mto Pangani, wanaweza kupata umeme wa *megawatt* 3.5. Huu ni umeme wa kutosha matumizi ya Wilaya yetu ya Korogwe. Ninaomba Wizara ilishughulikie suala hili.

Upo umuhimu wa kuwapeleka watafiti pale ili umeme uletwe kwa manufaa ya Taifa. Jambo hili ninalichangia kila mwaka lakini sijapata jibu. Ninaomba jibu sahihi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii muhimu, ila nasisitiza utekelezaji wa kero zangu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokwishawatangazia, sasa ni zamu Naibu Waziri na baadaye Mheshimiwa Waziri mwenyewe mtoa hoja. Halafu ndiyo tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, sasa nafurahi kumwita Mheshimiwa Naibu Waziri ili aweze kuchangia. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru kunipa fursa ya kuchangia hoja ya makadirio ya matumizi ya fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2007/2008 kama ilivyowasilishwa mbele yako na Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi - Waziri wa Nishati na Madini tarehe 13 Julai, mwaka huu 2007.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kuanzia tarehe 11 Januari, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Anne Makinda - Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri wa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano mnaonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake mahiri na shupavu.

Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi - Waziri wa Nishati na Madini kwa kuniamini, kunishirikisha na kuniongoza kuisimamia Wizara ya Nishati na Madini. Amekuwa msaada mkubwa kwangu. Pia namshukuru Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe - Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa mwongozo alioniachia wakati akiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wapiga kura wangu, wananchi wa Jimbo la Sengerema, pamoja na viongozi wa Chama na Serikali wa Wilaya ya Sengerema kwa ujumla kwa ushirikiano wanaonipa. Nawapongeza sana kwa kufanikisha ujenzi wa shule za sekondari katika Kata zote 25 za Halmashauri ya Wilaya yetu ya Sengerema na hatimaye kufanikisha kupeleka wanafunzi wote waliofaulu mtihani wa darasa la saba kwa mwaka 2006 kujiunga na masomo ya sekondari kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mafanikio haya yamepatikana chini ya uongozi thabiti na imara wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza - Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela. Namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Msekela. Naomba tuendelee kushirikiana ili kufanikisha malengo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru mke wangu Blandina Ngeleja, kwa kunilea, kunitunza, kunishauri na kuendesha majukumu ya familia yetu. Mwenyezi Mungu azidi kumjalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kutoa salamu za rambirambi kwa familia za Marehemu waliofariki hivi karibuni kwa ajali mbalimbali zikiwemo za magari na nyingine ikiwemo Mikoa ya Mbeya, Arusha na Singida, zikiwemo familia za waliokuwa Wajumbe wa Bodi ya Chama Kikuu Cha Ushirika Mkoani Mwanza *NCU*, Marehemu Stephen Kazi, Marehemu William Kasubi na Mzee Hezron Ndono.

Pia natoa pole kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa Mpachanjia. Namwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi. *Amin!*

Aidha, ninawaombea majeruhi wakiwemo Mheshimiwa Modesta Bulugu - Diwani wa Viti Maalum Sengerema na Kaimu Mwenyekiti wa Nyanza *NCU* anayetibiwa hospitali ya Muhimbili, wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani na salamu hizo, sasa naomba kuchangia kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuchangia kwa kufafanua hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kuongea hapa Bungeni. Nitaanza na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga - Mbunge wa Tabora Mjini, ambaye aliwasilisha taarifa kwa niaba ya Kamati ya Biashara na Uwekezaji. Kulikuwa na hoja kadhaa, kwamba Wizara isaidie kwa ukaribu zaidi kuirekebisha *STAMICO* ili shirika hilo liweze kuitumika kuendeleza wachimbaji wadogo na kutoa ushauri. Hii ilikuwa ni hoja ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, ushauri tumeupokea na Serikali inakamilisha mchakato kuhusu hatima na majukumu ya *STAMICO.* Hoja ya pili, ilikuwa wachimbaji wadogo wa Mererani waungane ili waweze kupata maeneo makubwa. Tunakubali ushauri, tutaendelea kuwashawishi wachimbaji hao waungane ili wapate maeneo makubwa kupunguza msongamano, wachimbe kitaalam na kuondoa tatizo mitobozano. Sheria ya Madini iangaliwe upya kuhusu uchimbaji wa madini wima kwa kuwa madini ya *Tanzanite* yanakwenda mshazari. Hii ilikuwa ni hoja nambari tatu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya mwaka 1998 haimlazimishi mchimbaji kwa kwenda wima, bali inawataka wachimbaji kuchimba ndani ya maeneo yao na kuheshimu mipaka ya leseni ambayo ni lazima iwe wima kuelekea chini ardhini. Kuruhusu uchimbaji bila kuzingatia mipaka ya leseni kuna athari kubwa kiusalama na kunaweza kusababisha maafa. Hoja nyingine ilikuwa itungwe sheria ya kuzuia wageni kuchimba madini ya vito. Ushauri tumeupokea. Suala hili litajadiliwa wakati wa kudurusu Sera na Sheria ya Madini.

Hoja nyingine ilikuwa vijengwe viwanda vya kuchonga vito karibu na kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro. Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhamasisha uanzishaji na utekelezaji wa mpango wa kuanzisha *EPZ* ya viwanda vya vito katika eneo hilo.

Hoja nyingine ilikuwa watalaam wa Kitanzania waliokuwa wanafanya kazi na Alex Stuwart watumike kujenga uwezo wa ndani wa Wizara. Ushauri huu tumeupokea na tunaahidi kuendelea kuufanyia kazi.

Hoja nyingine ilikuwa, Chuo cha Madini Dodoma kijengewe uwezo zaidi. Ushauri huu tumeupokea. Katika mwaka 2007/2008 Wizara itaendelea kukiimarisha Chuo. Fedha zimetengwa kwa ajili ya mafunzo kwa wakufunzi na ujenzi wa miundombinu inayojumuisha maabara, maktaba na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, alichangia kwa kutoa hoja kadhaa. Hoja ya kwanza, alitaka kujua Watanzania wanashirikishwa vipi kumiliki migodi mikubwa. Sheria ya Madini ya mwaka 1998 inatoa fursa sawa kwa wageni na Watanzania katika umiliki wa migodi mikubwa. Tatizo lililopo kwa Watanzania ni ugumu wa kupata mitaji na kwa namna nyingine ujasiriamali hafifu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni ilikuwa, ni kampuni zinapouza hisa nje ya nchi, Serikali inapata nini? Kulingana na Sheria ya Kodi ya mwaka 2004, hisa zinazomilikiwa ama nje au ndani ya nchi zinapouzwa hazilipiwi *capital gains tax* mauzo ya hisa ndani ya nchi hulipiwa *stamp duty* ya asilimia moja ya hisa. Lakini zinazomilikiwa nje ya nchi na kuuzwa huko huko hazilipiwi *stamp duty* kwa vile ziko nje ya mamlaka ya sheria za kodi. Hata hivyo, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi, Wizara ya Nishati na Madini inaahidi kushirikiana na Wizara ya Fedha na *TRA* kupata uzoefu wa nchi nyingine na kulifanyia kazi suala hili ili kuangalia namna Taifa linavyoweza kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyoletwa mbele yetu hapa na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni ilikuwa, kama makampuni yanatoa *good will tax,* ni kweli makampuni hayo hayapati faida? Kampuni kubwa zinazochimba madini ya dhahabu hazijaanza kupata faida na hivyo hazilipi kodi ya mapato ya kampuni, yaani *corporate tax,* kampuni hizo pia hazilipi *good will tax* bali zinalipa malipo ya *ex-gratia* kwa mujibu wa makubaliano. Hata hivyo, kampuni hizo zinalipa kodi nyingine kama kodi ya zuio, *withholding tax* kodi ya mapato *(PAYE)* kodi ya mishahara, *levy,* vina kodi ya kuingiza bidhaa nchini *(import duty).*

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, alikuwa na hoja kadhaa. Hoja ya kwanza ilikuwa ni upotevu wa takribani shilingi bilioni 70 kuhusu ratili za almasi, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba fedha zilipotea. Kilichotokea ni tofauti ya kumbukumbu. Hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni kuwa Wizara haikuhakiki kiasi cha karati 473,051.90 za almasi zilizosafirishwa nje na *Williamson*

*Diamonds Limited* kati ya Januari, mwaka 2004 na Oktoba mwaka 2005 zenye thamani ya dola za Kimarekani 56,934,749.09 ikiwa ni sawa sawa na Sh. 71,343,794,390/= kwa kuzingatia mabadiliko ya *Exchange Rate* wakati huo. Maafisa wa Wizara ya Nishati na Madini na *TRA* walihakiki almasi hizo kabla hazijasafirishwa nje ya nchi. Sh. 71,343,794,390/= ni mapato, yaani *sales revenue* kwa *Williamson Diamonds Limited* kwa ajili ya mauzo ya almasi na hayakuwa mapato ya Serikali.

Hivyo, siyo sahihi kusema kuwa Serikali ilipata hasara ya Sh. 71,343,794,390. Kutokana na mauzo hayo. Serikali ilipata jumla ya dola za Marekani 4,590,643.83 sawa na Sh. 5, 752,443,889/=. Dola 2,128,733.60 zilikuwa ni ada ya uchambuzi na dola 2,461,910 ni mrabaha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu upotevu wa shilingi trilioni 1.3 kwa mujibu wa taarifa ya Alex Stewart kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alichangia. Taarifa ya Alex Stuwart haijasema kuna upotevu wa *Tanzania shillings 1.3 trillion,* isipokuwa imesema ukaguzi wa migodi ya Bulyanhulu, *Geita Gold and Pride* na *North Mara* hadi mwaka 2003 imebaini kuwa kuna matumizi ya takriban shilingi bilioni 1.12 ambazo tayari nyaraka au vielelezo vya kutumika kwake mbazo hapakuwa na *documents* za ku-*support.*

Aidha, imesema, matumizi haya yanahusika na gharama ya uwekezaji na uendeshaji wa migodi hiyo. Serikali imeanza kuifanyia kazi taarifa ya Alex Stewart ikiwa ni pamoja na kufuatilia kuhusu nyaraka za matumizi hayo. Hivyo, sio vyema kuanza kutumia taarifa ambazo hazina uthibitisho na za upande mmoja kuwa ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa mkataba kati ya Serikali na *Williamson Diamonds Limited* wa mwaka 1994 unaonyesha kuwa baada ya miaka mitano *Williamson Diamonds Limited* ingeanza kulipa kodi kwa Serikali. Kwa nini hawajaanza kulipa kodi mpaka wakati tunaongea?

Mheshimiwa Spika, *Williamson Diamonds Limited* haijalipa gawio kwa wanahisa wake wote wawili, yaani *De Beers* na Serikali ya Tanzania kutokana na kwamba mtiririko wa ukwasi, yaani *cash floor* ya kampuni haijawa nzuri. Vile vile tangu mwaka 1994 *Williamson Diamonds Limited* haijalipa kodi ya mapato ya Kampuni ya *Corporate Tax* kutokana na kampuni kuwa na malimbikizo ya hasara ya miaka mingi, yaani *accummulated losses* licha ya kwamba *Williamson Diamonds Limited* ilipata faida katika miaka ya 2000 na mwaka 2004.

Hata hivyo, *Williamson Diamonds Limited* imekuwa ikilipa mrabaha na kodi kama vile kodi ya zuio, kodi ya kuagiza vifaa kutoka nje, kodi ya mishahara na kodi ya barabara. Kati ya mwaka 1997 na mwaka 2005 *Williamson Diamonds Limited* ililipa mrabaha na kodi mbalimbali zenye jumla ya takriban Dola za Marekani milioni 20.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi. Alikuwa na hoja kadhaa, hoja ya kwanza

ilikuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu wa ukanda wa Mlima Sekenke waliomba wapewe leseni. Alitaka kujua jambo hili limefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Sekenke, Wizara imetoa leseni nane kwa wachimbaji wadogo waliokuwa wamewasilisha maombi yao. Kama kuna maombi mengine, Wizara itayashughulikia kwa mujibu wa sheria. Tunamwahidi Mheshimiwa Mbunge, kama yapo mengine tutaendelea kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilikuwa imetolewa na Mheshimiwa Killimbah, ilikuwa wachimbaji wadogo walioko katika maeneo ya Kifuma na Misuna wamilikishwe maeneo hayo. Katika eneo hili kuna leseni moja ya uchimbaji mdogo wa madini ya *zircon* na maombi matano yamepokelewa na yanashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti - Mbunge wa Misungwi. Yeye alikuwa na hoja kadhaa. Hoja ya kwanza ilikuwa wachimbaji wadogo waliogundua dhahabu eneo la Buhunda, wamevamiwa na kunyang'anywa eneo lao na Kampuni ya *East Africa Mines.* Ufafanuzi wetu ni kwamba, mgodi ambao awali ulikuwa unaitwa *East Africa Mines* inayo leseni Na. 1563 ya mwaka 2000 ya ukubwa wa kilometa za mraba 12.98 katika eneo la Buhunda.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo kulikuwa na wachimbaji wadogo, walikuwa wanachimba bila ya kuwa na leseni. Ndiyo maana hawakutambuliwa kisheria wakati wa utoaji wa leseni hiyo. Tunamwomba sana Mheshimiwa Mbunge na viongozi wengine tushirikiane kuwasaidia kutambuliwa kisheria wakati wa utoaji wa leseni hiyo. Tunamwomba sana Mheshimiwa Mbunge na viongozi wengine kuwahamasisha wachimbaji wadogo kuomba na kupata leseni katika maeneo wanayoyahitaji ili wawe na haki ya kuyamiliki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kampuni ya *East Africa Mines* kufukuza wachimbaji hawa wadogo, haitoi mchango wowote kwa vijiji jirani tofauti na Kampuni ya *Sub-Sahara* inayofanya utafiti wa dhahabu katika eneo la Ilubili iliyotoa mchango wa shilingi milioni tano kwa ujenzi wa shule. Hii ilikuwa ni hoja ya pili ya Mheshimiwa Shibiliti. Wizara itawasiliana na uongozi wa kampuni ya mgodi ili kuihamasisha kujenga mahusiano ya karibu na wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Ruth Msafiri - Mbunge wa Muleba Kaskazini. Hoja yake ambayo amechangia ambayo inaangukia katika Sekta ya Madini ilikuwa inahusu mchakato wa kudurusu Sera na Sheria ya Madini iendelee kwa bidii hususan eneo la utoaji na usimamizi wa leseni za madini ili kusaidia kuongeza mchango wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, ushauri huo tumeupokea. Kama tulivyosema kwenye bajeti yetu Muswada husika tutauwasilisha Bungeni mbele yako mwaka huu wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro alikuwa mchangiaji mwingine, Mbunge wa Jimbo la Mkinga. Yeye alikuwa na hoja kadhaa. Kasi ya kuimarisha Shirika la *STAMICO* ni ndogo. Serikali itoe uwezo wa Shirika hilo ili liweze kutoa mafunzo ya uchimbaji na teknolojia kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni hoja ya kwanza ya Mheshimiwa Mwandoro. Ni kwamba, ushauri tumeupokea. Tutauzingatia wakati wa kukamilisha mchakato wa hatima ya *STAMICO.*

Hoja nyingine ilikuwa, ardhi ya wananchi ithamanishwe na iwe hisa ya wananchi kwenye migodi na hisa zitolewe tokea mwanzo. Ushauri huu tumeupokea pia. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini, madini yaliyo chini ya ardhi ni mali ya umma. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuiona sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe. Yeye alitaka kujua Kampuni ya *Resolute* iko katika eneo la Nyakafuru na Masumbwe kwa miaka 10 sasa. Kama wamekosa madini waondoke ili wananchi wa maeneo hayo wachimbe.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu uliopo, shughuli za utafutaji madini zinachukua muda mrefu kabla ya mgodi kuanza. Kwa mfano migodi ya Bulyanhulu na Geita ilifunguliwa takriban baada ya miaka 30 ya utafiti uliofanywa na kampuni mbalimbali ikiwemo *STAMICO.* Kwa sasa kampuni ya *Resolute* inafanya utafiti wa kina, *detailed exploration* ukihusisha uchorongaji wa miamba, kuchukua sampuli za miamba, *core samples* kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira ili utafiti unaofanywa na kampuni hiyo ukamilike.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine aliyotoa Mheshimiwa Luhahula, ilikuwa, Serikali itenge eneo la Matabe kwa wachimbaji wadogo. Tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tayari Wizara yetu imeshaanza kuufanyia kazi. Wafanyakazi wa mgodi wa Tulawakwa wanaishi Kijiji cha Uyovu. Mgodi huo umechangia nini katika kijiji hicho cha Uyovu? Tutawasiliana na uongozi wa mgodi huo kuhamasisha mahusiano mema na vijiji jirani ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni ya Mheshimiwa Luhahula, ilikuwa kwamba marekebisho yafanyike katika ukurasa wa 49 wa mwambata wa hotuba ya Wizara. Vijiji vya Nungwiza, Ushirombo na Kanegele viko Bukombe na siyo Kahama. Ni kweli kwamba Vijiji vya Nangwiza, Ushirombo na Kanegele viko Wilayani Bukombe, marekebisho yatafanyika. Tunaomba radhi kwa hili na tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuiona kasoro hiyo.

Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina - Mbunge wa Geita alipata nafasi ya kuchangia na alisema hoja kadhaa. Hoja ya kwanza ilikuwa fidia ya wananchi 557 wa Kijiji cha Katoma wapo tayari kulipwa. Watu watatu wamepeleka kesi Mahakamani. Alitaka kujua kwamba kwa nini Serikali isiwalipe wale ambao wako tayari kulipwa wakabakia hawa watatu?

Mheshimiwa Spika, Serikali na Kampuni ya *Geita Gold Mine* imesikia kilio cha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Katoma kwa ujumla. Pamoja na watu hao watatu hao kuweka pingamizi, hundi za malipo kwa wananchi 553 waliokubali kulipwa fidia zimeandaliwa na zitapelekwa kwa Mkuu wa Wilaya ili wahusika walipwe.

Tunaomba Mheshimiwa Mbunge kwa hili tuendelee kushirikiana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ya Mheshimiwa Mabina ilikuwa wananchi 111 ambao maeneo yao yalifanyiwa tathmini huko Nyamatagata, kati ya hao ni 41 tu waliolipwa, waliobaki walipwe. Kampuni ya *Geita Gold Mine* wamelipa fidia kwa wananchi 39 kwanza kutokana na wananchi hao kutakiwa kuondoka haraka ili kupisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa mgodi. Wizara itawasiliana na uongozi wa *Geita Gold Mine* kuhusu hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine aliyoitoa Mheshimiwa Mabina ilikuwa wananchi wa Geita hawajanufaika na mgodi wa Geita. Athari zilizotokana na mlipuko wa baruti tarehe 28 Novemba, 2006 katika eneo la Katoma hazijafidiwa. Athari hizo zifidiwe.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Nazir Karamagi alipotembelea Wilaya ya Geita, alishauri tathmini ya mlipuko huo ifanyike ili kubaini madhara yaliyotokea. Alishauri kuwa kama kuna mwananchi yeyote ambaye ameathirika na mlipuko huo afuate taratibu za kisheria kudai haki zake. Mpaka sasa hakuna aliyejitokeza.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo aliitoa Mheshimiwa Mabina ilikuwa kwamba, kwa kuwa Vijiji vya Katoma, Katani, Magema na Nyakabale viko ndani ya eneo la machimbo ya *Geita Gold Mine* wananchi wa vijiji hivyo wafidiwe na wahamishwe ili kupisha shughuli za mgodi.

Mheshimiwa Spika, ushauri huo tutauwasilisha kwa Kampuni ya Geita ufanyiwe tathmini kabla ya Serikali kutoa tamko. Hoja nyingine ambayo aliitoa Mheshimiwa Mabina ilikuwa kwamba wachimbaji wadogo wamehama kutoka Matabe na kwenda Nyamatagata. Wachimbaji wadogo hao waruhusiwe kuchimba eneo la leseni ya *Geita Gold Mine.*

Mheshimiwa Spika, kisheria hairuhusiwi kuchimba ndani ya leseni ya mtu mwingine bila ya ridhaa yake. Serikali inaangalia uwezekano wa kulitenga eneo la Matabe kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Tunamwomba Mheshimiwa Mabina avute subira wakati utaratibu wa kisheria unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Dorah Mushi - Mbunge wa Viti Maalum. Yeye alitaka kujua *Tanzanite* ni madini pekee yanayopatikana Tanzania, Mkoani Manyara tu. Wachimbaji wadogo wamekuwa wakichimba madini hayo kwa kipindi kirefu, Wawejipatia uzoefu na manufaa makubwa yalipatikana, kwa

nini Serikali iliwanyang'anya wazalendo machimbo ya *Tanzanite* na kuwapa wageni? Madini haya yachimbwe na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tunaheshimu sana maoni na hoja ya Mheshimiwa Mbunge, lakini tunataka kufafanua kwamba, sio kweli kwamba Serikali iliwanyang'anya wazalendo machimbo ya *Tanzanite* na kuwapa wageni. Machimbo ya *Tanzanite* yaliyogunduliwa mwaka 1966 yalikuwa yakimilikiwa na Serikali kupitia kampuni tanzu ya *STAMICO* iliyojulikana kama *TGI* hadi mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 1997 Serikali iliamua kuligawa eneo hilo kwenye vitalu vinne. Vitalu vyenyewe vilipewa majina ya A, B, C na D na kuvimilikisha kwa njia ya zabuni. Kufuatia matokeo ya zabuni na maombi ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro, vitalu hivyo viligawiwa kwa kampuni ya *Kilimanjaro Mines* kitalu 'A' *, Building Utilities* kitalu 'B' *,Graftan* kitalu 'C' na *Arema Enterprises* kitalu 'D'. Umiliki wa vitalu hivyo, umekuwa ukibadilika kwa nyakati mbalimbali kutokana na mazingira na matakwa ya wamiliki isipokuwa kitalu 'A'. Kufuatia mabadiliko hayo, kwa sasa wachimbaji wadogo wanamiliki vitalu 'B' na 'D' na kampuni ya Tanzanite *One* inamiliki kitalu 'D'.

Kuhusu pendekezo la Mheshimiwa Mbunge kuwa *Tanzanite* ichimbwe na Watanzania pekee, ni suala la kisheria na litajadiliwa wakati wa kudurusu sheria hiyo. Hata hivyo, tunatoa angalizo kwamba mabadiliko yote ya kisheria yatakayotokea hayatahusu umiliki wa sasa. Hii ni hoja ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine aliyoitoa Mheshimiwa Dorah, ilikuwa kwa mujibu wa sheria kwa kuwa sasa Mererani ni eneo zuifu *(controlled area),* ni kifungu gani cha sheria kimetumika kuwanyang'anya wachimbaji wadogo maeneo hayo na kuwapa wawekezaji wa kigeni?

Mheshimiwa Spika, ni kweli eneo la machimbo ya Mererani ni eneo zuifu kufuatia kutungwa kwa kanuni za *Mererani Controlled Area* za mwaka 2002. Hata hivyo, kanuni hizo hazihusu umilikaji wa vitalu vya uchimbaji. Umilikishaji wa vitalu hivyo ulifanyika tokea mwaka 1997 kwa mujibu wa Sheria ya Madini. Kanuni ya *Mererani Controlled Area* haifuti umilikaji huo.

Hoja nyingine aliyoitoa Mheshimiwa Mushi, ni kwamba makubaliano ya *Tucson Protocol* yamefanyiwa kazi? Alitaka kujua. *EPZ* iwekwe Mererani kwa kuwa ni katikati ya Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, makubaliano ya *Tucson* yalihusu ushirikiano wa Serikali na wadau kuboresha udhibiti wa mtandao mzima wa biashara ya *Tanzanite.* Kudhibiti sehemu za uzalishaji na uuzaji wa madini ya *Tanzanite* kuwa na hati ya uthibitisho wa *Tanzanite* halali, wanunuzi wa *Tanzanite* wa nje wakubali kununua *Tanzanite* iliyoambatana na hati ya uthibitisho wa madini kuanzishwa *EPZ.* Makubaliano hayo yamefanyiwa kazi na yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

Kwanza, Kanuni za *Mererani Controlled Areas* zinatekelezwa ili kudhibiti uchimbaji na uuzaji wa *Tanzanite.* Pili, hati ya uthibitisho inatolewa na Idara ya Madini. Tatu, Idara ya Madini inaweka takwimu za biashara za *Tanzanite.* Hata hivyo, mfumo wa kuhakiki na kuchambua mwenendo wa madeni ya *Tanzanite* nchini na nje ya nchi haujakamilika.

Suala la kuanzishwa kwa *EPZ* maalum kwa *Tanzanite* bado halijakamilika pia. Ushauri wa wadau ni kuwa *EPZ* hiyo ianzishwe sehemu ambayo inagusa Mikoa yote mitatu, yaani *tripple point.* Uchaguzi wa eneo husika utafanywa na mamlaka iliyohusika ambayo ni Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine aliyoitoa Mheshimiwa Mushi, ni minada ya madini iliyokuwa ikiandaliwa na *TAMIDA* haijafanyika kwa muda mrefu na hivi sasa inafanyika Afrika ya Kusini. Wizara iwe makini kwani tunakosa mapato kwa kuachia vitu vyetu holela. Tumepokea ushauri na tunaufanyia kazi.

Mchangiaji mwingine alikuwa kaka yangu, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa - Mbunge wa Lupa. Alikuwa na hoja kadhaa. Hoja ya kwanza ilikuwa, inapobadilishwa Sera na Sheria ya Madini iwanufaishe Watanzania. Alikuwa anatoa ushauri. Ushauri tumeupokea na tunaufanyia kazi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kuliona hili.

Pia aliongelea mtambo wa kusaga mawe wa Matundasi ulioigharimu Serikali dola za Marekani laki tano hadi sasa. Kwa miaka minne alikuwa anahoji kwa nini haujafanya kazi? Mtambo huu umekodishwa kwa mzalendo mmoja ambaye ameshindwa kuuendesha kutokana na kukosa vitendea kazi kama vile magari ya kusombea mawe, *pumps* za maji na *compressors*. Serikali ifikirie wazo la kuongeza vitendea kazi vilivyotajwa ili kuwasaidia wachimbaji wadogo.

Aidha, inaonekana kuna malumbano kati ya mzalendo aliyekodisha mitambo na Serikali. Nini hatima ya malumbano hayo? Ni vyema ufumbuzi upatikane haraka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imejenga Kituo cha Mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo na uchenjuaji dhahabu cha Matundasi Chunya. Ujenzi wa mtambo wa kuchenjua mawe wa kituo ulikamilika mwaka 2002.

Kituo hicho kilikabidhiwa kwa mchimbaji mmoja wa kukiendesha ambaye kwa bahati mbaya ameonyesha kushindwa kazi. Wizara itazingatia maoni ya Mheshimiwa Mbunge, hususan ya kupanua au kuongeza vifaa au vitendea kazi vya uchimbaji kama magari, *compressor* na pampu za maji kwa vile wachimbaji katika eneo hili wako mbalimbali mno.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wizara yangu inatekeleza mpango wa kumbadili mwendeshaji ama mmiliki wa kituo hiki kwa vile ameshindwa kutekeleza kazi tulizokubaliana katika mkataba na hivyo kufanya kituo kutofikia malengo yake ya kuendeleza wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, ifikapo mwezi Oktoba, 2007 tutakuwa tumeshampata mchimbaji mdogo mwenye sifa zinazohitajika kukiendesha kituo hicho.

Mheshimiwa Dewji, Mbunge wa Kilwa alikuwa na hoja kadhaa, alieleza kwanza Kilwa ina hazina kubwa ya *Gypsum* hasa katika Kata za Mandawa na Kilanjelanje. Inasemekana kwamba *Gypsum* hiyo ni nzuri sana ila migodi imesimama kutokana na Kampuni moja kususia. Pesa nyingi zinapotea kwa kuagiza *Gypsum* kutoka Oman na Iran. Wizara inachukua hatua gani kuhusu mwekezaji anayesuasua?

Mheshimiwa Spika, Wizara itakagua eneo hilo na endapo itathibitika kuwa mmiliki wa leseni amekiuka masharti ya leseni yake, hatua za kisheria za kuifuta leseni zitachukuliwa ili kutoa nafasi kwa wawekezaji wenye uwezo wa kuchimba madini hayo. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha iwawekezaji na hivi karibuni wawekezaji kutoka China wamefika katika maeneo hayo na kuchukua sampuli kwa lengo la kutaka kuwekeza.

Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu aliongelea habari ya wachimbaji wadogo wa Mwanzilo Kata ya Igusule, wameondolewa na eneo kupewa kampuni ya *Sub-Sahara.* Kampuni hiyo iwalipe fidia wachimbaji hao. Tumesikia hoja ya Mheshimiwa Mbunge, tutafuatilia kuona na kupata ukweli halisi.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, aliongelea habari ya machimbo ya kokoto katika Kijiji cha Lilondo Kata ya Wino ambayo yanaleta uharibifu mkubwa wa mazingira na afya, *Tanroad* ambao ndiyo wamiliki wa mgodi huo washirikishe wananchi katika kurekebisha uharibifu huo. Mapendekezo ya mradi wa kurudisha hifadhi ya mazingira inawasilishwa Wizarani, Wizara inasemaje?

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, tunaufanyia kazi. Lakini pia namshukuru sana kwa kuendelea kusisitiza mwaliko ambao amekuwa akinialika kwa muda mrefu kwenda Jimbo la Peramiho na mimi narudia kumhakikishia kwamba nitaambatana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Ezekiel Maige, alitaka kujua ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ya kuwapatia maeneo ya kuchimba wachimbaji wadogo wa Kakola Kahama itekelezwe. Itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuwapatia wachimbaji wadogo wa Kakola maeneo ya kuchimba, Serikali inajadiliana na Kampuni ya *Barrick Gold Tanzania* kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo sehemu inayozunguka mgodi wa Bulyankhulu. Aidha, Serikali inaendelea kuainisha maeneo kwa ajili ya wachImbaji wadogo sehemu mbalimbali nchini. Kwa hatua ya kwanza tumeanza Mikoa ya pembezoni yaani Kagera, Mara na Mwanza. Hatua ya pili itakuwa ni Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni ya Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, ilikuwa, taarifa za Alex Stuwart zitumike kuimarisha usimamizi katika Sekta ya Madini. Tumefurahishwa na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na hili tutaendelea kulifanyia kazi. Pia alitaka kujua mwaka 2006 Mgodi ya *Truck* ulipata *operating profit* kubwa ya dola za Kimarekani 2,500 dhidi ya matarajio ya dola za Kimarekani 500,000,000.00 na hivyo wanahisa kupata gawio la asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtagundua kwamba Wizara hiyo wamegawana Naibu Waziri dakika 30 na Mheshimiwa Waziri dakika 45 kwa sababu walikuwa na saa moja na robo. Msidhani kwamba Waziri naye atachangia kwa dakika 60, ni dakika 45.

Mheshimiwa Mtoa hoja, Waziri wa Nishati na Madini, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nianze kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwako wewe binafsi, Naibu Spika - Mheshimiwa Anne S. Makinda na Mwenyekiti - Mheshimiwa Jenista J. Mhagama kwa jinsi alivyosimamia Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili makadirio ya matumizi ya fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2007/2008.

Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga - Mbunge wa Tabora Mjini kwa kuwakilisha taarifa yenye maoni na ushauri wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa - Mbunge wa Mkanyageni kwa kuwasilisha taarifa yenye maono na ushauri wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii kwa kuzungumza au kwa kutoa maoni kwa maandishi ndani ya Bunge lako Tukufu. Ushauri na maoni yao yatasaidia sana katika utekelezaji wa bajeti yetu kwa mwaka 2007/2008. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni 159. Waliochangia kwa kuzungumza ni 34 na waliochangia kwa maandishi ni 125. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama utaratibu unavyotaka, naomba niwataje kwa majina walilochangia kwa kuzungumza. Kwanza ni Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Jackson Muvangila Makwetta, Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw’, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri na Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja - Naibu Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani , Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandosya, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenye, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi na Mheshimiwa Paschal Constantine Degera. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mheshimiwa Philip Sang'ka Marmo, Mheshimiwa Dr. Cyril August Chami, Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu na Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi, Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa

Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika na Mheshimiwa Samuel John Sitta. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Naam! Mheshimiwa Spika pia. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Bujiku Phillip Sakila, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud na Mheshimiwa Eliatta Namdumpe Switi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki na mwisho ni Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe Mbunge wa Nachingwea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, bado unazo dakika zako hatukuzihesabu hizi wakati ukitaja majina. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja za Wabunge ambao sitaweza kuzijibu hapa kwa sababu ya muda tutazituma kwao kimaandishi na Wabunge wote watapata majibu ya hoja zote walizokuwa wamezitoa hapa Bungeni kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe ufafanuzi kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nifuate itifaki kwa kuanza na hoja za Kamati ya Uwekezaji na Biashara kama ilivyowakilishwa na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Katika kutoa hoja za Kamati, Kamati ilishauri kuwa *TANESCO* iwezeshwe kifedha na kwa Serikali kuitolea dhamana ili iweze kushiriki katika mipango yake ambayo imejiwekea katika mpango wake wa kujiwezesha kifedha.

Kimsingi Serikali inakubaliana na ushauri huo, lakini ilikwishaanza kuufanyia kazi kwa sababu imekwishatoa dhamana ya shilingi bilioni 235 ili waweze kupata mkono ambao ni *syndication loan.*

Walizungumzia juu ya umuhimu wa kutoa taarifa kwa wateja kuhusu kukatikatika kwa umeme, ushauri huo tumeufikisha *TANESCO* lakini kwa sasa hivi taratibu zilivyo kama kuna mpango wa kukata umeme *TANESCO* hutoa taarifa hizo, lakini kama unakatika bila kupanga kama ukatikaji huo ulikuwa ni mkubwa sana *TANESCO* hutoa taarifa hizo za tukio baadaye. Kamati ilishauri kwamba iharakishwe ununuzi wa *IPTL* na kurekebisha mitambo ili itumie gesi badala ya *diesel*. Ushauri huu wa Kamati umezingatiwa na kweli ndiyo lengo la Serikali na ndivyo tunavyofanya sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshauri kwamba wananchi washirikishwe katika ulinzi wa miundombinu pamoja na kupewa ajira wakati wa utekelezaji wa miradi ya *TANESCO*. *TANESCO* ina mikataba ya ushirikishwaji wa wananchi katika ulinzi, ujenzi wa miundombinu, wananchi wa eneo husika wanashirikishwa kwa kupewa ajira hususan za kibarua.

Serikali ya Muungano na ya Mapinduzi Zanzibar ziharakishe majadiliano na kupatikana kwa muafaka wa tatizo la kufanya utafiti wa mafuta katika mwambao wa Tanga na Pemba. Tunakubali ushauri huo na jitihada zinaongezwa na Serikali zote mbili kuharakisha utekelezaji wa makubaliano hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetoa ushauri kwamba *TPDC* iwezeshwe ili kuweza kushiriki katika *investments* ambazo zinatokea katika gesi na mafuta na wakashauri kwamba katika maduhuli inayoyapata ipewe *retention*.

Hoja kama hiyo, imetolewa na Wabunge wengi wakiwemo Mheshimiwa Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya. Kama Wizara, tunaliona ni wazo zuri, tumelipokea na tutaliwasilisha Serikalini kwa maamuzi.

Wizara katika kutoa maoni yake imesema kwamba miradi mingi ya maendeleo iliyokuwa imepangwa katika bajeti ya mwaka 2006/2007 kupewa fedha haikupata fedha hiyo. Wizara imeliona hilo na tumelizungumza katika hotuba niliyoitoa kwamba Serikali ilielekeza raslimali nyingi kwa ajili ya kukabiliana na matatizo yaliyotokana na ukame. Hayo ndiyo yalikuwa mapendekezo makuu pamoja na mengi ambayo yametokana na Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa - Msemaji Mkuu wa Upinzani alikuwa na hoja alizozitoa, ya kwanza alitaka maelezo ya kina niyatoe kutokana na ziada ya Sh. 3,496,668/= ambayo yameonyesha kwamba tuliyatumia kinyume na bajeti iliyokuwa imeidhinishwa.

Hizi kama mlisikia vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anatoa hotuba yake, hizi ni sehemu za fedha zilizotumika katika kukabiliana na matatizo ya umeme wakati umeme umekabiliwa na janga la ukame, *reallocation warrant* itatayarishwa na Wizara ya Fedha na itawasilishwa Bungeni kupata ridhaa.

Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa ametaka maelezo yatolewe juu ya ucheleweshaji wa mradi wa umeme wa *45 megawatt* kwa Tegeta kwa takriban mwaka mmoja. Majadiliano ya upatikanaji wa fedha za mradi kutoka Serikali ya Uholanzi yalichukua muda mrefu. Hata hivyo mikataba yote tayari imekwishasainiwa na Mhandisi Mshauri amekwishateuliwa.

Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa amehoji kwa nini Serikali ikakodi mitambo ya *diesel* huko Mwanza badala ya kutumia gesi inayopatikana hapa nchini. Hali ya dharura ya mgao wa umeme iliyokuwepo wakati huo hakukuwepo miundombinu ya gesi ambayo ujenzi wake kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge ungechukua muda mrefu na gharama kubwa ya kupeleka mpaka Mwanza. Kwa kufuatia kwamba miundombinu ni ghali na usingeweza kuichukua Mwanza kwa sababu ya mtambo mmoja tu wa kuzalisha umeme wa *megawatt 40.* Kwa kuzingatia hayo yote niliyoyazungumza, kwa hiyo, mitambo ya *diesel* kwa wakati ule ilikuwa ndiyo muafaka. *(Makofi)*

Vilevile Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa ni *Engineer,* anajua wakati ule kwamba wakati tulikuwa hatuzalishi umeme kutokana na vyanzo vya maji, kwa hiyo, nguvu ya umeme katika *grid* yetu ulikuwa ni mdogo kwani tulikuwa tunatumia *gas generators,* tulihitaji *support* kule Mwanza ili ku–*stabilize grid* yetu isiwe inakatikakatika mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa amehoji kwamba mitambo ya *DOWANS* ambayo imekodishwa kwa miaka miwili itaigharimu *TANESCO* shilingi bilioni 172.9

wakati mitambo ya *TANESCO WATSIRA* itagharimu shilingi bilioni 102 na akataka maelezo yatolewe kuhusu hilo.

Mheshimiwa Spika, gharama za mitambo ya *DOWANS* na *TANESCO WATSIRA* haziwezi kulinganishwa moja kwa moja kutokana na tofauti ya teknolojia za mitambo pamoja na masharti ya mikataba kutokuwa sawa. Gharama halisi za kukodisha mitambo ya *DOANS* ni dola 102 milioni sawa na shilingi bilioni 132 siyo kama shilingi 172.9 bilioni kama alivyosema na zile za *TANESCO WATSIRA* ni *Euro 57.55* sawa sawa na dola za Kimarekani 79.9 milioni au shilingi bilioni 101.

Gharama za *WATSIRA* zile nilizozitaja hazihusishi gharama za ununuzi wa gesi ya kuendeshea mitambo hiyo. Gharama ya *TANESCO WATSIRA* hazihusishi gharama ya uendeshaji *Operating and Maintenance Cost* wakati zile za *DOWANS* zinahusisha gharama za uendeshaji na utengenezaji wa mitambo. Gharama zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge za shilingi bilioni 172.9 kwa *DOWANS* zinahusisha ununuzi wa gesi.

Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa amezungumzia juu ya uhamasishaji wa kilimo cha *jetrofa* kusudi mwaka 2025 tuwe tumefikia asilimia 25 ya matumizi ya petroli kwa kuchanganya na *biodiesel.* Ushauri huo tumeuchukua. Hata hivyo, kutakuwepo na umuhimu wa kuhakikisha kwamba kilimo hiki hakiathiri uzalishaji wa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa ameshauri Sheria ya Utafutaji wa Mafuta ya mwaka 1980 ifanyiwe marekebisho kwa lengo la kuhakikisha jitihada za utafutaji wa mafuta nchini, ushauri huo tumeupokea.

Pia ameshauri Serikali ifufue kiwanda cha kusafisha mafuta cha *TIPPER* ili kununua mafuta ghafi na kuyasafisha ili tuwe na uwezo wa kudhibiti bei za mafuta ya petroli, tuwe na uwezo wa kuchanganya *bio fuel* na pia kutengeneza lami hapa nchini. Serikali tayari inafanya majadiliano na wawekezaji ambao wameonyesha nia ya kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta ghafi hapa nchini.

Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa vilevile ametoa mchango katika Sekta ya Madini. Sekta ya Madini amesema upitiaji upya wa mikataba ya Madini umefikia hatua gani? Upitiaji wa mikataba ni kazi inayoendelea, mafanikio yaliyopatikana hadi sasa ni pamoja na kama tulivyoeleza wakati nawakilisha bajeti yangu, wale wawekezaji ambao walikuwa na *MDAs* ambazo zilikuwa zinawaruhusu kuwa na kipengele cha asilimia 15 cha *Additional Capital Allowance* kuondolewa aidha kama alivyoeleza Naibu Waziri Kampuni kama *Barrick* na *Resolute Tanzania Limited* wameamua kwa hiari yao kutoa shilingi milioni saba na milioni mbili kama *ex-gratia.* Sasa hivi majadiliano yako mbioni kukamilika na *Geita Gold Mine*.

Pia aliuliza hivi, kiasi ambacho kinalipwa kwa Serikali sasa hivi kinalipwa kwa kutumia sheria gani? Kiasi cha fedha kinacholipwa na Kampuni ya Madini kwa sasa kinalipwa kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba kwanza ya Serikali na wawekezaji *MDAs.* Aidha, malipo ya Sh. 200,000/= yanafanyika kwa mujibu wa Sheria ndogo ya

Halmashauri za Wiliya zinazoundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982.

Aliuliza kwa nini mataifa yasiyochimba *TANZANITE* kwa mfano Kenya yanapata tuzo ya kuuza Madini haya kwa wingi katika soko la Dunia na siyo Tanzania na kuwa *report* ya Tanzania kuhusu mauzo ya *TANZANITE* kwa mwaka 2005 ni dola za Kimarekani milioni 16 wakati mauzo hayo katika soko la dunia yalikuwa dola za Kimarekani 400 milioni.

Mheshimiwa Spika, kimsingi madini yote ikiwemo *TANZANITE* husafirishwa kwa mauzo nje ya nchi chini ya usimamizi wa Wizara. Mwaka 2005 Tanzania iliuza nje Madini ya *TANZANITE* yenye thamani ya *USD* milioni 34 na siyo milion 16 na hatuna taarifa ya kuwa Kenya ilipewa tuzo ya kuuza Madini ya *TANZANITE* kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, tofauti kubwa ya thamani ya madini kati ya soko la ndani na masoko ya nje ni kutokana na usanifu ambao umeongeza thamani kubwa, yaani *Value Addition* kwenye madini hayo katika nchi kama India, Afrika Kusini, Thailand, Marekani na Israel.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, sitakwenda kwenye takwimu, lakini ukienda Marekani kwenye maduka ukasema unataka kununua *TANZANITE* ama unanunua *ring* ya *TANZANITE* kunakuwepo na kito kingine kama ni dhahabu, panakuwepo na jicho la *TANZANITE* ama *Pendant* ina jicho la *TANZANITE*. Hayo huwa yanahesabika kama *mauzo ya TANZANITE.* Kwa hiyo, mtu akija hapa anasema kwamba *TANZANITE* Marekeni zimekuwa dola milioni 400. Lakini hiyo ni kwa sababu ya uongezaji wa thamani na sisi tukifikia hapo tutakuwa tunapata thamani kama wanavyopata wenzetu.

Mheshimiwa James Philipo Musalika - Mbunge wa Nyangwale ameuliza, Kijiji cha Karumwa kipewe umeme. Uchambuzi uliofanywa na *TANESCO* umebaini kuwa gharama za kupeleka umeme katika kijiji hicho zinakadiriwa kuwa shilinig milioni 600.

Wizara inatambua kuwepo kwa maombi ya wananchi wa Kalumwa kupewa umeme na wamo katika orodha ya maombi chini ya utaratibu wa umeme vijijini utakaoanzishwa. Rai yangu kwa wananchi wa Karumwa ni kwamba kuharibu miundombinu kama kutoboa bomba la maji, yaani maji yanayosafirishwa toka Ziwa Victoria kupitia kijiji hicho kama walivyofanya, ni uhalifu na sio suluhisho la tatizo lao la kupata umeme na wanaofanya hivyo ni wahalifu na watachukuliwa hatua kali sana.

Mheshimiwa James Philipo Musalika amesema kwamba fidia ilipwe kwa wananchi kwenye mradi wa ujenzi wa njia ya umeme kwenda kwenye pampu za maji Ihehe.

Taarifa ambayo tunayo kutoka Wizara ya Maji, ni kwamba fidia hiyo imelipwa mwezi Juni, 2007.

Mheshimiwa Athumani Said Janguo amezungumzia kama walivyozungumzia Wabunge wengi, ametaja vijiji vyake vingi ambavyo havijapata umeme. Ombi lake tumelipokea, jitihada zitaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini ikiwa ni pamoja na vijiji vya Kisarawe.

Mheshimiwa Jackson Muvangila Makwetta amezungumzia juu ya Mfuko wa Umeme wa Kata. Sisi tumeshaanzisha Mfuko wa Umeme Vijijini, nafikiri utakidhi haja hiyo. Wananchi kuhamasishwa kulima miti ya mashamba ya Nishati, tunampongeza na ushauri tumeuzingatia kwa kushirikiana na Wizara na Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Raphael Massunga Chegeni, amezungumzia umeme kwamba upelekwe katika vijiji vya Kalemele Nyamisiro, Hospitali ya Mkula na hasa kwenye Jinari ya Ngasamo. Mradi kwa upande wa Jinari umeombewa fedha kutoka Serikali ya Ufalme wa Hispania chini ya *Phase* IIIC ya *Spanish Assistant for Rural Electrification of Agro Based Industry and District Township.*

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ametoa hoja kwamba kuna umuhimu wa kuharakisha kufikisha muafaka kuhusu suala la utafutaji wa mafuta Zanzibar na akaongeza, kwa nini mikataba inakamilika haraka Tanzania Bara lakini panapofika Mikataba Zanzibar yanaanza majadiliano?

Mheshimiwa Spika, suala la utafutaji mafuta Zanzibar limezua hisia mbalimbali kwa wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba. Hivyo, kwa kuzingatia kwamba Serikali zote mbili ni makini zikaona hili suala lazima liwekwe wazi. Kwa hiyo, Serikali hizo mbili zimelazimika kufanya mashauriano jinsi ya kutatua vizuri na njia ya ufumbuzi wa kuanza utafiti wa mafuta Zanzibar. Ninyi Waheshimiwa Wabunge mnaweza kuona ugumu ambao umekuwepo katika Kamati ya Mheshimiwa William Shellukindo jinsi ya kugawana mapato na kugawana matumizi hususan kwa maeneo ambayo Kikatiba ni ya Muungano.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed alizungumzia suala la gesi na mafuta ni la Muungano na hilo nimeishalizungumzia kama ambavyo alieleza. Pia alizungumzia taarifa ya Dr. Kipokola alisema iletwe hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya Jonnas Kipokola siyo siri na iliwasilishwa kwenye Semina ya Waheshimiwa Wabunge mara mbili. Mwezi Aprili, 2005 na mwezi Juni, 2005. Hata hivyo, taarifa hiyo itachapishwa na kupewa Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed alizungumzia kwamba iletwe Bungeni taarifa ya Alex Stuwart. Kampuni ya Alex Stuwart ilikuwa kama ni *Internal Audit* wa Serikali kwenye migodi inayochimba dhahabu. Kwa hiyo, inawakilisha taarifa zake Serikalini. Taarifa hizo zinaendelea kuchambuliwa na Serikali. Mimi mwenyewe nimeunda Kamati ya kufuatilia hizo taarifa na mpaka sasa hiyo Kamati inaendelea na

kazi yake. Ikimaliza, itaniletea taarifa hiyo kama kutakuwa na taarifa ambazo zinahitajika kuletwa Bungeni nitazileta.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed alizungumzia juu ya Kampuni ya *Mwananchi Gold Refinery*, akauliza inamilikiwa na nani? Akaomba yatolewe maelezo kuhusu fedha iliyotolewa na Benki Kuu ambayo inakaribia shilingi bilioni 6.9.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya tatu katika Afrika kwa utoaji wa dhahabu, lakini dhahabu hiyo inayochimbwa inauzwa ghafi. Vilevile majirani zetu wenye dhahabu hawana sehemu za kusafishia dhahabu yao.

Baada ya kutafakari hali hiyo, Serikali ilikubali kwamba Benki Kuu na *NDC National Development Cooperation* washiriki katika uanzishwaji wa karakana ya majaribio ya kusafisha dhahabu. Hicho ndicho kiini cha kuanzishwa kwa Kampuni ya *Mwananchi Gold Company*.

Mtazamo wa *Shareholding* ya *Mwananchi Gold Company* ni Kampuni binafsi ambayo Serikali inamiliki asilimia 35. Benki Kuu wana asilimia 20 na *NDC* ikiwa na asilimia 15, wamiliki wengine ni Mwananchi *Trust Limited* na *Masse.*

Katika uanzishwaji wa karakana ya kusafisha dhahabu Benki Kuu ilitoa mkopo wa dola za Kimarekani milioni 5.39. Sehemu kubwa ya mkopo huo ilikuwa ni kwa ajili ya kununulia eneo la majumba ya kiwanda, fedha za kununulia malighafi na kununua mitambo pamoja na ukarabati wa majengo. Mkopo huo umetolewa kwa taratibu za kibenki na Serikali inashikilia hatimiliki za eneo pamoja na mitambo.

Vilevile, malighafi zote zinazonunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Kiwanda hutunzwa Benki Kuu. Vilevile mauzo yote hupitishwa katika Akaunti ya Kampuni iliyopo Benki Kuu na mkopo huo unatozwa riba.

Mheshimiwa Spika, niende kwa mchangiaji mwingine ambaye karatasi yake nimepata sasa hivi, Mheshimiwa Kabwe Zitto. Mheshimiwa Kabwe Zitto tunampongeza kwa kuweza kusahihisha takwimu ambazo tulikuwa tumeziandika kwenye vitabu vyetu.

Katika aya ya nne ya hotuba yangu imeandikwa kwa makosa ya uchapishaji kuwa Sekta ya Nishati na Umeme ilikuwa kwa asilimia 3.3 badala ya ukuaji wa hasi wa asilimia 2.5 na mwenyewe hapo ningeomba asahihishe takwimu zake ikilinganishwa na asilimia 5.3 badala ya asilimia 5.1 mwaka 2005. Kulingana na takwimu tulizozitoa katika kitabu cha Hali ya Uchumi wa Tanzania katika mwaka 2005. Tunampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sahihisho hilo.

Mheshimiwa Kabwe Zitto wakati anachangia, amesema *Presedom* imeonekana katika mwambata kama mmiliki wa mgodi, lakini ilikwishanunuliwa na *Barrick*, takwimu za mwambata huo siyo sahihi. Kwa mfano, *Barrick* si kweli kuwa inamiliki

migodi minne kwa sasa. Ni kweli kuwa baadhi ya taarifa zilizopo kwenye mwambata zinahitaji kusahihishwa. Masahihisho yatafanywa.

Kuhusu Kampuni ya *Barrick* kumiliki migodi minne siyo sahihi. Ukweli ni kuwa, *Barrick* inamiliki migodi mitatu kupitia Kampuni zake tanzu ambazo ni Bulyanhulu *Gold Mine, North* Mara *Gold Mine* na Pangea *Minerals Rose Limited* Tulawaka.

Mheshimiwa Kabwe Zitto, ameuliza, imekuwa namna gani Wizara imesaini Mkataba mpya na *Barrick* kwa mradi wa Buswagi kabla ya ku-*review* Mikataba? Kwa nini Mkataba huo umesainiwa *London* na siyo hapa nchini? *Terms* zilizopo katika Mkataba huo ni zipi? Mheshimiwa Waziri atoe maelezo.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Buswagi katika tathmini ya Migodi ni *marginal mine* ambayo uhai wake siyo wa muda mrefu,bila ya kutumia fursa ya sasa ya bei ya dhahabu uwekezaji wake usingeweza kuwa wa faida. Hata hivyo, Mkataba wa Buswagi hauna mapungufu yaliyokuwemo kwenye Mikataba ya zamani.

Mheshimiwa Spika, ili mkataba wa Madini ukamilike na mimi niweze kuusaini inabidi kufuata ngazi zifuatazo:- Kwanza, mkataba huo uandaliwe na wataalam Wizarani, baadaye hupelekwa kwa Mwanasheria wa Serikali kutazama kama umeandikwa kufuatana na sheria, lakini mpaka hapo hauwezi kusainiwa mpaka upitie kwenye Kamati ya Ushauri ya Madini ambayo imeundwa Kisheria.

Mkataba huo wa Buswagi umepita katika hizo taratibu zote. Wakati Mkataba huo unajadiliwa kipindi cha Bodi ya *Barrick* ambao walikuwa wanapitia Mikataba mahali ambapo watafanya *investments* kilikuwa kimekaribia. Wakati ule mimi nilisafiri na Mheshimiwa Rais kwenda Uingereza na *NORDIC Countries.* Wakati naondoka niliacha Mikataba yote imekwishamalizika isipokuwa walikuwa wanamalizia kuiandika vizuri, lakini taratibu zote zilikwishakamilika.

Mheshimiwa Spika, Wizarani kwangu walipomaliza wakaniambia tatizo la Bodi ya *Barrick,* nikaambiwa, basi kama ni tatizo la Bodi mpeni Mwanasheria katika Wizara yangu aniletee nitakapokuwa mimi niusaini. Kwa hiyo, Mwanasheria wa Wizara yangu ndiye aliyeniletea huo Mkataba, ndiye niliyemtuma, sio Kampuni ya *Barrick*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anaweza akanibeza labda nilikuwa natumia ile harakati ya kutoka *Private Sector*, mnajua nimetoka *Private Sector,* natambua kwamba muda wa biashara ni muda. Kwa hiyo, kama niliagiza kuwa kama mkataba umekamilika niletewe mahali popote nilipo na ndicho nilichotumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kabwe Zitto amesema kwamba Wizara inajitamba kuondoa kipengele cha Sheria ambayo ni *fifteen percent un-redeemed capital*. Hicho ni kipengele cha sheria ambacho inabidi kuondolewa na Bunge. Hivi Wizara imepewa mamlaka gani hayo ya kufanya kazi ya Bunge?

Mheshimiwa Spika, nilipoisikia hiyo, nimeshtuka sana kwa sababu, hiyo ni uvunjaji wa sheria na Serikali iko makini. Kwa hiyo, pamoja na kwamba ninamheshimu sana Mheshimiwa Kabwe Zitto na sote tunamheshimu ni msomaji mzuri, lakini wakati mwingine lazima kuangalia vitu gani anasoma. Ukweli ni kwamba kipengele hiki cha Sheria kililetwa hapa Bungeni mwaka 2001 kwenye Bajeti kikabadilishwa. Bahati mbaya yeye hakuwepo na mimi vilevile sikuwepo, lakini nilikijua. Katika kubadilisha hicho kipengele, yale Makampuni tayari ambayo yalikwishaingizwa kwenye Mkataba usingeweza kuyafuatia. Hiyo kisheria ilikuwa inawahusu wale wageni wote ambao wataingia ya mabadiliko ya kipengele hicho. Kwa hiyo, hizo kampuni zote ambazo zilikuwa na *MDAs* yenye hicho kipengele ilikuwa haikuondolewa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo juhudi iliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kutusimamia kuhakikisha kwamba tunazungumza na hayo Makampuni na sasa makampuni makubwa *Barrick* na *Resolute Tanzania Limited* pamoja na Mwelekeo wa *Geita Gold Mine* wamekubali kukiondoa. Kwa hiyo, wamekiondoa hicho kwa hiari, hawakuwa wamebanwa na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kabwe Zitto amezungumzia Serikali kwamba iliuza hisa zake *percent* 15 Bulyankhulu kwa bei poa ambayo ni sawa na asilimia moja. Kwa nini tuliuza hisa tena kwa bei poa na kwa nini tena tuzungumzie juu ya kununua hisa?

Mheshimiwa Spika, wakati tunatoa takwimu na ambazo nimeona amezitumia Mheshimiwa Kabwe Zitto, takwimu za kibiashara huwa ni takwimu za wakati. Ukichukua takwimu za mwaka 2000 ukazileta kwa sasa zinakuwa hazioani. Wakati ule *Barrick* walitaka kuongeza uwekezaji katika utafiti wa Bulyankhulu. Serikali kwa wakati ule haikuwa na fedha za kuweza kuwekeza pale kubakia na hisa zake. Kwa kutokuwekeza isingefutika kabisa, lakini ingekuwa na hisa kidogo sana ambazo hazingekuwa na faida kwa Serikali.

Kwa hiyo, ikakubali kuziuza, lakini kuziuza kwake iliweka kipengele kimoja kwamba pamoja na kwamba haina hisa itakuwa inapata *dollar* za Kimerikani 100,000 kila mwaka kwa kipindi chote cha mgodi pamoja na kwamba haina hisa na ndivyo inavyofanyika mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwa Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, amezungumzia Kampuni ya *Artumas* kwamba ilichimba visima vinne bila mkataba na hiyo ikaonyesha kwamba ina imani na Tanzania. Kweli Kampuni ya *Artumas* ina imani na Tanzania, lakini sio kweli kwamba ilichimba visima vinne bila mkataba. Kila kisima kinachochimbwa kinachimbwa na kina *production sharing agreement.*

Mheshimiwa Spika, labda alichotaka kuzungumza ni kwamba walikuja wakaweka jenereta kabla ya Mkataba. Lakini kabla kuziwasha ilikuwa zitumike kuzalisha umeme si kwamba hawakuwa na mkataba, walikuwa na mkataba ambao unaitwa *interim power purchase agreement* ya mwaka mmoja. Alisema mikataba isainiwe haraka ili kuwapa uwezo *Artumas* kusambaza umeme Lindi na Mtwara. Ni kweli na mimi mwenyewe nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge nataka mikataba hiyo isainiwe haraka haraka kwa

sababu ikisainiwe hiyo mikataba, lakini kwa kuzingatia maslahi ya Taifa ile michango yote ya Lindi na Mtwara juu ya umeme itakuwa imekwisha. Kwa hiyo, mimi ni mdau wake.

Kwa sasa hivi mikataba ya kuzalisha na kusambaza umeme ipo katika hatua za mwisho za majadiliano likiwemo suala la upatikanaji wa fedha za *OLET* kutoka ya Serikali ya Uholanzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha amezungumzia sana vijiji vyake vyote ambavyo anavyo na akazungumzia Jimbo lake lilivyo zuri kwa uwekezaji. Kila mwekezaji akifika akikuta hakuna umeme anaondoka. Hilo tumelipokea na kweli *TANESCO* imekwishafanya upimaji na kubaini kuwa gharama za kusafirisha umeme mpaka sehemu kama alivyozungumza kiwanda kimoja cha matunda cha Kikola ni shilingi milioni 60 na maeneo mengine. Tunaona kwamba Mheshimiwa Mbunge avute subira, sasa hivi tutaanza mradi wa umeme vijijini na kama eneo lake alivyolieleza ni *potential* kama lilivyo bila shaka litapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, Omar Kwaangw' amezungumzia hoja kuu za msingi. Kwanza, kubwa ni kwamba kuna umeme katika eneo lake na umeme huo ni mkubwa lakini wanaotumia ni wachache. Sasa kwa nini usisambazwe kusudi turudishe gharama zilizowekezwa pale? Sisi tunakubaliana naye, hoja yake tumeichukua na katika mipango yetu ya baadaye nafikiri itabidi tuizingatie. *(Makofi)*

Vilevile katika hotuba yangu nilisema yale ambayo nitayafanya katika mwaka huu, ni pamoja na kuanzisha *Rural Energy Agency* na *Rural Energy Fund,* akasema sasa hilo ndilo linafanyika mwaka nzima. Hapana, atagundua kwamba tumeweka takriban shilingi bilioni 10 na kuna fedha nyingine kwenye *recurrent expenditure* ambazo mtaziona ambazo ni za kuanzisha Ofisi na kuajiri wataalam. Kwa hiyo, wataanza na wakishaanza wataanza na fedha zilizopo kuanza utekelezaji wa *Rural Energy Agency* kama tulivyopanga kisheria. Amezungumzia juu ya shilingi bilioni 10 kianzio cha Mfuko zitatumika namna gani. Sisi tunasema kwamba kuhusu hizo shilingi bilioni 10, Waheshimiwa Wabunge, ningependa kuwaambia kwamba kwa upande wa Mfuko wa *Rural Energy Agency,* Waheshimiwa Wabunge kama mlivyosema hapa kila mmoja anahitaji umeme na kweli hakuna Mheshimiwa Mbunge aliye bora zaidi ya mwingine wala Jimbo lililo bora zaidi ya lingine, kila Jimbo linastahili kupata umeme. Sasa namna gani mmoja apate na mwingine asipate?

Mheshimiwa Spika, sisi katika Wizara tunaahidi kwamba Mfuko huu wa *Rural Energy Agency* ambao tunao, tutautunisha uwe mkubwa zaidi kuliko ulivyo sasa hivi. Lakini tutazingatia vipaumbele kama tulivyoviweka kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kipaumbele cha kwanza ni kuhakikisha kwamba Makao Makuu yote ya Wilaya yanapata umeme.

Kwa hiyo, hizo shilingi bilioni 10 ambazo tunazo itakuwa ni kianzio cha kuanzisha kutekeleza ile Ilani kwa Wilaya ambazo hazina umeme kuanza kuwasogezea umeme; na tunafikiri kwamba kwa mwaka ujao Mfuko utakuwa endelevu tutaweza

kumaliza ama kupunguza zile Wilaya zitakazokuwa zimebaki na ku-*roll over* kuanza kutimiza ile ahadi yetu ya kuanza kusambaza umeme vijijini. Mfuko huo tulioanzisha wa bilioni 10 ndiyo unaanza na ukishaanza kutengamana utakuwa kama Wizara ya Mheshimiwa Andrew Chenge, tutakuwa tunakuja hapa kuiambia Tanzania nzima. Eneo gani litapata umeme na eneo gani litapata baadae na kwa wakati gani.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kikubwa tutahakikisha kwamba huo mgao utakaokuwa unapatikana ugawiwe sawa kwa maeneo kusiwepo eneo moja likawa bora zaidi ya eneo jingine. *(Makofi)*

Nimalizie kwa sababu muda ninaona umekwisha, kuna Mheshimiwa Mbunge ambaye atasimama kwenye Kamati ya Matumzi nisipomtaja, naye ni Mhesimiwa Halima Mdee aliulizia ucheleweshwaji na kukamilika kwa Mkataba wa *Richmond*. Umecheleweshwa miezi mitano? Je, faini na *penalties* zitalipwa namna gani?

Mheshimiwa Spika, kweli tulitegemea Mkataba wa *Richmond* ambao ni *Dowans* sasa hivi ungekuwa umekamilika tarehe 2 Februari, 2007, lakini kwa sababu za *Richmond* na *Dowans* wenyewe hawakuweza kukamilisha tarehe hiyo. Kwa hiyo, kipengele cha adhabu kinaingia. Kufika Januari, 2007 walikuwa wameishaingiza megawati 20 kwenye *grid* ya Taifa na kufika mwezi Mei, 2007 walikuwa wamekwishaongeza nyingine *megawatt* 40 zikawa *megawatt* 60. Sasa hivi ndiyo wamemaliza mtambo wa mwisho na wanafanya *commissioning* ya *megawatt* zilizobaki kusudi kufikisha *megawatt* 100. Lakini kwa mkataba, kiwango cha faini ni *dollar* za Kimarekani 10 kwa siku toka tarehe 2 Februari, 2007 na hizo fedha zitalipwa kwa *TANESCO*. Mwenyewe ni Mwanasheria, kila mtu anahisia zake, anazungumza kwa nini tusingeondoka kwenye mikataba? Wanasheria waliiangalia hiyo mikataba wakaona ingetugharimu zaidi kama tungeondoka kwenye Mikataba, afadhali tuwe kwenye Mikataba halafu tukamtoze hiyo faini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima Mdee alizungumzia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwafikishia wananchi wengi zaidi umeme na itatekelezwa namna gani. Kama nilivyozungumza Wakala wa Umeme ndiyo umeanza, siyo kwamba ni mwanzo wa *Rural Energy Agency* ilikuwa inapeleka umeme vijijini lakini kwa pole pole. Kwa utaratibu huu wa *Rural Energy Agency* tuna uhakika Wizara itapanda, ndege ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itaanza kupaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Waziri wa Nishati na Madini kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2007/2008 imetolewa na imeungwa mkono. Lakini kwa mujibu wa kanuni tutaiamua kwa hatua inayofuata. Kwa hiyo, Katibu hatua inayofuata.

**KAMATI YA MATUMIZI**

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 58 -Wizara ya Nishati na Madini

Kifungu 1001 - *Administration and General* … Shs. 2,182,194,000/=

**MWENYEKITI:** Tunachukua majina sasa. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa, Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Susana Lyimo, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Mheshimiwa John Cheyo.Nakwenda hivyo. Wale ninaowataja mjue ndiyo tayari, mkae. Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Nadhani tayari. Tunaanza na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niko katika *Vote* 58 *progromme* 10 *Sub-Vote* 1001, kifungu kidogo cha 250100 - Mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hoja yangu ya kule Wino na Madaba amenijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kufahamu, kama nilivyosema, *TANESCO* wali-*provider* barua maalum inayoonyesha kwamba bajeti ya mwaka jana umeme ungefika Peramiho na Peramiho ndiyo sisi tunahesabu kama ni Makao Makuu yetu ya Wilaya na Makao Makuu yetu ya Jimbo. Lakini hapa Mheshimiwa Waziri hajajibu kitu chochote! Sasa nataka kufahamu: Je, yale majibu ya mwaka jana yalikuwa sio ya kweli? Sasa kama yalikuwa sio ya kweli, basi naomba ieleweke hapa, na kama yalikuwa ya kusubiri, basi naomba hapa Mheshimiwa Waziri aniambie ili wananchi wale wapate kuelewa. Safari tu na Mheshimiwa Naibu Waziri bila kusema humu ndani ikaeleweka haitoshi!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba nimekwishazungumza na Mheshimiwa Jenista Mhagama mara nyingi sana na akanieleza tatizo lake la Peramiho na akanieleza ahadi zilizotolewa. Kweli nilikwenda Wizarani na nilisikitika tu nilipoangalia vitabu vya bajeti sikuona kifungu hicho cha Peramiho, na ikaniwia vigumu nikakosa mahali pa kutoa hizo fedha kusudi kufikisha umeme huo kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi kuna mradi wa kupeleka umeme kutoka Makambako kwenda Songea mpaka Mbinga  ambao uko chini ya Ufadhili wa Sweden na katika mradi huo sehemu ya Peramiho imeunganishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maelezo ya ziada.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Waheshimiwa Wabunge wengi wamesimama kuhusu suala la umeme. Ningependa kurejea maelezo aliyoyaelezea Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka huu tumepanga vipaumbele ambavyo wote mmevikubali.  Tumeanza na miundombinu, elimu na maeneo kama hayo.  Mwaka ujao alichotoa ahadi hapa ni kwamba eneo la umeme litapewa kipaumbele kama tulivyotoa kipaumbele kwenye miundombinu.  Kwa hiyo, ningependa kuwahakikishia Wabunge ambao maeneo yao hayana umeme na tumeahidi katika ilani kwamba tutayatekeleza, lakini hatua kwa hatua kuanzia mwaka ujao wa fedha.

**MHE. LUCAS  L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.  Pamoja na maelezo, natumia fungu 58 *sub-vote* 1101 *item* 250100 - *basic salary.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mchango kwa kuzungumza, lakini vile vile nimetoa mchango kwa maandishi.  Hili la kwanza ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelitolea ufafanuzi niliandika kwa ajili ya umeme katika Jimbo la Nzega na Jimbo la Bukene.  Niseme tu hapa, ule mchele ambao niliahidi asubuhi hapa nimeufikisha kwako na nimeufikisha kwa Mheshimiwa Waziri ingawa hakutaka hata kunipa shukrani hasa kwa wananchi wa Wilaya ya Nzega kwa kumpa mchele wa "Tule na bwana."

Lakini, hoja yangu ni kwamba, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri je, katika hili ile miradi ambayo ilikuwa imeahidiwa mwaka wa jana itazingatiwa iwe ni hiyo hiyo au itaanzishwa miradi mingine mipya kwa sababu tayari tumeshawaambia wananchi wasubiri.  Sasa tukiwaambia wasubiri tena mwaka mmoja, je, watazingatia hiyo hiyo au wataanza tena miradi mingine mipya?  Hilo ni kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika hoja yangu ya maandishi na ya kuzungumza, hapa nilizungumzia vile vile juu ya mchanga unaosombwa na wawekezaji wa migodi kupelekwa nchi za nje.  Katika hotuba ya Waziri hajasema, katika majibu yake hajasema, hata Naibu Waziri hajasema chochote juu ya upotevu mkubwa ambao unaofanywa kwa mchanga wa dhahabu.  Nilikuwa nimetoa maelekezo kwamba Wizara ieleze ni kiasi gani cha mchanga ambao umeshabebwa mpaka sasa hivi? Ni kiasi gani cha fedha ambazo zimepatikana kwa mchanga huo unaobebwa kupelekwa nje kwa madini ya dhahabu na madini mengine ambayo yanapatikana?

Lakini nikatoa mapendekezo kwamba kwa sababu tumeshindwa kusimamia vizuri, ndiyo maana wawekezaji wanatumia nafasi hiyo kuiba rasilimali kubwa hii, basi mkataba upitiwe upya ili mchanga huo usisombwe tena mpaka pale teknolojia itakapopatikana hapa nchini.  Lakini Mheshimiwa Waziri hajajibu chochote na kwa

sababu bado natumia fungu kwa kutumia kanuni ya 81(b) asinilazimishe nikaingia kwenye 81(c) ambayo tutaingia matatani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu na la mwisho...

**MWENYEKITI:** Hapana. Mawili. Tumeweka utamaduni kwamba ni mawili, ama sivyo mnachukua nafasi hii kutunga tena hotuba ndefu. Kwa hiyo, ni hayo mawili.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa samahani, nilikuwa nimeliandika. Nishukuru kwamba nimepokea kweli mchele wa "Tule na bwana" lakini katika kuupokea mchele huo nimehakikisha kwamba Wabunge wote wanaona sio hongo. Kwa hiyo, kwa niaba ya Wizara tunakushukuru na tunawashukuru wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tutakuwa na miradi mipya katika ile ya umeme vijijini? Tulichofanya na utakavyoona kwenye *development budget* yetu, miradi yote ambayo ilikuwa ya mwaka jana tumeirudisha katika mwaka huu na wengine waliosimama watazungumzia kwamba mbona huo mradi una fedha kidogo? Ulikuwa na shilingi milioni 900 kama Mheshimiwa Kasella-Bantu alivyouliza. Ulikuwa na shilingi milioni 900 sasa umekuwa shilingi milioni 50 tu, hii ni kwa sababu ya kutokuwa na fedha na kwa sababu tunajua huu mradi tulikuwanao tukasema utafiti wa njia uendelee kwa fedha kidogo kwa sababu tukiutoa, itaonekana kwamba huo mradi tumeuondoa kabisa kwenye ramani. Kwa hiyo, tumeweka fedha za kuendeleza utafiti ili kusudi tutakapopata hizo fedha nyingi tutakapopewa kipaumbele kwa bajeti ijayo ile miradi ambayo ipo tayari iweze kukamilika.

Lakini pili najua Mheshimiwa Selelii amezungumzia kwa uchungu na anapozungumza mradi wa zamani ambao ukija kuangalia kweli umepotea, ni ule mradi wa *Line* ya Kilovoti 132 kutoka Tabora kupitia Urambo kwako Mheshimiwa Spika, kufika Kaliua kwa Mheshimiwa Kapuya mpaka Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kulikuwa na mawazo, kulikuwa na mpango wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa toka Tabora kupitia Kaliua na Uvinza hadi Kigoma kwa kwa *line* ya kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 390. *Line* hiyo ingeunganishwa na ile iliyopo sasa ya kilomita 190 kutoka Shinyanga hadi Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo *line* hiyo, Shinyanga - Tabora - Kigoma ingekuwa na urefu wa kilomita 550. Upembuzi wa kifundi umeonyesha kuwa *line* ya kilovoti 132 ya Shinyanga - Tabora mpaka Kigoma ingekuwa na matatizo ya kiufundi kwa kuwa na umeme ambao ungefika Kigoma ukiwa hafifu na *line* ingekuwa na uwezo wa megawati 60 ambazo hauwezi kuwa wa manufaa endelevu kwa maendeleo ya Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuzingatia umuhimu wa kiuchumi wa bonde la Malagarasi, tutafanya tathmini ya uwezekano wa *line* ya msongo mkubwa na ikiwezekana kiufundi iwe ya kilovoti 220 ya kuunganisha Shinyanga - Tabora - Urambo -

Kaliua - Uvinza mpaka Kigoma ili tuweze kutengeneza *loop* ya *northwest grid* kufika Kigoma halafu kurudi mpaka Tabora, lakini yenye msongo wa kilovoti 220, ya msongo wa kilovoti 132 itakuwa haifai kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho alilouliza Mheshimiwa Selelii ilikuwa ni mchanga. Hili suala tumelizungumza mara nyingi hapa Bungeni na litakuwa kwenye *Hansard*. Ile jiolojia ya miamba ambayo iko pale inapatikana chini ya ardhi Bulyankhulu, ina madini yaliyochanganyikana na dhahabu, shaba na fedha. Sasa asilimia tu ambayo unaweza ukatoa dhahabu nafikiri ni asilimia 45 ili uweze kupata asilimia 55 iliyobaki, lazima utumie *smelters* za kitaalamu. Mpaka sasa hivi, hiyo *smelters* haipatikani ama Tanzania ama nchi zilizotuzunguka Afrika, tuliposema kwamba kuna wawekezaji ambao wamejitokeza Mwanza ambao mpaka sasa hivi tunawaweka hamasa kusudi waweze kuwekeza mitambo hiyo na wakishaiwekeza tatizo la kusafirisha mchanga litakuwa limemalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selelii naona hujaridhika?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli haya mawili ya kwanza nimeridhika na maelezo yake, hili la tatu juu ya mchanga bado sijaridhika. Kwa utaratibu unaotumika sasa hivi wa kupeleke mchanga nchi za nje Japan na kwingine ambako unapelekwa na Australia bado usimamizi sio mzuri. Katika hili, Waziri hajakiri kwamba usimamizi ni mbaya ndiyo maana unatokea upotevu wa mchanga ambao unasababishwa na wawekezaji na wasafirishaji wanaosafirisha kwenda Bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa pendekezo kwamba usimame usibebwe mpaka hapo utakapobebwa kama walivyofanya pale Mwadui. Mwadui kutokana na kukosa teknolojia walichimba wakasubiri mpaka teknolojia ilipofika ndiyo wameanza sasa hivi ku-*refine* pale pale Mwadui kwa teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini na sisi kwa sababu ni asilimia 55 ambayo tunakwenda kuichukua kule, tusingoje mpaka teknolojia ile ifike ili tuje ku-*refine* hapa hapa nchini? Au basi angesema namna gani anasimamia ili mchanga ule usipotezwe na mapato yale tuyajue yote.

Katika mchango wangu wa maandishi, niliuliza, ni kiasi gani cha fedha ambazo tumezipata? Ni kiasi gani cha dhahabu ambazo zimesafirishwa kwenda nje, lakini kwa sababu hatujasimamia vizuri ndiyo maana nakosa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika hapo, aeleze vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi. Nadhani lengo la Mheshimiwa ni kwamba muache hili zoezi la kupeleka mchanga. Inawezekana hiyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mtu anawekeza anaweka ile *Business Plan* ambayo mnakuwa nayo ambayo inaonyesha kiasi gani madini yapo na ili aweze kuwekeza mtaji na aweze kupata madini hayo na ndipo mnaingia mkataba. Kwa hiyo, suala la kusimamisha mgodi Bulyankhulu halipo isipokuwa suala ambalo lipo ambalo la msingi ni usimamizi uko namna gani? Nafikiri hilo ndilo la maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi huo imewahi kuulizwa hili swali Bungeni sijui na Mheshimiwa Hamad Rashid, tumeeleza vizuri usimamizi ulivyo toka mchanga unapotoka chini ya ardhi ukafika juu, kuna watu wetu wa madini lakini vile vile kuna Alex Stuwart kwa upande wetu.

Halafu vile vile kuna *TRA* wanatoa *sample* wanayotoa kwa kila *container* ambalo limeshatengenezewa kuwa *concentrates*, wanatoa kwa kilogramu moja moja, moja inaletwa hapa *GST* kwetu nyingine inapelekwa Maabara ya *Southern and East Africa Mineral Centre (SEAMIC),* ambayo iko pale Dar es Salaam.

Hiyo inatupa *indication* ya ile kwa kila *container,* sio *container* moja, ina madini kiasi gani? Baada ya kupata kiasi cha madini, wanapata mrabaha kutokana na hiyo, wakishatoka pale ndiyo inakwenda kwenye *Smelters* kule ama Japan ama China. Baada ya kumaliza, wale waendesha *Smelter*s wanatoa takwimu za mwisho *container* kabla halijatoka pale Bulyankhulu yule mwenye mali anaweka *seal* na *TRA* wanaweka *seal* kusudi hiyo *container* itakapokuwa inatoka hapa Tanzania ioneshe haijawa *tempered*.

Asubuhi wakati Waheshimiwa wakichangia, kuna Mheshimiwa Mbunge ameuliza: Je, kama ni hivyo ni vigumu kupata dhahabu kutoa kwenye huu mchanga, kwa nini walikuwa wamesikia watu walikuwa wana-*temper* na makontena humo katikati? Kuna vitu viwili, inawezekana kweli kwamba mchanga uliotoka chini ukawekwa kwenye *container.* Kama kuna usimamizi mbovu, ukawekwa kwenye *container* kwa hiyo, haujazungushwa kuwa ule mchanga wa-*concentrate.* Kwa hiyo, huo tunauita ni wizi wa kawaida tu. Kwa hiyo, mwizi inabidi ashikwe. Lakini inawezekana wale watu wengine wanachukua tu kwa ujinga, wanafikiri kwamba ni dhahabu. Kwa hiyo, wakifika kule hawana cha kufanya, wanautupa kwa sababu hawana cha kufanya nao.

Kwa hiyo, kwa sababu hatujaweza kushika mtu ambaye ana mchanga kama ule waliozungumza isipokuwa wale wanaowazungumza ni wale ambao wamechukua ile *concentrate* na wengine wameweza kushtakiwa, kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Mbunge labda kama ana ushauri mwingine zaidi ya kusimamisha huo mgodi atuambie. Kama hawaamini Alex Stuwart mwaka huu, tumesema kwamba sasa hiyo kazi tutafanya wenyewe Watanzania wazalendo. Kwa hiyo, kazi kubwa itakuwa ni kusimamia kuhakikisha kwamba madini hayapotei.

Lakini amezungumzia kidogo tu juu ya Mwadui. Labda nichukue muda wako, amezungumzia kidogo juu ya Mwadui kwamba walikuwa wamesimama walipopata teknolojia, ndiyo wamechimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliposimama Mwadui ilikuwa ni kwamba teknolojia ambayo inaweza ikatoa ile almasi ndogo kwenye mchanga mdogo ilikuwa haipo wakati ule. Kwa hiyo, ikaonekana huo mgodi wakiendelea kuchimba hauna faida ikawa ni hasara.

Kwa hiyo, wakaona kwamba ufungwe na kwa kweli mtu aliyekuwa Mwadui *Williamson Diamond* zamani sana akifika, kama angefika wakati mgodi ulikuwa umefungwa angelia machozi. Kwa sababu majumba yalikuwa yameharibika, barabara za lami kwa sababu walikuwa wamefungwa wakaona kwamba hamna faida. Ni baada ya teknolojia kugundulika kwamba wanaweza kuchambua ile ndogo ndiyo tena wakauanzisha. Ndiyo sababu tu na sio sababu kwamba walikuwa na sababu ya kusafirisha kwenda nje.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa maana ya kanuni maelezo yako yanatosheleza, kinachotakiwa ni ufafanuzi. Sio Mbunge kupata kile anachotaka na wengine wazingatie hilo.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote* 58 *program* 10 *sub vote* 1001 kifungu kidogo 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia, nilizungumzia suala la umeme kutoka Inonelo kuelekea Ihelele kwenye ule mradi. Nikaelezea kwamba sasa hivi kuna vurugu ile Kampuni imeanza kung'oa nguzo kuanzia kule Isesa na Mbarama. Lakini kuna mvutano baina ya wananchi na ile Kampuni. Waziri hajanijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kuna utaratibu upi kama jinsi ambavyo nilikuwa nimeuliza! Kwa nini wasishughulikie kwa maana kwamba zibaki zile nguzo kwa maana ya kupatiwa umeme vile vijiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu ufafanuzi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jacob Shibiliti kwa kufuatilia suala hili. Ni bahati mbaya tu hatukuweza kumfikia kwa sababu ya muda mfupi tu. Isipokuwa hoja yake tumeisikia na tumeipokea ili tukirudi tuweze kuangalia mikataba ambayo tunayo kati ya sisi na huyo mkandarasi tuone inatuwezesha namna gani. Kama kutakuwepo uwezekano wa kuweza kuibakiza pale akatafute mingine kule anapokwenda ndiyo utakuwa uamuzi mzuri. Lakini kwanza tuangalie mikataba inasemaje na tuzungumze na huyo mkandarasi.

**MWENYEKITI:** Niende upande wa Upinzani, natoa heshima kwa Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote 58 program 10 sub-vote* 1001 kifungu 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilikuwa nachangia niliulizia suala la gesi na mafuta kama ni sehemu ya shughuli ya Muungano. Katika ukurasa 128 wa Katiba kuna nyongeza ya kwanza inazungumzia maliasili na mafuta pamoja na mafuta yasiyochujwa pamoja na gesi asilia. Haya ni mambo ya Muungano.

Katika kitabu cha *Revenue* cha Wizara kuna *sales of gas* mwaka jana walipata shilingi bilioni 6.4 halafu wakapata shilingi bilioni 11.8 na mwaka huu wanategemea kupata shilingi bilioni 8.6. katika *revenue* za gesi. Lakini mazungumzo bado yanaendelea baina yake na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kufahamu, huu mgawano wa mapato haya unafanyikaje wakati bado mazungumzo yanaendelea na jambo hili ni la Muungano katika kipindi chote hiki? Hilo lilikuwa ni swali langu la kwanza.

Lakini la pili ni kwamba kama walifikia makubaliano ya kwamba waendelee upande wa Bara, kwa nini makubaliano hayo kwa sababu hili suala la Muungano yasiwe yamefikiwa vile vile kwa kutekeleza kwa upande wa Zanzibar? Hilo nilitaka anipatie ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Alex Stuwart report*, nashukuru Waziri amesema kwamba ile ripoti ya Dr. Kipokola atаileta Bungeni. Kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 63 Bunge hili lina mamlaka ya kuisimamia Serikali na katika *Immunity and Privileges Act* Bunge hili linapata mamlaka ya kupata nyaraka yoyote Serikalini. Tunapodai taarifa yoyote kutoka Serikalini tunaidai kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa sheria. Anieleze Waziri ni kifungu gani cha sheria au Katiba anachokitumia kunikatalia kuitoa taarifa ya Alex Stuwart katika Bunge hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Hamad Rashid kwa maswali yake ya kila wakati kutaka kujua kwa undani. Sasa hivi mapato yote ambayo tunayapata, suala la kwa mfano maduhuli tunayopata kwa mfano upande wa madini tunakuwa na vipengele vya *retention* kwamba Wizara i-*retain* asilimia 25 lakini asilimia nyingine ziende kwenye Mfuko wa Serikali ambao Mfuko wa Serikali mnasema ni Mfuko wa Muungano ambao hata na Zanzibar mafao yake yako kutoka pale.

Lakini kwa upande wa gesi asilia ambayo sasa hivi tunayo tumejaribu kama Waheshmiwa Wabunge walivyopendekeza kwamba *TPDC* iwe na *retention*. Imekuwa vigumu kwa sababu ya hicho kipengele, kwa sababu hiyo gesi ni ya Muungano, yote inayopatikana inabidi iingie kwenye Mfuko Mkuu na kuna Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo bado inaendelea, sijapata taarifa kwamba imemaliza kwamba wanaangalia namna yaku-*fund* Muungano na hiyo itahusu vyanzo vyetu vya mapato vinavyoingia kwenye bajeti ya Muungano na matumizi yanayokwenda kwenye Muungano. Mauzo kwa hii gesi asilia ambayo tunapata sasa hivi inakwenda kule. Bahati mbaya tungekuwa hivyo hata na Zanzibar, lakini Zanzibar kwa sasa hivi haijapatikana gesi wala mafuta.

Suala la Alex Stuwart, Mheshimiwa Mbunge, alisema kwamba ripoti yoyote itolewe Bungeni, lakini hasa hakusema ripoti anayohitaji ni ripoti gani? Maana yake Alex Stuwart ni *internal auditor* anatupa ripoti nyingi. Sasa ripoti gani *specific?* Mwenyewe anataka kutuambia, ama tuchukue yale makaratasi yote ambayo toka tumemwajiri Alex Stewart anatuletea tulete hapa Bungeni. Nami nafikiri kwamba, Bunge linasimamia Serikali. Taarifa na nyaraka za Serikali unaweza ukazihitaji lakini Bunge nafikiri litakuwa linakwenda mbali kama tumemwajiri *auditor* wa kutusaidia kuchunguza, ametuletea na sisi tumeunda Kamati ya kuangalia aliyoyachunguza. Sasa hata kabla hatujaangalia na hayo tuyalete hapa Bungeni. Nafikiri tutakuwa tumekwenda mbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad naona pengine unahitaji kufafanua vizuri zaidi swali lako.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza labda Waziri pamoja na uzoefu wetu mdogo tulioambiwa humu Bungeni, lakini ajue tu katika mapato ya Muungano Serikali ya Zanzibar inapata asilimia 4.5 kutokana na misaada. Hata juzi Waziri wa Fedha wa Zanzibar alisema katika Baraza la Wawakilishi kwamba anasikitika kwamba *budget support* aliyotegemea kupata hakupata kutoka Serikali ya Muungano. Kwa hiyo, sio kweli kwamba yale mapato yanayotoka katika Muungano yanagawanywa kama alivyosema asilimia 4.5 inayotokana na misaada kutoka nje. Naendelea kusahihisha tu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kwamba, nilichouliza hapa na ufafanuzi ni suala zima la Katiba na Sheria kwamba suala la gesi na mafuta ni suala la Muungano. Ni dhahiri kwamba *formular* yote inayotaka kutumika ingetumika katika Jamhuri ya Tanzania hii. Kwa hiyo, unapofanya mambo haya nusu nusu halafu kuna mapato yanapatikana hayana *formular,* inakuwa ni tatizo la msingi. Sasa nafikiri Waziri angenisaidia: Je, haya mapato ambayo yameshapatikana hivi sasa ambayo yanaingia kwenye Mfuko wa Muungano mengine yako kwenye *retention,* katika hiyo *retention* Zanzibar wanapata nini? Labda angenisaidia hilo. Hasemi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la Alex Stuwart alilosema, Alex Stuwart wamekuwa na mkataba na Serikali wa muda. Kwanza miaka miwili halafu ukaongezwa muda, wamelipa dola milioni 65. Tunachotaka kufahamu sisi, katika dola milioni 65 walizolipwa, taarifa yake inasema nini ili Bunge hili ambalo ndilo linasimamia matumizi na mapato ya Serikali liweze kujua. Sasa tunaambiwa kama ni taarifa tu zimekuja na kadhalika na kwa taarifa, hata ukitazama bajeti ya Serikali, Serikali inasema inailipa Alex Stuwart asilimia tatu ya *royalty,* ni 1.9 analipwa Alex Stuwart.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama vitabu vya Wizara, mapato yao yote ya *royalty* ni shilingi bilioni 54 katika miaka mitatu iliyopita. Kwa hiyo, ukichukua 54 na 65 waliyolipwa lazima kuna fedha nyingine walizolipwa kwa sababu kule wanalipwa 1.3% *only*. Kwa hiyo, haifiki hata ile idadi. Tunauliza Bungeni hili, hizo fedha nyingine walizowalipa Alex Stuwart zinatokea wapi? Hayo ni masuala tunataka kujua.

Maana tunadai hiyo ripoti ije hapa ndani ya Bunge na hayo ni mamlaka ya Kikatiba ya Bunge hili na Bunge hili lina mamlaka ya kupata taarifa tunazohitaji. Tunahitaji taarifa ya Alex Stewart kwa sababu ni mkataba maalum wala sio *audit* kama alivyosema, hata *Auditor General* anatuletea ripoti hapa ndani. *Auditor General* analeta ripoti ndani ya Wabunge. Kwa hiyo, tunaomba taarifa ya Alex Stewart atueleze ni kifungu gani kilichomwezesha Dr. Kipokola iletwe, hii nyingine haiwezi kuletwa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kumwambia kwamba haya maduhuli yanayotokana na gesi yanaingizwa kwenye mfuko wa ku-*fund* the *union.* Ku-*fund the union* maana yake ni kuwezesha Serikali ya Muungano ifanye kazi na kuna maeneo mbalimbali ya Muungano. Sikusema kwamba igawanywe na ndiyo sababu inakwenda ku-*fund the union,* ndiyo sababu inaingizwa kwenye mfuko huo ambao ile asilimia aliyoizungumzia ya 4.5, ndiyo inakwenda moja kwa moja Zanzibar wala haiingia katika Mfuko wa kugharamia Serikali ya Muungano.

Sasa hizi zinakwenda moja kwa moja kwenye sehemu ya Muungano. Lakini ndiyo nilikuwa nasema katika mazungumzo ambayo yanaendelea na katika Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo wakija na *formular* nyingine sisi ni watekelezaji tu. Lakini kwa sasa hivi hizi fedha zinaingia kwenye Mfuko ambao unagharamia Serikali ya Muungano.

Suala la Alex Stewart nafikiri watakuwa wameninukuu vizuri kwenye *Hansard*. Sikusema kwamba taarifa ya Kipokola italetwa Bungeni, nimesema taarifa ya Kipokola tutawapa kila Mbunge. Tutaziweka kwenye *pigeon holes,* kila Mbunge atapewa. Sio kusema italetwa hapa kusudi ijadiliwe. Sisi tutawapa kila mmoja kwenye *pigeon holes.* Lakini kwa nini tutawapa hiyo taarifa? Ni kwa sababu hiyo taarifa ya Kipokola tumeitumia kwa kiasi kikubwa sana katika kudurusu hii Sera na Sheria ya Madini ambayo itakuja hapa, kusudi wakati Waheshimiwa Wabunge wanachangia hiyo, wawe na taarifa ya Kipokola wakati wanachangia Muswada huu utakapofika hapa Bungeni. *(Makofi)*

Ku-*compare* ile ripoti ya Alex Stewart na *Auditor General.* Taarifa ya *Auditor General* iko *mandated* kisheria lazima ije Bungeni kwanza. Lakini la pili, kitu kikubwa cha pili tunapoleta hapa tunasema, *Auditor General Report* ya mwaka 2004/2005 iko wapi? Mwaka 2006/2007 iko wapi? Hatusemi *Auditor General Report* walete ripoti zote zilizoanzishwa toka tupate uhuru. Kwa hiyo, lazima uwe *specific* kwa sababu sisi tunapata ripoti nyingi, sasa wewe unataka ripoti gani? Tunasema uwe *specific.* Ukishakuwa *specific,* mimi ningejua. Sasa ukisema *generally* ripoti za Alex Stewart ninashindwa.

Lakini la muhimu sana Mheshimiwa Mbunge alikuwa anazungumzia kupata shilingi milioni 60 na kitu unazozungumzia ni dola milioni 47 kufuatana na takwimu zetu mpaka kufikia Mei, 2007. Ukaguzi uliofanywa na Stuwart umetusaidia, mwanzoni tulikuwa tuna wasiwasi kama alivyosema na Mheshimiwa Selelii kwamba madini yetu

yanaibiwa na hususan ilipoingia hili la kusafirisha mchanga tukasema basi ndiyo tunapoteza kila kitu.

Kwa hiyo, Alex Stewart alitusaidia kuhakikisha kwamba hakuna kinachoibiwa. Lakini katika nyakati mbalimbali alibaini kwamba tunajua tunaposema nyakati mbalimbali ni kwamba pale mgodi ni endelevu na sio kusema umesimama. Kama ni *investment* sio kusema leo ume-*invest* wanaendelea ku-*invest more all the time.* Akasema tunabidi kuwa waangalifu na jinsi wanavyoweka thamani ya *investments* zao, jinsi ya operesheni *costs* zao inavyokuwa, kuwa labda hata na jinsi wanavyoweka fungu la fedha kwa ajili ya mazingira wakati wanafunga mgodi. Hiyo ndiyo alikuwa ameanza na kwanza kama hii ya mazingira ndiyo alikuwa amemaliza, katika hii alikuwa hajaifanya huko nyuma.

Lakini baada ya hapo, sio kwamba anasimama anaendelea kwa hiyo, kila mwaka *periodically* wanakuwa wanatuletea taarifa. Ndiyo sababu mimi nimeshindwa kujua taarifa gani alikuwa anazungumza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani hii kwa maana ya Kamati ya matumizi, ufafanuzi aliotoa Mheshimiwa Waziri unatosheleza. Kilichopo tu ni kwamba ndani ya Kanuni za Bunge zipo Kanuni ambazo zinaweza kutuwezesha kupata taarifa za ziada zozote zinazohitajika na wala sio kweli kwamba Serikali, ninavyoona mimi inaweza kukataa tu kutoa taarifa ambayo inahusu uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, mtazame, tutaweza kupata hizo taarifa kwa kulingana na Kanuni nyingine.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuweka bayana kwamba Bunge hili ndilo linaloisimamia Serikali. Hatuwezi hata siku moja kukataa kuleta taarifa yoyote inayotakiwa na Bunge ili tusimamiwe vizuri. Hatuwezi kukataa! Tunachosisitiza hapa ni kwamba, kama alivyoeleza Waziri, lazima uwe *specific*, unataka taarifa gani kwa ajili ya kitu gani na tutafuata utaratibu uliopo ndani ya Kanuni kuleta taarifa hizo zinazohitajika Bungeni. Lakini isijengeke dhana hapa kwamba Serikali inakataa kuleta Mikataba, hapana! Twendeni kwa utaratibu, ndicho tunachosema! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Nakushukuru kwa ufafanuzi huo!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana! *Vote 58, Programme 10, Sub-vote 1001 - Adiminstration and General*, Kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilikuwa na mambo mawili, lakini moja itabidi nilifute kwa sababu nakiri leo kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Waziri amejibu *at least* nimeridhika kwa asilimia 60 bila ya kuleta masuala ya kisiasa. Kwa maana hiyo, hii asilimia 40 niliyobakiza, nafikiri nitaipata katika vifungu, naweza nikaridhika katika vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, katika ripoti yangu au hotuba yangu nilizungumzia masuala ambayo yana utata katika ufafanuzi wake katika vipindi tofauti. Mkataja suala la Meremeta na suala la *Mwananchi Gold Mine*. Kwa maana hiyo, nataka kuja katika hotuba ya Kikao cha Kumi na Tatu cha Bunge hili, terehe 29 Juni, Mheshimiwa Waziri wa Nishati alitoa tamko la Serikali kuhusiana na Meremeta. Kutokana na tamko lile, Mheshimiwa Waziri alitamka kwamba kampuni ya Meremeta ni *joint venture* ya *fifty fifty* baina ya Serikali na kampuni ya *TRINEX* ya Uingereza na hii kampuni ya *TRINEX* ikawa *incorporated* hapa hapa Tanzania. Hii kampuni ya Meremeta kwa ujumla madhumuni makubwa ilikuwa ni kusaidia Kikosi cha Nyumbu cha JWTZ. Sasa, tuna taarifa au zipo taarifa kwamba *Central Bank* ilitoa shilingi bilioni 55 za *bonds* na wakanunua Dola 1,118,396,460.36 na hizi fedha zikawa *transferred* kwenda *Nedbank* kupitia *HSB Bank* iliyoko *New York* kwa ajili ya kulipa madeni ya Meremeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi ninaohitaji, sera ya nchi hii ninavyofahamu mimi kwamba tulibinafsisha mashirika ili Serikali kutokubeba mzigo wa uendeshaji na madeni, ndio lengo kubwa la kubinafsisha. Sasa, pesa hizi zote Dola milioni 118, halafu baadaye Benki hiyo hiyo *BoT* ikatuma Dola 13,340,168 kwa *TanGold* kupitia *NBC*. Sasa, suala liko hapa ambalo linahitaji ufafanuzi. Huu ubia wa Meremeta ambao ni Serikali na *TRINEX* ya *fifty fifty, TRINEX* ililipa kiasi gani? Kampuni ya *TRINEX* walilipa kiasi gani kulipia madeni haya ya Meremeta iliyokuwa inadaiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ufafanuzi kwa sehemu ya mwanzo hapo. Ahsante!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, hizi takwimu unazozisema zinatokana na taarifa gani sasa?

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinatokana na taarifa tulizonazo ambazo zinatokana na mambo ya *auditing*.

**MWENYEKITI:** Hiyo bado ni ujumla mno! *Audit* ya nani? Kwa sababu lazima tujue uhalali, unataja takwimu kubwa, Dola milioni 100 na nini, Waziri ajibu. Lakini, lazima na yeye ajue *source* ili aweze kujiridhisha! Kama haijulikani, basi Mheshimiwa nakupa muda wakati mwingine, bado tuko hapa Dodoma, utaleta hii taarifa ili Serikali iweze kuielewa.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. *Vote 58, programme 10, Sub – Vote 1001*, Kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mchango wangu wa maandishi, nilimfahamisha Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mradi wa umeme ambao unakwenda, Buzimbwe, Bulamba, Kasuguti, Mayolo, Kasaunga…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege, hujaharibu kitu! Hebu keti kwanza! Nataka niwaombe kwamba nitawaita kwa majina. Wale wanaotaka kutaja majina ya

vijiji vya kupitiwa umeme ili tuokoe muda. Sasa, nitawaita wavitaje. Mheshimiwa Kajege kwanza, ukishamaliza nitamwuliza Mheshimiwa Manyanya, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Luhahula, tutakwenda namna hiyo kabla Waziri hujajibu, uvi-*note* tu, ama sivyo tutatumia muda mwingi. Kila mtu atasimama na kutaja vijiji, Waziri unatoa matumaini, mwingine tena anasimama kwa vijiji. Kwa hiyo, nadhani tutakwenda kwa utaratibu huo. Mheshimiwa Kajege hebu malizia eneo lako!

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mhehimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaja vijiji vya Buzimbwe, Bulamba, Kasuguti, Mayolo, Kasaunga, Namibu, Busambala, Bunele, Nambaza,…

**MWENYEKITI:** Taratibu basi! Wewe unavijua sana, lakini, wape nafasi maana wataviandika, si unataka kazi ifanyike!

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli!

**MWENYEKITI:** Vitaje sasa!

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Buzimbwe, Bulamba…

**MWENYEKITI:** Ninatumaini mnaotaja haya, mnafuata utaalamu kwamba ni *route* fulani, maana kama kila Jimbo litataja vijiji vyake bila mpangilio, mradi wa namna hiyo wala hauwezekani! Endelea Mheshimiwa!

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niende kwenye hoja yenyewe. Katika mchango wangu wa maandishi nilimfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba katika mradi wa kutoa umeme kutoka Bunda kuelekea Nansio tayari miundombinu ya umeme imeishapita katika baadhi ya vijiji ambavyo nimevitaja. Lakini, kwa bahati mbaya kwa muda wa miaka mitatu sasa hivi, hakuna umeme kwa sababu hakuna *Transfoma*. Sasa, nataka kujua katika zile bilioni tisa zilizotengwa: Je, *transfoma* za vijiji hivi zitanunuliwa katika mwaka huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

**MWENYEKITI:** Safi sana! Mheshimiwa Stella Manyanya. Waziri subiri kwanza, maana haya yanayofanana bora tutumie vizuri muda wa Kamati.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani itabidi nianze na vifungu kama kawaida. Vote 58, *Proramme 10, Sub-vote 1001,* Kifungu 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu ni hasa kuona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Fedha, Mradi wa Makambako Songea haujazungumzwa kabisa. Halafu wakati huo huo wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya Waziri wa Fedha, mimi naona ile ilizungumzia bajeti *in general*.

Lakini, pia kulikuwa na vitabu vilisambazwa kabla, vilikuwa vimetaja kabisa kwamba kulikuwa na pesa za kutoka Ubalozi wa Sweden zipo, lakini katika vitabu vipya imeondolewa kabisa. Tatizo hilo ni kubwa, siwezi kuwakosesha haki wananchi wa Ruvuma kwa sababu kuna tabia ambayo inajijenga sasa hivi, Mikoa ya Kusini au pembezoni kuhamishiwa miradi yake. Sasa kitendo cha kutokuwa na *continuity* kuonyesha kwamba mradi upo, angalau kuzungumziwa, naona ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutupokea sisi kufanya kampeni *negative* wakati wa uchaguzi wake kama hawa wananchi wa Ruvuma hawezi kuwaridhisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Hakuna haja ya vitisho. Ni kinyume! Wewe sema hoja yako tu. Kwa hiyo, Makambako – Songea tumeipata!

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *Vote 58, programme 10, Adiministration, Sub-Vote…*

**MWENYEKITI:** Naomba niwasamehe kutaja hiyo! Wote ninaowaita kwa ajili ya umeme vijijini, nawasamehe hilo ili tuokoe muda.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili. La umeme na la uchimbaji madini ya *Uranium…* Naweza kuendelea?

**MWENYEKITI:** Endelea, kwa kifupi!

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea kwamba kule Namtumbo kuna Mradi wa Uchimbaji Madini ya *Uranium* ambao upo katika hatua ya uchambuzi wa *sample* mbali mbali katika maeneo yale kwa ku-*drill*…

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, umeacha la umeme?

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili!

**MWENYEKITI:** Anza na umeme kwanza!

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nayaunga mkono kwamba mwakani kulingana na vipaumbele vya mwaka huu, umeme vijijini utaanza kukamilishwa mwakani. Naungana na hilo. Lakini, katika hili, Mheshimiwa Waziri wakati anaelezea kuhusu hili suala la umeme wa gridi kutoka Makambako kuja Ruvuma, alisema utafika Songea na Mbinga, alisahau Wilaya ya Namtumbo ambayo katika upembuzi yakinifu wa awali

ulitajwa na wale wataalamu walikuja mpaka Namtumbo. Nilikuwa tu nataka nipate ufafanuzi, Namtumbo imeondolewa wakati mradi huo utakapokuja? Naomba niendelee.

**MWENYEKITI:** Endelea!

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hili suala la *Uranium*, hoja yangu ni kwamba: Je, Serikali inafuatilia hii *prospecting* inayofanyika sasa hivi ya *Uranium*? Je, wale jamaa wanatoa taarifa inavyotakiwa kulingana na taratibu? Kwa sababu sasa hivi kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na *leakage* ya *redioactive* na wasiwasi wetu ni kwamba inaweza ikaja kutuathiri watu tunaoishi karibu na eneo lile au viumbe vinavyoishi katika eneo lile na kuna uoto wa asili na bioanuai ambayo imetunzwa kwa miaka yote hiyo. Sasa, tunataka kufahamu Serikali inaangalia ile *prospecting* inayofanyika pale? Je, zile Kampuni zina uwezo wa kuzuia kama kutakuwa na *leakage* ya *redioactive* tusije kuathirika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Tuendelee na umeme vijijini. Hilo, la *Uranium* na *Radioactivity* yake utali-*note*. Mheshimiwa Luhahula, nadhani ni umeme vijijini, taja *route* yako, usianze na mshahara na kitu chochote, endelea tu.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anajibu hoja ya Mheshimiwa Selelii alisema kwamba miradi ya zamani itaendelea. Bukombe ni mradi wa zamani ambao naamini hata mwaka jana katika bajeti tulipitisha. Lakini katika hotuba na wakati nachangia, imeonyesha katika hotuba ya Waziri hajaeleza chochote kwa maana kwamba pengine mradi ule sasa kwenda Bukombe haupo. Lakini, wakati huo huo mwaka jana wametenga shilingi milioni 100 ambazo zilisaidia kufanya shughuli ya mradi wa umeme kwenda Bukombe – Kagera, tuna mradi wa umeme Bukombe – Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri awahakikishie wananchi wa Bukombe kwa sababu hawajaonekana katika bajeti hii, aidha kwamba ni mradi endelevu utakaoendelezwa au kwamba ni mradi ambao umesitishwa kwanza mpaka mwakani tutakapotoa kipaumbele.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Laizer, ni umeme au?

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni umeme! Mimi nitaongea kwa kifupi sana. Kwanza, ningependa kusema kwamba Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu hoja za Wabunge, afahamu tu awe anajibu pande zote, kwa sababu aliegemea sana kwa wapinzani na umeme ni siasa. Kwa hiyo, hatuhitaji kama atajibu upande mmoja aache upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inashiriki umeme na nchi jirani. Kwa mfano Kagera wanapata umeme kutoka Uganda na tunapata umeme kutoka Zambia. Sasa ningependa kujua, kwa kuwa Longido iko mpkani na Kenya na Mji wa Namanga Kenya

na Mji wa Namanga Tanzania ni Mji mmoja, sasa, naona kwamba siyo gharama kubwa kusambaza umeme mji wa Namanga, hata Rais alipokuja Longido alisema kwamba hatuombi fedha kwa wafadhili za kuleta umeme Longido, tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nasema zipo. Mwaka jana hata kwenye vitabu zipo, umeme Longido imepangiwa shilingi bilioni 8.6 ambazo zinatosheleza kabisa kuleta umeme Longido. Je, hizo fedha zipo au zimehamishiwa sehemu nyingine? Kama zipo, zianze kazi hiyo kwa sababu ni karibu. Ni aibu kabisa Kenya ikiwa na mwanga huku sisi tunatumia koroboi na umeme uko hapo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba ya jirani pale Namanga ni kama mlango huu na hicho kiti chako. Sasa, upande wa Kenya wana umeme, sisi hatuna! Ninakubaliana kabisa na Rais aliposema kwamba hatutafuti fedha kwa wafadhili kuleta umeme Namanga na Longido. Fedha tunazo na zipo, hata mimi nakubaliana naye. Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, umeme vijijini. Mheshimiwa Abdul Marombwa akifutiwa na Mheshimiwa Hasnain Dewji.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Lakini, kwangu siyo umeme vijijini, nazungumzia fidia kwa wananchi wale ambao wamepitiwa na nguzo za umeme tokea mwaka 2005 mpaka sasa hivi fedha zao za fidia hazijapatikana. Wamevunjiwa nyumba zao, wamekatiwa mazao yao...

**MWENYEKITI:** Taja maeneo!

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo kuanzia Bunge mpaka unafika Kilwa, karibuni Wilaya ya Rufiji na Wilaya ya Kilwa, hizo mbili, mpaka leo hii fidia zao hazipo na tumeangalia katika vifungu hivi, hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwalipa wale wananchi. Sasa hivi, wananchi ni masikini, walikuwa wanapata fedha kutokana na mazao yaliyokatwa. Mazao yale yamekatwa, fedha hazipatikani, wala za fidia hazipo. Tunawawekaje wananchi hawa? Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze fidia za wananchi hawa zitapatikana lini?

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, langu ni hilo hilo la fidia. Wananchi wangu wa Kilwa, Rufiji na Mkuranga hawajalipwa fidia kutokana na nguzo zilizopita kwenye vijiji vyao. Nataka Waziri anipe kauli, watalipwa lini fidia hao wananchi wangu na jirani zangu?

**MWENYEKITI:** Umeme vijijini! Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Buneke tu, Bukene! Si inatosha nimekusemea! Haya sema usikike! *(Kicheko)*

**MHE. TEDDY L KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi! Hapa, kama alivyosema Mheshimiwa Selelii kwamba tulikuwa tumepata bajeti ya shilingi milioni 900 na Mheshimiwa Waziri akajibu kwamba tumepata shilingi milioni 50 sasa mwaka huu, lakini, ninachotaka kuuliza hapo au kuomba ufafanuzi zaidi kutoka kwa Waziri ni kwamba, hizi shilingi milioni 50 zitapatikana kweli na kazi itaanza kuonyesha

kwamba kuna matumaini ya kupata umeme endelevu na vile vile utakuwa endelevu kwa mwaka kesho kwamba sisi tuliokwishapitishiwa tayari, tunapata mwaka kesho, ila mwaka huu tunapata hii shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuanza. Hilo suala la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kulikuwa na maonyesho ya magari yanayotumia gesi asilia. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba tulivyoletewa yale maonyesho, maana yake tunajaribu kuondoka kwenye kutumia mafuta ya *Diesel* na *Petrol* na vile vile kwa watu wa mabasi na wa ili kupunguza gharama kwa wananchi na hivyo kupunguza gharama ya usafiri na vitu vingine vinavyoweza kupanda kutokana na *Petrol* na *Diesel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijasikia chochote kuhusu mkakati maalumu wa kutengeneza gari za Serikali hasa kama *political will*, halafu na nyingine za abiria na za daladala kwa sababu gesi asilia ipo na Kenya wanainyemelea, sasa, tuwaachie Kenya wachukue gesi yetu asilia na sisi tubaki tunang'aa macho au vipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante! Mimi naendelea na umeme vijijini kwa sababu ndio wengi. Nahisi Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshmiwa John Lwanji na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha ni hivyo hivyo!

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Upande wa Mtwara ambako kuna gesi hii ya *Mnazi Bay,* inatengeneza umeme kwa ajili ya Mtwara. Hivi karibuni limejitokeza jambo ambalo kwa kweli inabidi Waziri aweze kulifafanua. Umeme huu unapatikana Mtwara Mjini tu. Halafu ukitoka pale unakwenda mpaka Mingoyo moja kwa moja mpaka Nyango kwa Mheshimiwa Mbunge wa Mtama. Toka hapo, Tandahimba haipati, Newala haipati, Masasi haipati, Nachingwea haipati, Ruangwa haipati! Sasa, imebaki kilomita 36 tu kati ya Nyangao na Ndanda. Waziri akiunganisha hapa, basi sehemu hizo zote nilizozitaja zitakuwa nyeupe kabisa.

Kwa hiyo, tunataka kumwuliza Waziri, hivi ni kitu gani zaidi? Anaweza kusema kwamba mwaka huu wa 2007/2008 nitatekeleza, lakini ahadi hii ilikuwepo toka mwezi Januari mwaka huu, sasa ni miezi saba. Hivi kinachochelewesha zaidi ni nini? Sisi kupata nyaya, nguzo, kusambaza umeme kwa wananchi wetu hawa ndio kilio kikubwa kabisa na ndicho tunachotaka Waziri aweze kufafanua. Sio peke yangu naweza kuwazungumzia, hata Mawaziri waliopo katika eneo lile, Naibu Mawaziri, karibu kila mmoja analalamika juu ya hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa John Lwanji, kwa kifupi jamani, muda unakwenda!

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *route* ya Itigi. Itigi tuna umeme, lakini hii *route* ya kutoka Itigi kwenda Chunya, kuna kijiji cha Lulanga, Itagata, Kayui, Makale, Mtakuja, Mitundu, Kalangali, Kiyombo, Kilumbi, Mwamagembe, Kintanula na Rungwa, vijiji karibu 12 na viko kando kando ya barabara tu. Umeme Itigi upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *route* nyingine ni ya kutoka Manyoni kuja huku, unapita Kilimatinde, Solya, Chibumagwa, Chikuyu, Maweni na Kintinkhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivyo! Ahsante!

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ndogo sana. Katika kuchangia, nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba katika Kijiji cha Kisaki *Station* ambacho ni *Station* ya *TAZARA* wana jenereta kubwa sana ambayo *Regional Manager* wa *TANESCO* amekwenda kufuatilia mwito huo na Rais ametuambia kwamba atafuatilia; Je, sasa hivi wamefikia hatua gani? Ahsante sana!

**MWENYEKITI:** Naona hawa wa umeme, sina hakika kama la Mheshimiwa Mwanawetu linahusu umeme!

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshinmiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mimi kuhusu umeme sina mazungumzo zaidi kwa sababu mwenzangu ameshazungumza na Waziri Mkuu pia ametufahamisha jinsi gani itakavyokuwa. Tutazidi kusubiri kwa sababu nguzo tumeishaziona katika maeneo yetu zimeanza kusambazwa, lakini hatujui ni mpaka lini, labda tutaelezwa.

Ninachotaka kuzungumza ni kuhusu wawekezaji wa Kilwa. Hilo ndio haswa ambalo nilikuwa nimelikusudia. Kwa wananchi wa Kilwa wanapoletewa miradi huwa na matumaini kwamba watapata manufaa kwa miradi hiyo na Halmashauri kadhalika huwa inafikiria hayo hayo kuwa itapata faida na wananchi wake. Lakini, suala la miradi ya Kilwa limekuwa tatizo.

Nafikiri tangu *Songas* ilipoanzishwa baada ya kugundulika gesi sijui mwaka 1973, kulikuwa na Kamati ya Maendeleo ya Wananchi wa Kilwa ambao walikuwa wameangalia hali halisi itakuwa vipi. Kuna masuala ambayo yalionyesha kwamba hakuna tija katika mambo ya mradi huu wa gesi. Yapo ambayo tulielezwa kwamba tija itapatikana…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, unachangia, ama! Unatakiwa katika hatua hii kudai ufafanuzi. Maana unaanza kusema nazungumza, nazungumza! Hairuhusiwi! Tafuta jambo mahsusi, omba ufafanuzi!

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu ninalotaka kupata ufafanuzi ni kuhusu wawekezaji. Ni lini wao wataweza kutupatia Halmashauri asilimia zetu za mapato? Kwa sababu Serikali inapata asilimia 12.5 lakini Halmashauri ya Kilwa haipati hata senti moja na wananchi hawapati manufaa yoyote kuhusu mradi huu wa gesi

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninahitaji ufafanuzi, Halmashauri ifanye nini ili na yenyewe iweze kupata mapato kutokana na mradi huu?

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mrabaha wa Gesi sasa. Naona Waziri kwa haya ya umeme vijijini… Mheshimiwa Rwilomba umechelewa, haumo kwenye orodha yangu!

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumo kwenye orodha ya kwanza, tunashangaa umeturuka.

**MWENYEKITI:** Basi, watu wa Geita nipate mtu mmoja! Haya endelea Mheshimiwa Rwilomba umsemee na Mheshimiwa Mabina kabisa!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 21(4) inashauri kama hoja inayojadiliwa ni muhimu sana, basi Bunge linaweza likaongeza muda wa nusu saa ili kukamilisha kazi hiyo. Kwa hiyo, naomba tutumie hiyo, tuongeze muda wa nusu saa ili mjadala uende vizuri na kwa sababu hoja ni nyingi zilizowasilishwa ili ziweze kujibiwa vizuri. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia kwa maandishi, nilishauri na nimekuwa nikienda Wizarani kuomba kwamba umeme unaokwenda Bukombe, ili uweze kuwa wa manufaa na wa kiuchumi ni vyema upitie katika Vijiji vya Bukoli, Lwamgasa, Nyarugusu, Katoro halafu uelekee Bukombe. Sikuweza kujibiwa. Naomba nijibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa nimeulizia kuna wananchi wachimbaji wadogo wamehangaika sana, walikuwa wameomba kufuatia nia njema ya Serikali kuwasaidia maeneo ya kuchimba waweze kupata kibali kama alivyosema Waziri kuendelea kuchimba eneo la Matabi kuliko sasa hivi wanavyohangaika, wameomba tangu mwezi wa pili mpaka sasa hivi hawajapata majibu na wanahangaika na niliomba maelezo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri, naona haya ya umeme vijijini ni mengi, kuna Mwibara, Makambako, Songea, Namtumbo, Bukombe, Namanga, Kibiti, Kilwa Kusini, Bukene Ruangwa, Nachingwea, Itigi na Chunya. Nadhani kuna jibu la jumla kuhusu utekelezaji.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona jibu la jumla naona ni kama Mheshimiwa Kajege aliloliuzia la *tranforma* nafikiri tukiingia ule utaratibu wa umeme wa vijiji kwa bajeti itakavyokuwa kubwa ni kwa utaratibu

utakaokuwepo wakati ule ni rahisi kuliko mengine. Kuna mradi wa Makambako-Songea....

**MWENYEKITI:** Mimi ningekushauri Mheshimiwa Waziri kwa sababu vijiji ni vingi na ninaelewa mipango ipo katika hatua mbalimbali, ukitoa *commitment* kwamba tutapata kwa maandishi itatusaidia na tutaokoa na muda. Kwa hiyo, tutayapata maelezo haya kwa maandishi.

Mheshimiwa Dr. Slaa una dakika moja tu unaweza kupiga dakika moja?

**MHE. DR. WILBLOD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajitahidi katika dakika. Natumia *program* hiyo hiyo kwa sababu ya muda nisiisome yote.

Nilipokuwa nimechangia kwa maandishi nilikuwa nimemwuliza Mheshimiwa Waziri suala la *Tan Gold* yeye katika hotuba yake siku alipojibu hapa Bungeni alizungumzia kwamba *Tan Gold* inamilikiwa asilimia 100 na Serikali, lakini baadaye utata ukajitokeza katika hotuba yake akazungumzia kwamba kuna mkataba pia kati ya *Tan Gold* na *Randi gold*. Sasa nilimwuliza: Je, *Tan Fold* imeandikishwa wapi na *Tan Gold* hiyo iliyoandikishwa mahali ambapo ataniambia Wakurugenzi wake ni nani na hiyo *Tan Gold* inafanyakazi katika maeneo yapi? Hayakuonyeshwa mahali popote katika kitabu cha Waziri. Sasa kama *Tan Gold* inafanya kazi ya kutafuta madini, nilitegemea tutaiona hapa. Kwa ajili ya muda naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dakika mbili tu Mheshimiwa Waziri kwa yale yaliyosalia matumizi ya gesi kwenye gari hili aliloliuliza Dr. Slaa na labda uwape Kilwa Kusini na kadhalika mambo ya fidia.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda haraka haraka. Waheshimiwa Wabunge wa CCM, naomba mnisamehe nikianza na Mheshimiwa Slaa kwa sababu walikuwa wanaliandika kwenye magazeti na wakati mwingine kwa kulipotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tan Gold* kama Mheshimiwa Dr. Slaa alinisikia wakati natoa kauli, nilisema inamlikiwa na Serikali *one hundred percent* nitumie kingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tan Gold* ni kampuni binafsi ya watu wengi na ambao wametafuta kwamba *Tan Gold* wahusiane naye kuwatafutia madini lakini nje ya Buhemba. Kwa hiyo, *Tan Gold* ni *complete separate* kampuni wala hatuna hisa hata moja isipokuwa tu ni ushirikiano wa kutafuta madini.

Sasa Waheshimiwa Wabunge ambao nitazungumza haraka haraka, Bukombe imo kwenye bajeti na unafadhiliwa na Sweden tumeomba hela Sweden.

Mheshimiwa Lekule, Longido ni ahadi ya Rais na mimi nimekutana naye na hiyo tutahakikisha kwamba inaanza kutekelezwa kwenye pesa kidogo ambazo tutakuwa nazo. Vijiji vya …

**MWENYEKITI:** Vijiji tulikwishakubaliana utajibu tu kwa maandishi tutayapata hayo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Kuhusu maswlai ya Mheshimiwa Malombwa na Mheshimiwa Dewji yanayohusu fidia, sasa hivi tunatafuta fedha za fidia, lakini nataka kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge, najua humu Bungeni tunatoka maeneo mbalimbali. Kuna Waheshimiwa Wabunge, walionifikia wakatuambia jamani sisi tuleteeni umeme vijijini, tutajitolea hatutaki fidia kusudi kupunguza gharama za umeme vijijini. Lakini kuna wengine watataka fidia, hili halitawahusu wa Kilwa na kwenda Lindi, lakini maeneo mengine wakiwa na masharti ya namna hiyo yatawacheleweshea kufikisha umeme wanapotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kasella – Bantu aliyozungumzia kutumia *gas* na mimi nilikuwa nimekwishazungumza kwamba nangoja kwanza. Sasa *TPDC* inafanya matayarisho na inafanya kama *feasibility* ya huo mradi na imekwishaleta gari la maonyesho.Nangoja wakishamaliza halafu wakaweka miundombinu *especially* kama wanavyotaka kufanya kama Dar es Salaam wanataka kuweka miundombinu nitakuwa wa kwanza kwenda kushauri Serikali kwa sababu ile inaweza ikatumia *double* ukawa una-*switch*. Nitakuwa wa kwanza kwenda kushauri Serikali kwamba tutumie hiyo *gas* kwamba tukiwa Dar es Salaam tukitoka huko ndiyo tu-*switch* kuingia maeneo mengine.

Halafu Mheshimiwa Vita Kawawa, nataka kumtolea wasiwasi kwamba sasa hivi kinachofanyika ni utafiti na siyo uchimbaji. Lakini madini ya *Uranium* yanakuja wanapochimba yanakuja *nature* inayoitwa *Uranite*, *Uranite* haina *radiation,* kwa hiyo, haina matatizo na wanazotoa sasa hivi ni *sample* na sisi tunawafuatilia kwa ukaribu sana kusudi tuweze kuhakikisha siyo tu hawa tu wa *uranium* lakini wote ambao wana *license* huwa kila mara wakati wanatoa taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tumekwishapita muda baada ya ile hoja ya kuongeza muda kuanguka, sasa inabidi tutumie kanuni ya 81 (6) ambayo inatuingiza katika kupitisha mafungu haya kwa ujumla *(guillotine).*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts... Tshs. 1,205,654,400/=*
Kifungu 1003 – *Policy Planning ………… ” 250,796,000/=*
Kifungu 2001 – *Minerals………………… ” 2,966,473,100/=*
Kifungu 2002 – *Madini Institute………… ” 781,186,700/=*
Kifungu 2003 – *Research and Laboratory*
*Services ……..... … … “ 1,264,881,200/=*
Kifungu 2004 – *Transort – London …… “ 1,493,706,400/=*
Kifungu 3001 - *Energy and Petroleum.. .” 41,549,559,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**FUNGU – 58 – Wizara ya Nishati na Madini**

| | | |
|---|---|---|
| *Kifungu 1001 – Administration and General... ... ... ... ... ...* | *Tshs.* | *250,000,000/=* |
| Kifungu 1003 – *Policy Planning………..* | *"* | *200,000,000/=* |
| Kifungu 2001 – *Minerals…………………..* | *"* | *1,047,408,000/=* |
| Kifungu 2002 – *Madini Institute ………* | *"* | *500,000,000/=* |
| Kifungu 3001 – *Energy and Petroleum.. ..* | *"* | *312,409,584,900/=* |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa taarifa ya Kamati, kwa heshima na taadhima nakuomba kwa idhini yako niwataje Wabunge watatu ambao walichangia kwa maandishi lakini nilisahau kuwataja. Nao ni Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa John Paul Lwanji na Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo.

Baada ya hayo, sasa naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2007/2008 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe makisio ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu. Kanuni ya 104 (2) nitaomba kusoma maneno yanayohusika, nitaomba tu kusoma maneno ambayo yanahusika.

"Mara tu baada ya hoja ilikuwa ikijadiliwa kuamuliwa Mbunge yeyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya kanuni hii aweza kusimama mahali pake na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule. Baada ya hapo Mbunge huyo atatoa taarifa ya hoja yake kwa maandishi kwa Katibu na hoja itashughulikiwa wakati unaofaa kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli uliowekwa na kanuni ya 23 (4)."

Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Mkataba mpya wa Mgodi wa Buzwagi ambao Mheshimiwa Waziri ameeleza maelezo ambayo siyo sahihi, amedanganya na ameeleza vitu ambavyo kwa kweli sivyo ambavyo vipo katika Mkataba ambao ameusaini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa rasmi ya mdomo kwamba nakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule kuchunguza mkataba mpya wa Madini ambao Waziri wa Nishati na Madini ameusaini bila kuzingatia maagizo ya Rais ya kupitia mikataba ya Madini aliyoyatoa mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Hiyo ni taarifa tu na haina madhara yoyote. Tutasubiri sasa utakapoleta kwa maandishi ndiyo tutajua mchakato wa kuishughulikia chini ya kanuni ya 23 (4). Ahsante.

Baada ya hapo, kwa kuwa muda umefika, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,
Tarehe 17 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*